Ishara 9 za kanisa linaloendelea vyema kiroho

Makanisa mengi leo yamepoteza mwelekeo

Ishara ya kwanza

Kanisa linaloendelea vyema kiroho ni kanisa ambalo mahubiri yake yanafafanua Biblia na si mawazo ya wanadamu.

Yaliyomo katika sura.

Tutatazama mambo matatu kuhusu umuhimu wa neno la Mungu katika kanisa. Kwanza, kazi ambayo neno la Mungu linafanya katika kuleta uzima. Pili, kazi ambayo neno la Mungu linafanya katika utakaso. Tatu, kazi ya mhubiri wa neno la Mungu.

Kuna mambo mengi leo ambayo watu wanatafuta katika makanisa. Wengi unapaowauliza kuhusu kanisa ambalo wanapenda kulihudhuria, watakueleza mambo tofauti tofauti. Kwa mfano, mmoja atakuambia kwamba anapenda kuhudhduria kanisa ambalo mchungaji wake ni kijana na anahubiri kwa nguvu sana; wengine watakuambia kwamba wanapenda kanisa ambalo mhubiri wake anafanya miujiza; wengine watakuambia kwamba wanapenda kanisa ambalo wanacheza mziki mzuri sana na wachezaji wa vyombo wanajua kutumia vyombo vyao vyema kabisa; wengine pia watasema kwamba wanapenda kanisa ambalo mjengo wake ni mkubwa sana na ni maridadi kabisa. Katika haya yote tunaona kwamba yale ambayo wengi wanapenda katika makanisa ni kinyume na mafundisho ya Biblia kuhusu kanisa la kweli.

Wakati mtu anatafuta kanisa la kuhudhuria, kuna mambo mengi ambayo anafaa kuzingatia sana. Lakini swali muhimu ambalo tunafaa wote kujiuliza ni, je, kanisa ambalo ni la kweli kulingana na mafundisho ya Biblia, ni kanisa la aina gani?

Kuna vitabu vingi sana ambavyo vimeandikwa kuhusu swali hili: je, kanisa ambalo linafaa ni kanisa la aina gani? Kwa wengi kanisa ni mahali pa kufanya urafiki, mahali pa kupata pesa, mahali pa kusherekea au mahali pa watoto na wanawake. Kuna vitabu vingi ambavyo vimeandikwa vikionyesha kwamba mambo haya ndiyo ambayo yanajumlisha kanisa la kweli.

Je, wewe unawaza aje kuhusu jambo hili? Je, kanisa ambalo linafaa, ni kanisa la aina gani? Ikiwa wewe ni mtu ambaye anatafuta kanisa la kushiriki, basi unafaa sana kuzingatia sana swali hili. Pia hata kama kweli wewe ni mshirika wa kanisa fulani, unafaa kuzingatia swali hili sana. Pia hata kama unasema kwamba wewe umetosheka mahali ulipo, unahitaji kujua kanisa ambalo linafaa ni kanisa la aina gani. Ikiwa pia uko katika kanisa fulani na wewe unalitumikia kanisa hilo, basi unahitaji kujua jinsi unafaa kuwa wa faida kwa kanisa lako. Unafaa kujua msingi halisi wa kanisa lako ni gani. Pia ikiwa wewe hujaokoka, unahitaji kuhudhuria kanisa kila mara ili usikie mafundisho ya neno la Mungu, na kwa hivyo unahitaji kujua kanisa la kweli ni la aina gani.

Unafaa kuwa mwangalifu sana kuhusu jambo hili, kwa sababu kuna wengi ambao watakuambia kwamba kanisa ambalo linafaa ni lile ambalo linacheza muziki vizuri sana au lile ambalo mchungaji wake ni kijana na anahubiri kwa nguvu sana au lile ambalo linawapatia watu pesa au linafanya miujiza. Swali ambalo unafaa kujiuliza wakati unaambiwa mambo kama haya ni, je, haya kweli ndiyo mafundisho ya Biblia kuhusu kanisa la kweli?

Kusudi kuu la kitabu hiki ni kuuliza na kujibu swali hili. Je, kanisa ambalo linafaa ni kanisa la aina gani?

Katika kitabu hiki nitakupatia ishara 9 ambazo zinaonyesha kanisa ambalo linafaa au kanisa la kweli. Sisemi kwamba ishara hizi ndizo za pekee katika kanisa la kweli. Kuna mambo mengine kama ubatizo, meza ya Bwana ambayo ni muhimu lakini nimeyataja tu kwa ufupi. Kitabu hiki hakina mafundisho yote kuhusu kanisa na kazi yake. Kile ninafanya ni kushughulikia mambo fulani ambayo ni muhimu kabisa katika kanisa la kweli ambayo yamepuuzwa. Hata kama watu hawaelewi kabisa kuhusu ubatizo na meza ya Bwana, hawajaacha kufanya mambo haya. Yale ambayo tutajifunza katika kitabu hiki ni mambo ambayo yamesahaulika kabisa katika makanisa mengi.

Hakuna kanisa kamilifu, hata lile ambalo ninachunga si kamilifu. Lakini hii haimaanishi kwamba makanisa yetu hayafai kuwa jinsi Mungu ameyakusudia yawe. Ni kusudi langu kuhimiza jambo hili.

Mahubiri ambayo yanafafanua Biblia na si mawazo ya wanadamu

Ishara ya kwanza ya kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kwamba mahubiri ambayo yanahubiriwa humo, yanafafanua Biblia na si mawazo ya wanadamu. Hii ndiyo ishara ya kwanza na muhimu zaidi kuliko zingine, kwa sababu ikiwa ishara hii inatekelezwa vyema, basi ishara zingine zitajitokeza zenyewe. Hii ndiyo ishara kuu na ikiwa katika kitabu hiki utasoma tu sura hii pekee, basi utakuwa umesoma sura ambayo itakufaidi zaidi. Sura hii itakusaidia kujua kile ambacho ni muhimu sana na ambacho wachungaji wote wanafaa kukitilia maanani. Pia utasaidika kwa kujua kile ambacho washirika wanafaa kutarajia kutoka kwa wachungaji wao. Kazi kuu ya kila mchungaji ni kufafanua Biblia wakati anapohubiri.

Hii ni ishara kuu sana kwamba hata kama utaweza kutimiza zile ishara zingine nane na kukosea katika hii moja, basi mambo hayatakuwa sawa katika kanisa lako. Hii ni kwa sababu msingi wa haya mambo mengine manane, ni mahubiri ambayo yanafafanua Biblia. Lakini ikiwa jambo hili la kufafanua Biblia ndilo la kwanza kutimiza katika kanisa lako, basi jua kwamba kanisa hilo litakuwa linaendelea vyema kiroho na litakua katika imani kwa sababu Mungu atakuwa anafanya kazi ndani ya wote ambao wanahudhuria, kwa nguvu za Roho Mtakatifu kupitia kwa neno Lake.

Je, mahubiri ambayo yanafafanua Biblia ni mahubiri ya aina gani? Haya si mahubiri ya maada. Mahubiri ya maada yanazingatia jambo fulani badala ya kuzingatia kifungu cha Biblia. Mchungaji anaweza kuamua kuhubiri kuhusu jambo fulani kama maombi, kuwalea watoto au utakatifu. Kile mhubiri anafanya wakati anahubiri, anakusanya mistari fulani fulani katika Biblia ili aweze kuhakikisha ukweli wa maada ya mafundisho yake. Unaposikia mahubiri haya utasikia kwamba hayatoki tu katika kifungu kimoja cha Biblia bali katika vifungu tofauti tofauti vya Biblia.

Pia mahubiri haya ya maada yanaweza kutoka katika kifungu kimoja cha Biblia ambacho kinazungumza wazi kabisa kuhusu maada yaa mahubiri. Kwa ufupi ni kwamba mahubiri ya maada ni mahubiri ambayo mchungaji anayatumia kuthibitisha kile anataka kuhubiri na kusema.

Mahubiri ambayo yanafafanua Biblia, ni mahubiri ambayo yanazingatia kifungu fulani cha Biblia kwa kukifafanua jinsi kimeandikwa na kueleza ukweli ambao unapatikana katika kifungu hicho. Mahubiri haya huwa yamekusudiwa kuoonyesha mamlaka ya neno la Mungu, kwamba Biblia kweli ni neno la Mungu. Mchungaji ambaye anahubiri neno la Mungu ni yule ndiye yule anasikia ni nini Mungu anasema katika neno lake. Yeye ni mtu ambaye anajinyenyekeza kwa ajili ya neno hilo. Manabii wa Agano la Kale na mitume wa Agano Jipya hawakuambiwa tu waende wazungumze maneno yao, bali walipewa ujumbe ambao walihitajika kuhubiri yaani neno la Mungu. Vivyo hivyo, wachungaji wa leo wana mamlaka ya kuhubiri kutoka katika neno la Mungu bora tu wahubiri kwa kufafanua neno la Mungu. Wachungaji hawajaambiwa tu waenda wahubiri kile ambacho wanaona ni chema, wao wameamrishwa wazi kabisa waende wahubiri neno la Mungu pekee. Hii ndiyo amri kuu kwa wachungaji wote (2 Timotheo 4:1-2).

Wachungaji wengi huwa wanakubali mamlaka ya neno la Mungu na wanakiri kuamini kwamba Biblia ni ya kweli. Lakini ikiwa wachungaji hawa hawatajifunza na kuendelea kuhubiri mahubiri ya kufafanua Biblia, hawakui katika kuhubiri kwao. Lengo kuu ya kuhubiri, si kuchukua maana yako na kuiweka katika mstari fulani. Lengo kuu la kuhubiri ni kufundisho yale ambayo mstari wenyewe unafundisha. Kwa mfano si vyema kwa mchungaji kuanza kuamua atahubiri kuhusu kutoa sadaka na halafu kuchagua mstari fulani ambao utautumia kupotosha watu. Ni rahisi kusoma mstari mmoja katika Biblia na kuutumia kujihimiza lakini inaweza kuwa kwamba Mungu hakukusudia kile ambacho wewe umepata katika mstari huo. Unaweza tu kufahamu mafundisho wa mstari wa Biblia kulingana mafundisho ya kifungu chote ambao mstari huu unapatikana. Utaweza kuuelewa sana ikiwa utausoma pamoja na mistari mingine ambayo iko katika kifungu hicho. Kwa kufanya hivyo ndipo utaweza kuelewa kabisa ni nini Mungu alikusudia kutokana na kifungu hicho chote.

Mhubiri yeyote kila wakati anafaa kuwa anajifunza kutoka kwa Biblia. Hafai kutumia Biblia kama kisingizio cha kile ambacho anataka kusema au kile ambacho ameamua tayari. Ukitazama vyema utaona kwamba mara nyingi mhubiri ambaye hahubiri kwa kufafanua vifungu katika Biblia, yeye huwa anahubiri kile ambacho ameamua atahubiri. Mara kwa mara utapata kwamba kusanyiko la wakristo ambao wanapokea mahubiri haya. Huwa wanasikia tu kile ambacho wanajua au walitarajia. Utapata kwamba hakuna chochote ambacho huwa kinaongezwa katika kufahamu kwao. Mara kwa mara watu kama hawa huwa hawajifunzi kutoka kwa Biblia.

Kufafanua Biblia ni kufundisha au kujifunza kutokana na yale ambayo yako katika kifungu fulani badala ya kufundisha au kujifunza kile ambacho unataka kusikia na kufunza. Kila mara tunapojitayarisha kufundishwa au kujifunza kutokana na kifungu fulani, tunafaa kuomba Mungu atufundishe yale ambayo yameandikwa katika kile kifungu. Katika Biblia, Mungu hutufunza mambo mengi. Kwa mfano, tunajifunza kuhusu wokovu wetu na inamaanisha nini kutubu na mambo mengi ambayo Roho Mtakatifu huendelea kutufunza kila wakati tunaposoma Biblia. Haya mambo yote hatukuyajua wala kuyafahamu. Mara kwa mara wakati tunajifunza kwa kufafanua Biblia, huwa Mungu anatufundisha maana ya yale ambayo tunayasoma. Mambo haya hutufunguwa mioyo yetu kwa kuuona ukweli ambao unapatikana katika neno Lake. Wachungaji ambao huwa hawahubiri kwa kufafanua Biblia huwa wanawafanya watu ambao wanawasikiza mwaka baada ya mwaka kukosa kukua katika ukristo wao. Wao huwafanya washirika hawa kuwa wafuasi wao badala ya kuwa wafuasi wa Mungu. Washirika hawa huwa wanamsikiza mchungaji sana kuliko kumsikiza Mungu. Kile ambacho tunahitaji na kuomba juu yake ni kwamba tutakuwa watu wa Mungu kwa kupitia kwa neno Lake. Neno hili ni lazima lihubiriwe kwa kutuongoza kwa Mungu badala kwa mwanadamu. Kile ambacho tunahitaji sana, ni kusikia kutoka kwa Mungu na si kwa mwanadamu yeyote. Kwa hivyo kila mchungaji anafaa kuhakikisha kwamba watu ambao anawahubiria neno la Mungu wanasikia kile ambacho Mungu anasema kutoka kwa neno Lake na si kutoka kwa mawazo yake mwenyewe. Lazima mchungaji ajitolee kwa Mungu ndipo ataweza kuwafaidi watu wa Mungu.

Kazi kuu ya Neno la Mungu

Tunafaa kuhakikisha kwamba kila wakati mahubiri yetu ni ya kufafanua Biblia kwa sababu neno la Mungu ndilo linafaa kuongoza mahubiri yetu. Kila kanisa linafaa kuhakikisha kwamba linaongozwa na neno la Mungu pekee kwa sababu Mungu mwenyewe amechagua kwamba watu watapata uhai kiroho kutokana na neno hili. Hivi ndivyo Mungu amekuwa akifanya kazi katika historia yote; amekuwa akitumia neno lake kuwaletea wengi uhai wa kiroho.

Kuna wakati nilialikwa mahali fulani kuhubiri. Nilipokuwa ninazungumza kuhusu Biblia na yule ambaye alikuwa amenialika, aliniambia jambo ambalo lilikuwa la kushangaza sana. Aliniambia kwamba kanisa ndilo lilifanya Biblia iwepo. Ukweli ni kwamba watu wa Mungu hawezi na hawajawahi kutengeneza neno la Mungu. Biblia inasema, “Kwa mapenzi Yake Mwenyewe alituzaa kwa Neno la kweli kusudi tuwe kama mazao ya kwanza katika viumbe vyake vyote” (Yakobo 1:18). Ukisoma kitabu cha Mwanzo utaona kwamba Mungu ameumba kila kitu kwa neno Lake pekee. Katika Mwanzo 12, Mungu alimwita Abrahamu kutoka katika nchi yake kwa neno Lake pekee; katika Eziekieli 37, Mungu alimpatia Ezekieli maono ambayo alikuwa ayazungumze kwa Waisraeli ambayo yalikuwa kwamba Mungu alikuwa ayafufue maisha yao kwa neno Lake. Mungu mwenyewe alituma neno Lake kwa njia ya Mwanawe Yesu Kristo ambaye ndiye Neno aliyefanyika mwili (Yohana 1:14); katika kitabu cha Warumi tunasoma kwamba Roho Mtakatifu anatumia neno la Mungu kuwapatia watu wake uzima wa milele. Mungu katika nyakati zote amekuwa akifanya kazi kupitia kwa neno Lake. Watu wa Mungu hawajawahi kutengeneza neno la Mungu.

Tumeona kazi kuu ya neno la Mungu katika maisha yetu, sasa tujifunze umuhimu wa kuhubiri Biblia katika makanisa yetu. Ninataka kuzungumzia mambo haya matatu; Kazi ya neno la Mungu katika kuleta uhai wa kiroho, kazi ya neno la Mungu katika kazi ya utakaso wa watu Wake na kazi ya mhubiri wa neno la Mungu katika kanisa.

Kazi ya neno la Mungu katika kuleta uhai wa kiroho

Tutaanza pale ambapo Biblia inaanzia. Katika kitabu cha Mwanzo 1, tunaona kwamba Mungu aliumba kila kitu kwa neno Lake peke. Tunapoendelea kusoma, tunaona kile ambacho kilifuatilia baadaye. Katika Mwanzo 3, tunasoma kuhusu kuanguka dhambini kwa Adamu na Hawa. Hapa tunaona kwamba wakati Adamu na Hawa walianguka dhambini, walifukuzwa kutoka katika uwepo wa Mungu. Lakini kutokana na neema kuu ya Mungu, wao hawakupoteza tumaini kabisa. Hata kama wao hawakuwa katika uwepo wa Mungu tena, Mungu aliwapa ahadi. Katika Mwanzo 3:15, Mungu alimlaani nyoka. Alimwonya kwamba uzao wa mwanamke

ungemponda kichwa chake. Haya yalikuwa maneno ya kwanza ya tumaini ambayo Adamu na Hawa walisikia baada ya kuanguka dhambini.

Tunapoendelea kusoma, tunasoma katika Mwanzo 12 kwamba Mungu alitumia ahadi katika neno Lake kumwita na kumvota Abrahamu kutoka katika nchi yake. Kwa neno Lake, Mungu ameumba watu wapya ambao wamelisikia neno hilo na kuja kwake Mungu kwa imani. Mungu ameumba watu wake kupitia kwa neno Lake.

Abrahamu hakuweka kamati ambayo ilichunguza neno la Mungu ili aweze kufahamu kabisa ni nini Mungu anasema. Bali neno la Mungu lilimjia Abrahamu mwenyewe na akaahidiwa baba wa mataifa yote ya ulimwengu. Abrahamu alitii neno hilo mara moja. Alimwamini Mungu ambaye alikuwa amemwambia mambo hayo. Tunajua sote hadithi ya wazao wa Abrahamu ambao waliongezeka sana katika nchi ya ahadi na baadaye walielekea Misri ambako waliishi katika utumwa kwa miaka mingi sana. Wakati mambo yalionekana kwamba huenda utumwa huo ulikuwa wa milele, je Mungu alisema nini? Mungu alituma neno Lake na katika kitabu cha Kutoka 3:4, Mungu alianza kwa kumwita Musa. Musa hakuweza kuelewa kabisa kuhusu kichaka ambacho kilikuwa kimeshika moto. Kutoka katika kichaka hicho, Mungu alizungumza neno Lake kwa Musa. Neno la Mungu halikumfikia tu Musa pekee bali liliwafikia watu wa Israeli wote wakati Mungu aliwaita wawe watu Wake.

Tunaposoma Kutoka 20, tunaona kwamba Mungu aliwapatia watu wake neno Lake na kwa kulipokea neno hilo, watu hao walifanyika Wake. Ni kupitia kwa neno la Mungu watu wa Israeli walifanyika kuwa watu wa Mungu. Tunaposoma Agano la Kale, tunaona kwamba neno la Mungu liliwajia wengi, na wengi wao walilipokea na kuokoka. Jambo hili linatufundisha kwamba neno la Mungu lilifanya kuu miongoni mwa watu wa Mungu. Hii ndio sababu neno la Mungu liliwajia watu wake mara nyingi. Kwa mfano tunasoma katika 1 Wafalme 18:1 kwamba, “Baada ya muda mrefu, katika mwaka wa tatu, neno la Bwana likamjia Eliya.” Maneno kama haya, “neno la Bwana lilikuja”linapatikana katika Agano la Kale zaidi ya 3,800. Neno la Bwana ndilo linaumba na linaongoza watu wake. Ni wale tu ambao wameokoka ndiyo wanaoamini neno la Mungu. Wale wote ambao hawajaokoka, hawawezi kuamini neno hili.

Je, tunajuaje wale ambao wameokoka na kumwamini Mungu? Tutawajua tu ikiwa wamepokea neno la Mungu na kuokoka. Wao wameamini neno la Mungu na wanalitegemea katika kila jambo katika maisha yao. Wao hawaamini tu neno, lakini pia wanamwamini Mungu ambaye ndiye anayenena nao. Wakati tunasoma Agano la Kale tunaona kwamba Mungu alizungumza na watu wake kupitia kwa neno Lake. Mkristo ni mtu ambaye anatembea kwa imani na si kwa kuona. Huwa mkristo anatumainia maisha ya milele anapokuwa anaishi hapa ulimwenguni kuliko jinsi anavyojitoa kwa vitu ambavyo anaviona kwa macho yake. Katika maono ya Ezekieli katika sura ya 37, tunaona kwamba uzima huja kwa kupitia kwa neno la Mungu.

“Mkono wa Bwana ulikuwa juu yangu, Naye akanitoa nje kwa Roho wa Bwana na kuniweka katikati ya bonde lililokuwa limejaa mifupa tele. Akanipitisha pande zote kwenye hiyo mifupa, nami nikaona mifupi mingi sana ndani ya lile bonde, mifupa iliyokuwa imekauka sana. Akaniuliza, 'Mwanadamu, mifupa hii yaweza kuishi?' Nikajibu, 'Ee Bwana Mwenyezi, Wewe peke yako wajua.' Ndipo akaniambia, 'Itabirie mifupa hii na uiambie, 'Enyi mifupa mikavu, sikieni neno la Bwana! Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo kwa hii mifupa: Nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi. Nitawawekea mishipa, nami nitaifanya nyama ije juu yenu na kuwafunika kwa ngozi. Nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtakuwa hai. Ndipo mtakapojua kuwa Mimi ndimi Bwana” (Ezekieli 37:1-6).

Haya ni maono ya kuhimiza wengi. Ikiwa wewe ni mchungaji ambaye kuna wakati unaona kwamba kanisa ambalo unalichunga linakufa au ikiwa unakumbuka wakati ulikuwa huna tumaini lolote la wokovu, basi pata himizo kutoka kwa kifungu hiki cha Ezekieli. Hiki ni kifungu ambacho kimejawa na tumaini kubwa sana kwa wale wote ambao wameokoka. Katika mistari ya 7-10, tunaona kile ambacho kilitendeka wakati Ezekieli alitii kulingana na maono hayo. Anasema,

“Basi nikatabiri kama nilivyoamriwa. Wakati nilipokuwa ninatabiri, kukawa na sauti, sauti ya kugongana, nayo mifupa ikasongeleana, mfupa kwa mfupa mwenziwe. Nikatazama, mishipa ya nyama vikatokea juu ya mifupa na ngozi ikaifunika, lakini hapakuwa pumzi ndani yake. Ndipo aliponiambia, 'Utabirie upepo, tabiri na mwanadamu uuambie, 'Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo, 'Njoo kutoka pande nne, Ee pumzi, nawe upulizie pumzi ndani ya hawa waliouawa, ili wapate kuishi.' Hivyo nikatabiri kama alivyoniamuru, nayo pumzi ikawaingia, wakawa hai na wakasimama kwa miguu yao, jeshi kubwa mno” (Ezekieli 37:7-10).

Mungu anafafanua maono haya ya Ezekieli. Anasema mifupa hii ilidhihirisha nchi ya Israeli ambapo walikuwa wanasema “tumaini letu limetoweka, tumekatiliwa mbali” (Ezekieli 37:11). Jibu la Mungu kwa Israeli lilikuwa kama lile ambalo lilikuwa kwa mifupa: “Nitatia Roho yangu ndani yenu nanyi mtaishi” (Ezekieli 37:14). Je, Mungu alikuwa afanye jambo hili kwa njia gani? Je, Mungu alikuwa anaenda kuweka Roho Wake ndani ya Waisraeli kwa kutumia njia gani ili waweze kuishi? Jibu ni kwamba alikuwa anaenda kufanya hii kwa kutumia neno Lake. Kwa ufupi ni kwamba Mungu alimwita Ezekieli ahubiri ujumbe wa Injili kwa wale wote ambao wamekufa kiroho. Kwa kupitia kwa mahubiri ya neno la Mungu, huwapa maisha mapya wale ambao wamekufa kiroho. Mungu alimfanya Ezekieli kutabiria mifupa ambayo ilikuwa imekufa ili iweze kupata uhai tena. Vivyo hivyo Mungu amewatuma watumishi wake ulimwenguni kote kuwahubiria ujumbe wa Injili wote ambao hawajaokoka ili waweze kuokoka. Wakati Neno la Mungu linahubiriwa, huwa analifanya liwape uhai wale wote ambao wamekufa kiroho.

Maono ya mifupa ambayo ilikuwa imekauka yanatuonyesha jinsi Mungu alimwita Ezekieli aje na kuhubiria watu wa Israeli ambao hawangemsikiza. Pia maono haya yanatuonyesha jinsi Mungu alivyoumba kila kitu kwa nguvu za neno Lake. Pia tunakumbushwa kile ambacho kilitendeka wakati Neno la Mungu Alikuja hapa ulimwenguni, yaani Kristo Yesu. Biblia inasema, “Huyu Neno alikuwepo ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, haukumtambua” (Yohana 1:10). Ni kupitia kwa Neno hilo yaani Kristo Yesu, Mungu alianza kujitengenezea watu wapya hapa ulimwenguni. Mungu alimwambia Ezekieli azungumze na mifupa ambayo ilikuwa imekauka. Mifupa hiyo ilipata pumzi. Roho ambaye aliipatia pumzi alitumia neno la Mungu na pumzi hiyo ilikuwa uhai. Je, unaona uhusiano kati ya uhai, pumzi, Roho, mazungumzo na neno la Mungu? Hili ni kumbusho kubwa sana kuhusu huduma wa Bwana Yesu Kristo. Kwa mfano kuna wakati ambapo Yesu Kristo alileteawa “mtu mmoja kiziwi, ambaye pia alikuwa na kigugumizi, wakamwomba aweke mkono wake juu ya huyo mtu na amponye. Baadaye Yesu akampeleka yule kiziwi kando mbali na watu, Yesu akatia vidole vyake masikioni mwa yule mtu. Kisha akatema mate na kuugusa ulimi wa yule mtu. Ndipo Yesu akatazama mbinguni, akavuta hewa kwa nguvu akamwambia, “Efatha!' yaani, 'Funguka!” Mara masikio yake yakafunguka na ulimi wake ukaachiliwa akaaza kuongea sawasawa” (Marko 7:32-35). Bwana Yesu Kristo alizungumza na kiziwi na masikio yake yakafunguliwa. Bwana Yesu anawaita watu wake waje kwake kwa njia ile ile Ezekieli alitabiri: “Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama” (Ezekieli 36:26).

Huu ndiyo utukufu wa kweli ambao tumepokea sisi ambao tumeokoka. Nilimwambia mtu mmoja ambaye ni mfuasi wa dhehebu la Mashahidi wa Yehova kwamba, mkristo wa kweli anajitambua kwamba yeye ni mwenyewe dhambi na kwamba hawezi akajiokoa kwa nguvu au kwa kazi zake za dini. Yeye anajitambua kwamba anamhitaji Mungu pekee ampe maisha mapya. Tunamhitaji Mungu pekee ili aweze kuuondoa moyo mgumu wa dhambi na atupatie moyo mpya ambao utampenda Yeye na neno Lake. Huu ndio moyo ambao tunahitaji na ni moyo ambao Kristo anaweza kutupa pekee Yake. Kristo anawafanya watu kuwa wapya. Watu ambao wanapokea uhai wa Mungu ndani mwao wanaposikia neno la Mungu na kwa neema Yake kuwawezesha kutii neno hilo. Neno la Mungu ndilo huleta uhai wa kiroho. Biblia inasema, "Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.....Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu" (Yohana 1:1,3-4). Ni kupitia kwa Kristo Yesu tumepata kufikiwa na neno la Mungu. Bwana Yesu Kristo alituonyesha jambo hili kupitia kwa huduma wake hapa ulimwenguni. Kuna wakati wanafunzi wake walimwambia kwamba kuna watu ambao walikuwa wanamtafuta ili afanye miujiza. Yesu Kristo alijibu, "Twendeni mahali pengine kwenye vijiji vya jirani, ili niweze kuhubiri huko nako, kwa sababu hicho ndicho nilichokuja kukifanya" (Marko 1:38). Unaposoma kitabu cha Marko, utaona kwamba Kristo Yesu alifahamu kabisa kwamba alikuwa amekuja hapa ulimwenguni kufa kwa ajili ya dhambi zetu (Marko 10:45). Lakini ili jambo hili lifahamike kwa watu, alihitaji kwanza ahubiri neno la Mungu.

Sisemi kwamba dini ya ukristo ni dini ambayo inahusu tu maneno. Kile ninamaanisha ni kwamba neno la Mungu ni la muhimu sana katika dini ya ukristo. Unaposoma Biblia unaona kwamba Mungu ni Mungu ambaye anafanya kazi. Lakini pia utaona kwamba popote anapofanya kazi, Yeye huwa anazungumza. Yeye huwa anazungumzia kile amefanya ili tuweze kukifahamu vyema. Mungu huwa haachi matendo yake pekee yazungumze kumhusu Yeye, bali Yeye huzungumza katika neno Lake ili aweze kutufafanulia kazi Yake kuu ya wokovu. Kwa sababu Mungu ni Mungu ambaye anazungumza, pia sisi ametufanya tufanane Naye kwa hili. Unapotazama wanadamu, je huwa tunajuana aje? Je, huwa tunajuaana kwa kuangaliana tu? Mume na mke huwa wanajuana kwa kuzungumza na kujuana zaidi kwa kuja pamoja. Maneno ni ya muhimu sana katika uhusiano au ushirika wowote.

Kuna hali ambazo mazungumzo hayawezekani kabisa. Kwa mfano huwezi kuzungumza na mbwa wako hata kama yeye anakusikia, hawezi akazungumza nawe. Kwa sababu tumejitenga na Mungu kwa sababu ya dhambi zetu, Mungu ni lazima atuzungumzie ikiwa kweli tutamjua Yeye. Mungu hawezi kujulikana ikiwa hatazungumza. Pia hatuwezi kumjua bila Yeye kujifunua kwetu kupitia kwa neno Lake. Bila Mungu kujidhihirishe wanadamu hawawezi kumjua, na hii ndiyo sababu aliandika Biblia. Kwa sababu tumetenda dhambi, hatuna uwezo wa kumjua Mungu hadi azungumze. Mungu asipozungumza, tutaangamia milele jahanum.

Tunaona jambo hili wazi kabisa katika Agano Jipya. Kwa mfano katika Warumi 10:17 tunasoma, "Basi, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo." Neno la Kristo ndio ujumbe mkuu wa injili. Katika ujumbe huu, Mungu amejitambulisha kwetu sisi ambao tumetenda dhambi na kujitenga Naye. Pia katika ujumbe huu tunafahamu kwamba, kwa upendo wake mkuu, wakati Yesu Kristo alikuja, ni Mungu mwenyewe alikuja hapa ulimwenguni. Pia katika ujumbe huu tunafahamu kwamba Kristo Yesu aliishi maisha makamilifu na alikufa msalabani kwa niaba ya wale wote ambao watamwamini. Yeye pia alifufuliwa kuwa ushahidi kwamba Mungu alikubali dhabihu Yake kwa ajili ya wenye dhambi na kwamba sasa anatuita tutubu dhambi zetu na tumwamini Yeye pekee kama jinsi Abrahamu alivyoamini neno la Mungu wakati lilimjia alipokuwa katika nchi yake (Mwanzo 12).

Paulo aliandika katika Warumi 10:9 kwamba, "kama ukikiri kwa kinywa chako kwamba 'Yesu ni Bwana' na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka." Kuamini na kutegemea ukweli kwamba Mungu alimfufua Kristo kutoka kwa wafu ndio njia ya wokovu na kuletwa katika jamii ya Mungu. Kwa mara nyingine tena tunaona kwamba Mungu amewaumba watu wake wapya kwa nguvu za neno Lake. Neno hili ni Kristo Yesu mwenyewe. Biblia inasema, "zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbali mbali, lakini katika siku hizi za mwisho anasema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye ameweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu" (Waebrania 1:1-2).

Ikiwa tunataka kuishi tukitumainia mji mkuu ambao ni mbinguni, lazima tulizingatie neno la Mungu kwa sababu hilo ndilo neno ambalo Roho Mtakatifu hutumia kuwafanya watu kuwa wapya. Makanisa mengi yanajaribu kuwafanya watu wapya kwa kutumia njia zingine kando na neno la Mungu. Tunaweza kuwaleta watu pamoja kwa wingi wa ukabila, kwa ajili ya kazi fulani, au katika makundi fulani fulani. Pia tunaweza kuwaleta watu pamoja kwa sababu ya jinsi wanavyofanya mambo fulani.
Tunaweza kufanya mambo mengi sana kama njia ya kuwaleta watu katika makanisa, lakini ukweli ni kwamba watu wa Mungu yaani kanisa la Mungu linaweza kuwepo kutokana na neno la Mungu. Martin Luther alisema kwamba katika huduma wake, "yeye alifundisha, kuhubiri na kuandika neno la Mungu" na ikiwa hakufanya hivi, basi yeye aliona kwamba hakuwa amefanya lolote. Kulingana na yeye katika kila jambo, neno la Mungu lilifanya yote. Neno la Mungu huwa ndilo linaleta uzima wa milele na kuwahifadhi watu wa Mungu katika uzima huo.

Kazi ya neno la Mungu katika utakaso

Ni lazima tuanganzie lengo ambalo neno la Mungu hufanya katika kazi ya utakaso. Ni lazima neno la Mungu liwe msingi wa maisha yetu binafsi na yale ya kanisa kwa sababu Roho Mtakatifu huwa anatumia neno hili kutupatia imani. Pia Roho Mtakatifu anatumia neno hili kutufanya tukue kiroho. Hili ni jambo la kweli unaposoma Biblia. Wakati Yesu alijaribiwa na Shetani jangwani katika Mathayo 4:4, alinukuu maandiko katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati: "mwanadamu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Bwana" (Kumbukumbu la Torati 8:3). Pia tunasoma katika Zaburi 119:105 kwamba "Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga katika njia yangu."

Tunaposoma kuhusu historia ya Israeli na Yuda katika Agano la Kale, tunapata jambo hili mara kwa mara. Katika utawala wa mfalme Yoseia katika siku za kuanguka kwa Yuda (2 Mambo ya Nyakati 34), neno la Mungu lililetwa na likasomwa mbele yake mfalme. Yoseia alirarua mavazi yake kama njia ya toba na akalisoma neno hilo mbele za watu wote. Kulikuwa na kutubu katika nchi hiyo wakati neno la Mungu lilipohubiriwa kila mahali. Mungu huwa analitumia neno lake kuwatakasa watu wake na kuwafanya wawe kama Yeye mwenyewe.

Hivi ndivyo Bwana Yesu Kristo alivyofundisha. Katika Yohana 17:17 aliomba, "Uwatakase kwa ile kweli, Neno Lako ndilo kweli." Tunasoma katika Waefeso kwamba, "Kristo alivyolipenda Kanisa akajitoa kwa ajili yake kusudi alifanye takatifu, akilitakasa kwa kuliosha kwa maji katika Neno lake" (Waefeso 5:25-26).

Tunahitaji neno la Mungu ikiwa tutaokoka. Pia tunalihitaji ili tuendelea kukua katika utakatifu. Neno Lake huwa halitupatii tu uzima, bali pia huwa linatuongoza na kutubadilisha katika mfano wa Mungu mwenyewe ambaye huwa anazungumza nasi katika neno hilo.

Kanisa la Kikatoliki lilikuwa na msemo ambao ulisema kwamba, “mkristo habadiliki.” Ukweli ni kwamba kila wakati kanisa na mkristo huwa wanatakaswa kulingana na neno la Mungu. Kanisa lenye afya huwa linasikia neno la Mungu na huwa linaendelea kusikia neno hilo kila wakati. Kanisa kama hili huwa limejumlisha wakristo ambao wanasikia na kusoma neno la Mungu kila wakati. Neno hili huwa linawatakasa kila wakati.

Ikiwa mkristo au kanisa fulani linataka kuongozwa na kutakaswa na Mungu, lazima wasome na watii neno la Mungu wakati wowote. Mungu huwa anatufanya tuwe kama Yeye kupitia kwa neno Lake.

Kazi ya Mhubiri wa neno la Mungu

Je, kazi ya mhubiri wa neno la Mungu ni nini? Ikiwa unatafuta kanisa zuri, hili ni jambo la maana sana kuzingatia. Haijalishi una marafiki wangapi katika kanisa ambalo uko. Haijalishi muziki katika kanisa hilo ni mzuri kiasi gani. Mambo haya yanaweza kubadilika. Kila mshirika anafaa kujitolea kusikia mahubiri ambayo yanatoka kwa mhubiri ambaye anahubiri ukweli wa Biblia. Hili ndilo jambo kuu ambalo kila mshirika anafaa kulifanya.

Jarida moja liliandika kwamba, “badala ya mhubiri kuhubiri injili kwa walimwengu, yeye hutafuta kujua watu wanawaza nini kumhusu na mahubiri yake. Yeye hutafuta kujua kile ambacho watu wanataka kusikia. Anapokipata, yeye hujaribu sana kuhubiri hicho. Yeye hutaka kuhubiri kile ambacho kinamfanya ajulikane na wengi.”

Mambo hayafai kuwa hivi. Wahubiri hawajaitwa kuhubiri kile ambacho wengi wanataka kusikia. Ikiwa mhubiri atafanya hivi, hatakuwa amewasaidia wengi. Hatujaitwa kuhubiri historia au mawazo ya watu fulani au mawazo yetu. Tumeitwa kuhubiri neno la Mungu kwa kanisa la Mungu na kwa wale wote ambao hawajaokoka. Ni kutokana na mahubiri yake, Mungu huwaletea wafu wa kiroho uzima na kuwahimiza wote ambao ni wake. Kila mtu ambaye anasoma kitabu hiki, hata mimi ambaye nimekiandika, sote tumezaliwa tukiwa wenye dhambi mbele za Mungu. Jambo la kuhuzunisha ni kwamba, tunajaribu katika nguvu na uwezo wetu kutafuta njia zingine ambazo dhambi zetu zinaweza kuondolewa. Kila mmoja wetu anataka kutafuta njia ambayo itamwezesha kuepuka hukumu ya Mungu. Kwa sababu nguvu zetu na uwezo wetu haziwezi kutusaidia kamwe mbele za Mungu, kila mmoja wetu anafaa kuwa na kiu ya neno la Mungu ili tusisikie tu yale ambayo tunataka kusikia, bali tusikie kile Mungu anasema kwetu. Ni vyema sana kusikia neno la Mungu kwa sababu Roho Mtakatifu huwa anatufanya kuwa watu wapya kupitia kwa neno la Mungu.

Kwa sababu ya hii, Paulo hakumwambia Timotheo kwamba tengeneza kamati ichunguze haya. Bali Paulo alimwambia, “Uhubiri Neno” (2 Timotheo 4:2). Hili ni jambo kubwa sana. Mitume katika kanisa la Yerusalemu waliamua kwamba kanisa liwachague watu wengine ili wajishughulishe na kugawa chakula na mambo mengine na wao watumie muda wao kwa kuomba na kulihudumia lile neno (Matendo ya Mitume 6:4). Je, kwa nini waliamua hivi? Waliamua hivi kwa sababu neno la Mungu ndilo neno la uzima (Wafilipi 2:16). Hii ndiyo kazi kuu ya kila mhubiri; kuhubiri neno la uzima ambalo ndilo huletea nafsi maisha.

Leo kuna wakristo wengi ambao wanashitumu mahubiri ya ufafanuzi wa Biblia. Wao wanasema kwamba leo tunahitaji mahubiri ambayo yanawasisimua watu na kuwafurahisha mioyo sana. Wanasema kwamba tunafaa kuhubiriwa neno la Mungu kwa njia ambayo inazungumza kuhusu maisha ya watu ya kila siku. Hawa wanasema kwamba mahubiri ya kufafanua Biblia ni mahubiri ya zamani. Lakini hata kama wanasema hivyo, ukweli ni kwamba mahubiri ya aina hii ni ya maana sana na yanahitajika sana katika makanisa yetu leo. Leo watu wengi wamechanganyikiwa sana kuhusu mahubiri ya kweli na yale ambayo si ya kweli. Katika kizazi hiki ambacho watu wengi wamechanganyikiwa na kuwachanganya wengine, ni bora sana ikiwa tutawasikiliza wale ambao wanahubiri neno la Mungu. Ni lazima tuwe tayari kuongozwa, kutosheka na kutii neno la Mungu. Hili ni jambo la maana katika maisha yetu.

Ukweli ni kwamba kuna wakati ambapo tutaona mambo yote kwa macho yetu na hatutahitaji kuhubiriwa tena. Wakristo wengi wanatarajia na kutazamia siku hii ambapo watamwona Kristo Yesu kwa macho. Hili ndilo kuu la mafundisho ya Biblia: “nao watamwona uso wake” (Ufunuo 22:4). Wakati huu tutakuwa na Mwokozi mwenyewe na tutamwona kwa macho yetu ya kiasili.

Lakini kwa sasa ni lazima tufahamu kwamba hali hiyo haijafika. Kwa sasa bado tunaishi katika uwepo wa dhambi ya wazazi wetu wa kwanza na ile dhambi yetu mwenyewe. Siku hiyo ya mwisho, tutamwona Kristo kwa macho yetu. Lakini kwa sasa wakati huo haujafika. Hata hivyo hatufai kukata tamaa hata kidogo. Kwa sasa tunaishi kwa imani na ni Mungu mwenyewe ambaye anatupatia imani hii kupitia kwa neno lake. Kwa hivyo kama Nuhu na Abrahamu na mitume wote, tunategemea Mungu na neno Lake pekee.

Je, jambo hili linamaanisha nini kuhusu maisha ya makanisa yetu leo? Hii inamaanisha kwamba neno la Mungu lazima liwe msingi wa kila jambo. Mahubiri ya ufafanuzi wa Biblia ndiyo msingi wa kanisa ambalo linakua. Ikiwa makanisa yanataka kukukua katika imani, lazima yazingatie mahubiri ambayo yanafafanua Biblia. Usisikilize yale mabaya ambayo wengi watasema kuhusu mahubiri haya. Ukweli ni kwamba ukiwa wewe ni mchungaji, zingatia kuhubiri mahubiri ya aina hii na utaona kazi kuu ya Mungu katika maisha ya watu ambao unawahubiria. Kuzingatia kwa makini neno la Mungu ndiyo njia ya kupata wokovu na kuleta mabadiliko katika maisha ya wengi ambao wanaokoka. Biblia inasema, “Kwa kuwa katika hekima ya Mungu, ulimwengu kwa hekima yake haukumjua Yeye, ilimpendeza Mungu kuwaokoa wale waaminio kwa upuzi wa lile neno lililohubiriwa” (1 Wakorintho 1:21). Leo tunahitaji tu kusikia neno la Mungu pekee. Leo tunaona watu wengi ambao wanajiita wakristo na makanisa mengi ambayo yanapuuza neno la Mungu.

Ninajua kwamba kuna wengi ambao wanafanya kazi mahali ambapo wao huwa wanapokea simu nyingi sana. Miongoni mwa simu hizo utapata kwamba kuna zile simu ambazo ni za dharura na zingine si za dharura. Wakati unapokea simu kama hizi unashughulika kwa haraka sana. Biblia ni neno la Mungu na wakati tunalisoma, huwa Mungu anazungumza nasi. Lakini hata kama Mungu huwa anazungumza nasi, huwa hatutilii maanani neno hilo kila wakati na huwa hatuchukui muda kutafakari juu ya neno hilo. Mara kwa mara mawazo yetu huwa yamejawa na mambo mengi ya ulimwengu kama kuwa matajiri na jinsi ya kujifurahisha katika ulimwengu huu. Kufanya mambo haya si dhambi lakini ni lazima tufahamu vyema kabisa inamaanisha nini wakati tunasema kwamba Biblia ni neno la Mungu. Kile huwa tunamaanisha ni kwamba, ni lazima tulisikilize na tulitii neno la Mungu.

Siku hizi za leo utaona wengi ambao wanakubali kwamba Biblia ni neno la Mungu lakini huwa hawatii neno hili. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba kuna wengi ambao wanajiita wakristo lakini unapoona maisha yao, wanaishi tu kama wale ambao hawajaokoka. Je, ni uzuri gani ambao utajiletea ikiwa unasema kwamba Biblia ni neno la Mungu lakini uwe hulisomi na huombi kuhusu neno hilo na hulitii?

Mahubiri ni lazima yawe yanaeleweka jinsi Mungu ameyakusudia. Ni lazima wale wote ambao wanasikiliza mahubiri wafahamu kwamba wanasikiliza neno la Mungu. Washirika wa kanisa wanafaa kuwahimiza wachungaji wao wahubiri mahubiri ambayo yanafafanua Biblia. Wanafaa kuwaombea wachungaji wao ili waweze kuhubiri mahubiri ambayo yanafafanua Biblia. Wakati wanapata wahubiri ambao wanahubiri wakifafanua Biblia, wanafaa kumshukuru Mungu sana. Ni jambo jema sana kuhubiri ukweli na kuuhubiri kwa njia ambayo watu wanapata kujua kwamba ukweli huu umetoka kwa neno la Mungu. Wakristo wote wanahitaji kusikia neno la Mungu likihubiriwa na si jambo lingine lolote.

Je, kanisa zuri ni kanisa la aina gani? Kanisa zuri ni lile ambalo linazingatia mahubiri ya kweli ambayo ni neno la Mungu. Katika kanisa hili neno la Mungu ndilo linalo waongoza watu na watu katika kanisa hili wanalitii neno hilo. Ni kanisa ambalo linazingatia neno la Mungu zaidi kuliko jambo lingine lolote kwa sababu, “mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa neno litokalo katika kinywa cha Mungu” (Mathayo 4:4).

Ishara ya pili

Mpango wa Mungu katika wokovu

Katika sura hii tutatazama kuhusu Mungu na mpango wake katika wokovu. Tutajifunza ni nini Biblia inafundisha kuhusu Mungu na jinsi alivyo kama anavyofunuliwa katika Biblia.

Je, unawaza nini kumhusu Mungu? Je, wewe unawazaje kuhusu Mungu ambaye alimtuma Kristo aje afe kwa ajili ya dhambi zako na kuhusu Mungu huyo huyo ambaye anawahukumu wenye dhambi? Je, unamfahamu Mungu kwa njia gani na jinsi alivyo? Ninajua kwamba mazungumzo haya kwa wengi hayana umuhimu wowote. Kuna wengi wataniuliza, je kwa nini unataka kumaliza muda wako bure ukitaka kujua watu wanawaza nini kuhusu Mungu?

Kuna wakristo wengi ambao wanawaza kwamba hawahitaji kujua mafundisho muhimu ambayo yanapatikana katika Biblia. Wao wanadai kupenda Biblia lakini hawafanyi yale ambayo Biblia inawaagiza wafanye. Kuna mambo mengi ambayo watu wanaamini kuhusu Mungu na mengi ni ya kweli lakini mambo hayo wengi hawaoni umuhimu yake kabisa. Mambo haya huwa wengi wameyaacha kwa sababu wanasema kwamba wao wanataka dini ambayo haina masharti mengi na dini ambayo inawaruhusu kufanya jinsi wanavyotaka wenyewe.

Je, kile unaamini kimebadilisha maisha yako kweli? Je, siku yako ya mwisho ya kuketi kanisa, maneno ambayo uliyaimba yalimaanisha nini kwa moyo wako? Je, ulijichunguza kulingana na yale ambayo uliyaomba? Je, maneno ambayo uliyasikia yakihubiriwa yalibadilisha maisha yako kwa njia gani? Je, kwako unajali kama yale ambayo ulisema au uliimba au ulisikia yakihubiriwa yalikuwa ya kweli? Je kwako kuna maana yoyote kuhusu mambo haya? Je, wewe ni kama wale ambao wanasema, 'kuna umuhimu gani katika kuamini yale ambayo ninasikia ikiwa ninajitolea kuwa kanisani kila wiki na kutoa pesa nyingi wakati wa sadaka? Bora tu nimefanya mambo haya, nimetosheka.” Swali langu kwako ni, je, kuna umuhimu gani katika yale ambayo unaamini?

Unapotazama na kusoma Biblia, utapata kwamba katika Biblia yote, Mungu anafunua mpango mmoja ambao ni wokovu wa watu wake kutoka katika dhambi zao kupitia kwa Yesu Kristo. Wakati Mungu aliwaongoza watumishi wake kuandika Biblia, alipanga kwamba wakati walikuwa wanaandika, walikuwa wanaandika yale ambayo alikuwa anafunua wazi kabisa kwa watu wote wakati ulipowadia. Si hali kwamba wale ambao Mungu alitumia kuandika Biblia walikuwa wanaandika maneno yao ambayo hayakuwa na mpangalio wowote. Kile tunafaa kujua ni kwamba wakati walikuwa wanaandika ni Mungu alikuwa anawaongoza kuandika mpango wake ambao ni wokovu wa watu wake. Kila kitabu cha Biblia kinazungumza kuhusu mpango huu na si kitu kingine. Kwa hivyo, wakati tunasoma Biblia ni lazima tujue kwamba tunasoma neno la Mungu. Wakati tunasikia neno la Mungu na kuliamini, lazima tujue kwamba neno hilo halibadiliki kamwe. Kuamini kwa kweli ni kuamini neno la Mungu.

Katika sura tuliomaliza, tulisoma kuhusu umuhimu wa mahubiri ambayo yanafafanua maandiko. Tunafaa kujishughulisha sana na kile ambacho tunafundishwa kwa sababu hicho ndicho muhimu. Tunafaa kutazamia wachungaji ambao wanatuhubiria neno la Mungu na si kitu kingine. Pia tunafaa kuwa waangalifu sana kuhusu mahubiri ya wachungaji ili tuweze kujua kama kweli yale wanafundisha yanatoka katika neno la Mungu au la. Hatuhitaji tu, mtu ambaye anajua kuongea tu, bali tunahitaji yule ambaye katika mahubiri yake anafuata na kufundisha neno la Mungu jinsi linavyofunzwa. Hili ni jambo la muhimu sana ikizingatiwa sana mafundisho kuhusu Mungu na jinsi alivyo. Mojawapo ya ishara kuu za kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho, ni kanisa ambalo linafahamu vyema Mungu na jinsi alivyo na njia zake kwetu.

Kwa hivyo, katika sura hii, tutaangalia hadithi kuu katika Biblia. Ikiwa tutapata mafundisho haya ya hadithi hii, basi tutamfahamu vyema Mungu ambaye alitupatia neno Lake. Kwa ufupi hadithi ya Biblia ni kuhusu Mungu ambaye: Mwumbaji, Mtakatifu, Mwaminifu, Mwenye upendo na mwenye kutawala kila kitu.

Kuwa mwangalifu wakati tunajifunza mambo haya yote jinsi Biblia inavyoyafundisha na utaona tofauti kubwa iliyoko ikiwa utaamini mambo haya.

Mungu wa Biblia ni Mungu Mwumbaji

Tukianzia mahali ambapo Biblia huanzia, tunaona kwamba Mungu wa Biblia ni Mungu Mwumbaji. Yeye ndiye aliyewaumba watu wote ulimwenguni na aliwaumba kwa njia ya ajabu sana. Kuna watu ambao wanaona Biblia ikiwa kitabu chenye mafundisho tofauti tofauti ambayo hayana lengo kwa sababu wao wenyewe huwa hawaifahamu. Biblia ni kitabu ambacho kimejawa na historia. Katika Biblia tunasoma yale ambayo yanaendelea na Mungu na viumbe vyake ambavyo Yeye mwenyewe aliumba. Ninajua kwamba kuna watu ambao huwa hawapendi historia, lakini hata hivyo ni lazima tufahamu historia vyema kwa sababu Biblia ni kitabu ambacho kimejawa na historia. Unapoanza kusoma Biblia utaona kwamba inaanza bila kuwepo kwa chochote. Lakini unavyoendelea kuisoma, unaona kwamba vitu vinaanza kuwepo kwa nguvu za neno la Mungu. Baada ya kuumba vitu vingine, aliumba viumbe fulani na akivipatia uhai na vikawa hai. Kilele cha uumbaji wake ni wakati alipomwumba mwanadamu. Alimwumba mume na mke katika umbo lake mwenyewe.

Katika kitabu hicho hicho cha Mwanzo, tunasoma kuhusu hadithi ya Bustani ya Edeni na kuanguka kwa mwanadamu katika dhambi.

Kuanzia hapo tunaona kwamba mambo yalibadilika kabisa. Dhambi ilienea katika ulimwengu huu. Tunaona kizazi cha Kaini ambacho kilikuwa kiovu kabisa. Tunaona Mungu akihukumu ulimwengu siku za Nuhu kupitia kwa gharika. Hata baada ya Nuhu, watu waliendelea kutenda dhambi na hii inaonekana wakati wa kujenga kwa mnara wa Babeli.

Baada ya haya yote, Mungu alimwita Abrahamu kutoka katika nchi yake. Kuanzia kwa Abrahamu, Mungu alifunua kupanga mpango wa kuwaokoa na kuwafanya wawe viumbe vipya wale ambao walikuwa wameteuliwa Naye. Baada ya kuishi maisha ya starehe kwa miaka michache, Waisraeli walifanywa watumwa katika nchi ya Misri. Baada ya miaka 430 katika utumwa, Mungu aliwakomboa kutoka katika utumwa huo na baadaye aliwapatia sheria yake na kuwaingiza katika nchi ya Ahadi (Kanani).

Baada ya muda mrefu, kulikuwa na wakati wa Waamuzi halafu baadaye ufalme ulianzishwa katika nchi ya Isaraeli, Sauli akiwa mfalme na baadaye Daudi. Baada ya Daudi kufa, mtoto wake Solomoni alirithi kiti cha ufalme na akawa mfalme wa nchi ya Israeli. Baada ya Solomoni kufa, mtoto wake Rehoboamu alikuwa mfalme. Chini ya uongozi wa Rehoboamu, nchi ya Israeli iligawanyika mara mbili ikawa mataifa mawili. Taifa la kaskazini na taifa la kusini. Kuabudu kwa sanamu kulienea katika mataifa haya yote. Kwa sababu ya dhambi hii ya kuabudu sanamu, Mungu alituma watu nchi ya Ashuru ambao waliangamiza taifa la kaskazini katika mwaka wa 722 K.K. Baada ya zaidi ya karne moja, aliwaadhibu watu wa nchi ya kusini (Yuda) kwa kuwaleta Wababeli ambao waliwapeleka katika utumwa. Kwa miaka 70, Waisraeli walikuwa katika utumwa na baadaye walirudi na kuujenga mji wa Yerusalemu na pia wakalijenga hekalu. Watu wa taifa la Yuda wakiwa wamerudi kutoka kwa utumwa lakini wakiwa hawana chochote na wakiwa watu wakuhurumiwa sana na ambao hawakuwa na uwezo wowote. Historia ya Agano la Kale inaishia hapa.

Kwa hivyo Agano la Kale litauonyesha kuhusu Mungu ni nani na kile ambacho anafurahia.

Katika Agano la Kale, Mungu anatuonyesha kikamilifu inamaanisha nini kuishi pamoja Naye na inamaanisha nini kujua Mungu na kuwa na ushirika Naye. Katika historia hii yote, tunaona inamaanisha nini kuwa watu wa Mungu na ni nini Mungu anapendezwa nacho. Tunafaa kufahamu vyema ukweli ambao Biblia inasema kuhusu Mungu na kuhusu sisi wenyewe. Mafundisho ya kweli katika makanisa yetu yanafaa kuzingatia kile ambacho Biblia inafundisha hata kama wengi hawakipendi. Ikiwa tunataka kujifundisha mafundisho ya kweli ya Biblia, ni lazima tujitahidi kufahamu hata yale mafundisho ambayo yako katika Biblia lakini yanaonekana kuwa magumu kufahamu kwa haraka. Mafundisho kama haya ndiyo msingi wa kufahamu Mungu wetu. Mahubiri ambayo yanaonyesha wazi Mungu na mpango wake katika wokovu, ni ishara ya kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho.

Jambo linajitokeza wazi kabisa wakati tunasoma katika Biblia kuhusu Mungu Mwumbaji, ni kwamba, Yeye aliumba na akachagua taifa moja kuwa watu wake maalumu. Kuna wengi ambao wanaweza kusema kwamba, wakati Mungu alichagua, Yeye hakufanya hivyo kwa njia nzuri. Mtu akisema hivi, hatakuwa mwaminifu kwake mwenyewe kwa sababu chochote Mungu anakifanya, anakifanya akiwa Mungu mwenyewe upendo na Mwaminifu. Hakuna mwanadamu yeyote ambaye anafaa kusema kwamba Mungu hafanyi mambo fulani vizuri au kwamba Yeye si Mwaminifu.

Historia katika Biblia inatuonyesha kwamba Mungu wa Biblia ni Mungu Mwumbaji na pia Yeye ni Mungu na pia Mungu ambaye anachagua vile anayopenda. Hata kama hatuelewi kila kitu kuhusu jambo hili la kuchagua, ukweli ni kwamba hivi ndivyo Biblia inavyofundisha. Furaha ya wokovu hutokana na kufahamu vyema kwamba wokovu wetu umetoka kwa Mungu na si uamuzi wetu. Kufahamu jambo hili vyema, ni kufahamu Mungu na kujifahamu sisi wenyewe. Ni lazima tujue na kufahamu kwamba Mungu ndiye Mwanzilishi mkuu, Mpeanaji mkuu, Mwumbaji wa ulimwengu, Mwumbaji wa watu wake, na Mwanzilishi wa imani yetu. Hivi ndivyo mambo yalivyo.

Mungu wa Biblia, ni Mungu Mtakatifu

Biblia inatueleza kwamba Mungu ni Mtakatifu. Ikiwa tunataka kufahamu hadithi ya Biblia, ni lazima tufahamu kwamba Mungu ambaye ametuumba, pia ni Mungu ambaye ni Mtakatifu na anapenda utakatifu. Kuna wengi ambao huwaza kwamba baada ya Mungu kuumba mwanadamu, alimwacha ili ajiendeleze katika maisha yake bila Yeye kuyaongoza. Wanawaza kwamba Mungu hashughuliki kamwe na viumbe vyake na kwamba hana haja navyo kamwe. Tunaposoma Biblia, tunasoma kumhusu Mungu ambaye ni Mtakatifu na anapenda Utakatifu.

Wakati tunashiriki meza ya Bwana, huwa tunayasikia maneno haya ya Bwana wetu Yesu Kristo: “Kikombe hiki ni agano jipya katika damu Yangu, imwagikayo kwa ajili yenu” (Luka 22:20). Neno hili agano linamaanisha kwamba kuna uhusiano na ushirika kati ya watu wawili. Huu ni uhusiano na ushirika ambao unapatikana hata katika Agano la Kale. Kujitolea kwako katika Agano hili ndilo jambo la muhimu kabisa katika uhusiano na ushirika huu. Kwa mfano katika ndoa, mtu huwa anajitolea kabisa mbele za Mungu kumpenda na kumjali mwenzake ipasavyo. Kwa hivyo tunaposoma katika Biblia kuhusu jambo la Agano, tunasoma kuhusu Mungu ambaye anapenda utakatifu na ambaye amejitolea kabisa kuwa na uhusiano na ushirika nasi.

Kwa sababu Mungu ni Mungu ambaye anapenda utakatifu, ni lazima mambo fulani yafanyike ikiwa tunataka kuwa katika uhusiano na ushirika Naye. Katika Biblia, tunasoma kuhusu Mungu ambaye ni Mtakatifu na anatuita sisi wanadamu ambao tumezaliwa tukiwa wenye dhambi kuwa katika uhusiano na ushirika Naye. Kwa sababu sisi ni wenye dhambi, ni lazima jambo fulani lifanyike ikiwa kweli tutakuwa katika uhusiano na ushirika mwema na Mungu. Ni lazima dhambi zetu zifidiwe. Kwa sababu kila mwanadamu amezaliwa akiwa mwenye dhambi na ako mbali sana na Mungu, tunahitaji kupatanishwa na Mungu ikiwa kweli tutakuwa na uhusiano na ushirika mwema Naye. Kulingana na Biblia, kila mtu ni mwenye dhambi na kwa hivyo anahitaji kupatanishwa na Mungu. Swali ni, je, hili litafanyika kwa njia gani?

Tunahitaji kupatanishwa na Mungu kwa sababu dhambi imetutenganisha na Mungu (Mithali 15:29; Isaya 59:2; Habakuki 1:13; Wakolosai 1:21; Waebrania 10:27). Kulingana na Biblia kila mtu ni mwenye dhambi (1 Wafalme 8:46; Zaburi 14:3; Mithali 20:9; Mhubiri 7:20; Marko 10:18; Warumi 3:23) na hakuna hata mmoja ambaye anaweza kujiokoa kutoka katika dhambi zake (Warumi 3:20; Wagalatia 2:16). Kwa sababu tumetenda dhambi na kuvunja sheria takatifu ya Mungu, tunahitaji kupatanishwa na Mungu.

Katika Agano la Kale, watu Israeli walihitajika kutoa kuchinja wanayama kama fidia ya dhambi zao. Wakati tunasoma kuhusu sadaka na dhabihu za Agano la Kale, hatufai kuwaza kwamba jambo hili la kufidia dhambi zetu linatekelezwa kwa nguvu na uwezo wa mwanadamu. Si kwa nguvu zetu ambapo tunapata kusamehewa na Mungu, bali ni kwa nguvu za Mungu mwenyewe. Mungu mwenyewe ametufunulia njia ambayo tunafaa kuitumia ikiwa tutapatanishwa Naye katika uhusiano na ushirika mwema. Mungu

mwenyewe katika neno lake, amezungumza nasi kuhusu jinsi tunafaa kupatanishwa Naye.

Tunaposoma Biblia, tunapata kwamba kutoa dhabihu na sadaka ilikuwa tabia. Kwa mfano tunasoma kwamba, Kaini na Abeli walitoa sadaka. Kondoo wa pasaka alikuwa atolewe kama sadaka (Kutoka 12). Kondoo huyu alikuwa awe bila doa lolote na alikuwa achinjwe. Damu yake ilikuwa ipakwe juu ya milango ya watu ambao Mungu alikuwa aokoe. Maisha ya mtoto wa kwanza wa kiume ambaye aliwakilisha jamii yake nzima yangechukuliwa ikiwa hawangepaka damu hiyo kwa milango yao. Mungu alisema kwamba, "Damu itakuwa ishara kwa ajili yenu ya kuonyesha nyumba ambazo mtakuwemo, Nami nitakapoiona damu, nitapita juu yenu. Hakuna pingo ya uharibifu litakalo wagusa ninyi nitakapoipiga Misri" (Kutoka 12:13). Dhabihu hii ilikuwa imtosheleze Mungu pekee. Katika kitabu cha Walawi tunapata dhabihu zilizotolewa mara kwa mara kama funzo kwa watu kwamba dhambi ni mbaya sana kwa sababu inamchafua mtu; inagharimu maisha ya mtu yote na kwamba ni dhambi ambayo inamtenganisha mwanadamu na Mungu.

Pia unaweza kuona jambo hili katika ujenzi wa hekalu. Mungu Mtakatifu ni lazima ajitenge mbali sana na watu waovu. Dhabihu hizi zilikuwa zikionyesha kwamba tunahitaji kuwa watakatifu na kwa sababu sisi si watakatifu tunahitaji kipatanisho ili tuwe watakatifu na tukubalike mbele za Mungu. Dhabihu hizi zinaturejesha katika uhusiano na Mungu. Dhabihu hizi zilikuwa ziwe sadaka zenye gharama ambazo zilihitajika kutolewa pamoja na kukiri dhambi kulingana na jinsi Mungu amesema.

Dhabihu ambazo zililetwa ziliamuriwa na Mungu. Dhabihu za Biblia hazikuwa ziletwe na wale ambao walijiwazia kuwa wema, bali zililetwa na kufanywa na wale ambao walijua wao wenye dhambi wakuu. Pia dhabihu hizi hazikuletwa na wale ambao hawakujua ni nini walikuwa wakifanya, bali zililetwa na wale ambao walijua kwamba wamefanya dhambi na wanahitaji msamaha wa dhambi zao. Damu ya mnyama ambaye alitolewa kama dhabihu ndiyo ilihitajika ili mwenye hatia aweze kusamehewa. Dhabihu hizi zilionyesha kwamba dhambi ni kitu hatari sana na kwamba kinagharimu uhai. Dhabihu zote zilikuwa za kujitolea na zenye kugharimu sana. Pia zilikuwa zitolewe na mwenye dhambi mwenyewe.

Dhabihu hizi zote zilikuwa zinafundisha kuhusu kifo chake Yesu Kristo kwa ajili ya wenye dhambi. Mungu alikuwa anawatayarisha watu wake kwa Yule ambaye hakuwa na dhambi yoyote, ambaye angekuja na afe kwa ajili ya dhambi za watu wake, yaani Yesu Kristo. Dhabihu hizi zilifundisha kwamba dhambi ni kitu ambacho kinachafua mtu. Hii ndiyo sababu katika hekalu kuliwa na mahali ambapo paliitwa Patakatifu pa Patakatifu, kuonyesha jinsi dhambi inavyomzuia mtu kumfikia Mungu. Dhabihu hizi zilionyesha kwamba kulihitajika utakaso kutoka kwa dhambi. Pia zilionyesha kwamba dhambi ni kitu hatari sana na kwamba kulihitajika kifo ili dhambi ifidiwe. Zilionyesha kwamba wokovu na msamaha wa dhambi ni mambo ya gharama kubwa sana.

Hii ndiyo sababu Siku ya Upanisho ilikuwa siku kubwa sana katika nchi ya Isreali. Siku hii ilihusu kutolewa kwa dhabihu moja ambay**o** ilikuwa ifidie dhambi za watu wa Israeli wote. Ilikuwa kumbusho kwa watu wote kwamba zile dhabihu zote walikuwa wametoa hazikuweza kuondoa kabisa dhambi zao (Walawi 16). Kuhani mkuu ambaye alikuwa mwakilishi wa watu aliingia mahali Patakatifu pa Patakatifu siku moja kwa mwaka na alitoa dhabihu kwa ajili ya watu wa Israeli mbele za Mungu. Kuhani mkuu aliingia humo na damu ya mbuzi ambaye alikuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi (Waebrania 9:7). Kwanza alijitakasa mwenyewe kwa sababu hata yeye mwenyewe alihitaji kuwa ametakasika kabla ya kufanya dhabihu hii. Halafu baada ya yeye kufanya dhabihu kwa ajili ya dhambi zake, yeye alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi za watu wa Israeli. Wakati alileta damu hiyo katika mahali Patakatifu pa Patakatifu, je ni nani aliyeona damu hiyo? Jibu ni kwamba Mungu mwenyewe ndiye aliyeona damu. Sababu ya dhabihu hii ni, kwamba wanadamu waweze kupatanishwa Mungu.

Ni jambo la kuangazia sana kwamba dhabihu hii ilitolewa kila mwaka. Mataifa mengine yalifanya dhabihu kila wakati bila kujali, bora tu wao wametoa dhabihu hizi. Nchi ya Israeli walikuwa wameambiwa kwamba haijalishi wako katika hali gani, wao walihitajika kutoa dhabihu hii kila mwaka. Hii ilifanyika hivyo ili waweze kukumbushwa kwamba wao walikuwa katika dhambi kila wakati na kwamba dhambi hiyo iliwatenga kutoka kwa Mungu. Pia walikuwa wafahamu kwamba hawasamehewi kwa sababu ya dhabihu zao, bali kwamba ni Mungu ambaye anatengeneza njia ya kumfikia kwa kusamehe dhambi za watu wake.

Je, mambo haya yote yanamaanisha nini kwetu? Je, sisi ni watu wa aina gani? Je, sisi ni wenye dhambi kama watu katika Agano la Kale, au je, wao walikuwa wenye dhambi wakuu kwa sababu ya wingi wa dhabihu ambazo walihitaji kutoa? Je, wewe unawaza nini kuhusu jambo hili? Je, kwa kawaida watu ni wabaya ama ni wazuri? Jinsi unavyowaza kuhusu maswali haya itadhihirisha jinsi mawazo yako yalivyo kuhusu jinsi kanisa linafaa kuwa. Ikiwa unawaza kwamba kwa kawaida watu ni wazuri, basi kwako kanisa ni mahali ambapo tunaenda ili tuweze kupata kuhimizwa na kuelezwa jinsi tunafaa kuendelea jinsi tulivyo. Ni kusema kwamba kile tunahitaji kufanya ni kuendelea tukiishi jinsi tulivyo na kwa njia hii tutampendeza Mungu sana.

Lakini ikiwa mawazo yako ni kwamba mwanadamu ana kasoro, na kwamba yeye amekufa kiroho na yeye ana hatia mbele za Mungu na ametengwa mbali sana Naye, basi hii itamaanisha kwako kwamba kuna jambo muhimu ambalo kanisa linafaa kufanya. Hii itamaanisha kwamba makanisa yanafaa kuhubiri injili ya Kristo ya kweli. Hii inamaanisha kwamba makanisa yote yanahitaji kuhubiri kifo cha Yesu Kristo kwamba ndiyo ya pekee kwa wanadamu kupatanishwa na Mungu. Makanisa yanafaa kuwaeleza wengi jinsi wote wanafaa kutafuta msamaha wa dhambi zao na maisha mapya ndani ya Kristo Yesu.

Makanisa yatakuwa tofauti kulingana na jinsi yanavyomfahamu Mungu na jinsi yanavyofahamu wanadamu. Kuwa watu wa Biblia ni kujua kwamba Mungu ni Mtakatifu na pia kwamba kwa asili sisi wanadamu tumekufa katika dhambi na makosa na kwamba tuko chini ya hukumu ya Mungu.

Mungu wa Biblia ni Mungu Mwaminifu

Mungu ni Mungu Mwumbaji, Mungu Mtakatifu na pia Mungu ni Mwaminifu. Katika kitabu cha Kutoka 34:6-7, Mungu alizungumza na Mose na kumwambia maneno ambayo ni ya kushangaza sana ikilinganishwa na mambo ambayo tumesoma hadi sasa. Mungu alisema, "Bwana, Bwana Mungu Mwenye huruma na neema, asiye mwepesi wa hasira, mwingi wa upendo na uaminifu, akidumisha upendo kwa maelfu, pia akisamehe uovu, uasi na dhambi, lakini haachi kuadhibu mwenye hatia, huadhibu watoto na watoto wao kwa ajili ya dhambi ya baba zao hata katika kizazi cha tatu na cha nne." Swali ni, je, ni namna gani Mungu ambaye ni mtakatifu na mwenye kuadhibu wenye dhambi anaweza kuwa mwenye neema ya rehema juu ya wale ambao ni wenye dhambi? Tunaona kwamba ndipo hasira ya Mungu iondolewe, lazima kuwa na kuteseka na kufa kwa mtu mmoja ambaye ni mtakatifu kwa niaba ya wengi wenye dhambi.

Katika nyakati za Kristo Yesu, watu walikuwa wakijiuliza kama kweli Masiya atakuja. Watu hawa wa Israeli walipuuza jambo hili sana. Unaposoma vitabu vya injili katika sura zake za kwanza, utaona kwamba watu wa Israeli walikuwa wakingoja Masiya ambaye alikuwa ameahidiwa na Mungu aje. Mungu alikuwa amezungumza kupitia kwa Musa kwamba angemleta nabii mkuu (Kumbukumbu la Torati 18:15-19). Lakini wakati Nabii huyu alipokuja yaani Kristo Yesu, watu walimkataa kwa sababu hakuja kwa njia ambayo walimtarajia aje nayo. Yaani Yeye alikuja akiwa mtu wa mateso mengi ambaye alikataliwa na watu wengi na ambaye alikuwa afe kwa niaba ya wengi ili waweze kusamehewa dhambi zao. Ndani mwake, unabii kuhusu Masiya Mfalme na ule wa Masiya ambaye anateseka, ulitimia.

Agano zote mbili yaani Agano la Kale na lile Jipya yote yanatufundisha kuhusu Masiya Mfalme na mwenye kuteswa ambaye ndiye tumaini letu lote. Bwana Yesu Kristo anatufunulia wazi mafundisho ya Kutoka 34. Anatuonyesha jinsi Mungu huwa anasamehe dhambi zetu wakati huo huo akiwaadhibu wenye hatia.

Ikiwa mtu anataka kumwelewa Kristo Yesu, lazima aelewe ile kazi ambayo Kristo alikuja kufanya hapa ulimwenguni. Yeye alikuja ili wewe na mimi tuweze kuwa na uhusiano na ushirika mwema na Mungu. Yeye ni Yule ambaye alikuwa ameahidiwa na Mungu na Yule ambaye alikuwa anatarajiwa na wengi. Adamu na Waisraeli walikosa kuwa waaminifu kwa Mungu, lakini Kristo Yesu ambaye hakuwa na dhambi alishinda majaribu yote. Kristo Yesu ndiye Nabii ambaye alikuwa ametabiriwa na Musa na pia Yeye ndiye Mfalme ambaye alikuwa amezungumziwa na Daudi. Yeye ndiye alikuwa Mwana wa Mungu (Danieli 7). Mambo haya yote yalimika katika Kristo Yesu wa Nazareti. Yeye ndiye alikuwa Neno la Mungu ambaye alifanyika mwili. Yeye ndiye alikuwa ametabiriwa kufa kwa niaba yetu wenye dhambi. Yeye ndiye aliyekuwa Mwana-Kondoo wa Mungu ambaye alisulibishwa kwa ajili ya watu wake.

Yesu Kristo ndiye aliyekuwa timizo kamili la ahadi za Mungu. Mungu wetu ambaye ni Mwumbaji na ni Mtakatifu, pia ni Mungu Mwaminifu.

Mungu wa Biblia ni Mungu wa upendo

Mungu Mwaminifu ni Mungu pia wa upendo. Yeye ni Mungu ambaye anawapenda watu wake wote wa agano. Mungu ametuumba katika mfano Wake mwenyewe. Yeye ametuumba tuwe katika agano pamoja Naye. Je, inawezekanaje kuwa kwamba Mungu angesamehe uovu na wakati huo asiwaadhibu wenye hatia? Jibu la swali hili linapatikana katika Kristo Yesu. Yeye ambaye hakuwa na hatia, alichukua hatia yetu na akaadhibiwa kwa niaba yetu. Hili ndilo jambo ambalo Kristo alifundisha katika Luka 24:27, 45-47 kwamba, “Naye akianzia na Mose na manabii wote, akawafafanulia jinsi maandiko yalivyosema kumhusu Yeye....Ndipo akafungua fahamu zao ili waweze kuyaelewa maandiko. Akawaambia, 'haya ndio yaliyoandikwa: Kristo atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu. Toba na msamaha wa dhambi utatangazwa kupitia Jina Lake, kwanzia Yerusalemu.'” Hivi ndivyo ilivyotabiriwa kwamba Kristo angeonyesha upendo wake kwa watu wake kwa njia ya ajabu sana. Isaya alitabiri kwamba, “Hakika alichua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa. Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona. Sisi sote, kama kondoo, tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, Naye Bwana aliweka juu yake maovu yetu sisi sote” (Isaya 53:4-6).

Haya ndiyo yale ambayo Kristo aliyafanya kwa upendo wake. Yeye mwenyewe aliwafundisha wanafunzi wake kwamba, “Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai Wake kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi” (Marko 10:45). Paulo naye alizungumza kumhusu Kristo kwamba, “Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kishikamana nacho, bali alijifanya si kitu, akifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba!” (Wafilipi 2:6-8).

Katika mahubiri ya Petero, Petero anasema, “Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo: Yesu wa nazareti alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza, maajabu na ishara, ambayo Mungu alitenda miongoni mwenu kwa kupitia Yeye, kama ninyi wenyewe mjuavyo. Huyu mtu akiisha kutolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa kwa kujua kwake Mungu tangu zamani, ninyi kwa mikono ya watu wabaya, mlimwua kwa kumgongemea msalabani. Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana Yeye kushikiliwa na nguvu za mauti” (Matendo ya Mitume 2:22-24). Katika Agano Jipya tunapata kwamba Mungu ni Mungu ambaye ni mwaminifu kwa ahadi zake kwa sababu ya Agano lake na upendo mkuu juu ya watu Wake. Kwa sababu ya upendo na Agano hili, ndipo tunapata kwamba leo kuna wengi ambao wameokoka.

Je, inamaanisha nini kuwa mmoja wa watu wa Mungu wa Agano? Kwa ufahamu wa wazi kabisa, je inamaanisha nini kuwa mkristo? Je, ni nini inafanyika wakati mtu anaokoka? Je, jambo hili linamaanisha tu kufanya uamuzi au kuomba ombi fulani? Je, kutubu kunamaanisha nini? Je, mtu anahitaji kweli kutubu? Je, tunahitaji kuamini? Ikiwa kweli tutaamini, je itawezekanaje tuamini ikiwa Biblia inasema kwamba sisi tumekufa katika dhambi na hatuna uwezo wa kuamini injili ya Kristo?

Ikiwa kweli tutaamini, basi inamaanisha kwamba ni lazima Mungu afanye jambo hili. Ukweli wa wokovu wetu unatuonyesha jambo fulani la muhimu kumhusu Mungu. Yohana aliandika, “Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu.....Twampenda Yeye kwa sababu Yeye alitupenda kwanza” (1 Yohana 4;10,19). Mungu wa Biblia ni Mungu ambaye anaupendo wa ajabu.

Mungu wa Biblia ni Mungu ambaye anatawala kila kitu.

Mwisho tunaona Mungu ambaye anatawala ila kitu na katika utawala Wake kila kumbe kinajumlishwa katika upendo Wake.

Mara kwa mara sisi wakristo huwa tunaomba: “Ufalme wako uje. Mapenzi yako yafanyike hapa duniani kama huko mbinguni” (Mathayo 6:10). Je, tumewahi kujiuliza hii inamaanisha nini? Watu wengi huomba juu ya vile vitu ambavyo wanajua kwamba watawezi kuvitimiza kwa nguvu zao na kuhusu vile ambavyo hawawezi huwa havitaji kabisa. Wao huwa hawataki kuwaza juu ya vitu ambavyo wanajua hawawezi kuvipata kwa nguvu zao. Wao hawataki kuamini ahadi ambazo hawawezi kujihakikishia kama kweli watazipata.

Wakristo hawafai kuwa hivi. Wakristo wote tunafaa kuwa na tumaini ambalo linazidi matakwa yetu na nguvu zetu. Petero aliandika kwamba, “Lakini kufuatana na ahadi Yake, sisi tunatazamia kwa furaha mbingu mpya na dunia mpya, ambayo haki hukaa ndani

yake" (2 Petro 3:13). Mstari huu unatuelekeza kwa timizo la mwisho na la lile tumaini la kwanza la Biblia. Timizo hili ni katika Kristo Yesu na kulingana na mpango wa utawala wa Mungu katika Kristo Yesu juu ya watu Wake wa Agano.

Tunapata tumaini hili katika kitabu cha mwisho cha Biblia. Kitabu cha Ufunuo kinatuonyesha kilele cha mipango ya Mungu ambayo ni kuwa na uhusiano na ushirika mwema na watu Wake. Tunaona ushindi wa kanisa na kuumbwa kwa mbingu na nchi mpya (Ufunuo 21:1-4; 21:22-22:5). Katika haya tunaona kilele cha timizo la ahadi za Mungu kwa watu Wake. Wakati huu watu wa Mungu wote watafikia kilele cha utakatifu wao na wao wataishi pamoja na Mungu. Bustani la Edeni litarejeshwa jinsi lilivyokuwa. Katika mji mtakatifu (Ufunuo 21:2), Mungu ataishi miongoni mwa watu Wake milele. Hapa ulimwenguni ndipo Mungu ataishi pamoja na watu wake.

Hii ndiyo habari njema ambayo sisi wakristo tunafaa kuwaelezea wote. Haya ndiyo maono yetu ya mbeleni. Si kwamba ni sisi ambao tulipanga mambo haya, bali ni kwamba ni Mungu ambaye ameyafunua kwetu. Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa na mtu ambaye maisha yake yalikuwa yamefika mwisho. Yohana ambaye aliandika kitabu hiki alikuwa katika utumwa. Lakini hata hivyo, alikuwa na tumaini kubwa katika Mungu ambaye anatawala kila kitu. Alijua kwamba watawala wa ulimwengu hawawezi kufanya lolote ambalo linaweza kufanya mipango ya Mungu ikose kutimika. Yohana alijua kwamba kuna Mungu ambaye atahakikisha kwamba mipango yake inakamilika. Hata kama yeye alikuwa katika utumwa, Yohana alikuwa na tumaini kwa sababu alijua Mungu ni nani.

Mafundisho haya ya Biblia kuhusu mpango wa Mungu kukomboa watu wake na kiumbe chake yanatuletea tumaini la kuishi katika mbingu na nchi mpya. Ahadi ya Mungu kwamba ulimwengu wote utajazwa na maarifaYake, itatimia katika mbingu na nchi mpya. Mungu wa Biblia, ni Mungu ambaye anaahidi na pia ni Mungu ambaye ni mwaminifu kwa ahadi zake. Je, unaona umuhimu wa jambo hili? Mungu, ni Mungu ambaye anatimiza mipango yake. Wakristo wote wanafaa kuhimizwa kwamba Mungu wao ataendelea kuwajali na kuwalinda. Wanafaa kukumbuka kwamba, kuendelea kwake Mungu kutujali si kwa sababu tumekuwa waaminifu, bali ni kwa sababu Mungu ameendelea kuwa mwaminifu kwa ahadi zake. Kwa sasa kuna vita kati ya wana wa Mungu na wale wa Shetani: ufalme wa giza na ule wa nuru. Hizi nguvu za giza zinawapinga watoto wa Mungu kila wakati. Lakini hata kama kuna upinzani mkubwa sana, Mungu bado ndiye anayetawala ulimwenguni kote. Yohana ambaye aliandika kitabu cha Ufunuo alikuwa na tumaini si kwa sababu alijitegemea bali ni kwa sababu alimtegemea Mungu pekee ambaye anatawala kila kitu.

Mambo haya ni ya muhimu sana kuyaelewa na kila mkristo. Jinsi unavyowaza kuhusu Mungu, ndiyo itachochea jinsi unavyoishi maisha yako. Ni lazima tumfahamu Mungu jinsi Biblia inavyomfunua kwetu. Ni jambo hatari sana kwa mtu yeyote kukosa kumfahamu Mungu au kuwa na shaka kuhusu Mungu. Kuwa na kiongozi katika kanisa ambaye haamini kwamba Mungu anatawala kila kitu au ambaye haelewi mafundisho ya Biblia kuhusu jambo hili, ni jambo hatari sana. Mtu kama huyu, ni mtu ambaye katika moyo wake hauko tayari kumwamini Mungu. Ikiwa kanisa lina mtu kama huyu akiwa kiongozi, yeye atakuwa kiziuzi kwa watu kufahamu mafundisho ya Biblia inasema kwa sababu hatawafundisha watu mambo ambayo yeye mwenyewe haamini.

Tutaweza tu kumjua Mungu ikiwa tutasoma na kutii Biblia. Hatuwezi kumfahamu Mungu kwa mawazo yetu. Leo kazi ya kuwahubiria wengi waokoke inaonekana kana ni kazi ya mwanadamu na siyo ya Mungu. Wengi wanazungumza kuhusu Mungu kana kwamba Yeye aliumbwa katika mfano wa mwanadamu ilhali ni mwanadamu ambaye aliumba katika mfano wa Mungu. Ikiwa tunataka leo kuwa na makanisa ambayo yana afya kiroho, lazima tumwombe Mungu awalete wafanyakazi ambao wanaamini katika utawala wake juu ya kila kitu na kila jambo. Ikiwa Biblia itafundishwa kwa uaminifu, basi makanisa mengi yatakuwa yenye afya kiroho.

Ninajua kwamba wengi ambao wanasoma mambo haya wanayapata kuwa mambo mapya kwao kwa sababu wamekuwa wakiwaza tofauti na jinsi Biblia inavyofundisha. Ninakusihi kwamba usife moyo kwa sababu hii ndiyo njia kwako ya kujua ukweli kumhusu Mungu. Biblia imejawa na hadithi za watu kama wewe. Kwa sababu nchi ya Israeli ilikuwa ikisubiri kuja kwa Masiya, jambo hili liliwafanya mara kwa mara waendelee kumwamini Mungu. Mwiba ambao Paulo alikuwa nao, ulimfanya aweze kumtumikia Mungu kwa njia ambayo huenda hangetumika hivyo ikiwa mwiba huo hangekuwa nao. Mwiba huu ulimkumbusha kwamba yote hayako sawa maishani mwake, bali yeye alikuwa mtu mdhaifu na kwa hivyo alihitaji kumtegemea Mungu kwa kila kitu.

Hivi ndivyo ilivyo nasi leo. Huwa tuko katika hatari kubwa kiroho wakati tunapowaza kwamba mambo yako sawa na kwamba hatuna udhaifu wowote. Tunafaa kujua kwamba Mungu ni mwenye haki wakati anawahukumu watu milele. Tunafaa kujua kwamba Mungu ndani ya Kristo ametutengenezea njia ya kuepuka hukumu huu ikiwa hatutajitegemea wenyewe bali tutamtegemea Kristo pekee. Kupitia kwa Kristo Yesu, ndipo tunapata njia ya kweli ya kuwa na amani na Mungu. Mwanadamu wa kawaida hana imani ya kumwamini Mungu. Mwanadamu huwa kila wakati anaamini katika vitu vya ulimwengu na huwa anashikilia kwa vitu hivi kana kwamba hivi vitu vya ulimwengu ni vya milele. Watoto wa Mungu wote wanajua kwamba kuna vitu vingi sana ambavyo Mungu amewawekea watoto wake na vitu hivi ni vya milele. Hata kama vitu ambavyo tuko navyo sasa vinaonekana kuwa vizuri sana, kwa wale wote ambao wameokoka Mungu amewaandalia vitu bora zaidi kuliko hivi ambavyo vinaonekana hapa ulimwenguni.

Ikiwa wewe ni mtoto wa Mungu, jua kwamba Mungu amekuandalia vitu vizuri sana kuliko vile ambavyo viko katika ulimwengu huu. Yohana aliandika kuwahimiza watoto wa Mungu wote kwamba, "Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana Naye, kwa maana tutamwona kama Alivyo" (1 Yohana 3:2). Paulo pia aliandika kuhusu jambo hilo hilo akisema, "Tazama jinsi kilivyo kina cha utajiri wa hekima na maarifa ya Mungu! Tazama jinsi ambavyo hukumu Zake, hazichunguziki na ambavyo njia Zake zisivyotafutikana! (Warumi 11:33). Mistari hii inatufundisha kwamba ile siku Yesu Kristo atarudi tutapewa miille mipya, tutakuwa bila dhambi yoyote na tutaishi pamoja na Yesu Kristo milele. Haya ndio mambo ambayo yanafaa kutuhimiza katika maisha yetu hapa ulimwenguni.

Huyu ndiye Mungu wa Biblia: Mungu Mwumbaji, Mungu Matakatifu, Mungu Mwaminifu, Mungu mwenye upendo na Mungu mwenye kutawala kila kitu. Biblia yote inazungumza kumhusu huyu Mungu. Biblia inahusu ahadi za Mungu na ahadi ambazo zimetimizwa na Mungu. Katika Biblia, Mungu anatuita ili tumwamini Yeye na neno Lake. Katika Biblia tunamwona Mungu akitupatia Neno lake na ahadi zake. Mungu anatarajia kutoka kwetu kwamba tutatii neno hilo na kumwamini Yeye. Kila wakati tunapoendelea kusikia neno la Mungu na kulitii, huwa uhusiano wetu na Mungu unaimarika. Huyu ni Mungu ambaye tunaweza kuamini na tunafaa kumwamini kwa sababu neno Lake ni la kweli. Je, utamwamini?

Ishara ya tatu

Kanisa linaloendelea vyema kiroho linahubiri Ujumbe wa Injili

Ujumbe wa injili si tu kwamba sisi tuko sawa
Ujumbe wa injili si tu kwamba Mungu, ni Mungu wa upendo tu
Ujumbe wa injili si tu kwamba Kristo anataka kuwa rafiki wetu tu
Ujumbe wa injili si tu kwamba tunafaa kuishi maisha mazuri tu
Ujumbe wa injili ni kutubu na kuamini.

Ujumbe wa Injili

Habari za mambo ya ulimwengu ni biashara kubwa sana leo. Habari hizi hupatikana katika runinga, redio, simu, mtandao na katika magazeti. Habari hizi zinawafaidi si tu wale ambao wanapata pesa kutoka katika kazi hiyo, lakini pia kwa wale ambao wanasoma na kuzitazama na kuzisikia. Katika habari hizi tunasoma kuhusu mambo ya uchaguzi wa raisi na jinsi mambo yanavyoendelea katika nchi fulani fulani ulimwenguni kote. Kuna watu ambao wanapenda sana mambo ya habari hizi kuliko mambo mengine yote.

Huwa kila wakati tunahaja sana ya kujua habari hizi kwa sababu tunataka kujua kile ambacho kinaendelea ulimwenguni. Kuna watu ambao hawawezi kuishi bila kusoma gazeti au kutazama au kusikia habari hizi.

Vivyo hivyo, dini ya ukristo inahusu habari na habari hii ni habari njema. Hii ndio habari nzuri zaidi ulimwenguni kote ambayo kila mwanadamu anafaa kuisikia na kuifurahia na kuipokea. Lakini hata kama hii ni habari njema kwa watu wote, mara kwa mara kuna wale ambao wanaihubiri habari hii kwa njia ambayo haieleweki au kwa njia ambayo ni ya kupotosha. Habari hii inamhusu Mungu pekee na wengi huwa wanapotosha watu kwa kuwaeleza kwamba hii habari inahusu mambo mengine kando na Mungu mwenyewe.

Habari hii ya dini ya ukristo, si habari ambayo imetungwa na watu fulani ambao ni wakristo wakitaka kuwafanya wengine kuwa wafuasi wao. Bwana Yesu Kristo Mwenyewe alizungumza kuhusu habari hii njema. Wakati alipokuwa anazungumza kuhusu habari hii, Bwana Yesu Kristo alinukuu nabii Isaya katika mahubiri Yake (Luka 4:16-21;Isaya 52:7; 61:1). Jinsi Bwana Yesu Kristo alivyozungumza kuhusu habari hii, ndivyo pia mitume wake walivyozungumza, na pia wakristo wote leo wanapaswa kuzungumza hivyo. Wote walizungumza na wote wanazungumza kuhusu habari hii, yaani habari njema.

Je, habari njema ni gani? Katika mafundisho haya, tunataka kujua kabisa habari njema ni gani. Sura hii kuhusu mafundisho ya habari njema, ni ya muhimu sana na ni lazima usiyasahau au kuyapuuza. Haya ni mafundisho kuhusu habari njema. Sura tatu zifuatazo zitashughulikia jambo hili la wokovu. Katika sura ambayo inafuata, tutazama jambo la kumgeukia Mungu. Katika sura ya tano ya kitabu hiki, tutatazama jinsi ya kuwaeleza wengine habari hii ambayo ilitugeuza na kutuleta kwa Mungu. Katika sura hii ya kitabu hiki, tutatazama habari hii njema ni gani. Je, ujumbe wa Kristo ni nini? Je, ule ujumbe ambao sisi wakristo tunahubiri ni upi?

Je, habari njema ni nini? Je, habari hii njema ni kwamba mambo ni sawa nami? Au kwamba Mungu ni mwenye upendo? Je, ni kwamba Kristo ni rafiki wangu? Au ni kwamba ninafaa kujitahidi kuishi maisha mazuri? Je, habari njema ya Kristo Yesu ni nini?

Habari si tu kwamba sisi tuko sawa

Watu wengi huwa wanawaza kwamba dini ya ukristo ni dini ambayo huwa inawasadia watu wengi kujihisi vyema. Wanawaza kwamba jukumu la mtu ni kuenda kanisani na kusikiliza mahubiri ya mchungaji. Wanawaza kwamba kwa kuenda tu kanisani na kuyasikiliza mahubiri, ametimiza jukumu lake na yeye sasa hana haja ya kuyatii. Hii ndiyo sababu hata baada ya wengi kuhudhuria kanisa kwa muda na kusikiliza mahubiri, wanabaki na kiu kubwa sana ambayo hawawezi kujitosheleza. Hii inaonyesha kwamba kuna kasoro katika maisha ya mwanadamu?

Je, kwa nini kuna kasoro katika maisha ya mwanadamu? Hili ndilo swali ambalo kila mmoja wetu anafaa kujiuliza. Tunaposoma Biblia, tunapata kwamba Biblia haikubaliani na wengi ambao wanawaza kwamba maisha ya mwanadamu ni sawa. Kuna wengi ambao wanawaza kwamba kile mwanadamu anahitaji kufanya ni kukubali tu kwamba yeye ni mwenyewe dhambi na kuwa na tumaini kwamba mambo yatakuwa mema mbeleni. Biblia inakataa jambo hili kabisa. Biblia inafundisha kwamba kupitia kwa Adamu na Hawa ambao ndiyo wazazi wa kizazi chote cha wanadamu, wanadamu wote walianguka dhambini na kuwa waasi dhidi ya Mungu.

Kwa hivyo hakuna mwanadamu ambaye ni mwenye haki au ambaye amezaliwa akiwa na uhusiano mwema na Mungu. Kulingana na mafundisho ya Kristo Yesu, hali ya mwanadamu ni mbaya sana kwamba tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ikiwa kweli tutakubalika na Mungu (Yohana 3:1-7). Pia Biblia inafundisha kwamba, tunafaa kuumbwa upya kwa sababu sisi tumezaliwa tukiwa tumekufa katika dhambi na makosa (Waefeso 2; 1 Wakorintho 15). “Makosa” ni neno ambalo linamaanisha dhambi, yaani linamaanisha kwamba kupotea kabisa. Dhambi zetu zimetufanya tusiwe katika uhusiano mwema na Mungu. Katika kitabu cha Yakobo tunakumbushwa kwamba, “Kwa maana mtu yeyote anayeishika sheria yote lakini akajikwaa katika kipengele kimoja tu, ana hatia ya kuivunja sheria yote.” (Yakobo 2:10-11). Biblia pia inafundisha kwamba, “Mshahara wa dhambi ni mauti” (Warumi 6:23).

Katika kitabu cha Yakobo sura ya 2, tunapata kujua ni kwa nini mshahara wa dhambi ni mauti. Katika Yakobo tunaona hatari ya kila dhambi. Yakobo anasema kwamba sheria ya Mungu si kama sheria za wanadamu ambazo zinapitishwa na wanadamu na kuondolewa na wanadamu. Bali tunaonyeshwa kwamba sheria ya Mungu huwa inadhihirisha jinsi Mungu alivyo. Sheria hii huwa inazungumza kumhusu Mungu mwenyewe. Kwa hivyo kuvunja sheria ya Mungu ni kumwasi Mungu mwenyewe na pia ni kuishi kinyume na Mungu mwenyewe.

Kwa mfano, ikiwa mke wako anakuuliza kwamba ukanunue vitu fulani sokoni. Unapokuwa sokoni, hununui vile vitu alikuuliza bali unanunua vitu vingine vingi na katika hali hiyo. Je, hii inataonyesha nini? Ukweli ni kwamba, hii itadhihirisha jinsi uhusiano wako ulivyo kati yako na mke wako. Ni lazima kuwe na sababu kubwa ni kwa nini uliamua kuacha kununua vile vitu vyote ambavyo mke wako alitaka ununue na kuamua kununua vile vitu ambavyo hakuhitaji yeye. Pengine wewe ulikuwa umemkasirikia mke wako na kwa hivyo hukua katika uhusiano mwema Hivi ndivyo ilivyo kwetu na Mungu.

Ikiwa tutaamua kwa makusudi kupuuza neno la Mungu na Sheria yake, basi itaonyesha jinsi uhusiano wetu ulivyo kati yetu na Mungu mwenyewe. Je, nini inaendelea kati yetu na Mungu?

Biblia inamdhihirisha Mungu kwetu si tu kama Mungu Mwumbaji, lakini pia Mungu mwenye upendo. Yeye hutaka tumtii Yeye pekee. Ikiwa tutaamua kupuuza neno Lake na sheria Yake, basi hiyo itakuwa ishara tosha kwamba sisi hatufahamu kabisa hali ya uhusiano na ushirika wetu Naye. Hatuwezi kuendelea kujiiita wakristo ikiwa makusudi tunaendelea kuvunja sheria Yake na kupuuza neno Lake. Sisi tumepungukiwa na utukufu wa Mungu. Tumevunja sheria yake Mungu. Kwa hivyo tuna hatia mbele zake Mungu. Sisi tunazaliwa tukiwa waasi dhidi ya Mungu. Mara kwa mara huwa tunavunja sheria ya Mungu kama tu vile Biblia inavyosema: tumekufa katika dhambi na makosa (Waefeso 2:1). Kitabu cha Warumi huwa kinaanza kwa kutueleza kuhusu jambo hili. Katika sura ya kwanza, tunasoma jinsi watu wa mataifa wametenda dhambi. Watu wote wa mataifa wametenda dhambi na kwa hivyo wamevunja sheria takatifu ya Mungu (Warumi 1:18-32.

Wakati Paulo aliandika haya, watu wa taifa la Isreali walianza kujiona kwamba sasa wao ni watakatifu. Katika sura ya pili ya kitabu cha Warumi, anaanza kwa kuwaeleza kwamba wao pia kwamba wametenda dhambi na kwa hivyo wao ni wenye dhambi. Anasema katika sura hiyo hiyo kwamba mtu yeyote ambaye anadai kwamba anajua yale ambayo yanampendeza na yale ambayo yanamchukiza Mungu, basi yeye mwenyewe anafaa kujua kwamba yeye ni mwenye dhambi. Katika sura ya tatu ya kitabu hiki Paulo anakamilisha mafundisho yake kuhusu dhambi kwa kusema, “Tusemeje basi? Je, sisi ni bora kuliko wao? La hasha! Kwa maana tumekwisha kuhakikisha kwa vyovyote kwamba Wayahudi na watu wa Mataifa wote wako chini ya nguvu ya dhambi. Kama ilivyoandikwa: Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja. Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu. Wote wamegukia mbali, wote kwa pamoja hawafai, hakuna atendaye mema, naam, hata mmoja. 'Makoo yao ni makaburi wazi, kwa ndimi zao hufanya udanganyifu. ' Sumu ya nyoka iko midomoni mwao. 'Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu.' 'Miguu yao ina haraka kumwaga damu, maangamizi na taabu viko katika njia zao, wala njia ya amani hawaijui' 'Hakuna hofu ya Mungu machoni pao.' Basi tunajua ya kwamba chochote sheria inachosema, inawaambia wale walio chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu. Kwa hivyo hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria, kwa maana sheria hutufanya tuitambua dhambi.” (Warumi 3:9-20).

Mambo haya yanaonekana kuwa mambo ambayo ndani mwake hakuna habari njema. Ukweli ni kwamba tutaweza tu kufahamu wapi tunafaa kuenda ikiwa tutafahamu jinsi tulivyo sasa. Hatua ya kwanza ya kuelekea katika njia ya ukristo ni kujua kwamba una shida kubwa sana na kwamba shida hii haipo kwa sababu wewe umeharibu maisha yako au kwamba umekosa kufanya jambo fulani kwa nguvu zako, bali ni kujua kwamba wewe umetenda dhambi dhidi ya Mungu na kwa hivyo wewe ni mwenye dhambi mbele zake Mungu. Baada ya kujua haya, basi utafahamu kwamba wewe unastahili ghadhabu ya Mungu na hukumu Wake milele.

Hii ndiyo hali ya mwanadamu yeyote: hapendi Mungu, anapenda dhambi, hawezi kupokea neno la Mungu kwa uwezo na nguvu zake na kuja kwake Kristo ili apokee wokovu. Hii ndiyo hali ya moyo wa mwanadamu ambaye anastahili kuhukumiwa. Je, unaona jinsi dhambi ilivyo hatari sana? Dhambi yote imetendwa dhidi ya Mungu ambaye ni Mtakatifu na mwenye upendo. Dhambi yote imetendwa na inatendwa na viumbe ambavyo Mungu mwenyewe aliviumba katika mfano wake mwenyewe.

Ukristo wa kweli unazungumza kuhusu dhambi ambayo mwanadamu ametenda dhidi ya Mungu na jinsi mwanadamu amepotea katika dhambi zake. Pia ukristo wa kweli hautuelezi tu hali yetu ya dhambi mbele za Mungu, bali pia unatueleza njia ya kutoka katika hali hii. Habari njema ya ukristo wetu si kwamba tumepotea katika dhambi tu, bali pia kwamba Mungu ana mpango wa kukomboa watu na viumbe vyote kutoka kwa dhambi. Mungu alituumba ili tuweze kumtukuza katika maisha yetu yote.

Unapoajua jambo hili, utaanza kuishi maisha yako kwa njia ya kumshukuru Mungu na hutaona ukristo ukiwa jambo ambalo ni la kuwaletea wengi uchungu na mateso. Ujumbe wa Kristo unatufundisha kuishi maisha mapya tukiendelea kuishi kwa imani tukiwa na hakikisho kuhusu maisha ya baadaye, yaani ya mbinguni. Habari njema haihusu tu kwamba sisi tuko sawa.

Habari njema si tu kwamba Mungu ni Mungu wa upendo.

Kuna wakati mwingi ambapo huwa tunasikia wengi wakihubiri kwamba habari njema ni kwamba Mungu ni Mungu wa upendo tu. Unaposoma sentensi hii kwamba Mungu ni Mungu wa upendo, kwa kweli ukiichunguza vyema utaona kwamba sentensi hii haikamilika. Biblia huwa haisemi tu kwamba Mungu ni Mungu wa upendo (1 Yohana 4:8).

Ikiwa wewe ni mzazi, labda kuna wakati ambapo ulimwambia mwanao asifanye jambo fulani. Lakini alikushangaza kujibu, “Ikiwa unanipenda, basi ungekuwa umeniacha nifanye jambo hilo.” Kwa kawaida tunajua kwamba si rahisi kumwacha yule ambaye unapenda afanye mambo fulani fulani mabaya. Kwa sababu ya kupenda, kuna wakati tunafanya mambo ambayo yanawaumiza wengine na wakati mwingine tunafanya yale ambayo yanawafaidi wengine. Kwa hivyo ikiwa tunasema kwamba Mungu ni Mungu wa upendo, basi ni lazima tuwe tunajua kweli hii inamaanisha nini?

Je, wakati Biblia inazungumza kumhusu Mungu, je huwa inazungumza tu kwamba Yeye ni mwenye upendo? Je, Biblia hiyo hiyo si huwa pia inasema kwamba Mungu ni Roho? Je, Roho huwa anapenda aje? Je, Biblia si huwa inasema kwamba Mungu ni mtakatifu? Je, Roho Mtakatifu huwa anapenda kwa njia gani? Je, si Biblia huwa inasema kwamba hakuna mwingine kama Mungu? Je, Mungu Mmoja katika ulimwengu wote huwa anapenda kwa njia gani? Je, utafahamu aje jibu kwa maswali haya ikiwa Mungu mwenyewe hatakuambia?

Katika sura tuliyomaliza, tuliona kwamba Mungu anajidhihirisha kuwa Mungu wa upendo, Mwumbaji, Mtakatifu na mwenye kutawala kila kitu. Waza juu ya maneno haya: Kuna Mungu Mmoja ambaye anaishi na ni wa kweli. Utakatifu Wake hauna kipimo. Yeye ni Roho ambaye amekamilika na haonekani. Hana mwili, hana viungo vya mwili, Yeye habadiliki wala haweze kubadilishwa, Yeye ni mkuu na Yeye ni wa milele. Mwanadamu hawezi kumfahamu kabisa, Yeye ni mwenye hekima yote, Mtakatifu kabisa, Yeye hufanya jinsi anapendezwa na Yeye hufanya kila jambo na mapenzi na mipango yake hayawezi kubadilishwa. Yeye pia ni mwenye upendo, mwenye neema, mwenye huruma, Mvumilivu, mwenye utajiri wa ukweli, mwenye kusamehe dhambi na uovu; mwenye kuwazawadia wote ambao wanamtafuta kwa kweli. Yeye pia huwaadhibu wenye dhambi na kuwahukumu milele wote ambao wanakataa kutubu; Yeye huchukia dhambi na Yeye huwaondolea wenye hatia, hatia yao.

Mungu ana uhai wote, utukufu wote, uzuri wote, baraka zote na Yeye hujitosheleza katika kila jambo. Yeye hahitaji chochote kutoka kwa viumbe vyake ili aweze kuendelea kuishi au kuwepo. Yeye hapati utukufu Wake kutokana na viumbe ambavyo ameviumba, Yeye anao utukufu na hii ndiyo hali Yake. Yeye hudhihirisha utukufu wake katika viumbe vyake, kwa viumbe vyake na juu ya viumbe vyake. Yeye ndiye chemchemi ya maisha yote. Yeye anatawala kila kitu, anatawala ndani ya wanadamu na juu ya wanadamu

akifanya jinsi anavyotaka au kupendezwa. Hakuna chochote ambacho kinajificha kutokana Naye. Yeye anajua kila kitu na anajitegemea tu Yeye mwenyewe. Yeye ni Mtakatifu katika ushauri wake wote na katika neno Lake na katika kazi Yake yote na katika amri Zake zote. Yeye anastahili kuabudiwa na kutumikiwa na viumbe vyake vyote. Yeye anapendezwa na haya.

Kuna Mungu Mmoja ambaye ni Mungu wa Utatu. Yeye ana nguvu zote na ni wa milele. Yeye ni Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Huyu ndiye Mungu ambaye anajidhihirisha katika Biblia. Yeye ni zaidi ya kuwa Mungu mwenye upendo. Yeye pia ni Mungu ambaye anataka watu wake wawe watakatifu. Biblia inasema, "Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote na huwa utakatifu, ambao bila kuwa nao, hakuna mtu atakayemwona Bwana" (Waebrania 12:14).

Tunapofahamu utakatifu wa Mungu, ndipo tutaweza kufahamu upendo wake. Tunapofahamu ukuu wa Mungu ndipo tutafahamu ukuu wa upendo wake. Habari njema si tu kwamba Mungu ni Mungu wa upendo.

Habari njema si tu kwamba Kristo Yesu anataka kuwa rafiki wetu.

Kuna wakati ambapo wahubiri wanawaeleza watu kwamba Yesu Kristo anataka kuwa tu rafiki wao au anatakuwa kuwa tu mfano kwao. Ukristo wa kweli hauhusu tu Kristo kuwa mfano. Mimi na wewe tuna jambo kubwa sana ambalo tunafaa kujali zaidi. Jambo hili ni dhambi ambayo tuko nayo na hatia ambayo tuko nayo kwa sababu ya dhambi hii. Je, tunafaa kufanya nini sasa? Ikiwa Kristo anataka tuje Kwake, je, hii itatendekaje ikiwa Yeye mwenyewe ni mtakatifu na ni mkamilifu?

Hata kama dhambi yetu ni kubwa sana na inatutenganisha na Mungu mwenyewe, tunasoma katika vitabu vya Injili kwamba Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Kristo mwenyewe alifundisha hivi: "Kwa kuwa hata Mwana Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi" (Marko 10:45). Bwana Yesu Kristo alifundisha kwamba chaguo lake la kumtukuza Mungu Baba msalabani Kalivari ndiyo msingi wa huduma wake. Si jambo la kushangaza kwamba msalaba wa Kalivari ndiyo mafundisho makuu katika vitabu vinne vya Injili. Je, hii inamaanisha nini? Je, kwa kifo cha Kristo ndiyo msingi wa Habari njema? Jibu ni kwamba, msalaba ndiyo njia ambayo Mungu anatumia kutuleta Kwake. Bwana Yesu Kristo alieleza jambo hili hata kabla litendeke. Katika Marko 8:27-38 tunasoma, "Yesu na wanafunzi wake wakaondoka kwenda katika vijiji vya Kaisaria Filipi. Walipokuwa njiani Yesu akawauliza, 'Watu husema mimi ni nani?' Wakamjibu, 'Baadhi husema wewe ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya na wengine husema wewe ni mmojawapo wa manabii.' Akawauliza, je, ninyi mnasema mimi ni nani?' Petro akajibu, 'Wewe ndiye Kristo.' Akawaonya wasimwambie mtu yeyote habari zake. Ndipo akaanza kuwafundisha wanafunzi wake kuwa Mwana wa Adamu atapata mateso mengi na kukataliwa na wazee, viongozi wa makuhani, na walimu wa sheria na kwamba atauawa na baada ya siku tatu atafufuka. Aliyasema haya wazi wazi, ndipo Petro akamchukua kando akaanza kumkemea. Lakini Yesu alipogeuka na kuwaangalia wanafunzi wake, akamkemea Petro, akasema, 'Rudi nyuma yangu Shetani! Wewe huwazi yaliyo ya Mungu bali ya wanadamu.' Ndipo akauita ule umati wa watu pamoja na wanafunzi wake, akasema, 'Mtu yeyote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate. Kwa maana mtu yeyote anayetaka kuiokoa nafsi ataipoteza, lakini apotezaye maisha yake kwa ajili Yangu na kwa ajili ya Injili ataiokoa. Mtu atafaidiwa nini kama akiupata ulimwengu wote lakini akaipoteza nafsi yake? Au mtu atatoa nini apate tena maisha yake? Mtu yeyote anayenionea aibu mimi na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na cha dhambi, Mwana wa Adamu, atamwonea aibu wakati atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu." Bwana Yesu Kristo anajizungumzia kutoka katika Agano la Kale kwamba Yeye ndiye Mwana wa Adamu ambaye alizungumziwa katika Danieli 7 na kwamba pia Yeye ndiye Yule ambaye alikuwa mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53. Kifo cha Kristo Yesu ni dhabihu ambayo ilihusicha umwagaji damu Yake. Biblia inazungumza kuhusu kifo hiki kwamba, "Lakini sasa katika Kristo Yesu, ninyi ambao hapo kwanza mlikuwa mbali na Mungu, sasa mmletwa karibu kwa ajili ya damu ya Kristo" (Waefeso 2:13; Warumi 5:9; Wakolosai 1:19-20). Bwana Yesu alichagua kufa siku ya Pasaka kuonyesha kwamba Yeye ndiye alikuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi za watu wake. Je, haya yote yanauhusiano gani na utumwa wa mwanadamu na dhambi? Tunapata hili wakati tunasoma katika Biblia kwamba tumekombolewa kutoka katika utumwa. Kama tu vile Mungu alivyowanunua Waisraeli kutoka katika utumwa katika nchi ya Misri, vivyo hivyo, tumenunuliwa na kukombolewa kutoka katika utumwa na kifo cha Bwana Yesu Kristo. Kifo cha Bwana Yesu Kristo ndiyo gharama ya uhuru wetu kutoka kwa dhambi. Ni kwa njia ya kifo cha Kristo Yesu, Mungu ametukomboa kutoka kwa dhambi zetu. Jambo hili ndilo Paulo analizungumzia katika waraka wa Wagalatia.

Pia kupitia kwa kifo cha Bwana Yesu Kristo, Mungu ametupatanisha Kwake mwenyewe. Kupitia kwa kifo cha Bwana Yesu Kristo, wakristo wana ushirika na Mungu, sasa hakuna uhasama wala uadui. Katika Agano Jipya tunasoma kwamba kifo cha Bwana Yesu Kristo kilituondolea hatia ambayo tulikuwa nayo mbele za Mungu. Agano hili, linatumia maneno "kuhesabiwa haki," ambayo yanamaanisha kwamba wale wote ambao wamemwamini Kristo wameondolewa hatia yao ya dhambi zao. Hii ilifanyika msalabani Kalivari wakati dhambi za wale ambao wameokoka na wale ambao wataokoka ziliwekwa juu ya Kristo Yesu na kuadhibiwa kwa ajili yao. Pia tunaambiwa kuhusu kifo cha Kristo Yesu kwamba, Yeye alizvua enzi na mamlaka (Wakolosai 2:15; Marko 3:22-27; Yohana 16:33; 19:30; Warumi 8:39; 1 Wakorintho 15:54-57; Ufunuo 5:5). Pia tunaona jambo hili katika vitabu vya Injili kupitia kwa kukombolewa kwa wale ambao walikuwa wamepagawa na mapepo.

Kazi ya Bwana Yesu Kristo ndiyo kazi ya ukombozi ambapo wenye dhambi ambao wamemwamini Kristo na wale ambao watamwamini, wanakombolewa kutoka katika utumwa wa shetani na dhambi. Pia kazi ya Kristo ni kazi ya upatanisho ambapo uadui kati ya Mungu na mwanadamu ambaye ameokoka unaondolewa. Pia kazi ya Kristo Yesu ni kazi ya kuondoa hasira ya Mungu juu ya watu wake ambapo hasira ya Mungu ilimwagwa juu ya Kristo Yesu wakati Yeye alikuwa msalabani.

Lengo la kifo cha Yesu Kristo halikuwa kuwawezesha wote wapate kuokoka, bali lilikuwa kuwaokoa wale ambao Mungu alikusudia waokoke kabla ya kuumbwa ulimwengu. Katika kazi ya Kristo Yesu msalabani Kalivari, Mungu alitimiza yote ambayo yalihitajika ili watu wake wote waweze kuokolewa kutoka katika dhambi zao. Kifo cha Kristo Yesu kilitosheleza kila hitaji ambalo Mungu alihitaji ili watu wake waweze kupata msamaha wa dhambi zao. Kwa hivyo, hakuna chochote ambacho yule ambaye anataka kuokoka anafaa kufanya ili apate kuokoka. Kile anahitaji ni kuja kwa Kristo Yesu kwa imani na kumwomba msamaha wa dhambi zake zote. Kifo cha Kristo Yesu msalabani Kalivari kinatosha kumletea yeyote wokovu kamili na kumhakikishia nafasi mbinguni.

Msingi wa mafundisho ya ukristo ni kifo cha Kristo Yesu msalabani. Kupitia kwa kifo cha Kristo Yesu, Mungu alionyesha upendo wake mkuu kwa watu wake na haki yake. Kwa hivyo Kristo si rafiki tu, bali Yeye ni zaidi ya rafiki. Kwa kifo chake, Kristo Yesu ndiye Mwana-kondoo ambaye alichinjwa kwa ajili yetu. Yeye ndiye Mkombozi wetu, Yeye ndiye ametuletea amani na Mungu, Yeye ndiye alichukua juu Yake hasira ya Mungu na ni Yeye ambaye amemshinda shetani. Haya yote yanajumlishwa katika maono makuu

ya Yohana alipkuwa kisiwani Patmo.

“Kisha mmoja wa wale wazee akaniambia, 'Usilie! Tazama Simba wa kabila la Yuda, wa uzao wa Daudi, ameshinda, ili kwamba aweze kukifungua hicho kitabu na kuvunja hizo lakiri zake saba.' Ndipo nikaona kati ya kile kiti cha enzi na wale viumbe wenye uhai wanne na miongoni mwa wale wazee, Mwana-kondoo amesimama, akiwa kama amechinjwa. Alikuwa na pembe saba na macho saba, ambazo ndizo zile Roho saba za Mungu zilizotumwa duniani pote. Huyo Mwana-kondoo akaja na kukitwaa kile kitabu kutoka kwenye mkono wa kuume wa yule aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi. Alipokwisha kukitwaa kile kitabu, wale viumbe wenye uhai wanne pamoja na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele ya yule Mwana-kondoo. Kila mmoja wao alikuwa na kinubi, nao walikuwa wameshika mabakuli ya dhahabu yaliyojaa uvumba, ambayo ni maombi ya watakatifu. Nao wakaimba wimbo mpya wakisema: “Wewe unastahili kukitwaa kitabu na kuzivunja lakiri zake, kwa sababu ulichinjwa na kwa damu Yako ukamnunulia Mungu watu kutoka katika kila kabila, kila lugha, kila jamaa na kila taifa” (Ufunuo 5:5-9).

Habari njema si tu kwamba Yesu ni rafiki wetu.

Habari njema si tu kwamba tunafaa kuishi maisha mazuri.

Makosa mengine makubwa ambayo wengi wanafanya ni kwamba wanawaza kwamba habari njema ya Biblia ni kwamba tunafaa kuishi maisha mazuri. Kuna wengi ambao wanawaza kwamba dini ya ukristo inajumlisha tu kuishi maisha mazuri mbele ya watu na hata wakati wako pekee yao. Wakristo huwa wanawaziwa kuwa watu ambao wanatenda matendo mema kwa wengine kama kuwasaidia watu, kujenga mijengo ambayo inawasaidia watu na kutetea haki za watu. Pia mkristo anawaziwa kuwa mtu wa dini ambaye anatenda matendo yake ya kidini kama kubatizwa, kushiriki meza ya Bwana, kuenda kanisani, kutii Amri Kumi za Mungu, kusoma Biblia na kuomba. Lakini hata kama watu wanawaza hivi, ukweli ni kwamba habari njema ya Biblia haipatikani katika mambo haya. Kuwa mkristo si kuwapenda wengine tu au kufanya mambo fulani ambayo inawafaidi wengine tu, hata kama mambo haya ni mazuri kufanya. Habari njema inasisitiza mabadiliko halisi kutoka ndani ya mtu. Habari njema si ujumbe ambao unawafanya watu kuwa wazuri zaidi. Habari njema ni ujumbe wa injili ambao ni furaha kwa wale wote ambao wanajijua kwamba kweli wao ni wenye dhambi na kamwe hawawezi kujiokoa na kujiingiza mbinguni.

Je, tunafaa kufanya nini na ujumbe huu wa injili? Je, mtu anafaa kufanya nini wakati amegundua hali yake ya kweli, yaani kwamba yeye ni mwenye dhambi na hawezi kujiokoa kamwe na kwamba tumaini la wokovu wake ni Kristo Yesu pekee? Kulingana na mafundisho ya Biblia, jibu ni kwamba mtu anafaa kutubu na kuamini. Mungu anatuamuru tutubu dhambi zetu na kumtegemea Kristo pekee. Tutatazame mambo haya yote kwa ufupi.

Toba

Katika Biblia, toba na kuamini ni mambo ambayo yametajwa pamoja. Wakati Paulo alikutana na wachungaji wa mji wa Efeso, alisema, “Kama nilivyowashuhudia Wayahudi na Wayunani kwamba inawapasa kumgeukia Mungu kwa kutubu dhambi na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo” (Matendo ya Mitume 20:21). Huu ndiyo ujumbe ambao unahubiriwa wazi kabisa katika Agano Jipya. Baada ya kusikia ukweli kuhusu dhambi zako, utakatifu wa Mungu, upendo wa Mungu kwa kumtuma Kristo Yesu, kifo cha Kristo Yesu na kufufuka Kwake ili sisi tuhesabiwe haki, basi unafaa ujue kwamba Mungu anataka uchukue hatua na kutubu na kumwamini Kristo.

Je, huku kutubu ni nini? Je, ni kuinua mkono wako na kuenda mbele ya kanisa na kurudia ombi fulani? Je, ni kuandika mambo fulani kwa karatasi kwamba wewe sasa umeokoka? Je, ni kuombewa na mchungaji au ni kuamua ubatizwe na kuwa mshirika wa kanisa fulani? Hata kama mambo haya yote huwa yanafanywa, hakuna hata moja ambalo litakuletea toba la kweli. Mtu yeyote wakati amesikia ujumbe wa injili kutoka kwa watumishi wa Mungu, anafaa kuupokea kwa kutubu na kuuamini. Baada ya kusikia ukweli kuhusu dhambi yetu, utakatifu wa Mungu, upendo wa Mungu kwa kumtuma Kristo Yesu na kifo cha Kristo Yesu na kufufuka kwake, ili sisi tuhesabiwe haki, basi tunafaa kutii maneno ya Kristo Yesu: “Tubuni na kuiamini habari njema” (Marko 1:15).

Kuamini

Toba na kuamini haviwezi kutengnishwa. Ni lazima tuuamini ujumbe wa injili, lakini je, tunafaa kuamini nini? Kwa mfano unaweza kuamini mambo fulani. Ni ukweli kwamba ziwa victoria linaenea katika mataifa matatu ya Afrika mashariki au kwamba gari ni chombo ambacho kinakimbia kwa kasi sana au kwamba ndege ya abiria hupaa angani. Lakini je, huu ndiko kuamini ambako Kristo anazungumzia? Jibu ni la. Kuamini ambako Kristo anazungumzia ni kule ambako kabisa ni kutegemea na kuamini katika ujumbe wa wokovu. Kwanza ni lazima tuamini kwamba kwa uwezo wetu kamwe hatuwezi kumpendeza Mungu hata kama tutaishi maisha mazuri. Hatufai kujiamini kwa kiwango fulani halafu pia tumwamini Mungu kwa kiwango fulani. Yaani hatufai kujiamini na wakati huo huo tunamwamini Mungu. Tunafaa kujua kwamba ni lazima tumtegemea Mungu pekee katika kila jambo na kumwamini Kristo pekee kwa ajili ya wokovu wetu.

Kuamini huku kwa kweli na kumtegemea Mungu kabisa ni tofauti kabisa. Kuamini huku kunahitaji imani pekee na toba. Ni lazima maisha yetu yabadilike kabisa kwa sababu tumetubu na kumwamini Kristo. Kuamini na kutubu ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa. Si kwamba unaweza kuamini halafu baada ya muda fulani utubu dhambi zako. Toba na Imani ni mambo ya kwanza mtu anafanya wakati anaanza kufahamu ni nini Biblia inasema kumhusu Mungu na mwanadamu. Mtu akidai kwamba ametubu dhambi zake na kumwamini Kristo lakini hakuna mabadiliko yoyote maishani mwake, ni ishara kwamba yeye hajatubu na kuamini kwa kweli. Mchungaji J.C. Ryle alisema kwamba, “kuna ukristo ambao unapatikana kila mahali leo ambao wengi wako ndani na wanawaza kwamba kweli wao ni wakristo. Ukristo wao ni wa bei rahisi, ni ukristo ambao hautaki kukosea yeyote na hautaki kujitolea katika jambo lolote, hauna gharama yeyote na hauna faida yeyote.”

Kutubu ambako Kristo Yesu anazungumza kuhusu hapa na kule ambako kuletwa kwa kuuamini ujumbe wa injili. Neno kutubu linamaanisha kubadilisha kabisa mawazo. Kwa sababu mawazo yako yanabadilika, ni lazima pia maisha yako yote yabadilike.

Kwa hivyo tunaona kwamba ukristo wa kweli si tu kuongoze mambo fulani fulani katika maisha yako, bali ni kubadilika kabisa

kutoka kwa mtu wa kale na kuwa mtu mpya ndani ya Kristo Yesu. Haya ni maisha ambayo yanageuzwa si kwa nguvu zetu, bali kwa nguvu za Mungu mwenyewe kutokana na kazi ya Bwana Yesu Kristo msalabani Kalivari. Kusema kwamba unaamini na maisha yako yawe hayajabadilika kamwe ni kudanganya. Maisha yetu yataweza kubadilika ikiwa mawazo yetu yatabadilika. Mabadiliko haya ni kazi ya Mungu katika maisha ya mtu. Katika sura ifuatayo tutatazama jambo hili kwa urefu.

Ninaomba kwamba haya yote ambayo tumesoma hapa yatakusaidia kufahamu kwamba habari njema, ni habari ambayo inaleta mabadiliko mapya. Hii si habari ambayo inazungumza kuhusu sisi na maisha yetu. Ni habari ambayo inazungumza kuhusu sisi wenyewe na hali yetu halisi, kuhusu Mungu na kumhusu Kristo Yesu. Mara nyingi mimi huwauliza watu wanielezea habari njema ni nini katika muda mfupi sana. Huwa ninafanya hivi kwa sababu ninataka kuwasaidia wengi kufahamu habari njema ni nini na kuwasaidia kujua kweli kama wao kile wanaamini ni cha kweli au la. Je, ikiwa wewe ni mkristo, umewahi kujiuliza kama kile unaamini ni cha kweli au la? Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni na kuishi miongoni mwa watu ambao hawakumpenda. Yeye alienda kila mahali akihubiri ujumbe ambao ni wa kuokoa. Baadaye alikufa msalabani kwa ajili ya wenye dhambi. Yeye ndiye njia kwa wote ambao wanataka kuokoka na kuingia mbinguni na katika Yeye ndipo tunapata kumwabudu Mungu jinsi anavyopendezwa. Huu ndiyo ukweli wa mambo. Mungu ndiye amefanya haya yote. Maneno mengine kutoka kwa watu kama, “wewe si mbaya sana, Mungu ni Mungu wa upendo, Yesu ni rafiki, unafaa kuisha maisha mazuri,” si habari njema ya ukristo wa kweli. Maneno haya ni ukweli nusu na hayafai kutegemewa hata kidogo katika jambo lolote kama habari njema. Lakini habari njema ni kwamba “Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.” (2 Wakorintho 5:21). Hii ndiyo habari njema ambayo tunafaa kuamini. Huu ndiyo ukweli.

Je, unasema nini kuhusu haya yote? Ninajua kwamba kuna wengi ambao watanijibu kwamba wao wanaamini katika mambo mengine. Hata leo katika nchi yetu kuna wengi ambao wanawaza kwamba ujumbe wa injili ni tisho sana kwa uhuru wao. Kwa sababu hii kuna ukristo ambao unaonekana kana kwamba umetoka kwa Mungu ilhali ni wa uongo. Ni ukristo ambao unaahidi vitu vizuri na maisha mazuri na ukristo ambao wanadamu wanafanya jinsi wanavyotaka na siyo jinsi Mungu anavyosema katika neno Lake. Ni jambo la kutisha sana kwamba watu leo katika nchi yetu hawajali kabisa ujumbe wa kweli wa Biblia. Kila mmoja anafaa kujua kwamba kuna wakati ambapo unakuja wakati mlango wa mbinguni utafungwa na kamwe hakuna hata mmoja ataweza kuingia humo. Wakati huo kutakuwa na machozi kwa wengi katika nchi yetu.

Swali langu kwa msomaji wangu ni hili, je umesikia ujumbe wa injili? Je, umeuamini au bado au unajitahidi katika mambo mengine? Je, unahudhuria tu kanisa kwa sababu unataka kutimiza jukumu tu au kuonekana na wengi kwamba wewe ni mtu wa Mungu? Je, wewe unaendelea kujiamini na kujitumikia?

Kusikia kwa ukweli kwa injili ni kuipokea. Je, wewe umeona kweli kwamba wewe ni mwenye dhambi na unahitaji kuokoka? Kumbuka kusikia kwa kweli ni kutubu na kuamini injili. Ujumbe wa injili si kwamba wewe ni mzuri na unahitaji kujiongezea mambo fulani fulani au kwamba Mungu anakupenda au kwamba Yesu anataka kuwa rafiki wako au kwamba unahitaji kubadilika hapa na pale. Ujumbe wa Injili ni kuhusu Mungu na hali yetu mbele zake. Habari hii ni kwamba dhambi za kale zimesamehewa na maisha mapya yameanza ambayo yanajumlisha uhusiano na ushirika mpya na Mungu ambaye ndiye aliyekuumba. Ushirika huu na uhusiano huu ni wa milele.

Je, utasikia wapi habari njema kama hii?

Ishara ya nne

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kanisa ambalo linafahamu vizuri Mafundisho ya Biblia kuhusu kuokoka.

Yaliyomo

1. Je, tunahitaji kubadilika?
2. Je, mabadiliko yanawezekana?
3. Je, ni mabadiliko ya aina gani ambayo yanahitajika?
4. Je, mabadiliko haya yatahusu:
- Mabadiliko katika mawazo
- Mabadiliko katika jinsi mtu anayoishi maisha yake.
- Mabadiliko haya yatahusu kumtegemea Kristo kabisa.
5. Je, mabadiliko haya yanafanyika kwa njia gani?
- Mabadiliko haya ni kazi ya Mungu pekee.
- Katika mabadiliko haya Mungu amempa mwanadamu jukumu la kufanya.
- Ni Mungu ambaye anatupatia imani ambayo inatuokoa.

Mafundisho ya Biblia kuhusu kuokoka.

Kulikuwa mtu ambaye alihukumiwa kwa kumfanyia mwingine makosa na kwa kufanya hivi alivunja sheria ya nchi hiyo. Kwa miaka mingi mtu huyu alifungwa gerezani. Baada ya kutoka huko, alikutana na yule ambaye alikuwa amemkosea na kumwambia, “Mimi nimebadilika kabisa.” Je, unawaza yule ambaye aliambiwa maneno hayo aliyakubali kweli? Je, ikiwa mtu huyu alikuwa amekukosea wewe, je, ungekubali kwa haraka kwamba kweli mtu huyu amebadilika? Leo watu wengi huwa hawaamini kwamba mtu yeyote anaweza kubadilika na kuwa mtu mzuri. Kwa mfano, wanasiasa, mawakili, wahubiri, walimu, watangazaji, wote wanaaminika kuwa watu ambao hawawezi kubadilika katika misimamo yao.

Kwa wengi leo, hekima ni kuweza kukabiliana na yale ambayo yanaendelea katika maisha yako bila kubadilika. Kwa watu hawa, wanawaza kwamba kukua ni kujikubali jinsi ulivyo na kutosheka hivyo. Kwao mtu hawezi kamwe kubadilika. Wale wote ambao wanawaambia watu mambo haya, ni wale ambao wanataka kuwafanya watu wawe ni watu ambao hawana furaha yoyote hata kama wao wanajiwazia kwamba kweli wanafaa kubadilika kwa sababu hawatosheke na jinsi walivyo.

Kiroho hakuna yeyote ambaye anafaa kujivunia hali yake ikiwa kwa kweli hajaokoka. Wale wote ambao hawajaokoka ni watu ambao wako katika hali mbaya sana ambayo haitamaniki hata kidogo. Kwa hivyo kumwambia mtu kwamba tosheka na jinsi ulivyo kwa sababu wewe hivyo ndivyo ulivyo na huwezi kamwe ukabadilika, ni kumwambia mtu kwamba ataosheke na kuingia jahanum.

Ukweli ni kwamba watu wengi wanatamani sana kubadilika. Hakuna mtu yeyote ambaye anafaa kutosheka na hali yake ya kiroho ikiwa kweli yeye hajaokoka. Hata katika maisha ya kawaida utaona hali hii ya kutotosheka katika maisha ya watu. Kwa mfano, kila wakati tunajitahidi kudumisha maisha yetu ya kimwili; utamwona mwingine ambaye analo gari, anataka kuwa na lingine; mama ambaye anabadilisha nyumba yake, ni kwa sababu hajatosheka na jinsi mpangilio wa nyumba yake ulivyo. Wengi pia wanabadilisha mahali pa kazi mara kwa mara. Lakini hata wakati tunafanya mambo haya, tunapata kwamba ndani ya mioyo yetu kwamba tumelemewa na hatuna tumaini lolote na tumenaswa. Je, katika hali kama hii, kuna uwezekano wa kubadilika kweli? Je, Biblia inasema nini kuhusu mabadiliko kamili? Katika sura hii, tunataka kutazama mabadiliko kamili ambayo ni makubwa sana maishani mwa mtu. Mabadiliko haya hutokea katika maisha ya mtu wakati anaokoka. Mojawapo wa ishara za kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kwamba watu wa kanisa hilo wanafahamu vyema mabadiliko makubwa ambayo yanatendeka kwa mtu wakati anaokoka. Tunapoendelea katika mafundisho yetu tukitaka kufahamu jambo hili la kubadilika vyema, tutafanya hivyo kwa kujiuliza maswali machache.

Je, kweli mabadiliko yanahitajika?

Swali la kwanza tunafaa kujiuliza ni kwamba, je, mabadiliko yanahitajika kweli? Kuna wengi ambao watasema hapana. Wengi nao ikiwa wataambiwa kwamba kweli wanahitaji mabadiliko haya katika maisha yao, wanaweza kujibu, 'kwa nini?' Pia watakuambia kwamba, usiwe mtu wa kuwaeleza wengine mambo ambayo hawataki. Wataendelea kukuambia kwamba,'usiwaze kwamba maisha yako ni bora sana kuliko maisha yangu, achana na mimi, wewe endelea maisha yako nami nitaishi yangu.'

Ukweli ni kwamba hata kama mtu huyu atazungumza maneno haya yote, Biblia inasema kwamba mabadiliko yanahiotajika. Biblia inafundisha kwamba ikiwa mtu yeyote hatabadilika, basi maisha yake yako katika hatari kubwa sana. Katika sura ambayo tumemaliza, tuliangalia jinsi mwanadamu ameanguka katika dhambi na ako na hatia mbele za Mungu. Yesu alisema, *"Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. Kwa kuwa kila atendaye maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili matendo yake maovu yasifichuliwe"* (Yohana 3:19-20). Paulo aliwakumbusha wakristo wa Efeso kwamba kabla ya wao kuokolewa walikuwa wamekufa katika dhambi na makosa (Waefeso 2:1). Paulo alikuwa anamaanisha kwamba watu wote ulimwenguni wamezaliwa wakiwa wamekufa kiroho. Katika sura ambayo tumemaliza, tuliona kwamba Paulo anasema katika Warumi 3:9-20, kwamba hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kujibadilisha mwenyewe. Anasema kwa kunukuu Agano la Kale: *"Tusemeje basi? Je, sisi ni bora kuliko wao? La hasha! Kwa maana tumekwisha hakikisha kwa vyo vyote kwamba Wayahudi na watu mataifa wote wako chini ya nguvu ya dhambi. Kama ilivyoandikwa: 'Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja. Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu. Wote wamegeukia mbali, wote kwa pamoja hawafai, hakuna atendaye mema, naam, hata mmoja. Makoo yao ni makaburi wazi, kwa ndimi zao hufanya udanganyifu. Sumu ya nyoka iko midomoni mwao. Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu. Miguu yao ina haraka kumwaga damu, maangamizi na taabu viko katika njia zao, wala njia ya amani hawaijui. Hakuna hofu ya Mungu machoni pao. Basi tunajua ya kwamba chochote sheria inachosema, inawaambia wale walio chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu. Kwa hiyo hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria, kwa maana sheria hutufanya tuitambue dhambi."*

Unapoasoma maneno haya, utaona ya kwamba kila mwanadamu anahitaji neema ya Mungu na wakati huo huo kujua kwamba si lazima Mungu amhurumie mwanadamu. Kile kila mwanadamu anafaa kutarajia kutoka kwa Mungu ni hukumu wala si neema. Hii ndiyo sababu wakati Roho Matakatifu anatuita, jambo la kwanza anafanya katika maisha yetu ni kutujulisha kuhusu dhambi zetu. Mtu huona dhambi zake jinsi zilivyo na kutambua kwamba kweli anahitaji msamaha wa Mungu. Yeye anatambua kwamba bila Mungu kumsamehe, basi maisha yake yako hatarini. Katika hali hii, si kwamba mtu huwaza kwamba kuna wakati ambapo anatenda au alitenda dhambi kubwa sana na mbaya sana na wakati mwingine alitenda dhambi kidogo na hazikuwa mbaya sana. Mtu hujua kabisa kwamba dhambi zake zote ni mbaya sana na zimemfanya awe na hatia mbele za Mungu. Yeye hutambua kwamba mbele za Mungu hakuna dhambi kubwa wala ndogo; dhambi zote ni sawa na ni chukizo mbele za Mungu.

Wakati Roho Mtakatifu anakudhihirishia dhambi fulani, Yeye hukuonyesha hatari ya dhambi hiyo na kufungua macho yako ili uone kabisa hatari kubwa ya dhambi hiyo. Mtu huanza kuhisi jinsi Daudi alivyohisi: "Dhidi Yako, Wewe peke Yako, nimetenda dhambi na kufanya yaliyo mabaya machoni Pako, ili Uthibitike kuwa mkweli unenapo na kuwa na haki utoapo hukumu" (Zaburi 51:4).

Unaposoma Biblia na kuona jinsi Mungu anavyofafanua hali ya dhambi ya mwanadamu, Yeye hutumia maneno kama haya; mwanadamu ana deni mbele Yake, mwandamu ako katika utumwa, mwanadamu ni maskini na amekufa kiroho. Hivi ndivyo Biblia inavyofafanua hali yetu. Wanadamu wote wako katika hali ya hatari sana na wanahitajika kuondoka katika hali hiyo kwa haraka sana. Ukweli ni kwamba, wanahitaji mabadiliko.

Je, mabadiliko haya yanawezekana?

Ikiwa tunakubaliana kwamba kweli mabadiliko yanahitajika, je mabadiliko haya yanawezekana? Kuna wengi ambao ukiwauliza kuhusu jambo hili la kubadilika, watakuambia kwamba kweli jambo hili haliwezekani hata kidogo. Lakini unaposoma Biblia, tunaona kwamba jambo hili linawezekana kabisa. Biblia haisemi tu kwamba tunahitaji mabadiliko, bali pia inasisitiza kwamba mabadiliko haya yanawezekana kabisa. Mungu ametuumba sisi sote na ndani mwetu ameweka uwezo wa kupenda, kujua na kumtumikia Yeye. Biblia inatuhimiza kwamba ni lazima tufahamu na tukubali kwamba sisi ni wenye dhambi mbele za Mungu na kwamba tunafaa kubadili maisha yetu na kumrudia Mungu. Hili ni jambo ambalo limefundishwa kwa wazi kabisa katika Biblia na linawezekana kutendeka. Wengi wetu tulishangazwa sana wakati tuliuposikia kwamba ujumbe wa injili ni ujumbe ambao unabadilisha mioyo ya wengi. Wakati mtu anazaliwa mara ya pili, Mungu huwa anampa moyo mpya na maisha mapya. Huu ndiyo ujumbe ambao tunapata katika Agano Jipya na ni ujumbe mkuu sana. Katika sura ya Yohana 3, Matendo ya Mitume 9, Waefeso 2 na 1 Petro 1 na mahali kwingi katika Biblia, tunapata ujumbe huu mkuu. Kulingana na Biblia, mabadiliko yanawezekana kabisa.

Je, ni mabadiliko gani ambayo yanahitajika?

Wengi wanakiri kwamba wanahitaji kubadilika. Lakini mabadiliko ambayo wanayasema ni yale ambayo yanahusu mambo ya ulimwengu huu tu. Kwa mfano, mtu anakiri kwamba kweli anafaa kubadilika kutoka kwa umaskini na kuwa mtu tajiri. Kwa hivyo mabadiliko haya ni yale ambayo yanatosheleza maisha yao na kuwafanya wawe wenye furaha katika vitu vya ulimwengu huu. Haya ni mabadiliko ambayo hayashawishi dhamira ya mtu kuhusu dhambi zake.

Biblia inasema kwamba mabadiliko ambayo tunahitaji ni yale ambayo ni ya kugeuka kutoka katika dhambi na kumgeukia Mungu. Neno toba, linamaanisha kugeuka kutoka kwa dhambi na kumgeukia Mungu. Tunafaa kuacha kujiwazia kwamba sisi ni wazuri ilhali Mungu mwenyewe anasema kwamba sisi ni mwenye dhambi. Dhambi zetu zinahitajika kusamehewa; za kale, za sasa na hata za mbeleni. Hali yetu ya mbeleni inafaa kubadilishwa kutoka jahanum katika hukumu wa Mungu hadi mbinguni kwa kusamehewa dhambi zetu kupitia kwa Kristo Yesu. Haya ndiyo mabadiliko makuu ambayo tunahitaji. Mabadiliko haya si tu kubadilisha maisha yetu hapa na pale. Ni kubadilika na kuja kwa Mungu kutumia njia ambazo Yeye mwenyewe ameweka. Ni kukubali kwamba kile ambacho amesema kutuhusu ni cha kweli. Hatua ya kwanza ya kurudi kwa Mungu wa kweli ni kutambua kwamba sisi si Mungu. Ni katika mabadiliko haya tunaokolewa. Jina lingine la mabadiliko haya ni wokovu. Ni kuzaliwa mara ya pili.

Tunahitaji kubadilika na kutoka katika hali ya kujiabudu na kuanza kumwabudu Mungu. Tunafaa kuhakikisha kwamba hatia yetu ya dhambi zetu inaondolewa na Mungu na tunapewa msamaha wa dhambi zetu kupitia kwa Kristo Yesu. Haya ndiyo mabadiliko tunahitaji.

Je, mabadiliko haya yatahushisha nini?

Ndipo mtu aweze kubadilika kwa kweli, ni nini inahitajika?

Kubadilika haimaanishi kwamba kukubali tu kwamba tunahitaji kubadilika

Wengi huwaza kwamba mabadiliko haya yanahusu tu kukubali katika mawazo yako kile ambacho unataka. Wao huwaza kwamba mtu anahitaji tu kufanya uamuzi au kujaza karatasi au kuomba maombi fulani. Mabadiliko ambayo wao huwaza juu yake ni kama kubadili mwenendo wa maisha na kuanza kuishi maisha mazuri kama kuenda kanisani, kuwafanyia wengine mazuri na kukosa kunywa pombe. Wanawaza ni kuamua kufuata kanuni fulani fulani.

Biblia inasema kwamba mabadiliko makuu ambayo tunahitaji yanahusu mambo makubwa sana kuliko haya. Yanahusu kugeuka kutoka katika dhambi zako na kumgeukia Mungu. Yanahusu kutubu dhambi zetu na kuanza kufuata Mungu. Mabadiliko haya yanahusu pia kugeuka kwa moyo ambako ndiko kutubu na kuamini Kristo na neno Lake. Mimi mchungaji, niniogopa sana kwa sababu hapa ndipo wengi huwa wanafanya makosa makubwa sana.

Kwanza, kuna watu ambao wanawaza kwamba wao wenyewe hawajaokoka, ilhali wakichunguza kulingana na Biblia wataona kwamba kweli wao wameokoka. Hawa ni watu ambao wanajua Biblia inasema kwamba mkristo hatendi dhambi. Lakini wanapoanguka katika dhambi, wao huwaza kwamba kweli hawajaokoka kwa sababu wamefanya yale yalio kinyume na Biblia. Ikiwa msomaji wangu wewe ni mtu wa aina hii ambaye wakati unapoanguka katika dhambi, wewe huwaza kwamba wewe si mkristo, wacha nikuhimize. Usijihukumu na kusahau kazi kuu ambayo Mungu anafanya katika maisha yako, kazi ambayo hata inaonekana kwa marafiki wako. Kuna mtu mmoja ambaye aliulizwa swali hili, je wewe umeokoka? Alijibu, “ikiwa sijaokoka, ninamwomba Mungu aniokoe na ikiwa nimeokoka, pia ninamwomba Mungu aendelee kunilinda.” Hili ni ombi zuri sana kwa sisi sote. Yule ambaye ameokoka kwa kweli, anaweza kusema kama John Newton alivyosema, “Mimi siko jinsi ninafaa kuwa. Mimi siko jinsi ningetaka kuwa. Mimi siko jinsi ninatumainia kuwa. Lakini ninaweza kusema kwa kweli kwamba, mimi siko jinsi nilivyokuwa. Kwa neema ya Mungu niko jinsi nilivyo sasa.”

Jambo la pili ambalo ni la kuogopesha ni kwamba, kuna watu ambao wanawaza kwamba wameokoka ilhali wao bado. Hili ni jambo ambalo wachungaji wengi wanalijua. Wakati mmoja mchungaji Spurgeon alikuwa anatembea barabarani. Mtu mmoja ambaye alikuwa amelewa alimwita: “Spurgeon! Je, unanikumbuka?” Spurgeon alimjibu, “hapana! Kwa nini nikukumbuke?” Huyu mtu alimjibu, mimi ni mmoja wa wafuasi wako!” Spurgeon alimjibu, “kweli wewe unaweza kuwa mmoja wa wafuasi wangu, lakini ukweli ni kwamba wewe mfuasi wa Mungu.”

Mchungaji Spurgeon alikuwa amejua jambo hili kwamba kuna watu ambao wamejifunza mengi kutoka kwa Biblia lakini hawajaokoka. Hawa wanaweza kuzungumza kama wakristo na kufanana kama wakristo. Lakini ukweli ni kwamba mioyo yao haijabadilishwa. Hawa ni watu ambao wanajiwazia kwamba kweli wao wameokoka na wanafurahia kuzungumza kuhusu jambo hili lakini maisha yao ni tofauti na vile wanavyozungumza.

Hawa husema kwamba wameokoka na huwa hawataki kuwa na shaka kuhusu jambo hili. Lakini ukweli ni kwamba hawana sababu yeyote ya kuwa na ujasiri huu. Wengi wao wamejihakikishia jambo hili na hawako tayari kusikia yeyote ambaye anataka kuwafanya wawe na shaka kuhusu jambo hili. Kuna tofauti kubwa sana kati ya kuwaza kwamba umeokoka na kupewa hakikisho na Roho Mtakatifu kwamba umeokoka. Hakikisho la kweli lina msingi thabiti. Kuwaza huwa kunamfanya mtu aanze kujiwazia jinsi hafai kujiwazia. Kuwa mwangalifu msomaji usije ukajiwazia kwamba umeokoka ilhali wewe hujaokoka. Ikiwa kwa moyo wako wote umemwamini Kristo, basi wewe umeokoka. Lakini ikiwa wewe unasema tu kwamba umeokoka ilhali bado, basi wewe unajidanganya. Ikiwa moyo wako umebadilishwa, na umechukia vitu ambavyo ulikuwa ukivipenda na kupenda vile vya Mungu ambavyo ulikuwa ukivichukia, ikiwa kweli wewe umetubu, ikiwa mawazo yako yamebadilishwa kabisa na ikiwa kweli wewe umezaliwa mara ya pili, basi una sababu ya kuwa na furaha tele. Lakini ikiwa kweli ndani mwako hakuna mabadiliko yoyote, hakuna upendo wa Mungu na neno Lake, hakuna upendo wa kuomba, hakuna kazi ya Roho Mtakatifu, halafu unasema kwamba kweli wewe umeokoka, wewe unajidanganya kabisa. Jua kwamba maneno yako hayatawahi kukuokoa. Kila mmoja wetu anafaa kuwa akiomba, “Bwana ninaomba kwamba unibariki kwa kunipa imani ya kweli, wokovu wa kweli na uwezo wa kumwamini Kristo kwa imani. Si kwa imani ya uongo bali ya kweli. Mungu nilinde kutokana na uongo.” Tunafaa kujua kwamba mtu anaweza kuwa mshirika mwenye bidii wa kanisa fulani lakini awe yeye si mmoja wa watoto wa Mungu.

Wokovu si kuacha tabia fulani fulani hapa na pale.

Kuna wengi pia ambao wanawaza kwamba mabadiliko yanahusu tu kuishi maisha mazuri. Mabadiliko haya, ni zaidi ya kuishi maisha mazuri tu. Mabadiliko yanahusu, mwanzo mpya na kuanza na kufanya yale ambayo yanakubalika machoni pa Mungu. Wokovu unahusu kubadilika kabisa.

Kumtegemea Kristo pekee.

Kulingana na Biblia, mabadiliko kamili yanahusu kumtegemea kabisa Kristo Yesu. Hatufai tu kujitahidi kwa uwezo wetu kuhesabiwa haki mbele za Mungu. Kuboresha maisha yetu hapa na pale na kuanza kuwaza kwamba mabadiliko haya yataficha dhambi zetu kutoka kwa Mungu na yatafanya tuwe wenye haki mbele za Mungu, ni kujidanganya. Badala ya kujitahidi, toba la kweli inahusu kumtegemea Kristo kabisa. Lanahusu kutegemea Kristo na kazi yake kwa ajili ya yetu. Mabadiliko yanahusu kufahamu kwamba kuenda tu kanisani haitatutosha, kufanya mambo mengi mazuri hayatuingizi mbinguni. Matendo yetu ya dini na yale mazuri hayawezi kutuletea wokovu.

Tunafaa kujua kwamba kwa sababu ya dhambi yetu, wanadamu wote hawana tumaini lolote. Haijalishi jinsi tumeendelea katika maisha yetu ya kila siku na kufanikiwa kwetu katika mambo ya ulimwengu huu, bado tunabaki tukiwa hatuna tumaini lolote. Tumaini letu ni Yesu Kristo pekee. Kristo Yesu aliishi maisha matakatifu ambayo yalikuwa yamekamilika kabisa na alikufa msalabani kwa niaba ya wale wote ambao watamwamini. Kupitia kwa kifo chake Yeye alishinda dhambi na sasa anamtuma Roho Mtakatifu katika mioyo ya wale wote ambao wanamwamini. Huu ndiyo msingi wa mabadiliko haya. Ni lazima tutubu dhambi zetu na kumwamini Kristo.

Je, mabadiliko haya makubwa yanatokea kwa njia gani?

Je, mwanadamu anafanya lolote katika mabadiliko haya?

Wengi wanasema kwamba ili tuweze kupata mabadiliko haya, lazima tufanye mambo fulani fulani. Ikiwa hatuwezi kujiokoa ni wazi kwamba ni Mungu pekee ambaye anaweza kutuokoa. Biblia inafundisha kwamba katika mabadiliko haya ni lazima tufanye mambo fulani. Bwana Yesu Kristo hakuwaeleza tu wanafunzi wake kwamba walihitaji kuacha kujitahidi katika lolote na kujua neema ya Mungu inatosha. Bwana Yesu Kristo hakuwaambia kwamba walihitaji kujichunguza kwanza ili waone kama kweli kulikuwa na ishara za neema ya Mungu katika maisha yao. Kile Kristo aliwaambia ni kwamba walihitaji kugeuka kutoka katika dhambi zao na kumgeukia Mungu. Tangu mwanzo wa huduma wake, Kristo aliwaambia watu kwamba mabadiliko makubwa ambayo walihitaji yalikuwa kugeuka kutoka kwa dhambi zao na kumgeukia Mungu. Je, wokovu ni jambo tu la kufanya jinsi unavyotaka?

Je, ni sisi ambao tunafanya kila kitu?

Je, tunahitaji tu kufanya uamuzi? Ikiwa mambo ni hivi, basi tuna uwezo wa kujifanyia mabadiliko haya. Kulingana na Biblia, ni wazi kwamba sisi tunafaa kufanya uamuzi huu na kwamba pia tunafaa kuwahimiza wote wafanye uamuzi huu: yaani kuacha dhambi na kumgeukia Mungu. Basi ikiwa mambo ni hivi, kwa nini tusiwaeleze wengi wafanye uamuzi huu? Je, si ni lazima tuwalazimishe wote wafanye uamuzi huu? Au si tutumie njia za ujanja kuwafanya waamue? Ikiwa tuna uwezo wa kuwafanya wafanye uamuzi huu, basi si bora hivi? Ukweli ni kwamba tunaposoma Biblia, tunapata kwamba jambo la wokovu si jambo ambalo mwanadamu anaweza kujifanyia.

Mungu ndiye anayetupatia imani ambayo inaokoa.

Kuna dini nyingi hapa ulimwenguni ambazo zinahubiri kwamba wokovu ni jambo ambalo mwanadamu mwenyewe anaweza kujifanyia. Biblia inafundisha kwamba mabadiliko haya yanahusu tabia na moyo. Haya ndiyo mabadiliko ambayo kila mwanadamu anayahitaji. Biblia pia inafundisha kwamba hatuwezi kuanza kuwa na mabadiliko haya mazuri ikiwa Mungu hajabadilisha mioyo yetu. Tuna uwezo wa kupenda na kumpenda Mungu kwa sababu tuliumbwa hivi katika mfano wake. Shida kubwa ambayo tuko nayo iko katika mioyo yetu. Huwa hatufanyi yale ambayo tuliumbwa tuyafanye. Hii ndiyo sababu ni lazima Mungu abadilishe mioyo yetu kwanza ikiwa kweli tutafanya yale ambayo alikusudia tuyafanye. Katika Biblia tunapata kwamba Mungu ameahidi kufanya hivi: “Nitawapa moyo mmoja na kuweka roho mpya ndani yao, nitaondoa kutoka ndani yao moyo wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama” (Ezekieli 11:19). Tunapata jambo hili katika mafundisho ya Biblia yote. Kazi hii ya kutupatia moyo mpya ni kazi ya Mungu pekee. Ni lazima afanye jambo hili ndipo tuweze kuyafahamu mafundisho ya Biblia (1 Wakorintho 2:14). Yesu Kristo mwenyewe alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu kama asipovutwa na Baba aliyenituma” (Yohana 6:44).

Biblia inazungumza kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Je, umewahi waza kuhusu jambo hili na kwamba linamaanisha nini? Maneno haya yalizungumzwa na Kristo Yesu mwenyewe katika Yohana 3. Katika sura hii ya Yohana tunasoma kumhusu mtu mmoja ambaye aliitwa Nikodemo ambaye alikuja kuzungumza na Kristo usiku na yeye alikuwa mtu wa dini sana. Nikodemo alitaka kujua kile alihitaji kufanya ili aweze kuingia katika ufalme wa mbinguni. Yesu hakumjibu kwamba alihitajika tu kuwa mtu mzuri kwa kuhudhuria kanisa kila Jumapili au kuwasaidia wengi katika mahitaji yao. Yesu alimwambia Nikodemo kwamba alihitaji maisha mapya. Nikodemo alimwuliza Kristo jinsi mtu anafaa kupata maisha haya na Yesu alimjibu kwamba ni Mungu pekee ambaye anaweza kupeana maisha haya. Kwa hivyo Nikodemo alihitajika tu kumwamini Kristo na kuishi maisha yake kulingana na ukweli wa Biblia.

Yesu Kristo alifundisha kwamba ni lazima tujitahidi ili tupate wokovu. Lakini pia alifundisha kwamba tunaweza kujitahidi vyema ikiwa Mungu ndiye anayetuongoza katika kujitahidi kwetu. Yesu Kristo alifundisha haya kutoka katika Agano la Kale. Kwa mfano katika kitabu cha Yoeli tunasoma kwamba, “Kila mmoja atakayeliita jina la Bwana ataokolewa” (Yoeli 2:32). Paulo alinukuu mstari huu katika Warumi 10. Ikiwa wewe umewahi kuhubiria mtu huenda labda umewahi kutumia mstari huu: “Kila mmoja atakayeliita jina la Bwana ataokolewa.” Yoeli aliandika maneno haya baada ya kuandika mengi kuhusu hukumu ya Israeli kwa sababu ya kutoamini kwao. Swali ni, je, ni kwa nini hawa watu ambao walikuwa hawamwamini Kristo walikuwa waliite Jina lake kwa ajili ya wokovu wao? Tunapata jibu katika mstari huo huo wa 32: “Kila mmoja atatakayeliitia jina la Bwana ataokolewa. Kwa maana juu ya Mlima Sayuni na katika Yerusalemu kutakuwako wokovu, kama Bwana alivyosema, miongoni mwa walionusurika ambao Bwana awaita.” Je, ni nani ambaye analiita jina la Bwana? Jibu ni, wale ambao Mungu mwenyewe anawaita.

Katika 1 Wakorintho 1:18-24, tunapata kwamba ni mwito wa Bwana ambao unabadilisha mambo. Kulingana na kifungu hicho, Wayahudi na Wayunani ujumbe wa injili kwao ni upumbavu. “Lakini kwa wale ambao Mungu amewaita, yaani, Wayahudi na Wayunani, Kristo ni nguvu na hekima ya Mungu.” Miaka mingi iliyopita, kuna kikundi cha watu ambao walikutana pamoja kwa maombi ili waweze kupanda kanisa. Katika mkutano wao, waliandika kile ambacho waliamini kuhusu Biblia na mafundisho yake kuhusu jambo hili la kuokoka ambalo walilifahamu katika maisha yao wenyewe. Walitaka jambo hili pia liwatendekee wengine kama lilivyowatendekea wenyewe. Waliandika kuhusu wokovu na walisema haya: “Tunaamini kwamba toba na imani ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa na huwekwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu ambaye hutuzaa mara ya pili. Roho Mtakatifu hutudhibitishia kuhusu dhambi zetu na kutuonyesha hatia yetu mbele za Mungu. hatari ambayo tukomo ikiwa tutaendelea katika

dhambi, ukosefu wa uwezo na nguvu kwetu kujiokoa na njia ya wokovu kupitia kwa Kristo Yesu. Ni kupitia kwa Kristo tunaweza kumgeukia Mungu kwa kutubu na kumwomba msamaha wa dhambi zetu. Wakati huo huo tukimpokea Kristo Yesu ambaye ni nabii, kuhani na mfalme na kumtegemea Yeye pekee ambaye ndiye Mwokozi kamili."

Tazama vile walivyosema kuhusu wokovu. Huwa tunaokoka kwa sababu huwa tumedhibitishiwa dhambi zetu, kuonyeshwa hatia yetu, hatari ambayo tukomo na ukosefu wa uwezo wa kujiokoa na njia ya wokovu kupitia kwa Kristo Yesu. Je, wokovu huu, hupatikana kwa njia gani? Jibu ni kwamba huwa unapatikana kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye huwa anatuzaa mara ya pili. Maandiko yao yanaweza kuambatanishwa na maandiko haya ya Biblia, "Basi, Mungu amewapa hata watu Mataifa toba iletayo uzima wa milele" (Matendo ya Mitume 11:18). Pia katika Waefeso 2:8 tunasoma kwamba, "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu."

Waefeso 2 ni kifungu muhimu sana kuhusu wokovu. Kulingana na Biblia, toba ni zawadi kutoka kwa Mungu na imani pia ni zawadi kutoka kwa Mungu. Huwa vinapeanwa si kwa sababu tumefanya jambo lolote zuri, bali kwa sababu Kristo alitufanyia kila kitu. Ikiwa unataka zawadi ya imani na toba, basi nenda Kwake Mungu kupitia kwa Kristo Yesu. Biblia inafundisha kwamba wokovu hunapatikana kupitia kwa neno la Mungu. Zaburi 19:7, inasema, "Sheria ya Bwana ni kamilifu, zikihuisha nafsi. Shuhuda za Bwana ni za kuaminika, zikimpa mjinga hekima."

Mara kwa mara tunapata katika Biblia kwamba wokovu hupatikana kupitia kwa mahubiri ya neno la Mungu. Mungu mwenyewe alipanga kwamba mambo yatakuwa hivi. "Kama vile mvua na theluji ishukavyo kutoka mbinguni, nayo hairudi tena huko bila kunywesha dunia na kuichipusha na kuistawisha, hivyo hutua mbegu kwa mpanzi na mkate kwa mlaji, ndivyo lilivyo neno langu lile litokalo kinywani mwangu. Halitanirudia tupu, bali litatimiliza lile nililokusudia na litafanikiwa katika kusudi lile nililolituma" (Isaya 55:10-11). Kuwa mwangalifu sana kwa maneno haya. Mungu hageahidi hili ikiwa Yeye mwenyewe si ndiye mwenye kuleta mazao, ambayo ndiyo wokovu wetu. Yaani watu wake wataitika Kwake. Tunasoma katika Matendo ya Mitume kwamba, kutokana na mahubiri ya injili katika mji wa Antiokia, "wote waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini" (Matendo ya Mitume 13:48). Yule ambaye amehubiri na yule ambaye amesikia na kuokoka, hakuna hata mmoja wao ambaye anaweza kutukuzwa katika jambo hili. Yule ambaye anaokoa si mhubiri, bali ni Mungu mwenyewe.

Wahubiri wa injili wameitwa kuwaelezea watu kwamba wanafaa kugeuka na kutoka katika dhambi zao na kumgeukia Mungu. Pia tunafaa kufahamu kwamba wakati Mungu anatuita kufanya kazi hii, Yeye hutuita kuhubiria watu ambao wamekufa kiroho, yaani kwa uwezo wao wenyewe hawawezi kuokoka. Hivi ndivyo Biblia inavyofafanua hali ya kiroho ya mwanadamu: Tunazaliwa tukiwa tumekufa kiroho (Waefeso 2). Je, wale ambao wamekufa kiroho watawezaje kumgeukia Mungu kwa imani? Wanaweza kufanya hivyo ikiwa Mungu mwenyewe atawapatia uhai wa kiroho. Je, Mungu huwa anawapatia uhai huu kwa njia gani? Tunasoma katika Agano la Kale na lile Jipya kwamba Mungu amechagua kuwapa uhai kiroho kupitia kwa mahubiri ya neno Lake. Tunaona jambo hili katika Ezekieli 37, maono ya mifupa ambayo ilikuwa imekauka. Mungu alimpatia Ezekieli maono ya kuenda na kuhubiria mifupa ambayo ilikuwa imekauka. Kupitia kwa mahubiri ya neno Lake, Roho Mtakatifu huwaletea uhai wa kiroho watu wake.

Katika Matendo ya Mitume 10 tunaona jambo hili vyema wakati Mungu alimwita Kornelio. Tunaweza kuwaza kwamba kwa sababu Mungu ni Mungu mwenye nguvu na mamlaka yote hakuhitaji kumtuma Peteo, bali angemwokoa tu Kornelio bila lake. Mungu hakumwokoa Kornelio bila yeye kusikia neno la Mungu kutoka kwa mtu ambaye alikuwa anamjua Mungu vyema. Mungu alimtuma Petro kwa nyumba ya Kornelio ili amhubirie Kornelio ujumbe wa injili. Ni kupitia kwa ujumbe huu Kornelio alipata kuokoka. Mmoja anaweza kujiuliza hivi, je ni kwa nini Mungu anatumia njia hii ndefu? Je, kwa nini asimwokoke tu mtu mara moja bila kutumia mahubiri ya neno lake? Unaposoma Biblia utapata kwamba kila mara Mungu alitumia njia hii. Mungu anapompa mtu uhai wa milele, Yeye hutumia mahubiri ya neno lake kufanya hivyo. Yeye hufanya jambo hili kupitia kwa habari njema ya Kristo Yesu. Yeye huwatumia watu wake kuhubiri habari hii kwa wote kwamba ni Kristo ambaye analeta mabadiliko ambayo tunahitaji. Hivi ndivyo Mungu anavyofanya kazi ya kuwaokoa watu wake na hivi ndivyo Amekuwa akifanya tangu kitambo. Mungu alikuwa na uwezo wa kumwokoa Kornelio bila kutumia Petro. Lakini alichagua amwokoe Kornelio kwa njia ambayo amekuwa akitumia siku zote; yaani kupitia kwa mahubiri ya neno lake. Baadaye Petro aliwaandikia wakristo akisema, "mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele" (1 Petro 1:23). Siku zote na katika nyakati zote, Mungu amekuwa akifanya hivi, kutoka kwa Nuhu, Abrahamu, Musa, taifa la Israeli, Yesu Kristo wakati aliwaita wanafunzi wake na hadi sasa bado Mungu anatumia njia hiyo hiyo. Kuhakikisha jambo hili, Bwana Yesu Kristo aliwaambia wanafunzi, "Si ninyi mlionichagua, bali Mimi ndiye niliyewachagua ninyi na kuwaweka mwenda mkazae matunda na matunda yenu yakapate kudumu" (Yohana 15:16). Hivi ndivyo Mungu amekuwa akifanya kazi yake.

Pia tunakumbushwa kuhusu maneno ya Petro siku ya Pentekote: "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu na kwa wale wote walio mbali na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu atamwita amjie" (Matendo ya Mitume 2:39). Baadaye Paulo alizungumza na wanawake fulani katika mji wa Filipi. Miongoni mwao alikuwa Lydia. Lydia alisikia ujumbe wa injili lakini ili aweze kuokoka, alihitaji kutii ujumbe huo. Alitii, lakini ilifanyika aje? Tunasoma kwamba, "Bwana akaufungua moyo wake akaupokea ujumbe wa Paulo" (Matendo ya Mitume 16:14). Hata Paulo mwenyewe alijua jambo hili kwamba ni Mungu ambaye anaokoa. Paulo alikutana na Kristo wakati alipokuwa anaenda kuwatatiza wakristo. Kristo mwenyewe alijidhihirsha kwa Paulo.

Katika Biblia kuna mifano mingi sana kuhusu jambo hili. Mara kwa mara Mungu ametuonyesha ukweli wa maneno ambayo Yohana alisema, "Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma mwanawe , ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Yohana 4:10). Huwa tunaonyesha kwamba tunafahamu kazi ya wokovu ni ya Mungu wakati tunaomba kwamba Mungu mwenyewe awaokoe watu wake. Kwa sababu tunafahamu kwamba ni Mungu ambaye anaokoa, basi tunafaa kumwomba kwamba atamtuma Roho Mtakatifu ili ujumbe wake wa injili uweze kuhubiriwa kwa uaminifu sana ili watu wake waweze kuokoka.

Kufahamu jambo hili vyema kabisa ni kuwa na afya kiroho. Kila kanisa ambalo linatumaini kuwa na afya kiroho, lazima washirika wake wafahamu jambo hili vyema kabisa. Ikiwa kuokoka kwako ni jambo ambalo linatukuza wewe na si Mungu, basi jua kwa hakika kwamba kweli umejidanya kabisa.

Mtu ambaye ameokoka ni lazima atende matendo mema. Ni lazima tujitolee kabisa katika wokovu na kufanya yale ambayo yanaambatana na wokovu wetu kulingana na Biblia. Lakini hata kama tunafanya mambo haya, tunafaa kujua kwamba wokovu ni zaidi ya kufanya matendo mema. Biblia inasema kwamba lazima mioyo yetu ibadilishwe na roho zipewe maisha mapya. Haya yote

hatuwezi kujifanyia. Mabadiliko ambayo kila mwanadamu anahitaji ni Mungu pekee ambaye anaweza kuyaleta. Kila mwanadamu anamhitjai Mungu ambadilishe.

Jambo ambalo linaogopesha sana ni kwamba makanisa mengi yamejawa na watu ambao wamejitolea kuishi maisha mazuri lakini ukweli ni kwamba wao hawajaokoka kamwe. Kwa mfano katika makanisa mengi kuna talaka nyingi sana. Je, kwa nini kuna jambo kama hili. Je, ni kweli kwamba wachungaji katika makanisa haya hawajahubiri vyema jambo la kuokoka? Je, inawezekana kuwa kwamba wao wamekuwa wakihubiri tu matendo mazuri na si wokovu wa kweli? Je, inawezekana kwamba wachungaji hawa wenyewe hawajaokoka na kwa hivyo hawaelewi kabisa wokovu ni nini? Kwa sababu ya haya, makanisa mengi leo hayana tofauti kubwa na vilabu vya burudani. Makosa haya ni ya wachungaji ambao wamekosa kuwa waaminifu katika majukumu yao ya uchungaji. Pia washirika wa makanisa haya ni wa kulaumiwa kwa sababu wao ndio wamewaacha wachungaji hawa waendelea katika tabia hii.

Kulingana na Biblia, toba na imani ni zawadi kutoka kwa Mungu kwetu. Wokovu wetu, mabadiliko yetu, yote yanafanyika kutokana na neema ya Mungu. Kwa hivyo katika haya tunaona kwamba mabadiliko yanahitajika na pia yanawezekana. Mabadiliko ambayo tunahitaji ni yale ambayo ni ya kuondoka katika maisha ya dhambi na kuishi maisha yetu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kufanya hivi, ni lazima tutubu dhambi zetu na kumwamini Kristo Yesu. Jambo hili linaweza tu kufanyika kwa neema ya Mungu kupitia kwa kuhubiri neno la Mungu.

Kwa sababu nimetoa mifano kutoka katika Biblia jinsi watu walivyookoka kwa kusikia na kutii neno la Mungu, basi ninajua kwamba sasa unaweza kuwa unajiuliza swali hili, je, kuna wale ambao wameokoka ambao ninaweza kujifunza kutoka kwao? Katika historia tunasoma kumhusu mtu mmoja ambaye aliitwa Augustine. Siku moja alipokuwa anatembea katika shamba alimsikia mtoto akisema, “chukua na usome, chukua na usome.” Augustine alikuwa akiishi maisha mabaya sana ya dhambi. Wakati aliposikia maneno haya, kando yake kulikuwa na Biblia ambayo ilikuwa na Agano Jipya pekee. Alichukua na kuifungua. Alipoifungua, alipate mistari hii katika kitabu cha Warumi ambayo ilisema, 'Nanyi fanyeni hivi, mkiutambua wakati tulio nao. Saa ya kuamka kutoka usingizini imewadia, kwa maana sasa wokovu wetu umekaribia zaidi kuliko hapo kwanza tulipoamini. Usiku umeendelea sana, mapambazuko yamekaribia. Kwa hiyo tuyaweke kando matendo ya giza na tuvae silaha za nuru. Basi na tuenende kwa adabu kama inavyopasa wakati wa mchana, si kwa kufanya karamu za ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uashareti, si kwa ugomvi na wivu. Bali jivikeni Bwana Yesu Kristo, wala msifikiri jinsi mtakavyotimiza tamaa za miili yenu yenye asili ya dhambi” (Warumi 13:11-13). Baada ya kusoma maneno haya, Augustine aliokoka.

Mwingine alikuwa Martin Luther ambaye alikuwa anatoka katika kanisa la Kikatoliki. Baada ya yeye kusoma vitabu vya Zaburi, Warumi na Wagalatia, alianza kuona kwamba haki ambayo Mungu anahitaji kutoka kwetu, ni haki ambayo haitoki kwetu bali kwa Mungu mwenyewe. Aliona kwamba haki hii ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa wote ambao wanamwamini Kristo Yesu. Baada ya kujua hili, alisema, “ni kama milango ya mbinguni ilikuwa imefunguliwa.”

Mwingine alikuwa anaitwa William Perkins kutoka mji wa Cambridge. Siku moja alipokuwa akitembea barabarani, alimsikia mama mmoja akimwambia mwanawe kwamba, “jichunge sana wewe, huenda utakuwa kama Perkins mlevi!” Mungu alitumia maneno haya kumdhitishia Perkins kuhusu maisha yake ya ulevi ambayo alikuwa akiishi. Aliona kwamba maisha yake ya ulevi yalikuwa mabaya kiwango kwamba hata jina lake lilikuwa linatumika kuwaonya wengine. Mungu alimdhibitishia dhambi zake na kumfanya aje kwa Kristo Yesu kwa ajili ya wokovu wake.

Mwingine pia alikuwa anaitwa John Bunyan. Siku moja aliwasikia wamama wawili wakizungumza kumhusu Mungu. Tangu wakati huo, hakuyasahau maneno ambayo wale wamama walikuwa wakiyazungumza. Mungu alitumia maneno hayo kumdhibitishia dhambi zake. Ndani mwake, aliaanza kujiuliza kama kuna kitu ambacho hakuwa nacho. Alijiuliza hili swali, “je mtu anaweza kumjua Mungu?” Huu Bunyan kwa miaka miwili alikuwa akisoma Biblia pamoja na mke wake ambaye alikuwa ameokoka. Mungu alitumia njia hii kumleta Bunyan kwa Kristo.

Mwingine alikuwa Spurgeon. Wakati moja kulikuwa na mawingu makali ya barafu. Aliingia katika kanisa na kuketi nyuma akiwa peke yake kwa sababu kanisa hilo halikuwa na watu wengi ndani. Shamasi mmoja wa kanisa hilo alimtazama alikuwa anahubiri na katika mahubiri yake, alimtazama Spurgeon na kusema, “Mtazame tu Kristo Yesu. Unahitaji kufanya hivyo, mtazame Kristo Yesu.” Alisema maneno haya mara kwa mara, “Mtazame tu Kristo! Mtazame tu Kristo!” Mungu alitumia maneno haya kumwokoa Spurgeon.

Mungu ametumia njia nyingi kutuletea neno lake ambalo ndilo linaokoa. Lakini kila wakati amelituma neno lake, amelituma ili aweze kutupatia toba na imani. Anafanya hivyo ili tuweze kutoka katika dhambi zetu na tumgeukie Yeye na tuokoke. Haya ndio mabadiliko ambayo tunahitaji kwa kweli.

Wale wote ambao wanawaza kwamba mtu hawezi kubadilishwa, ukweli ni kwamba kwa siku nyingi, Mungu amewabadilisha wengi na kuwaokoa. Ninajua kwamba kwa neema ya Mungu kuna wengi ambao wamebadilika kabisa. Ukweli ni kwamba mabadiliko haya yanawezekana kwa Mungu. Wakristo wote wanakubaliana katika hili kwamba, maisha yetu ya sasa ni maisha ambayo yamebadilishwa kabisa.

Kwa kawaida wanadamu wanabadilishwa na vile vitu ambavyo wanavipenda sana. Ukweli ni kwamba mabadiliko haya kulingana na vitu ambavyo wanavipenda ni ya muda tu. Kwa mfano, maisha ya mtu huwa inakua na kubadilishwa na kufafana na vile vitu ambayo anaabudu. Mtu yeyote akiwa ni kweli atajiona kwamba yeye ni kama yule mungu ambaye anaabudu.

Wengi wetu baada ya kujiona hivi, tumeona kwamba kweli tunahitaji kuokoka. Kwa neema ya Mungu, tumeokolewa. Ikiwa wewe hujaokoka, basi unahitaji kugeuka kutoka katika dhambi zako na kumgeukia Mungu. Wewe mwenyewe huwezi kujibadilisha na kuweza kufanya mapenzi ya Mungu. Habari njema kwako ni kwamba Mungu anaweza kukuokoa na kukubadilisha kabisa. Kile unahitaji ni kutii maneno ya Kristo Yesu: “Tubuni na kuiamini Habari Njema” (Marko 1:15).

Ishara ya 5

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kanisa ambalo lifahamu mafundisho ya Biblia kuhusu kumshuhudia Kristo

katika sura hii

1. Je, ni nani ambaye anafaa kushuhudia?

2. Je, tunafaa kushuhudia kwa njia gani?
(a) Waambie watu kwamba ikiwa watatubu dhambi zao na kuamini wataokolewa. Pia waeleze kwamba uamuzi huo utawagharimu sana
(b) Waambie watu umuhimu wa kufanya uamuzi wa kuokoka kwa haraka sana.
(c) Waambie watu hata kama uamuzi huu wa kuokoka unaonekana kuwa mgumu sana kufanya, ni uamuzi bora zaidi kufanywa.
(d) Tumia Biblia katika juhudi zako za kushuhudia
(e) Kumbuka kwamba maisha ya washirika wote na kanisa kwa ujumla ni msingi mkuu katika kazi ya kushuhudia Kristo.
(f) Kumbuka kuomba.

3. Je, kushuhudia Kristo ni kufanya nini?
(a) Si kuwalazimisha watu kutubu
(b) Si kutoa ushuhuda kukuhusu wewe
(c) si kukutetea haki au kufanya siasa.
(d) Si kutetea mafundisho ya Biblia
(e) Kazi yetu ni kuhubiri na si kuwaokoa watu.

4. Kwa nini tunafaa kushuhudia?
(a) Ni kutii amri ya Kristo Yesu (Mathayo 28:18-20)
(b) Ni kwa sababu tunawapenda wale wote ambao wamepotea katika dhambi zao.
(c) Ni kwa sababu tunampenda Mungu.

Je, wewe huwaza nini wakati unasikia neno kushuhudia? Je, wewe huwaza kuhusu wainjilisti wakuu kama Billy Graham? Au unawaza kumhusu yule mtu katika kitabu ambacho kinaitwa Msafiri?

Je, unaposikia mtu ambaye anashuhudia Kristo, wewe huwaza kuhusu mtu matakatifu au mtu mwenye kuwadanganya wengi? Kuhushudia ni jambo ambalo zinazungumziwa sana leo. Tunapowaza kuhusu kumshuhudia Kristo leo, je kushuhudia ni kupigana vita dhidi ya watu dini zingine au madhehebu mengine? Wakati jambo hili la kushuhudia Kristo linazungumziwa, maswali mengi na hisia nyingi huzuka. Kuna wakristo ambao huwa wanajihisi kwamba hawajafanya lolote katika jambo hili. Huenda labda huwa hawaelewi ni nini wanafaa kufanya na jinsi wanafaa kufanya. Hawa wakristo wako katika hali mbaya sana. Mojawapo ya ishara za kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kwamba kanisa hilo linaelewa vyema mafundisho ya Biblia kuhusu kushuhudia wengine Kristo na jinsi linafaa kutekeleza jambo hili. Hili ndilo jambo ambalo tutazungumzia katika sura hii kwa sababu ni jambo la maana sana kufahamu kwa washirika wote wa kanisa na wakristo wote popote walipo. Ni jukumu la kanisa kushuhudia Kristo kwa wote bila kuwabagua kwa misingi yoyote ile.

Unakumbuka wakati nilipokuwa ninaanza kitabu hiki, nilisema kwamba sura ya 3,4 na ya 5 kwa karibu zinaonekana kufundisha jambo moja ambalo ni wokovu. Lakini katika kila sura jambo hili la wokovu linashughulikiwa kwa njia tofauti. Katika sura ya 4 tulitazama wokovu ambao ndio mabadiliko ambayo yanatendeka katika maisha ya mtu. Tulifanya hivyo kwa kutazama jinsi Biblia inavyofundisha jambo hili. Katika sura ya 3, tulitazama yale ambayo yanajumlisha wokovu. Katika sura hii, tutatazama jinsi ya kuwaelezea wengi kuhusu ujumbe mkuu ya Biblia ambao umetubadilisha. Je, tunafaa kushuhudia wengine kwa njia gani? Je, kushuhudia ni kufanya nini na ni kwa nini tunafaa kushuhudia? Ili tuweze kufahamu vyema jambo hili, tutajiuliza maswali yafuatayo.

1. Je, ni nani ambaye anafaa kushuhudia Kristo?
2. Je, tunafaa kushuhudia kwa njia gani?
3. Je, kushuhudia ni kufanya nini?
4. Je, ni kwa nini tushuhudie Kristo?

Haya maswali manne, yote yanalenga jambo moja tu, kushuhudia Kristo na jinsi ya kufanya kazi hii vyema kwa utukufu wa Mungu pekee. Majibu kwa maswali haya ni sawa yote. Lakini haya maswali yatatuonyesha vyema kabisa jinsi tunafaa kufahamu jambo hili la kushuhudia Kristo. Ukweli ni kwamba hatuwezi kujibu kila swali kuhusu jambo hili la kushuhudia lakini ninajua kwamba yale ambayo yatasemwa hapa yatatusaidia kufahamu zaidi na kuwa watiifu kwa Mungu. Pia tutasaidika kuwa na makanisa ambayo yananawili kiroho katika jambo hili la kushuhudia Kristo. Kabla sijaendelea, ningependa kuwahimiza wasomaji wangu kwamba ikiwa mnaweza, tafuteni vitabu hivi vifuatavyo kwa sababu vitawasaidia zaidi katika kufahamu jambo hili ka kushuhudia Kristo. Hivi ni,

1. “Tell the Truth” ambacho kimeandikwa na Will Metzger katika lugha ya kingereza. Kitabu hiki ni moja wa vitabu bora sana ambavyo vimeandikwa vikifundisha kuhusu jambo hili la kushuhudia Kristo. Kitakusaidia sana kukuonyesha jinsi ya kufanya kazi hii na kukuwezesha kufahamu mafundisho ya injili na jinsi unafaa kueleza ujumbe wa injili kwa watu wote.

2. “Speaking of Jesus” ambacho kimeandikwa na Mack Stiles katika lugha ya kingereza. Kitabu hiki kimejawa na hadithi ambazo zitakusaidia sana kushuhudia wengi kumhusu Kristo. Pia katika kitabu hiki, kuna mifano ya watu ambao waliokoka baada ya kushuhudiwa.

3. “Revival and Revivalism” ambacho kimeandikwa na Iain Murray katika lugha ya kingereza. Hiki ni kitabu ambacho ni kizuri sana kwako kusoma. Katika kitabu hiki, mwandishi anatuonyesha jinsi kazi hii ya kushuhudia Kristo katika nchi ya Amerika ilivyobadilika kati ya miaka wa 1750-1858 na mafundisho kutoka kwa mabadiliko haya.

4. “Evangelism and the sovereignty of God” ambacho kimeandikwa na J.I Packer. Hiki ni kitabu kifupi sana na ni kizuri sana. Kina sura 4 pekee na kurasa chini ya 100. Kitabu hiki kinajibu maswali kuhusu kushuhudia Kristo kulingana na Biblia.

Je, ni nani ambaye anafaa kushuhudia Kristo?

Haijalishi mtu atahisi aje kuhusu jambo hili la kushuhudia Kristo, ukweli ni kwamba hili ni jambo ambalo hatuwezi kupuuza haswa ikiwa sisi tunasoma Biblia zetu kila siku. Jambo hili la kushuhudia linapatikana katika Agano Jipya lote. Vifungu kuhusu kueneza injili vinapatikana kuanzia mwanzo mwa Agano hilo hadi mwisho mwa Agano hilo. Paulo aliwaandikia Warumi akisema, "Mimi ni mdeni kwa Wayunani na wasio Wayunani, kwa wenye hekima na wasio wenye hekima. Ndiyo sababu ninatamani sana kuihubiri injili kwenu pia ninyi mlioko Rumi" (Warumi 1:14-15). Hapa Paulo anatueleza kwamba yeye ni mtu ambaye alikuwa ameitwa kumshuhudia Kristo kwa watu wote. Je, maneno haya yalimhusu yeye pekee na mitume pekee au pia hata sisi leo tunafaa kuyatii?

Tunaposoma Agano Jipya, hatupati kwamba mwito wa kushuhudia Kristo ulikuwa kwa Paulo na mitume wa Kristo pekee. Kristo alisema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa sababu hii enendeni ulimwenguni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafuzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, nanyi wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaamuru ninyi. Hakika Mimi niko pamoja nanyi sikuzote, hadi mwisho wa nyakati. Amen" (Mathayo 28:18-20). Maneno haya ya Bwana Yesu Kristo ni kwa wote ambao wamemwamini. Ni wazi kabisa wakati tunasoma Agano Jipya Mitume wa Kristo walitii maneno haya ya Kristo na walipeleka ujumbe wa injili kwa watu wote kila mahali. Unaposoma vitabu vya Biblia ambavyo viliandikwa na mitume pamoja kitabu cha Matendo ya Mitume, utaona kwamba mara kwa mara wao walikuwa wakifanya kazi hii ya kushuhudia Kristo kwa watu wote (Matendo ya Mitume 5:42; 8:25; 13:32; 14:7; 15; 21; 15:35; 16:10; 17:18).

Leo kuna wengi ambao wanajiuliza, je ni nani ambaye anafaa kushuhudia? Je, ni wahubiri wa injili pekee na wachungaji? Je, kushuhudia Kristo kunafaa kuwa siku moja ambayo ni Jumapili pekee wakati mchungaji anasimama katika madhabahu na kuhubiri? Je, hivi ndivyo kanisa lako linavyoshuhudia Kristo? Je, kazi ya kushuhudia ni kazi ya watu fulani tu au ni kazi ya wakristo wote? Unaposoma Biblia utaona kwamba, kazi hii ya kushuhudia ni kazi ambayo imepewa wakristo wote ulimwenguni kote. Unaposoma kitabu cha Matendo ya Mitume, utaona kwamba wakristo walitii Kristo kwa kujitolea kufanya kazi hii kwa sababu walifahamu kwamba hili lilikuwa jukumu lao. Katika kitabu hiki, hatusomi kwamba ni mitume peke yao ambao walihubiri injili. Katika Matendo ya Mitume 8:1-4 tunasoma, "Siku ile kukatukia mateso makuu dhidi ya kanisa huko Yerusalemu, waamini wote isipokuwa mitume wakatawanyika, wakakimbilia Uyahudi na Samaria. Watu wacha Mungu wakamzika Stefano na kumwombolezea sana. Lakini kwa habari ya Sauli alikuwa analiharibu kanisa, akiingia nyumba kwa nyumba, akiwaburuta wanawake, wanaume na kuwatia gerezani. Kwa hiyo wale waliotawanyika wakalihubiri neno la Mungu kila mahali walipokwenda." Si mitume ambao wanazungumziwa hapa kwamba walienda wakahubiri injili. Mistari hii inazungumza kuhusu wale ambao walikuwa wametawanyika kote (mstari wa 4) isipokuwa mitume. Mtu mwingine anaweza kusema kwamba kazi hii ni ya wachungaji pekee. Lakini unaposoma sura yote ya 8 ya kitabu hiki cha Matendo ya Mitume, utaona kwamba Filipo ambaye alikuwa shamasi ndiye tunaona akihubiri katika sehemu tofauti tofauti (Matendo Ya mitume 8:5-12, 26-40).

Katika matendo ya mitume 11:19-21, tunaona jambo hili likiendelea. Wale ambao walikuwa wametawanyika kwa sababu ya mateso baada ya kuwaua kwa Stefano, walienda mbali hadi, Foinike, Kipro na Antiokia wakiwahubiria Wayahudi ujumbe wa injili. Wengine walienda Kipro na Kirene na walianza kuwahubiria Wagiriki habari njema kuhusu Kristo Yesu. Katika kazi hii yote Mungu alikuwa pamoja nao na watu wengi waliamini na kumgeukia Mungu. Katika haya yote tunaona wakristo wengine kando na mitume wakieneza injili ya Kristo Yesu. Petro anawahimiza wakristo wote kwamba, "Siku zote mwe tayari kumjibu mtu ye yote atakayewauliza kuhusu tumaini lililomo ndani yenu. Lakini fanyeni hivi kwa upole na kwa heshima" (1 Petro 3:15). Petro aliandika haya kwa kanisa lote na si kwa viongozi wa makanisa pekee. Wakristo wote wana jukumu la kueneza injili ya Kristo Yesu kwa watu wote bila kuwabagua. Kazi hii ya kuhubiri injili itafanywa vyema ikiwa wakristo watapendana. Yesu Kristo alisema, "Amri mpya nawapa: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane. Kama mkipendana ninyi kwa ninyi, kwa njia hii, watu wote watajua kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu" (Yohana 13:34-35). Ikiwa wewe huonyeshi upendo kwa kila mshirika wa kanisa lako, wewe unaishi katika kutomtii Mungu na unazuia kazi ya kueneza injili ya kanisa lako. Mara mingi wakristo hupuuza jukumu hili la kueneza injili na kusema kwamba ni la wachungaji. Wao hufanya hivi kwa sababu huwa hawajui jinsi ya kufanya kazi hii.

Je, tunafaa kushuhudia kwa njia gani?

Je, tunafaa kuhushudia kwa njia gani? Jibu rahisi kwa swali hili ni, kwa kuhubiri neno la Mungu. Huu ni ukweli kwa sababu hivi ndivyo tunavyowaelezea wengi kumhusu Kristo. Lakini jambo hili linafaa kufanywa kwa njia gani? Hili ni swali la maana sana na linafaa kuzingatiwa sana.

Je, tunafaa kushuhudia kwa njia gani? Tunafaa kuanza aje ili tuwaelezea watu kuhusu injili ya Kristo? Je, ni kwa njia gani mtu anaweza kupata ujumbe huu wa injili kwamba Kristo ndiye Mwokozi? Je, wote wanafaa kuja kanisani ndipo wasikie mahubiri ya injili? Ukweli ni kwamba wote hawatakuja. Ikiwa mambo ni hivi, basi inafaa tufanye nini? Je, tutaeneza ujumbe wa injili namna gani? Je, tutawafikiaje watu na ujumbe wa injili?

Ukweli ni kwamba tunaweza kueneza ujumbe wa injili kupitia kwa vyombo vya habari kama runinga au redio, pia kupitia kwa mikutano ya injili, pia kupitia kwa kuzungumza na mmoja au kupitia vijitabu vya injili. Hata kama kuna mambo haya yote, je, tunafaa kushuhudia kwa njia gani ambayo ni sawa? Kuna mambo sita kutoka kwa Biblia kuhusu jinsi tunafaa kufanya kazi hii.

(a) Waambie watu kwamba ikiwa watatubu dhambi zao na kuamini wataokolewa. Pia waeleze kwamba uamuzi huo utawagharimu sana.

Ni lazima tuwe tayari kuwaambia watu ukweli wote ambao unapatikana katika Biblia bila uoga wowote. Watu wengi huwa hawataki kusema jambo ambalo wanaona kuwa linaweza kumfanya yule ambaye anamzungumzia kukataa kuokoka hata kama jambo hilo linatoka kwa Biblia. Mambo kama dhambi na hatia ya dhambi, toba na dhabihu ambayo ilitolewa kwa ajili ya msamaha wa dhambi, ni mambo ambayo wengi huwa hawataki kuzungumzia katika kazi yao ya kushuhudia Kristo. Huwa wengi hawataki ujumbe wa injili uhubiriwe kwa njia hii. Kuna mchungaji ambaye alisema kwamba, kuhubiri mambo kama dhambi na Kristo kuwa njia ya pekee ya kuingia mbinguni ni kuweka kizuizi kikubwa sana mbele ya wale ambao wanataka kuokoka. Kuna wengi kama huyu mchungaji ambao wanapinga mahubiri ya kweli ya Biblia. Wao wanawaza kwamba ikiwa utawaeleza watu kuhusu dhambi zao, wao hawataokoka. Wao wanawaza kwamba watu wanafaa kuhubiri mambo ambayo itafanya mioyo yao iwe na furaha, ndiyo mambo ambayo itawafanya wengi waokoke. Kulingana na Biblia, kuwaeleza watu kuhusu dhambi zao na hali yao mbaya, ni mojawapo ya kueneza injili ya Kristo Yesu. Tunaposoma mahubiri ya Petro katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura za kwanza, tunaona kwamba Petro hakuwa na uoga wowote kuwahubiria watu ukweli kuhusu dhambi zao. Katika kazi zetu za kueneza injili, hatuwezi kudhania tu

kwamba haya ni mambo ambayo watu wanayajua. Biblia inafundisha kwamba kwa asili kila mwanadamu ni mwasi dhidi ya Mungu. Ni lazima tuhubiri jambo hili kikamilifu. Ninajua kwamba hili si jambo rahisi kusema, ilhali ni lazima lisemwe kwa sababu huu ndiyo ukweli wa hali ya mwanadamu ambaye hajaokoka. Kuficha mambo mengine ya ukweli wakati tunaeneza injili ya Kristo, ni kukosa kuwa waaminifu kwa ujumbe wa injili na kwa Mungu mwenyewe. Hii ni kama kutangaza bidhaa fulani, lakini uwe umeficha bei ya bidhaa hizo.

(b) Waambie watu umuhimu wa kufanya uamuzi wa kuokoka kwa haraka sana.

Ni lazima tuwaonyeshe watu umuhimu wa kufanya uamuzi wa kuokoka kwa haraka sana na kwamba hawafai kungoja hadi wakati fulani ndipo waokoke. Ni lazima tuwaeleze kwamba wasiwe kama wale ambao wanajaribu bidhaa tofauti tofauti kabla ya wao kufanya uamuzi wanataka bidhaa gani. Ujumbe wa injili ya Kristo ni ule ule ambao unaokoa. Kwa hivyo hakuna ujumbe mwingine ambao mtu yeyote anafaa kuhubiri ili watu waweze kuokoka. Kulingana na neno la Mungu, Yesu Kristo ndiye njia ya pekee ya kufika kwa Mungu (Yohana 14:6; Matendo ya Mitume 4:12; Warumi 10). Je, Biblia inapeana njia nyingine kando na Kristo ambapo mwanadamu anaweza kupatanishwa na Mungu Mtakatifu? Ukweli ni kwamba hakuna njia nyingine kando na Kristo na ikiwa Kristo ndiye njia ya pekee, je mwenye dhambi anangoja nini? Biblia inasema, “Leo, kama mkiisikia sauti Yake, msifanye migumu mioyo yenu” (Waebrania 4:7). Unaposoma mafundisho ya Kristo Yesu, utaona kwamba katika mafundisho yake, aliwasihi wenye dhambi wasichelewe kufanya uamuzi wa kuokoka. Kwa mfano tunasoma, “Kisha Yesu akawaambia mfano huu: “Mtu mmoja alikuwa na mtini uliopandwa katika shamba lake la mizabibu, akaja ili kutafuta tini kwenye mti huo, lakini hakupata hata moja. Hivyo akamwambia mtunza shamba: 'Tazama, kwa muda wa miaka mitatu sasa nimekuwa nikija kutafuta matunda kwenye mtini huu, nami sikupata hata moja. Ukate! Kwa nini uendelee kuharibu ardhi?' Yule mtunza shamba akamjibu, 'Bwana, uache tena kwa mwaka mmoja zaidi, nami nitaupalilia na kuuwekea mbolea. Kama ukizaa matunda mwaka ujao, vema, la sivyo ukate” (Luka 13:6-9).

Si jambo baya kuwaelezea wenye dhambi kwamba wasipotubu dhambi zao wataangamia. Huu ni ukweli ambao kamwe hatufai kuuficha kutoka kwa watu ikiwa tunatarajia Mungu awaokoe. Mungu anampatia kila mtu na nafasi ya kuokoka lakini nafasi hiyo haiwezi kuendelea kuwepo milele. Mungu anatarajia kila mtu ambaye hajaokoka wakati anaposikia ujumbe wa injili ya Kristo, atii ujumbe huo kwa kuokoka. Kwa kawaida, historia huwa inajirudia kila mara. Lakini ukweli ni kwamba kuna siku ambapo Mungu atakomesha kila kitu, yaani kutakuwa na wakati wa mwisho wa kila kitu. Mungu ndiye ametupatia uhai na siku moja atachukua uhai huo. Tuna wakati mfupi sana wa kuishi hapa ulimwenguni na jinsi tunavyotumia wakati huu ni jambo la muhimu sana. Paulo aliwahimiza watu wa Efeso kwamba watumie muda wao vyema kabisa (Waefeso 5:16).

Ni vyema ikiwa kila mkristo anatumia muda wake kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tusiwe watu wa kuwaza kwamba wacha sasa nifurahie halafu baada ya miaka mingi na nimekuwa mzee basi nitaokoka na ndipo nitakapojitolea kufanya kazi ya Mungu. Ni lazima sote tukumbuke kwamba wakati ambao tunao ni mfupi sana. Biblia inasema, “Lakini ndugu zangu, nina maana kwamba muda uliobaki ni mfupi. Tangu sasa wale waliooa waishi kama wasio na wake nao wanaoomboleza, kama ambao hawaombolezi, wenye furaha kama wasiokuwa nayo, wale wanaonunua , kama vile vitu walivyonunua si mali yao, nao wale wanaoshughulika na vitu vya dunia hii, kama ambao hawahusiki navyo. Kwa maana dunia hii kama tunavyoiona sasa inapita” (1 Wakorintho 7:29-31). Je, ni hali gani ambayo ukomo sasa ambamo hutakuwamo kila wakati? Je, unatumia aje hali hiyo kwa utukufu wa Mungu? Mwamini Mungu kwamba atakutumia katika hali hiyo badala ya kila wakati kumwamini Mungu akufungulie mlango mwingine. Mwamini Mungu akutumie sasa badala ya kungoja wakati mwingine kwa sababu hata hujui kama huo wakati mwingine utakuwepo. Usikubali kudanganywa na vitu vya ulimwengu huu au mambo fulani fulani. Hizi ni nyakati za uovu (Waefeso 5:16), yaani hizi ni siku hatari sana na kwa hivyo lazima tukomboe wakati. Ni lazima tutumie kila wakati vyema kabisa kwa utukufu wa Mungu. Kama Paulo, tutasema, “Kwa kuwa sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apate kulipwa kwa ajili ya yale ambayo yametendwa katika mwili wake, yakiwa mema au mabaya. Basi, kwa kuwa tunajua kumcha Bwana, tunajitahidi kuwavuta wengine, lakini Mungu anatufahamu dhahiri, nami natumaini kwamba tu dhahiri katika dhamira zenu pia. Siyo kwamba tunajaribu kujistahilisha kwenu tena, lakini tunataka kuwapa nafasi ili mwone fahari juu yetu mweze kuwajibu hao wanaoona fahari juu ya mambo yaliyo moyoni. Kama tumerukwa na akili timamu ni kwa ajili yenu. Kwa kuwa upendo wa Kristo unatutia nguvu, kwa sababu tunasadiki kuwa mmoja alikufa kwa ajili ya wote, kwa hiyo wote walikufa” (2 Wakorintho 5:10-14).

(c) Waambie watu hata kama uamuzi huu wa kuokoka unaonekana kuwa mgumu sana kufanya, ni uamuzi bora zaidi kufanywa.

Katika kitabu cha Waebrania tunasoma kuwahusu wale ambao waliteseka sana kwa ajili ya imani yao ndani ya Kristo Yesu, lakini walivumilia. Katika Waebrania 12, tunasoma kumhusu Kristo Yesu mwenyewe kwamba alivumilia msalaba ambao ulikuwa mbele Yake.

Je, wakati tunakuja kwa Kristo na kuokoka, huwa tunapata nini? Huwa tunapata kuwa na uhusiano na ushirika na Mungu. Huwa tunapata msamaha wa dhambi zetu, uhuru kutoka kwa shetani na dhambi, tunaingia jamii ya Mungu, tunapata hakikisho la kuingia mbinguni na tumaini ambalo ni milele. Kusema ukweli kuhusu matatizo na mateso ambayo wakristo wanakumbana nayo wakati tunaeneza injili, si kuondoa baraka za wokovu. Hii haimaanishi pia kwamba sasa ni lazima kila wakati tuhubiri mateso ya ukristo. Tunafaa kila wakati kusema ukweli na kuwaambia wote kwamba kuna habari njema kwa mwenye dhambi ndani ya Kristo Yesu. Hata kama kuna mateso na matatizo katika ukristo, ni bora zaidi kuteseka na kutatizwa kwa sababu ya kumfuata Kristo kuliko mambo mengine yoyote.

(d) Tumia Biblia katika juhudi zako za kushuhudia.

Hatufai tu kutumia Biblia wakati tunawahubiria wengi katika kanisa. Tunafaa kujifundisha Biblia sisi wenyewe na pia kuwafundisha Biblia hiyo wengine. Kwa kutumia Biblia hii, unawaonyesha wale ambao unawafundisha kwamba yale ambayo unasema si mawazo yako wala maoni yako. Katika Matendo ya Mitume 8, tunamwona Filipo akimfundisha Towashi wa Kushi Biblia. Filipo alianza na Agano la Kale na alitumia neno hilo kumweleza huyu Towashi kumhusu Kristo Yesu.

Tunapoatumia Biblia wakati tunawaeleza wengine kumhusu Kristo, tunawaonyesha watu kwamba huwa hatusemi tu mambo yetu au maoni yetu, bali huwa tunasema yale ambayo Mungu ameandika katika neno Lake.

(e) Kumbuka kwamba maisha ya washirika wote na kanisa kwa ujumla ni msingi mkuu katika kazi ya kushuhudia Kristo.

Maisha yetu na yale ya washirika wenzetu wa kanisa yanafaa kuwa ushuhuda kwa injili ambayo tunahubiri. Hii ni mojawapo wa sababu kwa nini kuwa mshirika wa kanisa fulani ni jambo la maana sana. Kanisa lote linafaa kuonyesha ulimwengu wote inamaanisha nini kuwa mkristo. Tunafaa kufahamu vyema maana ya kuwa mshirika wa kanisa na pia tuwasaidie wakristo wenzetu kufahamu jambo hili. Mungu hatukuzwi tu katika maneno ambayo tuyazungumza, bali pia katika maisha ambayo tuyaishi. Hii haimaanishi kwamba wakristo ni watu ambao wamekamilika kabisa. Bali inamaanisha kwamba wakristo wanajitahidi kila siku kuishi maisha ambayo yanaambatana na neno la Mungu. Yesu Kristo katika mahubiri yake mlimani alisema, "Vivyo hivyo, nuru yenu iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16; 1 Petro 2:12). Hapa Kristo alikuwa anazungumza kuhusu jinsi tunafaa kuishi maisha yetu. Ikiwa tutaishi maisha matakatifu, wengi wataona na huenda wataamini ujumbe wa injili na kuokoka.

Kumbuka kwamba jambo hili linajumlisha jinsi washirika wote wa kanisa lako wanavyoishi maisha yao. Kristo Yesu alisema, "Amri mpya nawapa: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane. Kama mkipendana ninyi kwa ninyi, kwa njia hii, watu wote watajua kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu" (Yohana 13:34-35). Ishi maisha yako kwa upendo juu ya washirika wenzako kwa sababu huu ni msingi wa utakatifu wako na huduma wa kazi yako ya uinjilisti. Maisha yetu pekee haiyatoshi kuwa ushuhuda. Maisha yetu pamoja na ya wale ambao tunashiriki nao ni ushuhuda mkubwa sana katika kazi ya kumshuhudia Kristo.

(f) Kumbuka kuomba.

Kumbuka kwamba maombi ni jambo muhimu sana katika haya yote kwa sababu wokovu ni kazi ya Mungu na si yako wala ya mtu mwingine yeyote. Mwombe Mungu kwamba atakusaidia katika huduma huu wa kuhubiri neno lake kwa uaminifu. Pia omba kwamba Mungu atawaokoa wengi ambao utawafikia na ujumbe wa injili.

Je, kushuhudia Kristo ni kufanya nini?

Mara mingi huwa tunakosa kushuhudia vyema kwa sababu huwa hatujaelewa kushuhudia Kristo ni kufanya nini. Kwa sababu hii, tutajiuliza swali hili; Kushuhudia Kristo ni kufanya nini? Kuna mambo kadhaa ambayo watu wengi huwaza kwamba mambo hayo ni kushuhudia Kristo. Baadhi yao ni haya:

1. Kushuhudia Kristo si kuwalazimisha watu kutubu.

Kuna wale ambao wanawaza kwamba kushuhudia Kristo ni kuwalazimisha watu waokoke. Ikiwa mtu anaelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kushuhudia Kristo, basi atafahamu kwamba kushuhudia Kristo si kuwalazimishia watu mambo yale ambayo tunaamini. Wakati tunafanya kazi hii, tunafaa kufahamu kwamba, mambo ambayo sisi wakristo tunayaamini ni ya kweli. Mambo haya si mawazo tu ya watu fulani. Pia mambo haya ambayo tuyaamini na kuyatangaza si yetu wala hayatoka kwa wanadamu. Tunatangaza neno la Mungu na si mawazo yetu au ya mwanadamu yeyote. Wakati unashuhudia Kristo, huwa unaeneza ukweli kuhusu dini ya ukristo.

Wakati tunamshuhudia Kristo, huwa hatumlazimishi yeyote kuamini kile tunaamini. Kulingana na Biblia, kushuhudia Kristo ni kuwaelezea wengi habari njema na si kuhakikisha kwamba wameokoka au la kwa sababu kazi hiyo ya kuhakikisha wameokoka au la si yetu, ni kazi ya Mungu. Kulingana na Biblia, mazao ya kueneza injili ni kazi ya Mungu na si kazi ya mwanadamu na mbinu zake au elimu yake au tamaa yake. Biblia inasema, "Kwani, Apolo ni nani? Naye Paulo ni nani? Ni watumishi ambao kwa kupitia wao mliamini. Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye alikuza. Hivyo mwenye kupanda mbegu ni sawa na yule atiaye maji. Kila mmoja atalipwa kulingana na kazi yake" (1 Wakorintho 3:5-7; 2 Wakorintho 3:5-6).

Hili ni jambo muhimu sana ambalo tunafaa kulizingatia sana ikizingatiwa sana kwamba tunaishi katika ulimwengu ambao unachukia Kristo na haupendi neno lake. Wakati nilipokuwa katika chuo kikuu nilikuwa na rafiki wawili, mmoja alikuwa mwislamu na mwingine hakuwa na dini yoyote. Mimi nilikuwa na nia ya kumhubiria huyu ambaye alikuwa hana dini na pia rafiki mwislamu alikuwa na nia ya kumbadilisha awe mwislamu. Siku moja tulipokuwa tunazungumza, rafiki wangu mwislamu akasema, 'Nimechoka na nchi ya wakristo ambayo viongozi wake wote ni wezi." Nami nikamjibu, 'nchi hii, si nchi ya wakristo. Kwa ukweli hakuna nchi ambayo ni ya wakristo ulimwenguni kote. Rafiki wangu alijibu, 'Hii ndiyo ubaya wa dini ya ukristo. Dini hii haitatui lolote katika maisha ya watu na pia haina mipango ya kuwasaidia watu kuishi maisha mazuri. Nilimjibu kwamba, 'Hii ni kwa sababu wakristo huwa wanaonyesha ukweli kuhusu hali ya mwanadamu.' Aliniuliza, je unamaanishi nini? Nilimjibu, dini ya Kislamu, ni dini ambayo inafikiria kwamba shida za mwanadamu zitatuliwa kwa kuishi maisha mazuri. Kulingana na dini hii, ikiwa mtu anataka kuwa mtu mzuri anaweza kufanya uamuzi huo hapo na hapo. Lakini dini ya ukristo haiko hivyo. Dini ya ukristo inafundisha kwamba, kuna shida kubwa sana kando na tabia ambayo tunaona kwa macho yetu. Dini ya ukristo inafundisha kwamba mwanadamu ameanguka katika dhambi kabisa na kwa hivyo moyo wake wote ni mbaya na hauwezi kutoa lolote ambalo ni zuri. Huu ni moyo ambao haupendi Mungu na kila wakati unamwasi Mungu. Dini ya ukristo haifundishi kwamba shida hii ambayo mwanadamu ako nayo inaweza tatuliwa na nguvu za mwanadamu au uwezo wake. Kwa wazi kabisa nilimwambia rafiki wangu kwamba, 'ninaweza kumwogopesha mtu kwa kutisha maisha yake ili awe mwislamu.' Alijibu, 'hiyo ni kweli.' Nikaendelea kumwambia, 'Siwezi kutisha maisha ya mtu ili nimfanye awe mkristo. Kuwa mkristo haijumlishi tu kufanya hili au kufanya lile au kufuata sheria fulani na kukosa kufanya jambo au mambo fulani. Kuwa mkristo ni kuwa na maisha ambayo yamebadilishwa kabisa na Mungu. Biblia inasema kwamba shida ya mwandamu haiwezi kamwe kutatuliwa kwa vitisho au kwa kulazimisha mtu. Kile mkristo anafaa kufanya ni kuhubiri habari njema kwa uaminifu kabisa, yaani Yesu Kristo na kifo. Pia anahitaji kuishi maisha matakatifu ambayo yanaambatana na neno la Mungu na kuomba kwamba Mungu atatumia neno lake kumshawishi mwenye dhambi kuhusu dhambi zake na kwamba Mungu atampatia mwenye dhambi zawadi ambazo ni toba na imani ili aache dhambi zake na kumwamini Yesu Kristo. Kwa nguvu zangu, siweze kukufanya kuwa mkristo."

Kueneza ujumbe wa injili si jambo ambalo linafaa kuwa la kumlazimisha yeyote. Bali linafaa kuwa jambo la kutangaza habari njema kwa upendo. Tunafaa kuwaeleza wote injili ya Kristo bila kuwalazimisha kwa njia yoyote ile. Hatufai kutumia njia za ujanja ambazo haziko katika Biblia ili kuwalazimisha watu waokoke. Hata tukifanya hivi, hakutakuwa na wokovu wa kweli miongoni mwa watu. Kumbuka hili, kushuhudia kulingana na Biblia si kuwalazimisha watu waokoke.

2. Kushuhudia Kristo, si kutoa ushuhuda kuhusu maisha yako mwenyewe.

Kutoa ushuhuda kuhusu yale ambayo Mungu amekufanyia katika maisha yako, ndani ya hayo kunaweza kuwa na habari njema. Lakini pia unaweza kuwa unasema tu mambo ambayo si ya kumshuhudia Kristo. Kwa sababu unawaeleza watu kuhusu yale ambayo Kristo amefanya katika maisha yako, haimaanishi kwamba hii ni kuwaelezea injili ambayo inaokoa. Je, wakati unashuhudia kuhusu maisha yako, je, unawaeleza kuhusu yale ambayo Kristo alikufanyia msalabani Kalivari? Sisemi kwamba ni vibaya kuwaeleza watu kuhusu yale ambayo Kristo amekufanyia katika maisha yako. Kile ninasema ni kwamba katika mazungumzo yako nao kuhusu mambo haya, je unawaeleza kwamba Kristo anataka waokoke na si kwa sababu ya kuishi maisha mazuri, lakini kwa sababu wao ni wenye dhambi?

Ushuhuda kuhusu maisha yetu ni jambo la kila siku katika makanisa mengi leo. Leo wengi wanafurahishwa na ushuhuda kuhusu maisha ya watu na yale ambayo wamepata katika ulimwengu huu. Lakini hawana haja ya kujua mambo kumhusu Kristo na yale ambayo amefanya kwa ajili ya mwenye dhambi. Watu wengi hawataki kusikia ushuhuda kuhusu maisha, kifo na kufufuka kwa Kristo Yesu na jinsi mambo haya yanavyohusu maisha ya yule ambaye hajaokoka. Hii ndiyo sababu kutoa ushuhuda kuhusu yale ambayo yamekufanyikia katika maisha yako na kuhusu vitu ambavyo umevipata, haiwezi kumsaidia mtu wakati unamshuhudia Kristo.

3. Kushuhudia Kristo, si kuwasaidia watu kimwili au kufanya siasa.

Wakati tunatoa macho yetu kwa Mungu na kumtazama mwanadamu, huwa tunaanza kushughulika sana na mahitaji ya mwanadamu ya kimwili badala ya kuhubiri injili. Wakati huu sisi huanza kupuuza dhambi na kufurahia misaada ambayo tunapeana. Kumshuhudia Kristo si kugawana utajiri au kuwasaidia maskini hata kama mambo haya ni ya muhimu sana katika maisha ya ukristo. Ni jukumu la kila mkristo kumsaidia yeyote ambaye ana mahitaji. Kumshuhudia Kristo, ni kutangaza habari njema kwa wenye dhambi ili kwa neema ya Mungu wapate kutii ujumbe wa injili na waokoke. Kumbuka kwamba wakati unawasaidia wale ambao wako na mahitaji, unaweza kupata nafasi ya kuwahubiria neno la Mungu.

Jamii huwa zinabadilika kwa kupitia kwa mahubiri ya Injili na Mungu huwa anawaleta pamoja waume na wanawake katika kanisa lake kuonyesha jinsi Yeye alivyo kupitia kwa maisha ya wale ambao amewaokoa.

4. Kushuhudia Kristo, si kutetea mafundisho ya Biblia.

Kutetea dini ya ukristo au Biblia ni kujibu maswali na ubishi ambao unatokea kuhusu dini ya ukristo, Biblia, Kristo na kazi Yake. Ndiyo katika hali hii huenda inaweza kuonekana kwamba unaeneza Injili. Lakini hii si kueneza injili ya Kristo. Kutetea kuzaliwa kwa Kristo na bikira au kufufuka kwa Kristo ni jambo mzuri na linafaa, lakini kufanya hivyo si kueneza injili ya Kristo. Kutetea dini ya ukristo, ni kutetea imani ya ukristo. Kushuhudia Kristo au kueneza injili ni kufanya jinsi Kristo alivyoamuru, ni kuhubiri Yesu Kristo. Kushuhudia ni kueneza habari njema kumhusu Kristo Yesu na njia ya wokovu kupitia Kwake.

5. Kazi yetu ni kuhubiri na si kuwaokoa watu.

Tunafaa kukumbuka kwamba kazi yetu ni kushuhudia Kristo, si kuwaokoa watu. Lengo la kueneza injili ni kwamba wenye dhambi waokoke. Kwa hivyo, hatufai kuwaza kwamba sisi tunaweza kuwalazimisha watu waokoke au kwamba nguvu za kuwaokoa watu ni zetu. Kuwaza hivi ni makosa makubwa sana kwa sababu kunaweza kutufanya tuanze kuwalazimisha watu waokoke au kutumia mbinu ambazo hazipatikani katika Biblia.

Kulingana na Biblia kazi ya kueneza injili haifanywi kwa kutumia mbinu fulani fulani, bali inafanywa kwa kuhubiri neno la Mungu kwa uaminifu. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume tunasoma kuna wakati ambapo Paulo alihubiri injili na watu wachache tu waliokoka. Mhubiri ambaye aliitwa John Stott, alisema kwamba kueneza injili si kuwafanya watu waokoke, bali inamaanisha kutangaza habari njema bila kuwa na wasiwasi kwamba matokeo yatakuwa nini.

Kueneza injili ni kutangaza habari njema kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu na alifufuka kutoka kwa wafu kulingana na mafundisho ya Biblia. Yeye sasa ni Bwana ambaye anaishi na anatawala kila kitu na anapeana msamaha wa dhambi na anawapatia wote ambao anawaokoa zawadi ambayo ni Roho Mtakatifu. Katika 2 Wakorintho 2:15-16 Paulo anasema, “Kwa maana sisi kwa Mungu ni harufu nzuri ya manukato ya Kristo miongoni mwa wale wanaookolewa. Kwa wale wanaopotea sisi ni harufu ya mauti, lakini kwa wale wanaokolewa sisi ni harufu nzuri iletayo uzima. Ni nani basi awezaye kazi hiyo.” Katika mistari hii, Paulo hapeani ujumbe wa aina mbili tofauti na pia hasemi kwamba alitazama miongoni mwa hawa watu na akaona ni kina nani walikuwa wamechaguliwa na Mungu na ndiposa akawahubiria. Paulo aliwahubiria watu wote ujumbe sawa na wakati alipokuwa anawahubiria watu hawa ujumbe huu, kwa wengine ulikuwa harufu mzuri ya uzima na kwa wengine harufu ya kifo. Huduma huo ulikuwa na matokeo mawili.

Bwana Yesu Kristo alifundisha jambo hili wazi katika mfano wa udongo tofauti (Mathayo 13:1-23). Katika mfano huu, mpanzi alipanda mbegu sawa katika udongo tofauti tofauti. Mfano huu hausemi lolote kuhusu mpangilio wa mpanzi wakati alikuwa anapanda mbegu hizo. Huenda alitumia njia ile ile wakati alikuwa anapanda. Ujumbe wa mfano huo ni kwamba, kuna wale ambao watatii ujumbe wa injili na kuokoka na wengine hawatautii hata kama wote watasikia ujumbe ule ule.

Hatuwezi kusema kwamba njia fulani ambazo tunatumia ni bora kwa sababu tu ya kuwaona wengi wakiinua mikono yao na kurudia maombi fulani fulani. Ni lazima tufahamu ukweli huu vyema kabisa kwa sababu kukosa kufahamu ukweli huu, utafanya tuwe na makanisa na wachungaji ambao wanawadanganya watu. Ni jambo la hatari sana kuwaza kwamba kwa sababu unatumia mbinu fulani na kuwaona wengi wakidai kuokoka hapo hapo, basi mbinu hiyo inakubalika na Biblia. Tunafaa tujue kwamba hata kama sisi ni waaminifu kwa kuhubiri injili, kuna wale ambao hawatapokea ujumbe huo. Kwa sababu wengine wanakataa kutii ujumbe wa injili, haimaanishi kwamba tumetumia njia mbaya kuwaelezea habari njema.

Kukosa kufahamu vyema jambo hili, kutawafanya wengi washushwe mioyo katika kazi yao ya kueneza injili ya Kristo Yesu. Ninajua kwamba kuna wengi ambao kwa miaka mingi wamezungumza na wengine kuhusu injili lakini hawajaona watu hao wakiokoka. Watu kama hawa wanaweza kuwaza kwamba makosa ni yao. Biblia inafundisha kwamba huwa watu hawaokoki kwa sababu ya mbinu nzuri za yule ambaye anaeneza ujumbe wa injili. Pia ikiwa watu hawaokoki, si dhihirisho kwamba yule ambaye anaeneza ujumbe huo hakutumia mbinu nzuri. Kueneza ujumbe wa injili si jambo la kutumia mbinu zetu bali ni kuwa mwaminifu kwa ujumbe ambao tunatangaza. Wengi wetu ambao ni wakristo, tuliskia ujumbe huo wa wokovu kwa njia ambayo haikuwa ya kupendeza hata kidogo. Huenda yule ambaye alitueleza ujumbe huo alikuwa mtu ambaye alitulazimisha sana na hata kutoa maneno ya kututisha. Lakini hata

hivyo, kuna mambo ambayo yalizungumzwa naye ambayo yalikuwa ya kweli. Roho Mtakatifu alitumia maneno hayo kutuletea toba na imani.

Hii haimaanishi kwamba sisi tunafaa kukosa kuwa waangalifu jinsi tunavyo hubiri injili ya Kristo. Kuhubiri Kristo ni jukumu letu na tunafaa kulifanya kwa uangalifu sana. Ni kweli kwamba Mungu mwenye nguvu zote anaweza kubadilisha kila jambo na kulitumia kwa utukufu Wake, hata lile ambalo tumefanya kwa kutojua. Mwandishi mmoja alisema, "Kueneza injili si kuwalazimisha watu kukubali ujumbe wa injili. Kueneza injili si kujaribu kuwaonyesha watu kwamba kweli Mungu yupo na kwamba dini ya ukristo ni dini ya kweli. Si kumwalika mtu kwa mkutano fulani au kuwafanya watu wawaze kuhusu dini ya ukristo. Pia si kuvaa mavazi ambayo yana maandishi kumhusu Kristo Yesu na kazi yake. Mambo haya yote ni mazuri kuyafanya lakini hii si kueneza injili. Kueneza injili ni kutangaza mamlaka ya Mungu na yale ambayo amefanya ili wenye dhambi waweze kuokolewa. Ni kuwaonya wenye dhambi kuhusu hali yao mbaya na kuwaonyesha njia ya kutubu na kumwamini Kristo Yesu."

Leo tunaona kwamba kazi ya kueneza injili ni kazi ambayo inafanywa kwa njia ambayo ni ya kuwalazimisha watu watoe uamuzi fulani. Kwa kufanya hivi, huwa tunasahau kwamba kazi ya kuwaokoa wenye dhambi ni kazi ambayo inafanywa na mwenyezi Mungu pekee. Hii ni kazi ya neema ya Mungu kwa wenye dhambi.

Kazi ya kueneza injili si kazi ya kuwalazimishia watu wokovu bali ni kazi ya kueneza ujumbe wa injili ya wokovu kutoka kwa Bwana Yesu Kristo. Huu ni mwito wa kutubu na kumletea Mungu utukufu kwa kuzaliwa mara ya pili na kuokolewa. Wakati tunahubiri injili kwa uaminifu na watu wanakataa kuokoka, haimaanishi kwamba sisi tumefanya makosa. Huwa tunafanya makosa wakati tunakosa kufanya kazi hii ya kuhubiri injili kwa uaminifu.

Mtu anapofahamu kwamba kueneza injili si kuwafanya watu waokoke bali ni kuwaambia watu habari njema ya Mungu na yale ambayo Kristo Yesu amewafanyia, huwa matunda ya furaha yanapatikana. Wakati tunafahamu kwamba kazi yetu ni kuhubiri injili, huwa tunafanya kazi hii kwa furaha tukijua kwamba Mungu ako pamoja nasi..

Je, ni kwa nini tushuhudie Kristo?

Hili swali ambalo ni bora kuuliza na kulijibu. Je, ni nini huwa inatuhimiza tuwe na moyo wa kueneza injili ya Kristo Yesu?

Ukweli ni kwamba nia au sababu ni jambo la maana sana machoni pa Mungu. Pia ukweli ni kwamba kuna watu ambao wanahubiri injili kwa nia tofauti tofauti. Kunaweza kuwa na ubinafsi katika kufanya kazi hii. Kuna wale ambao wanaeneza injili kwa sababu tu wao wameamrishwa; kuna wale ambao wanaeneza injili kwa sababu wanataka kushinda mabishano fulani; kuna wale ambao wanaeneza injili kwa sababu wanataka kueneza mafundisho yao; kuna wale ambao wanaeneza injili kwa sababu wanataka kuonekana kwamba wao ni watu wa Mungu au wanataka kujulikana kwamba wao ni wainjilisti ambao wanafaulu katika kazi yao. Swali ni, je ni sababu gani nzuri ambayo inafaa kutuchochea kueneza injili ya Kristo Yesu? Kulingana na Biblia kuna sababu fulani ambazo ni bora kabisa na zinafaa kutufanya tueneze injili ya Kristo ni.

1. Kwanza, tunafaa kuwa na tamaa ya kutii mwito wa Kristo Yesu wa kueneza injili (Mathayo 28:18-20; 1 Wakorintho 9:16-17)
2. Pili, ni kwa sababu tunapenda kuwaona wale ambao wamepotea wanaokoka (Mathayo 9:36; Yohana 3:16; Warumi 10:1)
3. Tatu, kwa sababu unampenda Mungu (2 Wakorintho 5:9).

Kwa ufupi ni upendo kwa Mungu ndio inafaa kuwa jambo ambalo linachochea tamaa ya kutaka kueneza injili jinsi Mungu anavyotaka.

Upendo kwa Mungu ndio jambo la pekee ambalo linafaa kutufanya tuwe na moyo wa kueneza injili ya Kristo Yesu. Ikiwa tunajipenda wenyewe, basi kila kitu ambacho tutakuwa tunafanya kusudi litakuwa moja, kujiletea utukufu na kutaka kujulikana kama watu ambao tunajua sana kazi ya kueneza injili. Ikiwa hatuwapendi watu ambao wamekufa katika dhambi zao, hatuwezi kamwe kufaulu katika kazi zetu za kueneza injili. Ni upendo wa kweli kwa Mungu ambao utatufanya na kutusaidia kueneza injili ya Kristo jinsi inavyostahili. Ni upendo huu ambao utaleta matunda wakati mitindo ya wanadamu inakosa kufaulu. Ni upendo tu kwa Mungu ambao unafaa kuwa msingi wa yale yote ambayo tunayafanya.

Lakini zaidi kabisa ni upendo wa Mungu kwetu ambao utatulinda kutokana na hatari zote. Wakati tutajaribiwa kutaka kujulikana na wanadamu au kutaka kuonekana kama wale ambao wamefaulu katika kazi hii au kujaribu kutumia mbinu zingine kando na ukweli ambao unapatikana katika neno la Mungu, ni upendo tu kwa Mungu ambao utafanya tusimame imara kabisa na ukweli na njia ambazo zinapatikana katika neno lake.

Upendo huu kwa Mungu huwa unatuelekeza kuwa na tamaa ya kutaka Mungu pekee atukuzwe. Katika Biblia yote, Mungu hujitambulisha kupitia kwa viumbe vyake. Huwa tunahubiri neno la Mungu ili tumtukuze Mungu wakati ukweli kumhusu Yeye unajulikana kwa viumbe vyake. Mwito wa kueneza injili, ni mwito wa kuacha kujipenda na kutaka kujifurahisha ili tuweze kumtukuza Mungu katika maisha yetu na maisha ya viumbe vyake vyote. Hii inajumlisha kuwapenda watu ambao wameumbwa katika mfano wa Mungu hata kama wao ni maadui na Mungu. Hawa ni watu ambao wako mbali na Mungu na wanahitaji kuokolewa kutoka katika dhambi na hatia ya dhambi. Huwa tunamletea Mungu utukufu wakati tunaeneza ujumbe wa injili kuhusu yale ambayo Mungu amewafanyia watu wake wote kupitia kwa Kristo Yesu. Hii siyo njia ya pekee ambapo tunamletea Mungu utukufu, lakini ni njia moja kuu ambayo wale ambao wameokoka wanaweza kutumia ili kumletea Mungu utukufu. Petro aliwahimiza wakristo kwamba, "Mwe na mwenendo mzuri mbele ya watu wasiomjua Mungu, ili kama wanawasema kuwa ninyi ni watenda mabaya wayaone matendo yenu mema wamtukuze Mungu siku atakapokuja kuhukumu" (1 Petro 2:12).

Wakristo wote wanafaa kueneza injili ya Kristo Yesu. Tunafaa kufanya hivyo kwa uaminifu, kwa haraka na kwa furaha. Pia tunafaa kuishi maisha ambayo yanaambatana na neno la Mungu. Haya yote tuyafanye kwa utukufu wa mwenyezi Mungu.

Kuna makanisa mengi leo ambayo yamejawa na watu ambao wamelazimishwa kufanya uamuzi na wachungaji au wainjilisti, lakini kwa kweli wao hawajaokoka. Pia katika makanisa haya, wakristo wote wameonyeshwa kwamba hii ndiyo njia bora ya kueneza injili, yaani kuwalazimisha watu kufanya uamuzi. Pia kuna wale ambao walifanya uamuzi kwa sababu walitaka kuwafurahisha wazazi wao. Ukweli ni kwamba kwa kutumia njia kama hizi, makanisa haya yamewadanganya wengi na kwa sababu hii, yamejawa na watu ambao kweli hawajaokoka.

Tuombe Mungu kwamba atusaidie tuwe waaminifu Kwake na kwa neno Lake. Pia atusaidie kwamba hatutajaza makanisa yetu na watu ambao hawajaokoka, yaani wale tu ambao wamefanya uamuzi wa kufuata Yesu Kristo lakini Mungu mwenyewe hajafanya kazi katika mioyo yao. Kazi ya kuwaokoa watu ni kazi ya Mungu na si kazi ya mwandamu yeyote.

Tunafaa sisi sote kufahamu jambo hili kwa sababu wakati tunahubiri injili tusije tukawaza kwamba mahubiri yetu ndiyo itamfanya mtu aokoke. Kazi yetu ni kuhubiri na kuwaonyesha wote njia ya wokovu, si kumwokoa yeyote. Mungu pekee ndiye ana uwezo wa kuwafufua wale ambao wamekufa kiroho. Katika kazi hii, Mungu anaweza kumtumia yeyote kwa ajili ya utukufu wake. Yeye alichagua kuwatumia watu kama Musa ambaye alikuwa na kigugumizi na Paulo ambaye alikuwa anawatesa wakristo, kuwahubiria watu wa mataifa. Kwa kuwatumia watu kama hawa, Mungu alikuwa anajiletea utukufu. Ujumbe wa injili una nguvu. Wakristo wote binafsi na makanisa yote, tujitolee katika kazi hii ya kueneza injili ya Kristo Yesu. Tuombe Mungu atusaidie tuhubiri injili hii kwa uaminifu sana na kwa wazi kabisa ili wote waweze kuelewa.

Wakati tutafanya hivi, tutaanza kuona matunda ya kweli. Washirika katika makanisa yetu watakuwa watu ambao wameokoka. Ulimwenguni kote ujumbe wa injili utaanza kuonekana wazi kupitia kwa maisha ya wale ambao wameokoka kwa kweli.

Ninajua kuna wale ambao wanasema, ikiwa mtu anaamini katika kuchaguliwa, basi hafai kueneza ujumbe wa injili. Ukweli ni kwamba unaposoma historia ya kanisa, utaona kwamba wale ambao walikuwa wainjilisti wakuu katika kazi ya Mungu, waliamini kwamba wokovu ni kazi ya Mungu pekee na kazi hii inamjulisha kuchaguliwa. Yaani wale ambao wanaokoka ni wale ambao Mungu mwenyewe alichagua waokoke. Jambo hili halikuwafanya watu hawa wakose kueneza ujumbe wa injili. Ukweli ni kwamba Mungu Baba aliwachagua watu fulani waokoke, Mungu Mwana alifia watu hawa msalabani ili waokoke na Mungu Roho Mtakatifu huwaleta kwa Kristo iliwaokoke. Pia kwamba kuokoka ni kutii mwito wa Mungu wa neema kupitia kwa toba na imani. Pia kueneza injili au kushuhudia Kristo ni kuwa mwaminifu na kwa maombi kuwaeleza wengi kuhusu Kristo. Ikiwa mchungaji haamini mambo haya yote, basi atakuwa na watu ambao wanadai kuokoka kanisani mwake ilhali wao ni wenye dhambi. Yeye atajaza kanisa na watu ambao hawajaokoka. Yeye atakuwa anawaeleza tu hadithi ambazo zitawafanya wawe na huzuni mioyoni mwao na watakiri na kufanya uamuzi lakini hawatakuwa wametubu dhambi zao kwa kweli. Mbinu kama hiyo, haitawaletea uzima wa milele. Lakini huenda kwa sababu ya uamuzi wao, watabatizwa na kufanywa washirika wa kanisa, na hii haiwaokoi.

Tunafaa kufahamu jinsi ujumbe wa injili ni habari njema kwa mwanadamu ambaye amekufa katika dhambi zake. Ujumbe huu hauji kwa mwanadamu kumweleza kwamba yeye ni mtu mzuri hapa na pale, bali unamweleza kwamba yeye amekufa katika dhambi na hana uwezo wowote wa kujiokoa. Tusipofahamu jambo hili, tutafanya makosa makubwa sana na ujumbe huu utaonekana kuwa kitu ambacho hata mwanadamu anaweza kujifanyia mwenyewe.

Kazi ya kueneza injili haifanyiki kwa uwezo au nguvu zetu bali kwa uwezo na nguvu za mwenyezi Mungu. Ninajua kwamba kuna wakati katika kazi hii ambapo tunaweza kushushwa mioyo kwa sababu ya jinsi watu wanavyotupokea. Lakini hata wakati kama huu, tunafaa kujua kwamba kazi yetu ni kuhubiri injili na Mungu mwenyewe ndiye anayeleta mazao.

Kuna wakati Paulo alikuwa ameshushwa moyo. Mungu alimhimiza kwa maneno haya: “Usiogope, lakini endelea kusema wala usinyamaze, kwa maana mimi niko pamoja nawe, wala hakuna mtu yeyote atakayeweza kukushambulia ili kukudhuru, kwa kuwa kuna wengi katika mji huu ambao ni watu wangu” (Matendo ya Mitume 18:9-11). Katika mstari huu, Mungu alikuwa anamhimiza Paulo kwa kumweleza kwamba Yeye alikuwa na watu katika mji huo ambao alikuwa amewachagua waokoke na kwa hivyo Paulo alikuwa afahamu kwamba kazi ambayo Mungu alikuwa amemtuma aifanye haikuwa kazi bure au ya kumaliza tu muda.

Lazima tuhakikishe kwamba kazi hii ya kushuhudia Kristo inafanywa kwa njia ambayo ni ya kweli na ya kuzaa matunda ya kweli. Mbinu kama za kuwalazimisha watu kufanya uamuzi fulani zinafaa kukomaa. Tunafaa kuwaonyesha watu kwamba kurudia tu maombi fulani haimwokoi mtu yeyote. Tunafaa kuhakikisha kwamba washirika wa makanisa yetu watakuwa watu ambao kweli wameokoka na si tu wale ambao walifanya uamuzi fulani kwa kurudia maombi fulani tu.

Tunafaa kujua kwamba ni baraka kubwa sana kwetu kwamba Mungu ametupatia neno lake na ametuamuru kulitangaza ulimwenguni kote. Hii ni kazi ambayo tunafaa kujitolea kabisa kuifanya na hata kuifanya kwa bidii sana. Tukumbuke kwamba wakati tunawahubiria watu injili, huwa tunahubiria wale ambao kweli kulingana na neno la Mungu wamekufa kabisa katika dhambi zao na makosa yao. Kwa hivyo, hawa ni watu ambao kamwe hawawezi kufanya uamuzi wa kuokoka kwa sababu hawana uwezo wa kulipokea neno la Mungu kwa nguvu zao wenyewe. Hata wakati tunaifanya kazi hii, tukumbuke kwamba hii ni kazi ya Mungu na si kazi yetu wenyewe. Kwa hivyo tuifanye kwa bidii sana tukimtumainia Mungu kwamba atawaokoa watu wake.

Ni kwa sababu mtu fulani alikuwa mwaminifu katika kazi hii, ndipo wewe ulipata kusikia ujumbe wa Mungu na mwito wa Mungu kwako mwenye dhambi na ukaokoka. Kwa hivyo, tuombe wote kwamba tuwe waaminifu katika kazi hii na kwamba Mungu atatumia neno lake kuwaokoa wengi.

Ni lazima tujue kwamba ujumbe huu wa injili ya Kristo, ni ujumbe muhimu sana. Ikiwa hatutafanya kazi hii, basi hatutafahamu mengi kuhusu kazi hii. Ikiwa kweli tutafahamu vyema ujumbe huu wa injili, basi mioyo yetu, mawazo yetu ndimi zetu na chochote tulicho nacho, kitafurahia kufanya kazi hii.

Yesu alisema, “Kwa maana kinywa cha mtu huyanena yale yaliyoujaza moyo wake” (Mathayo 12:34). Je, moyo wako umejawa na nini? Je, unamaliza muda wako mwingi ukisema nini?

Ishara ya sita

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kanisa ambalo linafahamu kanisa ni nini.

Yaliyomo katika sura hii

1. Kanisa ni nini?

2. Kwa nini mtu anafaa kujiunga na kanisa fulani?
(a) Ili tuwe na hakikisho la wokovu wetu
(b) Ili tushuhudie ulimwengu
(c) Kuweka wazi injili ya uongo
(d) Kujengana kiroho
(e) Kumtukuza Mungu

3.Je, mshirika wa kanisa ni nani?

(a) Ni mtu ambaye amebatizwa
(b) Ni mtu ambaye anakubaliana na mafundisho ya kanisa ambalo anajiunga nalo.

4. Majukumu ya mshirika wa kanisa

(a) Ni lazima ahudhurie kanisa kila Jumapili
(b) Ni lazima ashiriki meza ya Bwana
(c) Ni lazima ahudhuria mikutano ya kanisa
(d) Ni lazima awe mtu wa maombi
(e) Ni lazima awe mtu wa kutoa kwa ajili ya kazi ya Mungu

Mafundisho ya Biblia kuhusu kuwa mshirika wa kanisa.

Leo watu wengi wanaogopa kujitolea kufanya mambo fulani kwa sababu wanaogopa kwamba wakati watakuwa wanajitoa katika mambo hayo, huenda wakakosa kupata yale ambayo yatawafaidi wao wenyewe. Kwa hivyo hata kama wao wanaona kwamba kuna mambo mengi mazuri ambayo wanayafanya, wao huwa hawataki kujitolea kabisa katika mambo hayo. Hivi ndivyo watu wengi wanaishi maisha yao leo.

Leo kuna wengi ambao wanajiita wakristo lakini ni wachache tu ambao wamejitolea kabisa kufanya yale ambayo Kristo amewaamuru wafanye. Je, wewe ni mkristo ambaye hajitolei kabisa katika ukristo wako? Siulizi kama kuna mkristo ambaye hana shaka, bali ninauliza kama mkristo wa kweli ambaye hajajitolea kabisa. Wengi wetu ambao ni wakristo wa kweli tuna shaka katika mioyo yetu. Lakini kuna yule ambaye ameamua kwamba yeye hatajitolea kabisa katika maisha yake kama mkristo. Ikiwa kuna mkristo kama huyu, je maneno haya ya Bwana Yesu Kristo yanamaanisha nini katika maisha yake: “Mtu yeyote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe na auchukue msalaba wake, anifuate” (Mathayo 16:24).

Leo tunaishi katika nyakati ambapo watu wengi wanachukia kuishi maisha ya ukristo wa kweli. Wao hawapendi kuwa washirika wa kanisa fulani. Kuna wengi ambao wanawaza kwamba Biblia haifundishi kwamba ni lazima mtu awe mshirika wa kanisa fulani. Wengi huuliza, je, si kanisa ni mahali ambapo watu wanaenda tu? Je, kuna haja gani kusema kwamba ni lazima mtu ajitolee kabisa kwa kanisa fulani? Je, katika matendo ya Mitume 8, yule Towashi baada ya kupokea ujumbe wa injili na kubatizwa, Je, alifanyika mshirika wa kanisa gani? Haya ni maswali ambayo wengi huuliza na kutosheka kwamba hakuna haja ya mtu kuwa mshirika wa kanisa fulani.

Pia kuna wengine ambao hujiwazia kwamba ikiwa mtu ameokoka, basi yeye anafanyika mshirika wa kanisa mara moja. Kwao mshirika wa kanisa ni mtu yeyote ambaye ameokoka. Huu ni ukweli ikizingatiwa kanisa lote la Kristo ulimwenguni. Lakini tunahitaji kufahamu kwamba kanisa hili moja limesambaa duniani kote, na ndio sababu tunapata makanisa mengi duniani kote. Kwa hivyo kila mkristo anahitaji kuwa mshirika wa kanisa fulani.

Ninajua kwamba ikiwa sisi sote tutafahamu jambo hili la kuwa mshirika wa kanisa, basi makanisa yetu yatapata kuhuishwa, tutaweza kushuhudia Kristo vyema kwa mataifa na tutaweza kumletea Mungu utukufu. Kumbuka kwamba sura hii ni moja ya sura ambazo zinapatikana katika kitabu hiki cha Ishara 9 za kanisa lenye afya au kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho. Kama tu vile nilivyosema katika utangulizi kwamba kitabu hiki hakina kila ishara ya kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho. Lakini katika sura 9 za kitabu hiki, ninaonyesha mambo muhimu katika maisha ya kanisa ambayo yamekuwa yamepuuzwa au yamesahaulika katika maisha ya watu wa Mungu leo.

Kwa mfano, leo unapotazama makanisa mengi utaona kwamba kanisa moja liko na washirika 100, lakini utapata kwamba kwa Jumapili moja wale ambao wanakuja kanisani ni 40. Swali ni, je wale 60 wako wapi. Je, kwa nini hawajakuja kanisani? Je, wote ni wagonjwa? Je watu hawa wanaelewa majukumu yao mbele ya Mungu kweli? Je, hali yao ya kiroho ikoje ikiwa hawajahudhuria kanisa? Je, tunafaa kujishughulisha na kuja kwao kanisani au la?

Katika sura hii tutatazama maswali matatu.
1. Je, kanisa ni nini?
2. Je, kwa nini mtu anafaa kujiunga na kanisa fulani?
3. Je, mshirika wa kanisa ni nani?

1. Je, Kanisa ni nini?

Neno kanisa halimaanishi mikusanyiko yoyote ya kidini mahali popote. Hutawahi kusikia mtu akisema kanisa la Wahiindi au kanisa la Wayahudi. Neno kanisa ni neno la Kikristo. Kusema kanisa, hatumaanishi mjengo. Mjengo fulani ni mahali ambapo kanisa hukutana.

Kulingana na Agano Jipya, kanisa ni watu ambao wanakiri wameokoka na kwa maisha yao wanatoa ushuhuda kwamba kweli wao wameokolewa kwa neema ya Mungu pekee, na kwa utukufu wa Mungu pekee kupitia kwa imani pekee ndani ya Kristo Yesu pekee. Hili ndilo kanisa la kweli na si mjengo. Kanisa la kwanza hawakuwa na mijengo kwa miaka 300 baada ya kanisa kuzaliwa. Watu ambao wamejitolea kwa Kristo Yesu mahali fulani, ndilo kanisa.

Kuna vifungu fulani fulani katika Agano Jipya ambavyo vinaonyesha kwamba kanisa la Kristo ni moja ambalo ni, wakristo wote ulimwenguni. Lakini pia kuna vifungu ambavyo vinaonyesha kwamba kanisa la Kristo Yesu ni vikundi vya watu ambao wameokoka mahali fulani fulani kote ulimwenguni. Hawa ni watu ambao wamejitolea kumfuata Kristo na pia wamejitolea kuhudumiana kama wakristo. Hii ndiyo maana ya neno kanisa katika Biblia. Kanisa ni mahali ambapo si wote wako, lakini ni mahali ambapo wote wanaweza kuingizwa ikiwa watafuata kanuni za kuingizwa humo, yaani yameokoka na watajitolea kwa ajili ya kanisa hilo.

Wale ambao wako katika kanisa ni watu ambao wako humo kwa Agano. Kwa hivyo si kila mtu ambaye anaishi mahali fulani ambapo kuna wakristo anaweza kusema kwamba yeye pia ni mkristo. Kuna Agano kati mkristo ya na Mungu. Mtu yeyote hawezi kuingia katika kanisa kwa misingi ya jamii yake au kabila au taifa au rangi. Huwezi kuwa mkristo kwa sababu baba au mama au watu wengi wa taifa lako ni wakristo. Kila mtu anaingizwa katika kanisa hili akiwa peke yake kwa misingi kwamba amefuata kanuni za kuingia humo. Kanisa ni la wale ambao wameokoka na Roho Mtakatifu anakaa ndani mwao. Ni la wale ambao Roho Mtakatifu amewazaa mara ya pili na kuwaweka pamoja.

Kwa sababu hii, wakristo wote wanafaa kuwa na tamaa ya kuona kwamba tunashirikiana kama wakristo kutangaza injili ya Kristo Yesu katika mataifa yetu yote. Unaposoma kitabu cha Matendo ya Mitume utaona kwamba hakuna kanisa ambalo lilikusudia kuwaleta watu katika ushirika wao ambao hawakuwa wameokoka. Unaposoma barua za Paulo, utaona kwamba alikuwa anawaandikia watu ambao walikuwa wameokoka. Kwa sababu hiyo aliwaita, Watakatifu wale ambao Mungu alikuwa amewaokoa. Kanisa ni mwili wa Kristo Yesu popote ambapo wakristo wako ulimwenguni. Hawa ni watu ambao wamejitolea kabisa kuishi maisha yao kwa ajili ya Kristo Yesu na kuhudumiana wao kwa wao.

2. Je, Kwa nini mtu anafaa kujiunga na kanisa fulani?

Kufahamu jambo hili ni vyema kabisa kwa sababu utujua ni nini Kristo anaikuita ufanye kama mkristo. Kujiunga na kanisa lolote haimwokoi mtu yeyote kama tu kutoa pesa nyingi kanisani au kubatizwa au matendo yako mema au elimu yako. Wale ambao hawajaokoka, hawafai kutaka kujiunga na kanisa, bali wanafaa kutafuta kujua jinsi ya kuwa mkristo.

Kwa wale ambao wameokoka, ukweli ni kwamba hatuwezi kuishi maisha ya wokovu bila kuwa pamoja na wengine. Kuwa mkristo haimaanishi tu kuwa mwaminifu kwa mke au mume wako; ama kutodanganya au kuwa mwaminifu kazini kwako, bali kunamaanisha pia kuwa katika ushirika na wakristo wengine.

Tumeitwa kuwa katika ushirika na wakristo wengine. Kanisa ni la kila mtu ambaye ameokoka. Kanisa ni kila mkristo.

Nina sababu tano ambazo kwa nini mtu anafaa kujiunga na kanisa ambalo linahubiri injili ya Kristo na ni kielelezo kwa kusihi maisha matakatifu.

1. Sababu ya kwanza ni kujihakikishia kwamba kweli wewe umeokoka.

Hufai kujiunga na kanisa kwa sababu unataka kuokoka, bali kwa sababu tunataka kuhakikisha kwamba kweli wewe umeokoka. Kumbuka maneno haya ya Bwana Yesu Kristo: “Yeyote mwenye amri Zangu na kuzishika ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, nami nitampenda na kujidhirisha kwake; Mkizishika amri Zangu mtakaa katika pendo Langu, kama Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake; Ninyi ni rafiki Zangu mkifanya ninayowaamuru; Sasa kwa kuwa mmejua mambo haya, heri yenu ninyi kama mkiyatenda” (Yohana 14:21; 15:10, 14; 13:17).

Haya ni baadhi ya maneno ya Kristo. Lakini katika Biblia yote kuna vifungu vingi sana ambavyo Kristo anatufundisha jinsi tunapaswa kumfuata kwa uangalifu sana. Wakati tunajiunga na kanisa, huwa tunajitoa kwa ndugu na dada zetu kwamba tutaishi maisha yetu kulingana na neno la Mungu. Huwa tunajitoa kwa ndugu na dada zetu ndani ya Kristo kutusaidia kukumbuka yale ambayo tumesahau na pia kuturekebisha wakati tumekosa.

Kuwa mshirika katika kanisa moja ni ushuhuda kwamba sisi tuko katika mwili mmoja wa Kristo Yesu ulimwenguni kote. Kuwa mshirika wa kanisa hakumwokoi mtu yeyote, bali ni ishara ya kwamba mtu huyu ameokoka. Ikiwa hatuonyeshi kwamba sisi tumeokoka, basi tutajuaje wenyewe kwamba tumeokoka kwa kweli? Yohana anasema, “Ikiwa mtu atasema, Nampenda Mungu, lakini anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo. Kwa maana kila mtu asiyempenda ndugu yake ambaye anamwona, atampendaje Mungu ambaye hajamwona?” (1 Yohana 4:20).

Kuwa mshirika wa kanisa ni kutaka kutambulika na wengine ambao wameokoka kama wewe. Ni kukubali kusaidiana na kuhimizana na wakristo wengine wakati tunahitaji kukumbushwa kuhusu kazi ya Mungu ambayo anafanya katika maisha yetu. Ni kuwa tayari kusahihishwa kulingana na mwenendo wa maisha yetu; jinsi tunavyozungumza na jinsi tunavyotembea na Mungu.

Tunafaa kuacha kujaribu kuishi maisha mazuri kwa nguvu zetu. Tunafaa kuwa na agano la pamoja na wengine kumfuata Kristo Yesu. Sisi wakristo tunafaa kuacha ubinafsi katika ufahamu wetu kuhusu maisha ya ukristo. Maisha ya ukristo haikuhusu wewe tu na wale ambao unajaribu kuwafikia na Neno la Mungu. Mungu pia amekusudia kwamba miongoni mwa wale ambao amewaokoa, kutakuwa na wale ambao unafaa kuwasaidia katika maisha yao ya ukristo.

2. Sababu ya pili ni kushuhudia ulimwengu.

Sababu nyingine kwa nini unafaa kujiunga na kanisa ni kwamba ulimwengu uweze kushuhudiwa. Pamoja tutaweza kueneza injili nyumbani, katika nchi yetu na nchi zingine. Tutafanya hivi kwa maneno tunapokuwa tunashiriki neno la Mungu na wengine na kwa kuwasaidia wengine kufanya kazi hii. Kwa kawaida kazi ya kanisa ni kueneza injili ya Kristo Yesu. Huwa tunasaidia katika kazi hii kwa matendo yetu ya upendo kama kuwasaidia mayatima na wale ambao wana mahitaji.

Huwa tunaeneza injili kwa kuwahubiria wale ambao hawajawahi kusikia ujumbe huu na kufanya ujumbe huu udhihirike katika maisha ambayo tunaishi. Wale ambao hawajaokoka, wanaweza kuona mwenendo wa maisha yetu na kuona jinsi injili inavyowabadilisha wengi. Hata kama hatujakamilika, Roho Mtakatifu ambaye anakaa ndani yetu atatumia maisha yetu kuwaonyesha wengi ukweli ambao unapatikana katika ujumbe wa injili ya Kristo Yesu. Hili ni jukumu ambalo tunalo sasa na hatutakuwa nalo huko mbinguni. Ni

mpango wa Mungu kupeleka ujumbe huu wa injili kwa ulimwengu wote. Ikiwa wewe ambaye unasoma haya hujajihushisha na kazi hii na umeokoka, basi ninakusihi uanze kufanya kazi hii.

3. Sababu ya tatu, ni kuweka wazi mafundisho ya uongo.

Wakati tunashiriki na wakristo wengine huwa tunaonyesha ulimwengu kwamba ukristo ni wa kweli. Kuna wengi wanafundisha kwamba mkristo ni mtu ambaye amekamilika, yaani yeye hana dhambi yoyote. Lakini ukweli ni kwamba mkristo ni mtu ambaye hajakamilika. Kwa hivyo mkristo si mtu ambaye anajiona kwamba amekamilika, wanajua kwamba wao wana dhambi ndani yake ambayo bado anapigana nayo.

Watu wengi huwa wanawaza hivi kwamba wakristo ni watu ambao wamekamilika na hawana dhambi yoyote ndani mwao. Hatuwezi kuondoa au kupinga mafundisho ya uongo ikiwa tutawaonyesha watu kwamba mkristo ni mtu ambaye amekamilika. Wakristo ni watu ambao wanajua kwamba wao hawajakamilika na kwamba ni kwa neema ya Mungu wao wameokoka. Wao wanajua kwamba walikuwa wenye dhambi wakuu mbele za Mungu na kwamba ni kwa sababu ya upendo wa Mungu kwao ndipo walipata kuokoka. Wanajua upendo huu wa Mungu kwao unadhihirishwa ndani ya Kristo Yesu. Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni na aliishi maisha matakatifu na baadaye alikufa juu ya msalaba na kufufuka kutoka kwa wafu katika ushindi dhidi ya dhambi na kifo kwa niaba ya wale wote ambao walikusudiwa kuokoka. Ni kwa imani pekee ndani ya Kristo Yesu wakristo wote tumeokolewa.

Msomaji ikiwa hujajiunga na kanisa lolote, ninakusihi leo kwamba jiunge na kanisa ambalo linaamini hivi. Jiunge na wakristo wengine ili mwendeleze ukweli ambao unapatikana katika neno la Mungu.

4. Sababu ya nne ni kujengana kiroho.

Sababu ya nne kwa nini mtu anafaa kujiunga na kanisa ni kwamba ili aweze kusaidiana katika kuwajenga wengine. Kujiunga na kanisa ni jambo ambalo litatusaidia kama wakristo kuondoa ubinafsi na kutufanya tuone umuhimu wa kuja pamoja kama watoto wa Mungu.

Tuwe waangalifu kwa sababu ni rahisi sana kujidanganya kwamba kwa sababu siku moja tulifanya uamuzi fulani wa kuja kwa Kristo Yesu, sasa sisi ni washirika wa kanisa fulani ambalo tunahudhuria. Kabla ujiwazia kuwa mshirika wa kanisa fulani, jiulize swali hili, je mimi niko na uhusiano wa karibu na Kristo Yesu ambao umebadilisha maisha yangu na ya wale ambao ninajiunga nao?

Je utajuaje kwamba kweli wewe una uhusiano huu na Kristo Yesu? Njia moja ambayo unaweza kufahamu jambo hili ni kujiuliza swali hili: Je, upendo wangu kwa Kristo Yesu unachochea jinsi ninavyowapenda wale ambao ni kanisa la Kristo? Je, umejitolea kabisa kuwapenda hawa? Au wewe ni mtu ambaye amekiri kuwapenda wale ambao ni wa Kristo lakini maisha yako ni kinyume na jinsi unavyokiri? Je, wewe ni yule ambaye unakiri kujua upendo huu wa Kristo lakini katika kuwapenda wakristo umeweka mipaka?

Kudai kwa aina hii ambako hakuambatani na maisha matakatifu, ni kudai kwa uongo. Lakini ikiwa utakataa kujiunga na kanisa, basi jua kwamba wakristo wengine hawatakusaidia. Wewe ni yule ambaye anaendesha meli yake pekee na anaenda njia yake mwenyewe. Wewe ni mtu ambaye anakuja kanisani wakati unataka au wakati mahubiri yanakupendeza au wakati mziki unachezwa vizuri au wakati mtu fulani anahubiri au unakuja kanisani wakati mambo fulani ambayo yanakupendeza yanafanyika.

Wakati unajitolea kuwa mshirika wa kanisa fulani huwa unajitolea kwa watu ambao watajaribu kukusaidia kusuluhisha mambo kama haya katika maisha yako. Kwa mfano ikipatikana kwamba wewe una shida ya kuwasengenya wengine, wakristo wenzako katika kanisa watajaribu kuzungumza nawe kuhusu jambo hilo. Ikiwa wewe unashushwa moyo na kutaka kukata tamaa, wakristo wenzako watakuhimiza.

Agano Jipya linatuonyesha wazi kwamba kumfuata Kristo kunajumlisha kuwajali na kuwashughulikia wengine. Huu ndiyo ukristo wa kweli ingawa huwa hatufanyi kazi hii kwa uangalifu sana, tunafaa kujitolea kabisa kuifanya kwa mioyo yetu yote.

Ni mpango wa Mungu kwamba tuwe washirika wa kanisa fulani. Mungu amekusudia wakristo washirikiane katika kila jambo. Wanafaa kujengana, kuhimizana, kufarijiana, kushughulikiana na kujaliana maslahi.

Mtu huwa ajiungi na kanisa kwa sababu yeye ni mtu mkamilifu na kwamba atalisaidia kanisa sana. Kumbuka kwamba kila wakati unapojiunga na kanisa fulani, wewe utaliletea kanisa hilo shida kadhaa kwa sababu wewe hujakamilika. Lakini usiache jambo hili liwe kizuizi kwako kujiunga na kanisa kwa sababu tayari katika kila kanisa kuna shida fulani fulani. Hivi ndivyo kanisa lilivyo. Kila mkristo ana shida zake. Lakini tunajua kwamba Mungu ako ndani yetu akifanya kazi ya kuondoa shida hizi. Kwa mfano, wewe unaweza kuwa mtu ambaye hamwamini mtu yeyote. Ukiwa ndani ya Kristo Yesu, Mungu huaza kufanya kazi katika moyo wako kuhusu jambo hili. Mungu huanza kukuonyesha kwamba Yeye ni mwaminifu na kwamba hata wakristo wenzako wanaweza kuwa watu waaminifu. Hata kama katika maisha yako unapatana na shida fulani fulani, ikiwa wewe kweli umeokoka, Mungu ako anafanya kazi katika maisha yako. Mungu atashughulikia shida hizi zako na atafanya hivyo kupitia kwa kanisa lake.

Mungu huwa hafurahishwi tu na jinsi wakristo wanavyo maliza muda fulani katika maombi au katika kusoma neno lake. Lakini pia Yeye huwa anapendezwa na pia huwa anafurahishwa na jinsi wakristo wanavyoshughulikiana na kujaliana hali katika maisha yao yote. Mkristo hafai kuwa mtu ambaye anajipenda na kwamba kila wakati yeye hujijali tu na hawajali wakristo wengine. Kuwa mshirika wa kanisa linafaa kuwa jambo ambalo linakufanya kuwa na moyo juu ya maisha ya wakristo wengine. Kukua katika ukristo, si jambo la mtu mmoja katika kanisa, bali ni jambo ambalo linahusu kanisa lote.

Biblia inasema, “Kwa hiyo, ndugu zangu, kwa kuwa tunao ujasiri wa kupaingia Patakatifu pa Patakatifu kwa damu ya Yesu, kwa njia mpya iliyo hai tuliyofunguliwa kwa ajili yetu kupitia kwenye lile pazia, yaani, mwili Wake, basi kwa kuwa tunaye kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu, sisi na tumkaribie Mungu kwa moyo mnyofu kwa imani timilifu, mioyo yetu ikiwa imenyunyizwa damu ya Kristo na kuwa safi kutokana na dhamiri ambayo nayo miili yetu ikiwa imeoshwa kwa maji safi. Tushike kwa uthabiti lile tumaini la ukiri wetu bila kuyumba-yumba, kwa maana Yeye aliyeahidi ni mwaminifu. Tuangalieni na kuhimizana sisi kwa sisi katika upendo na katika kutenda mema. Wala tusiache kukutana pamoja, kama wengine walivyo na desturi ya kukutana, tuhimizane sisi kwa sisi kadri tuonavyo siku ile inakaribia” (Waebrania 10:19-25).

Kuwa mshirika wa kanisa ni fursa ambayo tuko nayo kutimiza majukumu yetu kwa upendo juu ya wakristo wenzetu. Kwa kukubali kuwa mshirika wa kanisa fulani, ni kuonyesha kujitolea kwako katika kuhudhuria kanisa kila Jumapili, kujitolea kwako katika kumtolea Mungu katika kanisa hilo, kujitolea kwako katika maombi kwa ajili ya kanisa hilo na pamoja na washirika wa kanisa hilo na kujitolea kuhudumu katika kanisa hilo. Huwa tunasema kwamba tunajitolea kuwahudumia wakristo wenzetu katika kanisa hilo. Huwa tunahakikishia kanisa hilo kwamba kweli sisi tumejitolea kuwa wafuasi wa Kristo na kuhudumia Yeye pekee pamoja na wakristo wa kanisa hilo.

Tunaona jambo hili kuhusu la kuwa mshirika kanisa katika Barua za Paulo. Wakati tunajiunga na kanisa, huwa tunashirikishwa katika kazi ya kanisa, katika mikutano ya kanisa, katika uamuzi wa kanisa na katika mipango ya kanisa. Huwa tunakuwa na washirika ambao wanafurahia ushirika wetu katika mwili wa Kristo. Mshirika wa kanisa ni mtu ambaye hatalalamika kwamba hapati kile ambacho anafaa kupata, bali yeye atakuwa yule ambaye anajitahidi kuwafanyia wengine mema na kuona kwamba mahitaji yao yanashughulikiwa sawa. Kuwa mshirika wa kanisa si jambo tu ambalo linahusu tu mambo ya kiroho, bali pia linahusu mambo ya kimwili. Washirika wa kanisa husaidiana hata katika mahitaji yao ya kila siku. Hii hudhihirisha upendo kati ya wakristo.

Leo kuna wakristo wengi ambao hawajali kabisa mambo ya kuwa mshirika wa kanisa. Hii ndiyo sababu leo utapata vitabu vingi sana ambavyo vinazungumza kuhusu ukristo lakini havizungumzi kabisa kuhusu mambo ya kanisa. Katika barua ya Paulo kwa Wakorintho, Paulo aliandika kwamba karamu za roho zilikusudiwa “kulijenga kanisa” (1 Wakorintho 14:12). Hili linafaa kuwa lengo kuu la maisha ya ukristo. Ikiwa unawaza kwamba hakuna lolote ambalo unaweza kufanya katika ukristo wako, basi jua kwamba umejidanganya. Kila mkristo ana karama za rohoni ambazo anafaa kutumia ili kanisa la Kristo liendelee kujengwa. Kuwa mshirika wa kanisa ni baraka kubwa sana ambayo inaambatana na majukumu. Kuwa mshirika wa kanisa utasaidika sana kuweza kuwahimiza na kuwajenga wakristo wenzako, wakati huo huo pia wewe ukihimizwa na kujengwa katika ukristo wako. Hili ni jambo ambalo litakusaidia sana na kusaidia wakristo wenzako katika vita dhidi ya dhambi.

Katika kila kanisa, wakristo wanafaa kujitolea; kutembea pamoja katika upendo; kujitolea kusaidiana kiroho na kimwili kwa upendo. Msomaji wangu, je umeokoka? Na ikiwa umeokoka, je unawapenda watu wa Mungu na kujitoa kwa ajili yao? Je, unatumia karama ambazo Mungu amekupatia kwa ajili yao? Je, unatumia mali na kinywa chako kwa ajili yao?

Katika kanisa, kazi ya kuwasaidia wengi ni jukumu la kila mtu na pia ni jukumu la kanisa lote kwa ujumla. Tunafanya kazi hii kibinafsi na pamoja kama kanisa wakati tunafuata Kristo Yesu. Tunasaidiana wakati wa majaribu. Tunasaidiana wakati tunasoma neno la Mungu pamoja tukijiandaa katika vita vya kiroho na wakati tunaimba nyimba za sifa kwa Mungu na kuomba pamoja. Pia wakati huo huwa tunahimizana katika furaha na kushiriki shida na taabu pamoja. Bwana Yesu Kristo alisema, “Amri Yangu ndio hii: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi; Amri Yangu ndio hii, Mpendane” (Yohana 15:12;17). Yohana alisisitiza maneno haya wakati aliandika, “Watoto Wangu wadogo, tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali kwa tendo na katika kweli” (1 Yohana 3:18). Tushikane mikono kwa sababu sisi ni wakristo ili tuweze kulijenga kanisa la Kristo Yesu.

5. Kumtukuza Mungu.

Mwisho ni kwamba ikiwa kweli wewe ni mkristo unafaa kujiunga na kanisa ili umtukuze Mungu. Maisha ya wakristo wote yanafaa kuwa maisha ya kumtukuza Mungu. Petro aliandika, “Mwe na mwenendo mzuri mbele ya watu wasiomjua Mungu, ili kama wanawasema kuwa ninyi ni watenda mabaya, wayaone matendo yenu mema wamtukuze Mungu siku atakapokuja kuhukumu” (1 Petro 2:12). Petro alikuwa amefahamu mafundisho ya Bwana Yesu Kristo wakati aliandika mstari huu. Yesu Kristo alifundisha katika Mahubiri ya mlimani kwamba, “Nuru yenu iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni” (Mathayo 5:16). Mungu huwa anatukuzwa na matendo yetu kama wakristo ya kibinafsi na yale ambayo ni ya pamoja kama kanisa lake. Jinsi tunavyopendana kama wakristo huwa inadhihirisha kwamba sisi ni wafuasi wake Kristo Yesu. Yesu Kristo alisema, “Amri mpya nawapa: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane. Kama mkipendana ninyi kwa ninyi, kwa njia hii, watu watajua kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu” (Yohana 13:34-35).

Maisha ya kila mkristo yanafaa kudhihirisha kwamba kweli Yeye ni mtoto wa Mungu. Yesu Kristo alisema, “Nitalijenga kanisa langu” (Mathayo 16:18). Kwa sababu Kristo Yesu amejitolea kabisa kwa ajili ya kanisa lake, basi hata sisi ambao ni wake tunafaa kujitolea kabisa kwa Yeye.

Ikiwa wewe ni mkristo na umekuwa ukihudhuria kanisa ambalo linahubiri Biblia vyema na linasisitiza utakatifu, unaweza kuwa umeshushwa moyo kwa sababu ya jambo moja au lingine. Lakini ninakusihi kwamba hata kama mambo yako hivyo, usisahau majukumu yako kama mshirika wa kanisa hilo. Kumbuka kwamba msingi wako wa kuwa mshirika wa kanisa si yale ambayo unayafanya, bali ni kwa sababu wewe ni mtoto wa Mungu ambaye umeokolewa kwa neema Yake kupitia kwa imani ndani ya Kristo Yesu. Uhusiano ambao umeletwa ndani yake ni wa kumtukuza Mungu pekee. Hii ndiyo sababu ikiwa wewe ni mkristo, basi unafaa kujiunga na kanisa na kuwa mshirika humo.

Je, kuwa mshirika wa kanisa kunamaanisha nini?

Kuwa mshirika wa kanisa kunamaanisha kuishi maisha ya toba na kuamini. Kanisa ni jamii ya wale ambao wamezaliwa mara ya pili. Neema ya Mungu katika maisha yetu ambayo inatuwezesha kuishi maisha ya toba na imani inadhihirishwa na mambo mawili.

Kupitia kwa tendo la ubatizwa

Hii ndio hatua ya kwanza kwa mkristo ambaye ameokoka. Hili ni jambo ambalo Agano Jipya linafundisha; lazima mkristo abatizwe. Hili ni jambo ambalo Yesu Kristo mwenyewe aliamuru lifanywe (Mathayo 28:18-20) na pia linaonekana kutimizwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume na katika Agano Jipya lote. Ninajua kwamba kuna wengi ambao wanadai kuokoka lakini wao wanakataa kubatizwa. Kile kila mkristo anafaa kujua ni kwamba, kanisa halipewi mamlaka ya kutunga sheria, bali ni jukumu la kanisa kutii amri ambazo zimetungwa na Bwana Yesu Kristo katika neno Lake. Si jukumu la kanisa lolote kubadilisha au kurekebisha amri ambazo zimetungwa na Bwana Yesu Kristo. Kukataa kubatizwa au kukataa kushiriki meza ya Bwana au kukataa amri ambazo zimewekwa wazi kabisa katika neno la Kristo, ni kukataa ushirika miongoni mwa wale ambao ni wafuasi wa Kristo Yesu. Makanisa fulani fulani ambayo yanahubiri injili ya Kristo yameonyessha jambo hili kwa:

Kuandika kanuni fulani ambazo zinaambatana na neno la Mungu ambazo ndizo mwongozo wa makanisa hayo.

Maandishi haya yako katika makanisa na hata wakati mtu anafanyika mshirika wa kanisa, huwa ni lazima aweke sahihi yake kwa cheti cha maandishi haya. Wakati mtu anakubali kanuni zile, huwa anakubali kushiriki na kanisa lile katika mafundisho yake na mwenendo wa maisha ya watu wa kanisa hilo. Katika kanisa letu huwa tunasisitiza mambo haya.

1. Kuhudhuria ibada

Katika kitabu cha Waebrania 10:25, tunasoma kwamba hatufai kupuuza "Kukutana pamoja." Hii inamaanisha kwamba tunafaa kila wakati tujitolea kukutana pamoja kama wakristo. Hii inamaanisha kuhudhuria ibada zote za kanisa haswa zile za Jumapili.

2. Kushiriki meza ya Bwana

Wakati tunakutana kwa Meza ya Bwana huwa tunakumbuka kifo na kufufuka kwa Bwana Yesu Kristo. Pia huwa wakati huo tunaamua kuhudumiana kama watu wa kanisa moja. Ninajua kwamba kuna makanisa ambayo wakati unapokosa kwa Meza ya Bwana bila sababu ya kweli, huwa wanakuondoa katika ushirika wa kanisa.

3. Kuhudhuria mikutano ya kanisa

Kwa sababu wakristo wote ni kanisa moja, wakati wa mikutano ya kanisa ni wakati mzuri sana wa kukutana pamoja na kujadali mambo ya kanisa. Huu ni wakati muhimu sana katika maisha ya watu wa kanisa hilo. Hii ni mikutano ambapo kanisa linafanya uamuzi fulani wa muhimu sana.

4. Kuomba kila wakati

Biblia inawasisitizia wakristo kwamba, "ombeni pasipo kukoma" (1 Wathesalonike 5:17). Ikiwa kanisa lako lina orodha ya mambo ya kuombea, basi unafaa kuzingatia jambo hili ikiwa wewe ni mshirika wa kanisa hilo.

5. Hakikisha unatoa sadaka kwa ajili ya kazi ya Bwana

Biblia imejawa na maelezo kuhusu jinsi tunafaa kutoa. Kwa mfano Solomoni aliandika kwamba, "Mheshimu Bwana kwa mali zako na kwa malimbuko ya mazao yako yote" (Mithali 3:9). Kupitia kwa nabii Malaki, Mungu aliwahimiza Waisreali kwamba, "Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu. Nijaribu katika hili, asema Bwana Mwenye Nguvu, nanyi mwone kama sitafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka nyingi mpaka mkose nafasi ya kutosha au la" (Malaki 3:10).

Bwana Yesu Kristo pia Yeye alifundisha kwamba, "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa. Kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa" (Luka 6:38).

Paulo aliwaambia watu wa kanisa la Korintho kwamba, "Basi kuhusu changizo kwa ajili ya watakatifu. Kama nilivyowaagiza makanisa ya Galatia, fanyeni vivyo hivyo. Siku ya kwanza ya kila juma, kila mmoja wenu atenge kiasi cha fedha, kulingana na mapato yake na fedha hizo ziwekwe akiba ili nitakapokuja pasiwe na lazima ya kufanya mchango" (1 Wakorintho 16:1-2).

Paulo pia aliandika kwamba, "Kila mtu atoe kama anavyokusudia moyoni mwake, si kwa uchoyo au kwa kulazimishwa, kwa maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu" (2 Wakorintho 9:7).

Hili ni jukumu la kila mshirika wa kanisa. Kwa sababu kanisa ni mwili mmoja, basi ni lazima kila sehemu itimize jukumu lake. Kuwa mshirika wa kanisa si tu kwa kujulikana kwamba wewe ni mshirika, bali ni lazima tujitolee kabisa katika kila jambo kuona kwamba tunatimiza majukumu ambayo Bwana Yesu Kristo ametupatia.

Washirika ambao hawajitolei katika jambo lolote, huwa wanawachanganya wale ambao ni washirika wa kweli na wale ambao hawajaokoka kuhusu inamaanisha nini kuwa mkristo. Wale ambao tunajitolea katika kanisa katika mambo fulani fulani, hatuwasaidii hata kidogo wale ambao hawafanyi lolote ikiwa hatutawahimiza wafanya majukumu yao ya kiroho. Wakati tunajitolea katika majukumu yetu kwa furaha huwa tunawaonyesha wengine kwamba kweli sisi tumeokoka na tunampenda mwokozi wetu. Ni vigumu kuwa na hakikisho kwa mtu kwamba kweli ameokoka ikiwa yeye hataki kujihusisha na lolote katika kanisa ambalo anashiriki.

Tunafaa kuomba kwamba washiriki wa kanisa watajitolea kufanya majukumu yao kulingana na jinsi tumefundishwa na Bwana Yesu Kristo. Tuombe kwamba watu hawatapenda tu kuhudhuria makanisa, bali kwamba wale ambao wameokoka watajitoa kuwa washirika wa kweli wa makanisa na kwamba watajitahidi katika majukumu yao kwa utukufu wa Kristo Yesu.

Tuombe kwamba wale ambao ni washirika wa kanisa watajitlea kuhimizana, kuombeana na kurekebishana. Hatufai kuwaacha watu wawe tu washiriki wa kanisa kwa sababu wanataka tu kuonekana kwamba wao ni washirika wa kanisa fulani. Kulingana na Biblia mshirika wa aina hiyo si mshirika wa kanisa hilo. Kwa sababu kuwa mshirika wa kanisa kwa njia moja ni kushirikishwa katika mwili wa Kristo. Inamaanisha kuishi pamoja kama wasafiri katika ulimwengu huu tunapoelekea mbinguni. Pia ishara ya kanisa ambalo linaendelea vyema ni kuwa na ufahamu halisi kuhusu jambo hili la mshirika wa kanisa ni nani.

Kujiunga na kanisa fulani na kuwa mshirika huko ni ishara ya nje ambayo inaonyesha upendo wa Kristo na watu wake ambao uko katika moyo wa mtu. Kwa kawaida upendo huwa unadhihirika sana katika kujitolea kabisa kwa mtu na katika mambo yote. Kwa mfano kijana anaonyesha upendo wake kwa msichana kwa kufanya uamuzi wa kumwoa.

Tunasoma katika Waefeso 5:25 kwamba, "Ninyi waume, wapende wake zenu, kama vile Kristo alivyolipenda kanisa akajitoa kwa ajili yake." Katika Matendo ya Mitume 20:28 tunakumbushwa kwamba kanisa lilinunuliwa kwa damu ya Kristo Yesu. Ikiwa kweli sisi ni watu ambao wanamfuata Kristo, basi tutapenda kanisa lake ambalo alilinunua kwa damu yake.

Kwa hivyo usihudhurie tu kanisa hata kama ni vyema sana kuhudhuria kanisa, bali ikiwa umeokoka jiunge na kanisa na uwe mshirika wa kanisa moja. Jiunge na wakristo wengine. Fanya hivi ili wale ambao hawajaokoka waweze kusikia ujumbe wa injili na wale ambao ni wakristo wadhaifu waweze kuhimizwa na kushughulikiwa; na wale ambao ni wakristo ambao wamekua katika imani waweze kutumia uwezo ambao wamepewa na Mungu kuwafaidi wengine. Fanya hivi ili uweze kuwahimiza wachungaji na wale ambao ni vyongozi katika kanisa lako. Fanya haya yote kwa utukufu wa Mungu.

Unapotazama, utaona kwamba katika karne hii, watu wengi wamekuwa hawajali kanisa kabisa. Wanajali tu kujulikana wao wenyewe. Tuombe kwamba Mungu huisha makanisa yetu na kupitia kwa kupendana kama wakristo, upendo wa Mungu utadhihirika kwa ulimwengu wote.

Ishara ya 7

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kanisa ambalo linatekeleza nidhamu katika kanisa

I. Je, nidhamu katika kanisa ni mbaya?

II. Je, nidhamu katika kanisa ni nini?

III. Je, Biblia inafundisha nini kuhusu nidhamu katika kanisa?

1. Waebrania 12:1-14
2. Mathayo 18:15-17
3. 1 Wakorintho 5:1-11
4. Wagalatia 6:1
5. 2 Wathesalonike 3:6-15
6. 1 Timotheo 1:20
7. 1 Timotheo 5:19-20
8. Tito 3:9-11

IV. Je, wakristo wamekuwa wakishughulikiaje nidhamu katika kanisa?

V. Kuna wale ambao wanasema kwamba huwa kanisa lao halitekelezi nidhamu.

VI. Je, kwa nini tunafaa kuhakikisha kwamba kuna nidhamu katika makanisa yetu?
1. Ili tuweze kumfaidi yule ambaye anaadhibiwa
2. Ili tuwaonyeshe wengine hatari ya dhambi
3. Ili kanisa liweze kuendelea vyema kiroho
4. Ili kanisa liweze kushuhudia kwa pamoja
5. Ili Mungu aweze kutukuzwa katika maisha ya watu Wake

VII. Je, itakuaje ikiwa hatutilii maanani nidhamu katika makanisa yetu?

Mafundisho ya Biblia kuhusu nidhamu katika kanisa

Swali ambalo kila mkristo anafaa kujiuliza ni, je, wakristo wanafaa kuishi kivyao au tunayo majukumu juu ya wakristo wenzetu? Je, majukumu haya kwa wakristo wenzetu ni ya kuwahimiza tu kwa maneno mazuri au pia yanahusu kuwaambia ukweli wakati tunaona kwamba wao hawatembei vizuri katika imani yao? Je, hatufai kuwaeleza ukweli wakati tunaona kwamba wao wameanguka dhambini au mwenendo wao umebadilika na kuwa kama ule wa walimwengu? Ni jukumu la kila mkristo kuwa mlinzi wa mwenzake. Hata wakati mwingine itatubidi kuweka wazi mambo fulani ili yaweze kushughulikiwa na kanisa lote kwa njia ya kuwasaidia wakristo wenzetu.

Kanisa ambalo linaendelea vyema, ishara moja yake ni kwamba kanisa hili linazingatia nidhamu. Wakati tunatazama jambo hili, tutajiuliza maswali haya yafuatayo.

1. Je, nidhamu ni mbaya?
2. Je, nidhamu katika kanisa ni nini na inahusisha nini?
3. Je, ni wapi Biblia inazungumzia jambo hili la nidhamu na inasema nini kulihusu?
4. Je, wakristo ambao wameishi mbeleni wamelishughulikiaje jambo hili la nidhamu katika kanisa?
5. Kuna makanisa ambayo hayatekelezi jambo hili.
6. Je, kwa nini tutilie maanani nidhamu katika kanisa?
7. Je, itakuwaje ikiwa hatutatilia maanani nidhamu katika makanisa yetu?

1. Je, nidhamu ni mbaya?

Mafundisho kuhusu nidhamu katika kanisa ni mafundisho ambayo yanaonekana kuwa hayapendezi. Lakini ukweli ni kwamba kuna faida kubwa sana ikiwa tutajifunza mafundisho haya na kuyaelewa jinsi Biblia inayafundisha. Wakati tunasikia kuhusu nidhamu, huwa tunawaza kuhusu watoto na wazazi wao; haswa wakati mzazi anamchapa mtoto.

Ikiwa mtu anajiangalia ndani mwake vyema, ataona kwamba kweli yeye ni mtu ambaye anahitaji kurekebishwa. Ukweli ni kwamba hakuna hata mmoja wetu ambaye amekamilika. Kila mtu anahitaji kukumbushwa, kurekebishwa, kuhimizwa na kukemewa. Jambo moja kila mmoja anafaa kukubali ni kwamba sisi sote tunahitaji kuadhibiwa au nidhamu. Tusipuuze kwa kusema kwamba tuko sawa kana kwamba Mungu amemaliza kazi ya tukamilisha katika maisha haya.

Ikiwa kweli tutakubali kwamba tunahitaji nidhamu, basi tutaona kwamba nidhamu hii si kitu kibaya bali ni kitu kizuri kwetu ambacho

kinatusaidia katika maisha yetu ya kiroho. Ni kupitia kwa kuonywa na kuhimizwa kila wakati ndipo tutakua katika ukristo wetu na kuweza kshi maisha matakatifu. Kwa mfano ikiwa unaonywa kuhusu maneno ambayo unazungumza, utasaidika sana kuweza kujichunga kutokana na maneno ambayo unayazungumza. Tunapoenda kwa shule huwa tunafundishwa mambo fulani fulani kama njia ya kutuweka nidhamu. Katika jamii, kanisani na hata katika uhusiano wetu na wengine, huwa tunafundishwa mambo fulani ili tuweze kuwa na nidhamu katika mambo haya. Maneno mazuri ya ushauri ambayo umeyasikia kutoka kwa mtu fulani, yote yalikusudiwa kukusaidia kuwa na nidhamu.

Katika sura hii ya kitabu hiki, tutatazama jambo hili la nidhamu kulingana na mafundisho ya Biblia. Lakini tufahamu kwanza nidhamu si jambo baya.

2. Je, nidhamu katika kanisa ni nini?

Wakati tunasikia kuhusu nidhamu katika kanisa, huwa tunawaza tu kuhusu mambo mabaya. Mara kwa mara huwa tunajaribu kujitetea kwa kusema mambo kama, “Je, si Yesu Kristo alisema kwamba, usimhukumu yeyote ili hata wewe usihukumiwe” (Mathayo 7:1).

Ukweli ni kwamba katika Mathayo 7:1, Bwana Yesu alikataza kuhukumu wengine. Lakini unaposoma kitabu hicho hicho, utapata kwamba Bwana Yesu Kristo anatuhimiza kukemea wengine kwa sababu ya dhambi hata wazi kabisa (Mathayo 18:15-17; Luka 17:3). Wakati Kristo alikuwa akizungumza kuhusu kuhukumu katika Mathayo 7, hakuwa anaondoa mafundisho ya Mathayo 18.

Kumbuka kwamba Mungu mwenyewe ni hakimu na anatarajia tufanye jukumu hili lakini kwa upendo juu ya wengine. Mungu amepatia serikali jukumu la kuhukumu (Warumi 13:1-7). Katika Biblia pia tunahimizwa kujichunguza wenyewe (1 Wakorintho 11:28; 2 Wakorintho 13:5; Waebrania 4; 2 Petro 1:5-10). Pia tumeamriswa kuchunguza wakristo wenzetu pamoja kama kanisa (Mathayo 18; 1 Wakorintho 5-6). Kama kanisa ni lazima tuelezeana jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu ya wokovu.

Ikiwa kweli tunataka kuona makanisa yetu yakikua, ni lazima tuhakikishe kwamba wale ambao wanajiunga na makanisa yetu wawe ni watu ambao kweli wameokoka na wamejitolea kwa Bwana Yesu Kristo. Ni lazima tuwaonyeshe watu kwamba kuna tofauti kubwa sana kati ya kanisa la Kristo na ulimwengu. Lazima watu wafahamu inamaanisha nini kuwa mkristo wa kweli. Ikiwa kuna mtu ambaye anadai kwamba yeye ni mkristo lakini maisha yake ni tofauti kabisa na kile ambacho anadai kusema, basi tunafaa tuwe kama mtume Paulo ambaye alisema kwamba, kwa ajili ya utukufu wa Mungu na kwa uzuri wa mtu huyu, basi asiwe mshirika wa kanisa.

Nidhamu katika kanisa inafaa kuonyeshwa katika jinsi tunawakubali watu kuwa washirika wa kanisa. Katika 1 Wakorintho 5:9-10 tunasoma kwamba, “Niliwaandikia katika waraka wangu kuwa msishirikiane na wazinzi. Sina maana kwamba msishirikiane na wazinzi wa ulimwengu huu, au wenye tamaa mbaya, wanyang'anyi au waabudu sanamu. Kwa kufanya hivyo ingewabidi mtoke humu alimwenguni.” Unaposoma mistari hii utaona kwamba Paulo anaonyesha kabisa tofauti kubwa iliyoko kati ya kanisa la Kristo na ulimwengu. Je, sisi ambao ni wakristo leo, huu ndio msimamo wetu au sisi huwa tunaona kwamba hakuna tofauti ya kanisa la Kristo na ulimwengu. Kwa kusema hii simaanishi kwamba kanisa la Kristo limejawa na watu ambao ni wakamilifu na ulimwengu umejawa na wote ambao ni wabaya sana. Swali langu ni, je kuna tofauti yoyote katika ya watu wa kanisa la Kristo na wale ambao hawajaokoka? Kulingana na Biblia ni kwamba, kuna tofauti kubwa sana kati ya wale ambao wameokoka na wale ambao hwajaokoka. Kuwa mshirika wa kanisa ni kuwa mmoja wa mwili wa Kristo.

Kwa hivyo wakati tunawaleta watu katika ushirika wa kanisa, lazima tuhakikishe kwamba wanaishi maisha ambayo yanamtukuza Kristo. Ni lazima tuwaonyeshe umuhimu wa kujitolea katika kuwa mshirika wa kanisa. Ni lazima tuwaonyeshe umuhimu wa uamuzi ambao wanataka kufanya. Ikiwa tutakuwa waangalifu kuhusu wale ambao tunaleta katika ushirika wa kanisa, basi tutapunguza sana shida ambazo tutaweza kukumbana nazo katika kutilia mkazo nidhamu katika kanisa. Kwa sababu sitaweza kusema kila kitu katika sura hii kuhusu jambo hili, ningependa kukuhimiza kama unaweza utafute vitabu hivi kwa sababu vitakusaidia sana kuhusu jambo hili.

(i) “The compromuised Church” ambacho kimeandikwa na John Amstrong.
(ii) “Church Discipline” ambacho kimeandikwa R. Albert Mohler.
(iii) “Biblical Church Discipline” ambacho kimeandikwa na Daniel Wray.
(iv) “Democratic Religion” ambacho kimeandikwa na Grey Wills.
(v) “Manual of Church Polity” ambacho kimeandikwa na John L. Dagg.
(vi) “How Christians should live together in a church” ambacho kimehakikishwa na Mark Dever.
(vii) “Handbook of Church Discipline ambacho kimeandikwa na Jay Adams
(viii) “Life together” ambacho kimeandikwa Dietrich Bonhoeffer

III. Je, Biblia inafundisha nini kuhusu nidhamu katika kanisa?

Tutatazama vifungu 8 katika Biblia ambavyo vinazungumza kuhusu jambo hili la nidhamu katika kanisa.

1. Waebrania 12:1-14

“Kwa sababu hii, kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa namna hii la mashahidi, basi na tuweke kando kila kitu kinachotuzuia na ile dhambi inayotuzinga kwa urahisi, nasi tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa kwa ajili yetu. Basi tutazame sana Yesu mwanzilishi na mkamilishaje wa imani yetu, Yeye ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake alistahimili msalaba, Naye ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Mtafakarini sana Yeye aliyestahimili upinzani mkuu namna hii kutoka kwa watu wenye dhambi, ili kwamba msije mkachoka na kukata tamaa. Katika kushindana kwenu dhidi ya dhambi, bado hamjapigana kiasi cha kumwaga damu yenu. Nanyi mmesahau yale maneno ya kuwaonya yanayowataja ninyi kuwa wana, yakisema, 'Mwanangu, usidharau kuadibishwa na Bwana wala usikate tamaa, kwa sababu Bwana huwaadibisha wale awapendao na humwadhibu kila mmoja anayemkubali kuwa mtoto Wake.' Vumilieni taabu kwa ajili ya kufunzwa adabu. Mungu anawatendea ninyi kama watoto Wake, kwa maana ni mtoto yupi asiyeadibishwa na mzazi wake? Kama hakuna kuadibishwa (ambalo ni fungu la watoto wote), basi ninyi ni watoto haramu wala si watoto halali. Tena sisi sote tunao baba wa kimwili, waliotuadibisha nasi tukawaheshimu kwa ajili ya hilo. Je, si inatupasa kujinyenyekeza zaidi kwa Baba wa roho zetu ili tuishi? Baba zetu waliotuadibisha kwa kitambo kidogo kama wao wenyewe walivyoona vema, lakini Mungu hutuadibisha kwa faida yetu ili tupate kushiriki utakatifu Wake. Kuadhibiwa wakati wowote hakuonekani kuwa kitu cha kufurahisha bali chenye maumivu kinapotekelezwa. Lakini baaadaye huzaa matunda ya haki na

amani kwa wale waliofunzwa nayo. Kwa hiyo itieni nguvu mikono yenu iliyo dhaifu na magoti yenu yaliyolegea. Sawazisheni mapito ya miguu yenu, ili kitu kilicho kiwete kisidhoofishwe bali kiponywe. Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote na huo utakatifu, ambao bila kuwa nao, hakuna mtu atakayemwona Bwana."

Mungu mwenyewe huwa anatuadibisha na ametuamrisha kufanya hivyo katika kanisa lake. Hili ni jukumu la kanisa.

2. Mathayo 18:15-17

"Kama ndugu yako akikukosea, nenda ukamwonyeshe kosa lake, kati yenu ninyi wawili peke yenu. Kama akikusikiliza, utakuwa umepata tena ndugu yako. Lakini kama hatakusikiliza, nenda na mtu mwingine mmoja au wawili ili kila neno lithibitishwe na ushahidi wa mashahidi wawili au watatu. Kama akikataa kuwasikiliza hao, liambie kanisa, naye kama akikataa kulisikiliza kanisa, basi mtendeeni mtu huyo kama vile ambavyo mngemtendea asiyeamini."

Katika kifungu hiki tunapata mafundisho kuhusu nidhamu katika kanisa la Kristo Yesu. Je, wakati mtu akikukosea utafanya nini? Je, wewe hunyamanza na kukosa kuzungumza naye? Je, wewe uanza kuchukia mtu huyo kabisa na kuacha kuzungumza naye? Katika kifungu hiki cha Mathayo 18:15-17, Bwana Yesu Kristo anafundisha jinsi mtu anafaa kufanya wakati amekosewa.

3. 1 Wakorintho 5:1-11

"Kuna habari za kweli kwamba miongoni mwenu kuna uasherati ambao haujatokea hata miongoni mwa watu wasiomjua Mungu: kwamba mtu awe na mke wa baba yake. Nanyi mwajivuna! Je, haiwapasi kuhuzunika na kumtenga mtu huyo aliyefanya mambo hayo na ushirika wenu? Hata kama siko pamoja nanyi katika mwili, niko nanyi katika roho. Nami nimekwisha kumhukumu mtu huyo aliyetenda jambo hili, kama vile ningekuwapo. Mnapokutana katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo nami nikiwepo pamoja nanyi katika roho na uweza wa Bwana Yesu ukiwepo, mkabidhini mtu huyo kwa shetani, ili asili ya dhambi iangamizwe lakini roho yake iokolewe katika siku ya Bwana. Majivuno yenu si mazuri. Je, hamjui ya kwamba chachu kidogo huchachusha donge zima la unga? Ondoeni chachu ya kale ili mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Kristo, Mwana-Kondoo wetu wa pasaka amekwisha tolewa kuwa dhabihu. Kwa hiyo, tusiiadhimishe sikukuu hii, kwa chachu ya zamani, chachu ya nia mbaya na ouvu, bali kwa mkate usiotiwa chachu, ndio weupe wa moyo na kweli. Niliwaandikia katika waraka wangu kuwa msishirikiane na wazinzi. Sina maana kwamba msishirikiane na wazinzi wa ulimwengu huu, au wenye tamaa mbaya, wanyang'anyi au waabudu sanamu. Kwa kufanya hivyo ingewabidi mtoke humu ulimwenguni. Lakini sasa nawaandikia kwamba msishirikiane na mtu ye yote anayejiita ndugu lakini akiwa ni mzinzi, au mwenye tamaa mbaya, mwabudu sanamu au msingiziaji, mlevi au mdhalimu. Mtu kama huyo hata msile naye."

Katika kifungu hiki tunasoma kumhusu mtu mmoja ambaye alikuwa mzinifu katika kanisa la Korintho. Swali ni, je kwa nini Paulo alisema maneno haya yote? Je, jibu ni kwamba alikuwa amemchukia mtu huyo? Ukweli ni kwamba aliandika haya kwa sababu alikuwa anajua kwamba mtu huyo alikuwa anajidanganya kabisa katika ukristo wake. Huyo mtu aliwaza kwamba yeye akiwa mkristo anaweza kuendelea kuishi maisha ya dhambi. Yeye aliwaza kwamba kanisa lilikuwa limemkubali aendelelee kufanya tabia ambayo alikuwa nayo. Paulo anasema kwamba mtu wa aina hii ni mtu ambaye amedanganyika na ili mtu kama huyo aweze kuokolewa na pia kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ni lazima aonyeshwe kwamba jinsi anayoishi maisha yake ni kinyume kabisa na yale ambayo anayakiri.

4. Wagalatia 6:1

"Ndugu zangu, kama mtu akipatikana na dhambi fulani, basi nanyi mlio wa rohoni, mrejezeni upya mtu huyo kwa roho ya upole. Lakini jihadharini, ili ninyi wenyewe msije mkajaribiwa."

Mstari huu ni wa muhimu sana wakati tunawaza na kutekeleza nidhamu katika kanisa. Katika mstari huu, Paulo anatueleza jinsi tunafaa kumrejesha mtu ambaye amepatikana katika dhambi.

5. 2 Wathesalonike 3:6-15

"Ndugu, tunawaagiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, jitengeni na kila ndugu ambaye ni mvivu na ambaye haishi kufuatana na maagizo tuliyowapa. Maana ninyi wenyewe mnajua jinsi iwapasavyo kufuata mfano wetu. Sisi hatukuwa wavivu tulipokuwa pamoja nanyi, wala hatukula chakula cha mtu yeyote pasipo kukilipia. Badala yake tulifanya kazi kwa bidii usiku na mchana, ili tusimlemee mtu yeyote miongoni mwenu. Tulifanya hivi, si kwa sababu hatukuwa na haki ya kupata msaada kama huo, lakini ili kusudi tujifanye sisi wenyewe kuwa kielelezo. Kwa maana hata tulipokuwa pamoja nanyi, tuliwapa amri ili kwamba: 'Mtu yeyote asiyetaka kufanya kazi, wala asile.' Kwa kuwa tunasikia kwamba baadhi ya watu miongoni mwenu ni wavivu. Hawafanyi kazi bali hujishughulisha na mambo ya wengine. Basi watu kama hao tunawaagiza na kuwaonya katika Jina la Bwana Yesu Kristo wafanye kazi kwa utulivu na kujipatia mahitaji ya maisha yao wao wenyewe. Kwa upande wenu, ndugu, ninyi kamwe msichoke katika kutenda mema. Ikiwa mtu yeyote hayatii maagizo yetu yaliyoko katika barua hii, mwangalieni sana mtu huyo. Msishirikiane naye, ili kwamba apate kuona aibu. Lakini msimhesabu kuwa adui, bali mwonyeni kama ndugu."

Katika kanisa la Thesalonike, kuna wandugu ambao walikuwa wavivu na hawakutaka kufanya lolote. Ni wazi kwamba watu hawa walikuwa wanatetea hali yao ya uvivu kwa kusema kwamba hayo yalikuwa mapenzi ya Mungu. Lakini katika mistari hii, Paulo anawaonya wandugu wa kanisa hili kuhusu kushirikiana na watu kama hawa. Yeye aliwaonya wale ambao walikuwa wavivu kwamba walihitaji kufanya kazi ili waweze kushughulikia maisha yao wenyewe.

6. 1 Timotheo 1:20

"Miongoni mwao wako Himenayo na Aleksanda, ambao nimemkabidhi Shetani ili wafundishwe wasije wakakufuru."

Hawa ni wale ambao walikuwa hawaishi maisha yao kulingana na neno la Mungu.

7. 1 Timotheo 5:19-20

“Usiendekeze mashtaka dhidi ya mzee ila yawe yameletwa na mashahidi wawili au watatu. Wale wanaodumu katika dhambi uwakemee hadharani, ili wengine wapate kuogopa.”

Hapa Paulo anamhimiza Timotheo jinsi alifaa kufanya wakati viongozi wanapatikana katika dhambi.

8. Tito 3:9-11

“Lakini jiepushe na maswali ya kipuzi, mambo ya koo, mabishano na ugomvi kuhusu sheria, kwa sababu haya hayana faida tena ni ubatili. Mtu anayesababisha mafarakano, mwonye mara ya kwanza, kisha mwonye mara ya pili. Baada ya hapo, usihusike naye tena. Kwa kuwa unajua kwamba mtu kama huyo amepotoka na tena ni mwenye dhambi. Yeye amejihukumu mwenyewe.”

Katika kanisa ambapo Tito alikuwa mchungaji, kulikuwa na watu ambao walikuwa wanaleta migawanyiko katika kanisa juu ya mambo ambayo hayakuwa na umuhimu wowote.

Tunapoasoma mistari hii yote, tunaona kwamba Mungu anajali sana jinsi tunavyofahamu neno lake na jinsi tunavyoishi kulingana na neno hilo. Zaidi pia anajali jinsi tunavyoishi kama wakristo. Mambo yote ambayo yametajwa katika mistari hii ni mambo ambayo ni ya kweli ambayo yanahitaji kushughulikiwa nasi na ni mambo ambayo kanisa lote linafaa kuzingatia haswa katika mambo ya nidhamu.

Katika mistari hii, Biblia inaonyesha wazi kabisa jinsi nidhamu inafaa kutekelezwa: “Je, haiwapasi kuhuzunika na kumtenga mtu huyo aliyefanya mambo hayo na ushirika wenu?.....mkabidhini mtu huyu kwa Shetani....msishirikiane na wazinzi...mtu kama huyo hata msile naye” (1 Wakorintho 5:2,5,9,11); “Jitengeni” (2 Wathesalonike 3:6); “Ikiwa mtu yeyote hayatii maagizo yetu yaliyoko katika barua hii, mwangalieni sana mtu huyo. Msishirikiane naye, ili kwamba apate kuona aibu” (2 Wathesalonike 3:14-15); “nimemkabidhi Shetani” (1 Timotheo 1:20); “uwakemee hadharani” (1 Timotheo 5:20); “Jiepushe na watu wa namna hiyo” (2 Timotheo 3:5); “usihusike naye tena” (Tito 3:10).

Yesu Kristo pia alizingumza kuhusu nidhamu katika kanisa wakati alisema kwamba, “Kama akikataa kuwasikiliza hao, liambie kanisa, naye kama akikataa hata kulisikiliza kanisa, basi mtendeeni mtu huyo kama vile ambavyo mngemtendea asiyeamini” (Mathayo 18:17).

Hivi ndivyo Biblia inavyofundisha kuhusu nidhamu katika kanisa.

4. Je, wakristo ambao wameishi mbeleni wamelishughulikiaje jambo hili la nidhamu katika kanisa?

Wakristo ambao wamekuwepo mbele wamelishughulikia jambo hili. Ni wazi kwamba mambo ya nidhamu yalikuwa miongoni mwa mambo ambayo yalishughulikiwa katika mikutano kanisa karne ya 18 na ya 19.

Mwandishi mmoja ambaye aliitwa Dana alisema kwamba, “Kukosa kuzingatia nidhamu ya kanisa ni jambo baya sana.” Katika makanisa ya zamani, nidhamu ilizingatiwa kiwango kwamba wale ambao walikuwa wanaitekeleza, walifanya hivyo kwa kuwadhulumu wengine. Kwa hivyo watu wengi hawakuipendelea. Leo ni kinyume kabisa kwa sababu makanisa yamepuuza kabisa jambo hili la nidhamu na kufanya watu waishi maisha yao kana kwamba hakuna maagizo kuhusu jambo hili katika Biblia. Kwa hivyo tuombe Mungu kwamba atawaleta wachungaji ambao watasisitiza jambo hili kwa uangalifu kabisa na pia kwamba hawatatumia mamlaka yao vibaya katika jambo hili.

Mwingine ambaye anaitwa Greg Wills, anasema kwamba, katika karne ya 18 lilikuwa jukumu lao kuhubiri Biblia na kutekeleza nidhamu katika kanisa kulingana na mafundisho ya Biblia. Wakristo katika karne hii, walijitolea kabisa kuona kwamba kanisa linatekeleza nidhamu bila kutatizwa na serikali. Wills anasema kwamba kanisa la Southern Baptist kila mwaka liliwatoa wengi kutoka kwa ushirika kama 2%. Wakati walipokuwa wanafanya haya, kanisa hili liliendelea kukua sana. Kwa hivyo wale wengi ambao wanasema kwamba kutilia mkazo nidhamu katika kanisa ni jambo ambalo litawazuia wengi kujiunga na makanisa, si la kweli hata kidogo. Tunavyoendelea kujitahidi katika utakatifu ndivyo Mungu anavyotumia hali hiyo kuwaokoa wengi.

Kulingana na mafundisho ya Bwana Yesu Kristo, maneno yetu na maisha yetu yanafaa kueleza jambo moja. Ikiwa tutazungumza maneno ya Biblia lakini maisha yetu ni kinyume na yale ambayo tunasema, basi kazi yetu ya uinjilisti haitafaulu. Makanisa ambayo hayana nidhamu, yamekuwa kizuizi kikubwa sana kwa kueneza Injili ya Kristo Yesu.

Wills anasema kwamba jambo hili la nidhamu katika kanisa linapuuzwa kwa sababu wakristo wamegeukia mambo mengine kama kuupenda ulimwenguni na vitu vyake. Makanisa yanayozingatia sana mambo ya ulimwengu, ndiyo yanapuuza na kusahau mambo ya mbinguni. Kutoka mwaka wa 1850 hadi 1920 wakati watu walitaka sana kuwaona wengi wakijaa katika makanisa yao, nidhamu ilipungua katika makanisa. Nidhamu katika kanisa ndiyo tofauti iliyoko kati ulimwengu na kanisa.

Baada muda fulani, nidhamu katika kanisa ilipungua kwa sababu ilionekana kuwa mzingo kwa wengi. Wengi walikataa kuishi kulingana na nidhamu ya kanisa na makanisa yalianza kuogopa kuwatenga. Kwa sababu ya kutaka mijengo mikubwa, umati mkubwa, muziki na mahubiri ya kufurahisha, makanisa yalikataa na kupuuza kabisa nidhamu katika kanisa. Makanisa mengi ya kibaptisti yaliacha kuongozwa na utakatifu katika makanisa yao na kuanza kushughulikia wingi wa watu. Walisahau jambo la kuwarekebisha wale ambao walikuwa wanaenenda kinyume na kanuni za Biblia. Hakuna kanisa ambalo lilijitokeza na kuzungumza wazi kuhusu nidhamu katika makanisa ambayo ilikuwa imepotea. Hakuna mchungaji ambaye alijitokeza kukemea jambo la kuwataka wengi wajae katika makanisa badala ya kuwataka wengi waishi maisha matakatifu. Nidhamu hii ilipotea kabisa.

Majukumu ya mchungaji yalibadilika kwa sababu ya kukosa kutilia mkazo nidhamu katika kanisa. Awali kazi ya mchungaji ilikuwa kuona kwamba watu wanaishi maisha matakatifu na kwamba wanaendelea kukua katika ukristo wao. Lakini sasa ilijumlisha kuwalazimisha wengi kuokoka. Kutoa uamuzi wa kununua vifaa vya muziki na mikutano ya kufanya mambo mengine. Mchungaji aligeuka kuwa mtu ambaye anaitwa tu wakati kuna hali ya nidhamu ambayo ilikuwa ngumu sana. Kanisa sasa halikuwa mahali ambapo watu walionekana kuwa kitu kimoja na walijaliana na kupendana kama mandugu wa kiroho. Mchungaji alishughulika tu na mambo ambayo yalionekana kwamba huwa yanaweza kufanya kanisa liaibike au liangamie.

Katika mambo haya yote, kazi ya mchungaji ilipotea. Zaidi ni kwamba tofauti ambayo ilikuwapo kati ya ulimwengu na kanisa ilipotea. Jambo hili liliumiza kanisa sana na pia liliumiza maisha ya wakristo. Wakristo wa kweli wa mbeleni walijitahidi kuishi kulingana na nidhamu ya Biblia. Katika mwaka wa 1561, wakristo wengi walieleza kufahamu jambo hili katika maneno ya Belgic Confession. Walisema, ishara kuu za kanisa la kweli ni hizi: Kufundisha na kuhubiri injili ya Kristo; kushiriki baraka ambazo Kristo ameweka; kutilia mkazo nidhamu katika kanisa. Kwa ufupi ni kwamba kutekeleza kila jambo kulingana na neno la Mungu na kukataa kila kitu ambacho hakitokani na neno la Mungu. Ni lazima kanisa hilo limtambue Kristo Yesu kuwa kichwa cha kanisa. Ni lazima kanisa hilo lishikilie ukweli huu na likatae mambo mengine.

Ni wazi kwamba wakristo wa mbeleni walizingatia sana nidhamu katika kanisa.

5. Kuna makanisa ambayo hayatekelezi jambo hili.

Ikiwa mshirika wa kanisa mmoja anamkosea mshirika mwingine na kosa hilo liwe ambalo limefanyika mbele ya wengine, jukumu la yule ambaye amekosewa ni kuzungumza na yule ambaye amemkosea ili waweze kutatua jambo hilo. Lengo la kufanya hivi ni kurudisha ushirika kati ya wawili hawa kama tu jinsi tunavyofundishwa katika Mathayo 18:15. Ikiwa yule ambaye amekosa anakataa kuomba msamaha, ni jukumu la yule ambaye amekosewa kutafuta mtu mmoja au wawili kutoka katika kanisa wamsaidie kupatana na yule ambaye amemkosea kulingana na mafundisho ya Biblia katika Mathayo 18:16.

Ikiwa mtu huyu ataendelea kukataa, basi ni jukumu la yule ambaye amekosewa kupeleka jambo hilo mbele ya kanisa kulingana na mafundisho ya Mathayo 18:17. Ikiwa hata baada ya kuelezwa na kanisa bado ataendelea kukataa, basi ni jukumu la kanisa kupeleleza jambo hilo na kujua ukweli kabisa halafu kuchukua hatua ambayo Biblia imeweka.

Makosa ya mtu ambaye ameshitumiwa, yanafaa kuandikwa na mchungaji kupewa nakala pamoja na mashamasi na yule ambaye ameshitumiwa kabla ya kupewa kanisa lote. Ikiwa mtu yule hataungama makosa yake, basi Biblia inasema kwamba atengwe. Hiki ni kitendo cha sheria ambacho kimekubaliwa na Bwana Yesu Kristo kwamba kanisa ikitekeleze (Mathayo 18:17). Hakuna mshirika wa kanisa ambaye anafaa kutengwa kabla ya kuitwa na kusimama mbele ya kanisa na kuambiwa makosa yake na kupewa nafasi ya kujitetea. Mwenye kushitumiwa ana jukumu na fursa ya kujibu maswali yoyote ambayo anaulizwa na kanisa.

Mshirika wa kanisa anafaa kuadhibiwa kwa sababu ya:

- Kuishi maisha ya dhambi waziwazi bila kutubu.
- Kufanya mambo ambayo yatawafanya wengi kudharau kanisa.
- Kukosa kuhudhuria kanisa mara kwa mara bila sababu yoyote.
- Kufundisha mafundisho ambayo ni kinyume na mafundisho ya Biblia.
- Kukosa kutolea kazi ya Mungu kulingana na uwezo wake.
- Kutojali shughuli za kanisa au kufanya mambo ambayo yanaonekana kuleta utata au migawanyiko katika kanisa.
- Kujihusisha na watu ambao hawana haja kamwe na kanisa au yale ambayo kanisa linafanya.
- Kuishi kinyume na matakwa ya serikali na kinyume na maisha ya wale ambao wanakiri kuokoka.

6. Je, kwa nini tutilie maanani nidhamu katika kanisa?

Je, unajua kwamba kanisa lako linatekeleza majukumu yake vyema? Je, unajuaje kwamba mambo yanaendelea vyema katika kanisa lako? Biblia inafundisha kwamba upendo hufunika wingi wa dhambi. Makanisa mengi leo wanawaza kwamba tukiwaadhibu washirika si wengi ambao watakuja. Lakini tusipozungumza kuhusu dhambi zao, wengi watakuja. Mara nyingi huwa tunawaza kwamba kwa sababu kanisa ni kubwa na idadi yake ya watu ni kubwa mno, basi kanisa hilo linaendelea vyema kiroho. Kwa sababu ya wingi wa watu, wachungaji wengi huwa wanajidanganya kwa kuwaza kwamba kila kitu ambacho wanafanya ni sawa. Kwa sababu watu ni wengi katika kanisa lako, usiwaze kwamba mambo ni sawa.

Kuna makanisa ambayo yana maelfu ya watu. Watu huyapenda makanisa haya kwa sababu muziki ambao unachezwa huko ni wa kupendeza, mipangilio katika makanisa haya ni mizuri na watu huwa wanaingizwa katika huduma kwa haraka sana.

Kwa sababu kanisa linataka kuonekana kama ulimwengu ili liweze kuushuhudia ulimwengu, limekuwa kama ulimwengu. Kwa kufanya hivi, kanisa halionyeshi utakatifu ambao unafundishwa katika Biblia. Makanisa mengi leo, yamejawa na watu ambao ni wagonjwa kiroho na hawana mtu wa kuwashughulikia na kuwalinda kutokana na mafundisho kuhusu kuishi maisha matakatifu na kuwaonya kuhusu mafundisho ya uongo. Wakristo katika makanisa haya ni wale ambao wanahubiriwa kuhusu neema na unyenyekevu na kuhusu dhambi lakini huwa hawanyenyekei wala kukubali dhambi zao. Kuna wengi ambao wamepotea katika dhambi zao na wako katika makanisa ambayo hayana mtu wa kuwasaidia au kuwarekebisha.

Si rahisi kuwa waaminifu katika jambo hili la nidhamu wakati makanisa mengi hayashughulikii kamwe jambo hili. Si jambo rahisi kuwahimiza wengi kuwa washirika wa makanisa kwa sababu wengi huwa hawaoni maana ya jambo hili. Lakini hata kama si jambo rahisi, tunafaa kuomba Mungu atusaidie kuwahimiza wengi kuwa washirika wa kanisa.

Ukweli ni kwamba makanisa mengi leo yako katika hali mbaya sana ya kiroho. Lakini unapotazama makanisa haya, utaona kwamba yamejawa na umati wa watu lakini wao si washirika wa kanisa hilo na jambo la kuwa mshirika hawalifahamu kamwe. Tarakimu zinaonyesha kwamba miongoni mwa wale ambao ni wakristo, 5% hawajulikani, 10% hawapatikani makanisani, 25% hawahudhurii kanisa, 50% huhudhuria kanisa Jumapili, 75% hawahudhurii mikutano ya maombi, 90% hawasomi Biblia katika manyumba zao na 95% hawajawahi kushuhudia mtu yeyote kuhusu wokovu wa Kristo Yesu.

Kuna sababu kadhaa kwa nini watu hawatekelezi nidhamu katika kanisa. Ukweli ni kwamba hatufai kutekeleza nidhamu katika kanisa kwa njia ambayo ni ya kulipiza kisasi au ya chuki. Paulo aliawaambia Warumi, “Wapendwa, msilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, maana imeandikwa: 'Kisasi ni juu Yangu, Mimi nitalipa, asema Bwana” (Warumi 12:19). Nidhamu ya kanisa inafaa kutekelezwa kwa upendo juu ya mtu ambaye anaadhibiwa na upendo juu ya Mungu.

Pia nidhamu katika kanisa haifai kutekelezwa kwa kuwaza kwamba mtu huyu hapendwi na Mungu. Nidhamu si kuonyesha kwamba mtu fulani hapendwi au kwamba yeye hajaokoka na hafai kamwe. Tunafaa kutekeleza nidhamu katika kanisa kwa sababu ya upendo na uvumilivu na ili tunataka kurejesha mtu huyo.

Katika Mathayo 7:1-2 tunasoma kwamba, "Usihukumu ili usije ukahukumiwa. Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea." Wakati nidhamu Katika kanisa inatajwa, wengi huwa wananuku mstari huu. Kile Kristo Yesu anamaanisha hapa ni kwamba tusitoe uamze kwa yale ambayo hatujapewa mamlaka juu yake kuamua. Kulipiza kisasi ni jambo baya sana (Mathayo 5:40), lakini kutoa hukumu ya kweli kwa mambo ambayo tumepewa mamlaka juu yake ni sawa (Mathayo 19:28). Mungu huwa anataka kwamba watoto wake waishi maisha matakatifu ambayo yanamletea utukufu. Hatuna mamlaka ya kutoa uamuzi wa mwisho kwa chochote. Lakini siku moja Mungu atawaamuru watu wake watoe uamuzi mzuri, wa haki na hata ule uamuzi mbaya sana kwa viumbe vyake vyote (1 Wakorintho 6:2).

Siku ya leo kuna makanisa mengi ambayo yamechanganyikiwa sana kuhusu Mathayo 7:1-2. Wengi wanatumia mistari hii kama kisingizio cha kufanya dhambi na kutoshughulika kuhusu dhambi za wengine. Kanisa leo halitaki kuishi maisha yao kama kanisa lile la kwanza. Ikiwa mtu anamhukumu mwingine kwa sababu yeye anajiona kuwa mtu mtakatifu sana kuliko wengine, basi yeye atakuwa anaonyesha kwamba haelewi kabisa neema na huruma ya Mungu kwa watu wake. Lakini pia watu ambao hawajali dhambi katika maisha yao au katika maisha ya wengine, wao hawaonyeshi pendo takatifu la Kristo Yesu ambalo ndilo ishara ya kweli kwamba wao ni wake.

Wale ambao wanawaza kwamba wao ni watakatifu sana na kwamba wana mamlaka ya kuwahukumu wengine, wao hawaelewi neema na huruma ya Mungu kwao. Wale ambao hawajali dhambi katika maisha yao wala katika maisha ya wengine, wao huonyesha kwamba upendo ambao Kristo Yesu alikuwa nao kwao ndio upendo ambao wanafaa kuthibitisha wale ambao ni wake.

Huwa hutuwatengi watu kutoka katika makusanyiko yetu kwa sababu wao ni watu ambao hawajaokoka. Bali huwa tunawaondoa washirika katika ushirika kwa sababu wao wanaishi maisha ambayo hayaambatani na neno la Mungu. Nidhamu ya kanisa haijakusudiwa kulipiza kisasi kwa mtu yeyote. Huwa nidhamu hii inatekelezwa kwa unyenyekevu na kwa upendo wa Mungu kwa yule ambaye anaadhibiwa. Hivi ndivyo nidhamu inafaa kutekelezwa katika kanisa lolote.

Hizi ni baadhi za sababu za kutekeleza nidhamu katika kanisa.

1. Nidhamu inatekelezwa kwa uzuri wa yule ambaye anaadhibiwa.

Katika 1 Wakorintho 5:1-5, mtu huyu alikuwa amepotea kwa dhambi. Yeye alikuwa anawaza kwamba yale alikuwa anayafanya, yalikuwa yamekubalika na Mungu. Watu katika makanisa ya Wagalatia walidhani kwamba kujiamini lilikuwa jambo bora sana badala ya kumtegemea Mungu (Wagalatia 6:1). Alexanda na Himanayasi walidhani kwamba lilikuwa jambo bora kumkufufru Mungu (1 Timotheo 1:20). Watu hawa wote hawakuwa wanafanya yale ambayo yalikuwa yanampendeza Mungu. Kwa sababu ya upendo juu ya watu hawa, nidhamu ya kanisa ilifaa itekelezwe. Hatutaki kuwa makanisa ambayo yanawahimiza wanafiki ambao wamefanya mioyo yao kuwa migumu katika dhambi. Hatutaki hata sisi wenyewe kuishi maisha kama hayo wala kuwa katika kanisa ambalo linahimiza watu kuishi maisha haya.

2. Nidhamu inatekelezwa kwa uzuri wa washirika wengine ili waone hatari ya dhambi.

Paulo alimwambia Timotheo kwamba ikiwa kiongozi anatenda dhambi, basi anafaa kukemewa waziwazi (1 Timotheo 5:20). Hii haimaanishi kwamba kila wakati mchungaji anafanya jambo baya, basi washirika wanafaa kumkemea mara moja katika mikutano ya kanisa. Bali inamaanisha kwamba wakati kuna dhambi ambayo inatatiza kanisa haswa ile dhambi ambayo mtu amekataa kutubu, basi dhambi hiyo inafaa kuzungumziwa wazi kabisa ili wengine wapate kuonywa na pia waone hatari ya dhambi hiyo.

3. Nidhamu katika kanisa inafaa kutekelezwa kwa ajili ya uzuri wa kanisa lote.

Paulo akiandikia kanisa la Korintho aliwaambia kwamba hawakufaa kufurahia dhambi ambayo ilikuwa inaendelea miongoni mwao (1 Wakorintho 5:6-8). Aliwaambia, "Je, hamjui ya kwamba chachu kidogo huchachusha donge zima la unga." Hapa chachu ni mfano wa dhambi. Aliendelea kusema, "Ondoeni chachu ya kale ili mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Kristo, Mwana-Kondoo wetu wa pasaka amekwisha tolewa kwa dhabihu. Kwa hiyo tusiadhimishe sikukuu hii, kwa chachu ya nia mbaya na uovu, bali kwa mkate usiotiwa chachu, ndio weupe wa moyo na kweli."

Wakati wa Pasaka, mwana-kondoo aliuliwa na mkate ambao haukuwa na chachu uliliwa. Paulo anawaambia wakristo kwamba Mwana-Kondoo ni Kristo Yesu ambaye alichinjwa na wakristo wanafaa kuwa mkate bila chachu. Wakristo hawafai kupuuza dhambi miongoni mwao bali wanafaa kuishughulikia kwa kutekeleza nidhamu. Kanisa lote linafaa kuwa kanisa ambalo linakubalika machoni pa Mungu. Lakini hii haimaanisha kwamba tunafaa kila wakati kuwa tunatekeleza nidhamu tu na hatufanyi mambo mengine.

4. Nidhamu katika kanisa inafaa kutekelezwa kwa ajili ya ushuhuda wa kanisa.

Katika Mathayo 5:16; Yohana 13:34-35; 1 Wakorintho 5:1; 1 Petro 2:12, tunasoma kwamba nidhamu katika kanisa ni chombo cha kueneza injili. Watu wengi huwa wanaona maisha ya wale ambao wameokoka kuwa maisha tofauti sana na ya wale ambao hawajaokoka. Simaanishi kwamba wale ambao wameokoka maisha yao ni maisha makamilifu na hayana dhambi yoyote. Kile ninamaanisha ni kwamba wao katika maisha yao ya kila siku wanajitahidi kumpenda na kumfurahisha Mungu. Wakati kanisa linaanza kufuata mienendo ya ulimwengu, kazi ya kuwashuhudia wengi huwa inatatizwa kabisa. Wakristo wanafaa kuishi maisha yao kwa njia ambayo inawaleta wengi kwa Mungu.

5. Nidhamu katika kanisa inafaa kutekelezwa kwa kumtukuza Mungu kupitia kwa maisha yetu.

Tunaishi maisha yetu kwa ajili ya kumtukuza Mungu. Tuliumbwa na Mungu ili utukufu wake uweze kuonekana kupitia kwa maisha yetu (Waefeso 5:25-27; Waebrania 12:10-14; 1 Petro 1:15-16,2:9-12; 1 Yohana 3:2-3; Mwanzo 1:27). Katika Agano la Kale, Mungu aliwaamuru watu wake wote waishi maisha matakatifu (Walawi 11:44;19:2). Huu ndiyo msingi wa kanisa la Kristo (2 Wakorintho 6:14-7:1). Wakristo wanafaa kuwa watakatifu si kwa sababu ya sifa zao bali kwa sababu ya sifa na utukufu wa Mungu. Tunafaa kuwa

nuru ya ulimwengu huu ili watu wanapotutazama, wamtukuza Mungu (Mathayo 5:16). Biblia inasema “Mwe na mwenendo mzuri mbele ya watu wasiomjua Mungu, ili kama wanawasema kuwa ninyi ni watenda mabaya, wayaone matendo yenu mema wamtukuze Mungu siku atakapokuja kuhukumu” (1 Petro 2:12). Pia Paulo aliwaandikia Wakorintho kwamba, “Je, hamjui kwamba wasio na haki hawataurithi Ufalme wa Mungu? Msidanganyike, waasherati hawauridhi Ufalme wa Mungu, wala wapotoshaji, wala wezi, wala wenye tamaa mbaya, wala wafiraji, wala walafi, wala walawiti, wala wanaodhihaki, wala wanyang'anyi. Baadhi yenu mlikuwa kama hao. Lakini mlioshwa, mlitakaswa, mlihesabiwa haki kwa jina la Bwana Yesu Kristo na katika Roho wa Mungu wetu” (1 Wakorintho 6:9-11).

Bwana Yesu Kristo aliwaamuru wanafunzi wake kwamba wawafundishe watu yale yote ambayo alikuwa amewafundisha (Mathayo 28:19-20). Katika kitabu cha Ufunuo, tunasoma kuhusu kanisa ambalo ndiyo Bibi arusi wa Kristo. Kanisa hili linadhihirisha utukufu wa Mungu. “Huko nje wako mbwa, wachawi, wazinzi, wauaji, waabuduo sanamu na kila mtu apendaye udanganyifu na kuufanya” (Ufunuo 22:15). Hawa ni wale ambao hawatakuwa wameokoka.
Unapozingatia 1 Wakorintho 5, nidhamu katika kanisa ndiyo mojawapo ya mambo ambayo yanafanya kuwa mshirika katika kanisa liwe jambo la muhimu sana. Ukweli ni kwamba washirika wa kanisa ni wale ambao wanaweza kushiriki meza ya Bwana bila kuleta aibu kwa kanisa au hukumu katika maisha yao au aibu kwa Mungu na ujumbe wa injili (1 Wakorintho 11). Tunaposoma vifungu hivi vyote, tunaona kwamba sisi wakristo tunalo jukumu la kuwa watu watakatifu kuliko jinsi watu wengine walivyo.

Maisha ya mkristo yanafaa kuwa nuru ambayo inaangaza kwa wengine. Yaani maisha ya mkristo yanafaa kuwa maisha ya kumtukuza Mungu pekee. Ni ukweli kwamba kuna wale ambao watatuwazia vibaya sana. Lakini ukweli ni kwamba maisha ya mkristo yanafaa kuwa maisha ambayo yanashuhudia utukufu wa Mungu na kufanya ujumbe wa injili upendeze. Hili ni jukumu la kila mkristo.

Tunaweza kufundisha mafundisho haya kwa wengi na hata kuyasikia yakihubiriwa vyema kabisa. Lakini ukweli ni kwamba ni kanisa ambalo lina jukumu ya kutekeleza nidhamu. Kusudi kuu la nidhamu hii ni kumfanya yule ambaye ametenda dhambi atubu, kuonyesha kanisa hatari na ubaya wa dhambi, ni kwa uzuri wa kanisa lote na ni kwa ajili ya kuwashuhudia wale ambao hawajaokoka. La muhimu kabisa ni kwamba utakatifu wetu unafaa kudhihirisha utakatifu wa Mungu. Hili ni jambo ambalo tunafaa kulifanya si kwa ajili ya sifa zetu, bali kwa ajili ya sifa ya Mungu. Kanisa ambalo linatekeleza nidhamu kulingana na mafundisho ya Biblia, ni kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho.

Je, ni nini itafanyika ikiwa hatutatekeleza nidhamu katika makanisa yetu?

Ikiwa makanisa yetu hayatazingatia nidhamu, basi ni wazi kwamba hayatakuwa makanisa ambayo yanafuata neno la Mungu. Nidhamu inapoondoka katika kanisa, huwa ni ishara kwamba Kristo hayumo katika kanisa hilo. Maisha yetu ya ukristo ni lazima yadhihirishe utukufu wa Mungu. Tunafaa kupendana na ni lazima tuchungane kwa sababu sisi kuna wakati itapenda kufanya kinyume na neno la Mungu. Njia moja ya kuwapenda wenzetu ni kuzungumza nao kwa uaminifu sana na kwa upendo bila kudanganyana. Pia tunafaa kuwapenda wale ambao hawajaokoka kwa sababu tunataka pia wao wamjue Kristo. Zaidi tunafaa kupenda Mungu ambaye ni mtakatifu sana na ambaye ametuita kwa jina lake na ametuamuru tuwe watakatifu kwa sababu Yeye ni mtakatifu. Hii ni baraka kutoka kwa Mungu na ni jukumu letu kufanya jinsi ameamuru.

Unapoona makanisa ambayo yanaendelea vyema kiroho, ni ishara kwamba watu katika makanisa hayo wanajaliana na kupendana kiwango kwamba huwa wanaambiana ukweli bila kuficha lolote hata kama ni dhambi.

Ishara ya 8

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho ni kanisa ambalo lina tamaa ya kuona kwamba washirika wanamfuata Kristo katika maisha yao na wanakua katika imani yao.

Haya ndiyo mambo ambayo tutatazama katika sura hii:

1. Mafundisho ya Biblia juu ya kukua kiroho

2. Jinsi kanisa linafaa kuhakikisha kwamba linakua kiroho
(i) Mafundisho ambayo yanafafanua Biblia
(ii) Mafundisho kuhusu Mungu na mpango wake wa kuwaokoa wenye dhambi
(iii) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu Ujumbe wa Injili
(iv) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kuokoka
(v) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kueneza ujumbe wa Injili
(vi) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kuwa mshirika katika kanisa
(vii) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu nidhamu katika kanisa
(viii) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu uongozi katika kanisa

3. Tumaini la kukua
(i) Kazi ya mchungaji
(ii) Kukua pamoja kama kanisa

4. Umuhimu wa kukua

5. Je, nini itafanyika ikiwa hatukui?

Tamaa ya kanisa kuona kwamba washirika wanamfuata Kristo katika maisha yao na wanakua kiroho.

Leo kuna watu wengi ambao wanaongozwa katika kurudia maombi ya toba ili waweze kuokoka. Wengi wanaambiwa kwamba baada ya kurudia maombi hayo, Mungu huwa anawasamehe dhambi zao hapo na hapo. Lakini wanakosa kujua kwamba hii siyo njia ya wokovu hata kama njia yenyewe inaonekana kuwa mzuri na kile ambacho kinafanywa ni kitu kizuri. Ukweli kwamba hatuokoki kwa kurudia maombi fulani fulani ya toba. Tunaokoka kwa kumwamini Kristo Yesu pekee.

Kwa mfano kuna mtu mmoja ambaye aliitwa Nzai. Yeye alihisi kwamba alikuwa mtu ambaye alikuwa akifanya mambo mabaya sana na kwamba hakustahili hata kidogo kuitwa mtu mzuri. Siku moja alipatana na marafiki wake wawili ambao walikuwa wameokoka. Walipokuwa wanazungumza naye kuhusu Kristo Yesu na kazi yake kwa ajili ya wenye dhambi, aliwaambia ubaya wake nao wakamwonyesha kwamba kuna njia ambayo yeye anaweza kusamehewa dhambi zake. Mmoja wa marafiki wake alimwambia arudie maombi fulani ya toba. Baada ya yeye kurudia maombi hayo, aliambiwa kwamba Mungu alikuwa amemsamehe dhambi zake zote na kwamba sasa yeye alikuwa mtoto wa Mungu ambaye alikuwa anaenda mbinguni.

Tangu siku hiyo, Nzai alianza kuishi maisha mazuri na hata wengi waliwaza kwamba kweli yeye ameokoka. Alihudhuria kanisa moja ambayo ilikuwa inafundisha mafundisho ya kuwafurahisha wengi na kuwafanya washangilie zaidi. Mahubiri katika kanisa hili yalikuwa mafupi na yalijawa na hadithi nyingi za kufurahisha na alipenda kuyasikiliza sana. Yeye alipewa nafasi ya kuwafundisha watoto katika kanisa hili.

Lakini ukweli ni kwamba, Nzai hakuwa anafahamu Biblia na mafundisho yake. Yeye alikuwa na mawazo yake tu kuhusu Mungu ni nani na alikuwa anashiriki mawazo haya na wale ambao alikuwa anafundisha. Mawazo haya, hayakuwa yanatoka katika Biblia. Ni mambo alikuwa ameyasikia tu na kuyawaza tu. Yeye alijua kwamba bora tu ukubali kwamba wewe ni mwenye dhambi, Mungu angekuokoa. Alijua kwamba Yesu Kristo na Msalaba ni mambo muhimu sana, lakini hakufahamu umuhimu wake ni gani. Yeye aliwaza kwamba kuokoka ni kama kufanya uamuzi fulani wa kununua nyumba fulani au kutoinunua. Yeye aliwaza kwamba kazi ya kueneza injili ni kazi ya wale ambao wanafanya kazi katika kanisa pekee. Yeye hakuwa mshirika wa kanisa na wengi hawakujua jambo hili. Kulikuwa na wakati ambapo alishughulika sana na wakati ambapo yeye hakuwa anashugulika na lolote. Kuna wakati yeye alihudhuria kanisa kila Jumapili na wakati mwingine angehudhuria myezi kadhaa katika mwaka. Yeye alipendezwa na hali hii.

Ukweli ni kwamba Nzai alikuwa mkristo ambaye hakuwa anakua. Wengi pia leo wako kama huyu mtu. Leo watu wengi ambao wanadai kwamba wameokoka, maisha yao yanaonyesha kwamba kweli wao hawaonyeshi nia ya kutaka kukua katika ukristo wao. Kuna maswali manne ambayo tunafaa kujiuliza kuhusu jambo hili la kukua katika ukristo.

(i) Je, ni vyema kukosa kukua katika ukristo wetu?
(ii) Ikiwa mtu hataki kukua katika ukristo wake anafaa kufanya nini?
(iii) Je, kukua kiroho ni jambo la muhimu kweli?
(iv) Je, itafanyika nini wakati tunakosa kukua katika ukristo wetu?

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho linajulikana kwa jinsi linavyotilia maanani mambo ya kukua kiroho miongoni mwa washirika wake. Katika kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho washirika wote huwa na tamaa moja, kumfuata Kristo pekee katika maisha yao yote.

1. Mafundisho ya Biblia juu ya kukua

Je, kukua katika ukristo wetu ni jambo zuri au baya? Ukweli ni kwamba kukua katika ukristo wetu ni jambo ambalo limefundishwa wazi katika Biblia. Katika Mwanzo 1:22 tunasoma kwamba, “Mungu akivibariki akasema, 'Zaeni mkaongezeke mkayajaze maji ya bahari, nao ndege waongezeke katika dunia.'” Mungu pia alimwambia Adamu na Hawa kwamba pia wao walihitaji kuzaana na kuongezeka: “Mungu akawabariki na akawaambia, 'Zaeni na mkaongezeke, mkaijaze tena dunia na kuitiisha. Mkatawale samaki wa baharini, ndege wa angani na kila kiumbe hai kiendacho juu ya ardhi'” (Mwanzo 1:28).

Baadaye, baada ya gharika, Mungu aliamuru watoto wa Nuhu kwamba, “Ndipo Mungu akawabariki Noa na wanawe, akiwaambia, 'Zaeni mkaongezeke kwa idadi na mkaijaze tena dunia'” (Mwanzo 9:1). Unapoendelea kusoma kitabu cha Mwanzo, utaona kwamba Mungu alimwambia Abrahamu kwamba idadi ya kizazi chake itakuwa kubwa na itaongezeka. Wakati Waisraeli walienda nchi ya Misri, wao waliongezeka katika idadi. Hii ilikuwa ishara ya baraka za Mungu kwao. Mungu aliendelea kuwabariki hata wakati walikuwa nchi ya Kanani. Hata wakati Waisraeli walipelekwa katika utumwa kule Babeli, Mungu alizungumza nao kupitia kwa nabii Yeremia kwamba, “Oeni wake na mzae wana na binti, waozeni wana wenu wake nanyi watoeni binti zenu waolewe, ili nao pia wazae wana na binti. Ongezekeni idadi yenu huko, wala msipungue” (Yeremia 29:6).

Moja wa njia ambapo Mungu aliwahimiza watu wake katika Agano la Kale kuwa watakatifu ni jinsi alivyowabariki katika idadi. Tunasoma katika Zaburi, “Wenye haki watastawi kama mtende, watakuwa kama mwerezi wa Lebanoni, wamepandwa katika nyumba ya Bwana, watastawi katika nyua za Mungu wetu” (Zaburi 92:12-13). Katika kitabu cha Mithali Mungu anapeana maagizo jinsi tunafaa kukua katika njia hii. Tunaambiwa tuongezeka katika nguvu hata maarifa. Tunaongezeke katika hekima kwa kutembea na wale ambao ni wenye hekima (Mithali 24:5;13:20).

Hatufai kutafuta kukua katika njia ambazo si nzuri. Hatufai kupendezwa tu na kukua katika vitu vya ulimwengu huu kama kuwa na pesa au mali. Zaburi 49:16, tunapewa onyo kali sana: “Usitishwe na mtu anapotajirika, fahari ya nyumba yake inapoongezeka.” Kifo huwa inawanyang'anya wengi vitu vyao ambavyo wamevipata katika ulimwengu huu. Kwa sababu ya hii hatufai kupotozshwa na vitu vya ulimwengu huu. Katika Biblia tunasoma kwamba liwe liwalo, kanisa la Kristo lazima likue na lazima liendelee. Hili jambo liliahidiwa katika Agano la Kale na Kristo Yesu pia alilizungumzia katika Agano Jipya. Biblia inasema, “Kuongezeka kwa utawala wake na amani hakutakuwa na mwisho. Atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi na juu ya Ufalme wake, akiuthibitishia na kuutegemeza kwa haki na kwa adili, tangu wakati huo na hata milele. Wivu wa Bwana Mwenye Nguvu utatimiza haya; Ingawa mbegu hiyo ni ndogo kuliko mbegu zote, lakini inapokua ni mmea mkubwa kuliko yote ya bustanini, nao huwa mti mkubwa, hata ndege wa angani huja na kutengeneza viota katika matawi yake” (Isaya 9:7; Mathayo 13:32). Bwana Yesu Kristo mwenyewe anasema hapa kwamba Ufalme huu utatoka kwa mbegu ndogo na kua mkubwa sana.

Mbegu ni mfano wa Kristo Yesu ambaye alikufa msalabani na alizikwa . Baada ya siku tatu alifufuka na kuanza kuujenga Ufalme wa Mungu na unaendelea kukua hadi leo. Katika Matendo ya Mitume tunasoma kuhusu Ufalme huu mara kwa mara na jinsi ulivyokua. Tunasoma kwamba, “Basi ikawa katika siku hizo, wakati idadi ya wanafunzi ilipokuwa ikiongezeka sana.....Neno la Mungu likazidi kuenea, idadi ya wanafunzi ikazidi kuongezeka sana katika Yerusalemu hata makuhani wengi wakamwamini Kristo” (Matendo ya Mitume 6:1,7); “Lakini neno la Mungu likaendelea mbele na kuenea, nao wengi wakaambatana nalo” (Matendo ya Mitume 12:24); “Neno la Bwana likaendelea katika eneo lile lote” (Matendo ya Mitume 13:49); “Hivyo neno la Bwana likaenea sana na kuwa na

nguvu" (Matendo ya Mitume 19:20).

Katika mistari hii tunapata kwamba kulikuwa na kuongezeka kwa idadi ya washirika. Pia kuongezeka huko si kwa idadi tu ya watu, bali pia kuongezeka kwa kufahamu neno la Mungu na kuongezeka kwa utakatifu miongoni mwa wale ambao wanamwamini Kristo. Katika kitabu cha Waefeso 4:15-16 tunasoma kwamba, " Badala yake, tukiambiana kweli kwa upendo, katika mambo yote tukue, hata tumfikie Yeye aliye kichwa, yaani, Kristo. Kutoka Kwake, mwili wote huunganishwa na kushikamanishwa pamoja kwa msaada wa kila kiungo, hukua na kujijenga wenyewe katika upendo, wakati kila kiungo kinafanya kazi yake."

Kukua huku kunatokana na nguvu za Mungu Mwenyewe wala si za mwanadamu yeyote. Katika Wakolosai 2:19 tunasoma kuhusu Kristo kwamba Yeye ndiye "Kichwa ambaye kutoka Kwake mwili wote unalishwa na kushikamanishwa pamoja kwa viungo na mishipa, ambao hukua kwa ukuaji utokao kwa Mungu." Si mchungaji ambaye anafanya kanisa likue, bali ni Mungu. Mungu huwa anamtumia mchungaji kama chombo cha kuhubiri neno Lake. Paulo aliwandikia Wakorintho ambao walikuwa wakigawanyika kwa misingi ya wahubiri ambao walizungumza vyema sana. Aliwakumbusha kwamba, "Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye aliyekuza. Hivyo mwenye kupanda mbegu na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke Yake ndiye akuzaye" (1 Wakorintho 3:6-7).

Bwana Yesu Kristo naye alifundisha kwamba kukua kwa Ufalme wa Mungu hakutegemei sisi, bali kunategemea mapenzi ya Mungu. Katika Marko 4, Bwana Yesu Kristo alifundisha kwamba Ufalme wa Mungu ni kama mbegu ambayo inakua. Mbegu hiyo hukua hata wakati mkulima analala. Kukua kwa mbegu hii, hakutegemei mkulima au bidii yake, hata kama ni lazima afanye kazi yake kwa bidii, bali kunategemea Mungu mwenyewe ambaye ndiye hukuza mbegu. Ni Mungu mwenyewe ambaye anahakikisha kwamba kanisa lake linakua. "Usiku hulala na mchana huamka, nazo mbegu huota na kukua pasipo yeye kujua inavyokua" (Marko 4:27). Ni Mungu ambaye anasababisha mbegu kukua.

Hii ndiyo sababu wakati Paulo aliwaandikia Wathesalonike, hakuwaambia kwamba walijitahidi sana na kukua katika ukristo wao, bali yeye alimshukuru Mungu kwa kuwa aliwawezesha kukua katika ukristo wao. "Ndugu, imetubidi kumshukuru Mungu kwa ajili yenu sikuzote, kama ulivyo wajibu wetu, kwa sababu imani yenu inakua zaidi na zaidi na upendo wa kila mmoja wenu alio nao kwa mwenzake unazidi kuongezeka" (2 Wathesalonike 1:13).

Hii ndiyo sababu wakati Paulo alikuwa anataka watu wakue katika ukristo wao, yeye aliwaombea kwa sababu alifahamu kwamba kukua katika ukristo ni kazi ya Mungu. Kwa mfano katika 1 Wathesalonike 3:11-13 tunasoma kwamba, "Basi Mungu wetu na Baba yetu Mwenyewe na Bwana wetu Yesu atengeneze njia ya sisi kuja kwenu. Bwana na auongeze upendo wenu na kuuzidisha kati ya ninyi kwa ninyi na kwa wengine wote, kama vile tulivyo na upendo mwingi kwenu. Tunamwomba Mungu awaimarishe mioyo yenu katika utakatifu ili msiwe na lawama, mbele za Mungu wetu aliye Baba yetu wakati wa kuja kwake Bwana Yesu pamoja na watakatifu wote" (1 Wathesalonike 3:11-13). Katika kitabu cha Wakolosai pia tunasoma kumhusu Paulo akiwaombea wasomaji wake kwamba watakua katika ukristo wao. "Nasi tunaomba haya ili mpate kuishi maisha yanayostahili mbele za Bwana ili mpate kumpendeza kwa kila namna: Mkizaa matunda kwa kila kazi njema, mkikuwa katika kumjua Bwana" (Wakolosai 1:10).

Katika kusema haya yote simaanisha kwamba sisi ambao tumeokoka hatuna jukumu lolote katika ukristo wetu. Katika kitabu cha 2 Petro 3:18 tunasoma, "Kueni katika neema na katika kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo." Hapa Petro anawahimiza wasomaji wake kwamba wao wanalo jukumu la kuona kwamba wanakua katika ukristo wao. Anasema, "Kueni."

Je, tunafaa kufanya nini ili tuweze kukua katika ukristo wetu?

"Kwa sababu hii, jitahidini sana katika imani yenu kuongeza wema na katika wema wenu maarifa, katika maarifa yenu kiasi; katika kiasi, saburi, katika saburi yenu, utauwa, katika utauwa wenu upendano wa kindugu, upendo. Kwa maana haya yakiwa kwenu kwa wingi, nayo yakizidi kuongezeka yanawafanya kuwa wenye bidii na wenye kuzaa matunda katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo" (2 Petro 1:5-8). Ni lazima tujitahidi kukua katika ukristo wetu kwa kutilia maanani na kufanya mambo haya ambayo yametajwa hapa.

Petro pia alisisitiza umuhimu wa kulijua neno la Mungu ikiwa mtu anataka kukua katika ukristo wake. Alisema, "Kama watoto wachanga, waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya kiroho yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu, ikiwa kweli mmeonja ya kwamba Bwana ni mwema. Mwendeeni Yeye aliye Jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu bali kwa Mungu ni teule na la thamini Kwake. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa kuwa nyumba ya Roho, mpate kuwa ukuhani mtakatifu, mkitoa dhabihu za kiroho zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo" (1 Petro 2:2-5).

Kukua katika ukristo ni jambo ambalo limefundishwa wazi kabisa katika Biblia.

2. Jinsi kanisa linafaa kuhakikisha kwamba linakua kiroho

Jambo la pili ambalo tutaangazia ni hili kwamba, je, tunafaa kufanya nini ili tukue katika ukristo wetu?
Je, ni kanisa la aina gani ambalo litatekeleza vyema jambo hili? Haya ndiyo maswali ambayo ninataka kujibu.

(i) Mafundisho ambayo yanafafanua Biblia

Kanisa ambalo linahubiri mahubiri ambayo yanafafanua Biblia, litakuwa linawahimiza washirika wake kukua katika ukristo kwa sababu washirika wake watakuwa wanasikiliza Mungu akiwazungumzia kupitia kwa neno lake. Tunahitaji tu neno la Mungu ikiwa kweli tunataka kukua katika ukristo wetu. Kanisa ambalo mahubiri yake hayafafanui Biblia, liko katika hatari ya kukosa kukua. Ikiwa tunanataka kujua kweli ni nini hicho cha maana sana katika maisha yetu, lazima tumgeukia Mungu na kusikia kutoka Kwake. Tunahitaji kusikia neno Lake bila kupuuza sehemu zingine za neno hilo. Kuna mambo mengi katika Biblia ambayo huwa tunataka kuepuka ili tusisikie lolote kuyahusu kwa sababu huwa yanatufanya tusumbuke sana. Lakini ukweli ni kwamba hata hayo mambo ambayo hatuyapendi kusikia kutoka kwa Biblia ni neno la Mungu na ni lazima tuyasikie na tufanye jinsi Biblia inavyotuamuru ikiwa tunataka kukua katika ukristo wetu.

Tuombe Mungu kila wakati kwamba katika makanisa yetu, Yeye atawaleta wahubiri wa neno lake ambao wanalihubiri bila kulichagua na kupuuza sehemu fulani fulani za neno hilo. Ikiwa uko katika kanisa ambamo neno la Mungu linahubiriwa kwa njia ambayo si ya

uaminifu, basi mwombe Mungu kwamba atakupeleka katika kanisa ambamo neno Lake linahubiriwa kwa uaminifu bila kupuuza sehemu fulani fulani, bali linahubiriwa lote jinsi Mungu amelipatiana kwetu.

Tunapokuwa tunasoma neno la Mungu, tunaona upendo na huruma wake kwetu. Huwa tunafahamu mapenzi na mpango mwema wa Mungu kwetu. Huwa tunaona pia utukufu wa ujumbe wa injili. Tunaona jinsi Yeye huwa anatusahihisha. Tunapoendelea kusikia mahubiri ambayo yanafafanua Biblia huwa tunazidi katika kumtegemea Mungu na kuacha kuwategemea wanadamu na kujit4egemea wenyewe. Tunaanza kujali neno la Mungu zaidi kuliko mambo mengine yote. Kwa mfano ikiwa mchungaji wako wa kila siku hayuko kwa sababu fulani fulani, wewe hutatoroka kanisa au kuacha kuja wakati hayuko, wewe utaendelea kusikia neno la Mungu kutoka kwa yeyote ikiwa anahubiri kwa kufafanua Biblia. Si vibaya kupenda wachungaji wetu, lakini ni bora zaidi ikiwa tutapenda neno la Mungu zaidi ya jinsi tunavyowapenda wahubiri wa neno. Neno la Mungu ndilo msingi wa kanisa. Kanisa linajengwa na kukua juu ya neno la Mungu pekee. Tunakuja kanisa si kwa sababu ya jambo lingine lolote, basi kusikia neno la Mungu likihubiriwa kwa njia ya uaminifu na Roho Mtakatifu akilitumia neno hilo kuzungumza na mioyo yetu. Kupitia kwa neno la Mungu, huwa tunafahamu zaidi kumhusu Mungu na jinsi alivyo.

Kuwa mwangalifu sana kabla ya kujiunga na kanisa lolote. Kwanza hakikisha kwamba kanisa ambalo unataka kujiunga nalo linahubiri Biblia kwa kufafanua yale ambayo yameandikwa humo. Hakikisha pia kwamba mhubiri katika kanisa hilo ni mtu ambaye amejitolea kabisa kuwa mwaminifu juu ya neno la Mungu na kwamba analihubiri kwa uaminifu sana na bila kupuuza sehemu fulani fulani. Hakikisha kwamba yeye anahubiri kumtukuza Mungu na si kuwafurahisha wale ambao wanamsikiza. Neno la Mungu ndilo huisha nafsi zetu.

(ii) Mafundisho kuhusu Mungu na mpango wake wa kuwaokoa wenye dhambi

Kanisa ambalo linazingatia mafundisho ya Mungu na mpango wake katika kuwaokoa wenye dhambi litawasaidia wengi kukua katika ukristo wao.

Huwa tunakua katika ukristo wetu kwa kufahamu zaidi kumhusu Mungu na kuhusu maisha yetu wenyewe. Huwa tunakua kwa kufahamu zaidi kuhusu upendo Wake kwetu na jinsi alivyo. Tunakua wakati tunasoma Biblia kuhusu jinsi alivyowachagua watu wake na kufanya kazi pamoja nao katika hali ngumu sana za maisha haya. Huwa tunahimizwa kwa kuona kilele cha mpango wake na maana ya mpango huu. Huwa tunaanza kukua katika kufahamu na tunaanza kumwamini zaidi na zaidi.

Je, huwa tunakua kwa njia gani katika kumwamini Mungu? Ni kweli kwamba Mungu anatumia hali fulani fulani katika maisha yetu kutufanya tukue na tumwamini zaidi na zaidi. Hii ni fursa ambayo Mungu huwa anatoa kwetu kumwamini. Je, kwa nini tumwamini Mungu? Huwa tunamwamini Mungu kwa sababu Yeye amejidhihisha kwetu kwamba kweli Yeye anastahili kuaminiwa. Mungu amejidhihirisha kwetu kupitia kwa neno lake, kupitia kwa historia na kupitia kwa viumbe vyake. Haya yote yanadhihirisha kwamba kweli Yeye anastahili sifa na kuaminiwa katika kila jambo.

(iii) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu Ujumbe wa Injili

Kanisa ambalo linawasaida washirika wake kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu ujumbe wa injili ni kanisa ambalo linawasaidia wengi kukua katika ukristo wao.

Hitaji kuu ambalo tunalo kama wakristo ni kufahamu jinsi ya kumtegemea Kristo katika maisha yetu yote. Mtu mmoja ambaye aliitwa John Newton ambaye alikuwa akiwauza watu, baada ya kuokoka aliandika maneno haya: “Nilimwomba Mungu kwamba niweze kukua katika imani, upendo na katika neema yote. Pia niliomba kwamba niweze kujua wokovu wa Mungu na pia niweze kuwa mtu wa maombi sana. Nilitumaini kwamba baada ya maombi yangu, Mungu atajibu hapo na hapo na nguvu na upendo wake ataondoa dhambi zangu zote hapo na hapo na nitakuwa msafi kabisa bila dhambi yoyote. Badala ya matumaini yangu, alinifanya nihisi uzito wa dhambi ambazo zilikuwa zimejificha ndani ya moyo wangu na alifanya nihisi uchungu sana kwa sababu ya dhambi hizi.”

Tunapoanza kuona udhaifu wetu na jinsi tumeanguka katika dhambi, tunamshukuru Mungu kwa upendo wake kwetu. Ni lazima tuhubiri injili ambayo inawaonyesha watu kwamba kwa asili sisi tulistahili kuenda jahanum lakini kwa neema na upendo wa Mungu, Mungu ametuokoa sisi ambao tumeokoka na kwamba sasa sisi ni watoto wake na mbinguni ndiko makao yetu yalipo. Ujumbe wa injili si tu Mungu alitupenda, bali pia ni kwamba sisi ni wenye dhambi ambao wanastahili jahanum. Ni lazima tuwaonyeshe watu Kristo ambaye ndani mwake upendo wa Mungu unadhihirika kikamilifu kwetu. Yeye alimwaga damu Yake ili tuepushwe na jahanum kwa kumwamini Yeye pekee.

Kanisa ambalo linahubiri ujumbe wa injili vyema kabisa, litakusaidia kukua katika ukristo wako. Litakusaidia kukua katika fahamu yako juu ya Mungu na upendo wake kwetu. Unapoendelea kumfahamu Mungu zaidi na zaidi na yale ambayo alikufanyia ndani ya Kristo Yesu, utapata kwamba unazidi katika kukua katika ukristo. Je, unataka kukua katika ukristo wako? Tafakari juu ya ujumbe wa injili na uishi maisha yako kwa utiifu juu ya Mungu.

(iv) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kuokoka

Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kuokoka, kutakusaidia sana kukua katika ukristo wako.

Unapoelewa vyema hali yako ya kiroho na kufahamu kwamba Mungu ndiye tegemeo lako ambalo uko lao katika maisha yako ya ukristo, utaishi maisha yako kwa shukurani kwa Mungu kutokana na huruma na neema yake na mengi ambayo amekufanyia katika maisha yako yote. Unapofanya hivyo, tumaini lako linakuwa la hakika kwa sababu unajua kwamba tumaini lako halitegemei uaminifu wako bali uaminifu wa Mungu. Hili ni himizo kubwa sana kwa wale wote ambao wanajifahamu kuwa wenye dhambi. Mungu huwa anatupenda kwa sababu Yeye ni mwenye upendo.

Wakati tunafahamu kwamba wokovu wetu ni kazi ya Mungu katika maisha yetu, tutakuwa tumefahamu ukweli kutoka kwa Biblia kuhusu wokovu. Tutakuwa tumeelewa kwamba wokovu unapatikana kwa neema ya Mungu na si kwa matendo mema ya mtu.

(v) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kueneza ujumbe wa Injili

Ukosefu wa kukua katika maisha ya wale ambao wanadai kwamba wameokoka ni ishara kwamba wao walihubiriwa ujumbe wa injili kwa njia ambayo si ya Biblia. Wengi leo wamehubiriwa kwamba bora tu umerudia ombi fulani, basi wewe utakuwa umeokoka. Wengi wameelezwa kwamba kwa sababu wokovu ni kazi ya Mungu katika maisha ya mtu, basi yeye anahitaji tu kuomba na mambo mengine ni ya Mungu.

Ukweli ni kwamba kueneza ujumbe wa injili ni zaidi ya kurudia ombi. Ni lazima tuwaeleze watu kwa makini sana kwamba Mungu anapeana maisha mapya kutoka kwa yale ya dhambi kupitia kwa Kristo Yesu. Tunafaa kuwaeleza kwamba wanafaa kuokoka bila kusitasita. Wanahitaji kutubu dhambi zao na kumwamini Kristo Yesu.

Wakati tunaanza kuelewa vyema kuhusu ni nini Biblia inafundisha kuhusu kueneza injili, huwa tunaanza kumwamini Mungu kutusaidia wakati tunaeneza ujumbe huu wa injili ya Kristo Yesu. Tunaanza kumtii kwa sababu tutafahamu kwamba si kazi yetu kumwokoa yeyote, bali kazi yetu ni kuwa waaminifu wakati tunaeneza injili hii ya Kristo Yesu. Tutafahamu kwamba hatuhitaji kujibu kila swali ambalo linaulizwa na hatulielewi. Tutajua kwamba letu ni kuwaonyesha watu njia ya wokovu ambayo imani ndani ya Kristo Yesu. Tutajua kwamba tunafaa kwaombea na kuwapenda wale ambao tunawafikia na ujumbe huu. Kuelewa jambo hili kwamba wokovu ni kazi ya Mungu ni la kuhimiza wote ambao wanahusika katika kazi hii ya kueneza Injili ya Kristo Yesu.

(vi) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kuwa mshirika katika kanisa.

Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu kuwa mshirika katika kanisa ni jambo ambalo litawasaidia washirika wa kanisa kukua katika ukristo wao.

Kuishi maisha ya ukristo inamaanisha kujitoa kwa ajili ya kutumikiana kama ndugu katika Ukristo. Inamaanisha kuwa miongoni mwa watu wa Mungu na msingi wa maisha yao ni Kristo. Kwa kushughulika na maisha ya kila mmoja , huwa tunasaidiana kushughulika na dhambi ambayo bado iko katika maisha yetu na kuombeana na kuhimizana kutubu. Kwa kujitoa kwa ajili ya wengine tunafahamu upendo wa ndugu ni nini. Huwa tunapata kuhimizwa wakati tunaona kazi ya Mungu katika maisha ya wengine. Tunahimizwa wakati tunawaona watu wazee wakishughulikiwa na wale ambao wameokoka juzijuzi wakikua katika ukristo wao. Hata kama tunapitia majaribu fulani fulani katika maisha yetu, tunapata kuhimizwa wakati tunaona Mungu akifanya kazi katika maisha ya ndugu wengine. Hii ndiyo sababu Mungu huwa hatuachi kuwa peke yetu wakati anatuokoa. Kuwa mshirika katika kanisa huwa inatufanya tuwe na watu wa kutuchunga maisha yetu hata nasi pia kuchunga wengine na kuhimizana. Jambo hili hutusaidia sana kukua katika ukristo wetu.

(vii) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu nidhamu katika kanisa

Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu nidhamu katika kanisa ni jambo ambalo litawasaidia washirika wa kanisa kukua katika ukristo wao.

Kanisa leo linapata ugumu sana kuwaongoza wengi kumfuata Kristo Yesu kwa sababu kanisa limepuuza nidhamu. Kanisa kanisa ambamo nidhamu haijadumishwa, utapata kwamba humo washirika wamechanganyikiwa na pia watu wanaisha maisha ambayo hayaambatani na Biblia. Utapata mambo kama, “Fulani wa fualni amekuwa mshirika wa kanisa kwa miaka mingi lakini tazama jinsi anavyoishi maisha yake. Je, ni kwa sababu yeye ako kwa kamiti ya kuendesha shughuli za kanisa?”

Magugu ni mabaya sana na hakuna mkulima ambaye anayapanda kwa sababu yanaharibu mimea mizuri. Mpango wa Mungu kwa kanisa lake hautuongozi kupuuza magugu miongoni mwetu au kupuuza dhambi katika maisha ya watu fulani fulani kwa sababu fulani fulani. Kwa mpango wake, kanisa linajumlisha wale ambao hawajakamilika lakini wanapenda Mungu na Neno lake. Hawa ni watu wanajitahidi kuishi maisha yao kwa utiifu juu ya neno la Mungu. Ni watu ambao Mungu anafanya kazi maishani mwao. Hawa watu Mungu amewaamurisha wawe watakatifu kwa sababu Mungu mwenyewe ni matakatifu.

Kwa uzuri wa yule ambaye anaadhibiwa, kwa uzuri wa wakristo wengine, kwa uzuri wa kanisa, kwa uzuri kueneza ujumbe wa Injili na kwa utukufu wa Mungu, tutasaidiwa kukua katika ukristo wetu tunavyo tekeleza nidhamu katika kanisa.

(viii) Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu uongozi katika kanisa

Kuelewa mafundisho ya Biblia kuhusu uongozi katika kanisa itatusaidia sana kukua katika ukristo wetu. Jinsi Mungu anavyowaleta watu katika maisha yetu wale ambao amewachagua kuwa viongozi katika kanisa, huwa wanatusaidia kuona haswa kiongozi anafaa kuishi maisha yake kwa njia gani. Pia tunafahamu vyema mpango wa Mungu kwetu.

3. Tumaini la kukua

Kabla ya kuzungumzia kuhusu kukua kiroho, nitakueleza kwanza baadhi ya matumaini yangu katika huduma ambao Mungu ameniita kufanya. Kanisa ambamo nashiriki na maisha ambayo ninaishi ndilo jambo ambalo linaniwezesha kukua kiroho.

(i) Kazi ya mchungaji

Katika kazi yangu ya uchungaji, nitafanya kazi ya kuwatembelea washirika mara kwa mara. Tangu nilipojiunga na kanisa ambalo ninachunga sasa, nimezungumza na washirika wote kuhuus injili ni nini na ni vipi wao waliokoka. Ninataka kuwajua washirika wa kanisa langu moja kwa moja. Pia ninapanga kwamba baada ya muda fulani nitakuwa ninawahimiza wale ambao ni wachungaji wenzangu kwamba tuhakikishe kwamba tunakutana na washirika kwa maombi na kuwajulia hali katika maisha yao.

Katika mazungumzo yangu na washirika wa kanisa ambalo ninachunga nitawauliza maswali kama haya:
- Je, ni vipi umeendelea kukua katika ukristo wako tangu wakati nilipokutembea mwisho?
- Je, ni vipi umeendelea kukua katika tabia ya maisha yako tangu nilipokutembela mwisho?
- Je, ni katika sehemu gani ya maisha yako ambapo unahisi kwamba unahitaji kuongozwa?
- Je, ni kwa njia gani ambapo umepata kwamba unashushwa moyo katika juhudi zako za kuishi maisha matakatifu?

-Je, unataka kuombee kuhusu jambo gani?

Hivi ndivyo ninataka mambo yawe katika kanisa ambamo ninachunga na ninaomba kwamba hata makanisa mengi yataiga mfano huu.

(ii) Kukua pamoja kama kanisa

Ninaomba kwamba kanisa ambalo ninachunga washiriki wake wataishi maisha matakatifu kulingana na jinsi tumejitoe kwa Mungu na kwa kutumikiana kama ndugu na dada katika Kristo Yesu jinsi tumekubaliana. Maisha katika kanisa ni maisha ambayo tunafaa kuyaishi kwa pamoja na kwa upendo wa ukristo. Kila mshirika anafaa kujitoa kutumika kwa ajili ya Kristo Yesu na wandugu wenzake ndani ya Kristo Yesu.

Agano la Kanisa

Kwa neema ya Mungu, tumewezeshwa kutubu na kumwamini Bwana Yesu Kristo. Tumeacha kujiamini na sasa tunamwamini Kristo pekee. Baada ya kumwamini Kristo Yesu, tumebatizwa katika Jina la Baba la Mwana na la Roho Mtakatifu. Sasa katika maisha yetu yote tunaishi kwa neema na tutaendelea kuishi kwa neema. Tukanakuja pamoja katika kanisa na kushirikiana kama mandugu na madada kaatika Kristo. Kwa kufanya hivi tunajitoa kabisa kutumikiana kwa ajili ya Kristo Yesu.

Kama kanisa tunajitolea kufanya kazi ya Mungu na kuombeana. Tuanjitolea kudumisha umoja na amani miongoni mwetu. Tunatembea pamoja katika upendo wa kindugu; tunajaliana maslahi na kuchungana kwa uaminifu na kuhimizana na kuheshimiana kama wakristo wa Baba mmoja.

Tunajitoa kukutana pamoja na hatupuuzi kuombeana na pia kuwaombea wengine. Pia tunajitahidi kwa neema ya Mungu kuwaleta wengi katika ushiriki huu kwa kuwahubiria Injili ya Kristo Yesu ambayo ina nguvu za kuwafungua vipofu wa kiroho macho. Pia tumafurahia wakati wenzetu wanafurahia na pia huwa tunashirikiana wakati wa matatizo.

Lengo letu katika ulimwengu huu ni kuishi maisha matakatifu kwa neema ya Mungu kwa sababu sasa si ni viumbe vipya ndani ya Kristo Yesu. Hili ndilo jukumu letu sasa; kuishi maisha mapya.

Tunaendelea kwa uaminifu kueneza injili ya Kristo Yesu katika kanisa la Kristo kupitia kwa kutana pamoja na kuabudu, katika kubatiza wale ambao wameokoka, katika kushiriki meza ya Bwana pamoja, katika kutekeleza nidhamu katika kanisa na katika mafundisho ya kweli ya Biblia. Pia huwa tunajitoa sisi na mali yetu kwa ajili ya kazi ya Mungu na pia kwa kuwasaidia wandugu na wadada ambao hawana na hata wale ambao ni maskini. Tunajitoa kueneza injili ya Kristo Yesu kwa watu wa mataifa yote.

Pia tunajitoa kuungana na makanisa mengi ambayo yanafundisha ukweli wa neno la Mungu, kushikamana na kuendelesha ujumbe wa injili kote.

Katika haya yote, neema ya Bwana Yesu Kristo na upendo wa Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu uwe pamoja nasi. Amen.

Agano hili linatuonyesha kwamba kukua kama mkristo si jukumu tu la mtu mmoja binafsi na pia si la mchungaji pekee. Washirika wa kanisa wote wanahusisha wote katika majukumu haya. Hivi ndivyo tunavyoishi pamoja kama mwili mmoja wa Kristo. Unaposoma agano la kanisa letu utaona kwamba sote pamoja kama kanisa tumeamua kusaidiana kukua katika ukristo wetu. Simaanishi kwamba sasa kwa kufanya haya, tutakuwa tumekamilika, ukweli ni kwamba hatutakuwa wakamilifu lakini tumaini letu ni la kweli kwamba maisha yetu kama wakristo yatabadilika kila siku.

Ni tumaini langu kwamba katika letu na hata hilo lenu, sote tutafanya kazi pamoja na kuomba pamoja; tutatembea pamoja, na hatutapuuza kukutana pamoja na pia tutajitoa kuwasaidia wale wote ambao Mungu ataleta miongoni mwetu. Wakati wa furaha na shida tutakuwa pamoja. Tutajitahidi kuishi kwa amani pamoja na hawa na wengine na tutafanya kazi ya Bwana pamoja kwa kuwafikia watu wa mataifa wote.

Tunafanya haya yote kwa sababu tunajua kwamba wakati tutaondoka katika ulimwengu huu, tutakutana na wakristo wengine huko mbinguni na tutaendelea kufanya mambo haya kwa kikamilifu. Haya ndiyo mambo ambayo tunajitolea kuwafanyia wengine ili tukue na wao wakue katika ukristo wao.

4. Umuhimu wa kukua.

Je, kuna umuhimu wowote wa kukua katika ukristo wetu? Ukweli ni kwamba kukua katika ukristo wetu ni jambo la muhimu sana. Hii ndilo jukumu letu kama watoto wa Mungu. Wakati tunawaona washirika wakikua katika ukristo wao, je sifa ni kwa nini?

Jibu la swali hili linapatikana katika 1 Wakorintho 3:6: “Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye akuzaye.” Petero pia anasisitiza jambo hili kwa kusema kwamba, “Mwe na mwenendo mzuri mbele ya watu wasiomjua Mungu, ili kama wanawasema kuwa ninyi ni watenda mabaya, wayaone matendo yenu mema wamtukuze Mungu siku atakapokuja kuhukumu” (1 Petero 2:12). Hapa Petero alikumbuka maneno ya Kristo Yesu wakati alihubiri na kusema, “Vivyo hivyo, nuru yenu iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni” (Mathayo 5:16). Katika kazi yetu ya kuwasaidia wengi wawe wakristo na wengine wakue katika ukristo wao, ni kazi ambayo tunaifanya kwa utukufu wa Mungu na si watu mwingine yeyote. Hivi ndivyo Mungu atajidhirihisha kwa ulimwengu wote.

Kanisa ambalo linaendelea vyema nia yake kuu si kuwa na umati mkubwa wa watu, bali kuwa na washirika ambao wanakua katika imani yao ndani ya Kristo Yesu. Kanisa ambalo washirika wake wanakua katika imani ndilo kanisa ambalo kila mchungaji anafaa kujivunia.

Leo kuna wale ambao wanawaza kwamba imani ya ukristo huwa haikui. Ukweli ni kwamba kukua ni ishara kwamba mtu ana maisha ndani mwake. Ikiwa mkristo hakui katika imani yake, basi ni ishara kwamba Yeye hana uhai wa kiroho ndani mwake. Wakati ninazungumza kukua katika imani ni ninamaanisha kwamba mtu ambaye ameokoka ni mtu ambaye katika maisha yake ya kila hata kama yeye anapitia katika majaribu mengi, yeye bado anaendelea katika imani. Kumbuka kwamba ni wale tu ambao bado wako na

hai ndiyo wanaendelea kuishi. Vivyo hivyo wale ambao wameokoka na wanaendelea katika wokovu wao, hata kama majaribu makali yatawafikia, wao wataendelea kumwamini Mungu.

Paulo aliwaandikia wakristo katika Korintho kwamba wanafaa kukua katika imani yao (2 Wakorintho 10:15). Pia alitaka Waefeso wakue katika imani yao. Aliwaambia kwamba, "Badala yake, tukiambiana kweli kwa upendo, katika mambo yote tukue, hata tumfikie Yeye aliye kichwa, yaani, Kristo" (Waefeso 4:15; Wakolosai 1:10; 2 Wathesalonike 1:3). Kuna wakati wachungaji wanajaribiwa kushughulika sana na ni watu wangapi ambao wanahudhuria kanisa, ni wanagapi ambao wamebatizwa, ni wanagapi ambao wanatoa sadaka na watoa kiasi gani. Haya mambo yote hayadhihirishi kukua katika kanisa lolote, bali yanaonyesha tu idadi ya wale ambao wanahudhuria na matendo yao ambayo wanayafanya. Badala ya kuwa juu ya mambo kama ni wangapi wamehudhuria kanisa na ni pesa ngapi wametoa, tunafaa kujishughulisha na jinsi ya kushinda matatizo ambayo tunakumbana nayo kama wakristo na jinsi ya kusoma na kutii neno la Mungu.

Kukua katika imani ya ukristo si jambo ambalo linadhihirishwa kwa kuhisi furaha au kuzungumza katika ndimi au kujua sana Biblia. Pia si kupenda sana au kufurahia sana ndiko ishara ya kukua katika ukristo wako. Pia kusifu Mungu sana na kuwa na imani ndani mwake si ishara tosha kwamba mtu anakua katika ukristo wake. Hata kama mambo haya yote ni mazuri na yanaweza kuonyesha kwamba kweli mtu anakua katika imani yake, ukweli kwamba ishara ya kweli ambayo inadhihirisha kukua kwa kweli ni ongozeko na utakatifu ambao unatokana na kuishi maisha ya kujitolea na kujinyima. Kanisa linafaa kujishughulisha na kukua kwa aina hii miongoni wa washirika wake.

Maisha matakatifu miongoni mwa wale ambao wameokoka ni chombo ambacho Mungu huwa anatumia kuwafanya watu wake wakue katika ukristo wao. Wakati watu wa Mungu wanakua pamoja katika utakatifu na katika upendo juu ya wenyewe kwa wenyewe, wanaendelea kuona kwa wazi kabisa umuhimu wa nidhamu katika kanisa na umuhimu wa kuwahimiza wengine kukua katika imani hiyo hiyo. Kanisa ni chombo ambacho Mungu huwa anatumia kuwahimiza watu wake wakue katika neema. Ikiwa makanisani mwetu mawazo ya mchungaji ndiyo yanasikizwa sana kuliko neno la Mungu, ikiwa humo mtakuwa mahali ambapo Mungu hasikizwa na kuabudiwa kulingana na neno Lake na mahali ambapo ujumbe wa injili unapuuzwa na ushirika wa kanisa kutozingatiwa vilivyo, basi hilo halitakuwa kanisa ambalo linaangamiza nafsi za wengi. Kanisa la aina hii kamwe halitamtukuza Mungu. Hili litakuwa kanisa ambalo liko kinyume na neno la Mungu: "Basi kueni katika neema na katika kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Utukufu una Yeye sasa na milele. Amen" (2 Petero 3:18).

Katika ishara zote katika kitabu hiki, hii ndiyo ishara moja ambayo tunafaa kuwa waangalifu sana nayo kwa sababu kuna makanisa mengi ambayo yamejawa na watu wengi sana lakini watu hawa hawajali kabisa na makanisa ambayo wanayaita yao na pia hawajali kabisa kuhusu mambo ya Mungu. Katika makanisa mengi utapata watu wa aina mbali mbali. Katika kila kanisa kuna wale ambao ni wazuri na wanaishi maisha mazuri ambayo kwa nje yanaonekana bila dhambi. Pia kuna wale ambao kweli wameokoka na wanampenda Kristo sana kwa mioyo yao yote. Hawa ni watu ambao ni tofauti kabisa sana na wengine.

Kwa mingi nimekuwa nijiuliza kwa nini wale ambao wameokoka kweli ni watu tofauti kabisa na wale ambao hawajaokoka hata kama wanaonekana kuwa wao ni watu wazuri kwa nje. Jibu ambao nilipata ni kwamba, hawa ambao wameokoka kwa kweli wao wanaongozwa na neno la Mungu katika maisha yao yote.

Ikiwa tunataka kukua katika ukristo wetu na pia ikiwa kweli tunataka makanisa yetu yakue katika imani, lazima tulizingatia sana neno la Mungu. Lazima tulisoma neno hilo na tulitii neno hilo kaqtika kila hali ya maisha yetu. Tunafaa kumwomba Roho Mtakatifu atupatie mioyo ambaye ni minyenyekevu ambayo italipokea neno hilo na kulikubali. Kukua kwa kiroho ni jambo la lazima kwa kila mkristo kwa sababu kukua kwa kiroho kunadhihirsha kuwepo kwa maisha katika nafsi ya mtu.

5. Je, ni sababu gani ambayo inasababisha kanisa kukosa kukua?

Je, kwa nini wengine hawakui katika ukristo wao? Je, ni kwa sababu mtu hajaokoka? Paulo aliandika kwamba, "Ndugu zangu, mimi sikuwaza nanyi kama watu wa kiroho, bali kama watu wa mwilini, kama watoto wachanga katika Kristo" (1 Wakorintho 3:1). Kulingana na mstari huu, Paulo anasema kwamba katika kanisa la Korintho kulikuwa na wakristo ambao walikuwa wanaishi maisha yao tofauti na jinsi walivyokuwa wanakiri. Wao walikiri kuokoka lakini waliishi kinyume na maneno haya. Hapa Paulo anawaeleza kwamba hawafai kuwa watu wa aina hii ambao wanadai kuwa wameokoka ilhali wanaishi kinyume na kukiri kwao. Kwa hivyo Paulo anawaambia, waishi maisha yao kulingana na kukiri kwao.

Kuna wengi leo ambao wanaishi kama hawa na wanajidanganya kuwa wao wameokoka. Watu kama wao ni wale ambao wamechanganyikiwa kabisa na hawaelewi kuokoka ni nini na wao hawajaokoka.

Waza kuhusu inamaanisha nini kuwa mkristo. Sisemi kwamba mkristo ni mtu ambaye amekamilika kabisa na kwamba hana dhambi yoyote wala hafanyi dhambi yoyote. Kile ninamaanisha ni kwamba mkristo ni mtu ambaye amebadilishwa kabisa kutoka ndani, na moyo wake ni moyo ambao unakusudia kumpendeza Mungu katika kila jambo. Yeye sasa si mtumwa wa dhambi na dhambi si bwana wake. Bwana wake ni Kristo pekee na anajitahidi katika kila jambo kumpendeza.

Ikiwa wewe ni mkristo, mshukuru Mungu kwa sababu Yeye ndiye amefanya uwe mkristo. Yeye ndiye anayekupatia tamaa ya kuishi maisha matakatifu ambayo yanampendeza sana. Maisha haya unayaishi si kwa sababu ya nguvu zako, bali kwa sababu ya neema ya Mungu. Yeye ndiye anayekupatia nguvu za kukua katika ukristo wako. Kukua huko ni ishara ya maisha ya kweli ya kiroho na ni ishara ya kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho.

Ishara ya Tisa

Kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho, ni kanisa ambalo linaongozwa kulingana na neno la Mungu

Yaliyomo

1. Kanisa ambalo uamuzi wake unajumlisha washirika wote wa kanisa hilo
2. Mafundisho ya Biblia kuhusu viongozi wa kanisa

3. Uongozi katika kanisa kulingana na karama
4. Kuongoza kanisa kama Kristo Mwenyewe
- Bwana Mkubwa
- Mtu ambaye anawaongoza wengine vyema
- Kuwatayarisha wengine kuhudumu
- Kuhudumu
5. Uongozi kulingana na Jinsi Mungu alivyo.

Kuongoza kanisa kulingana na neno la Mungu

Dini ya ukristo inafundisha kwamba lazima kuwepo na uongozi na mamlaka katika jamii, katika familia na pia katika kanisa. Leo wengi hawatambui mamlaka au uongozi wa aina yoyote.

Je, Biblia inafundisha nini kuhusu mamlaka na uongozi katika kanisa? Kwa kujibu swali hili, tutatazama mambo matano kuhusu uongozi katika kanisa.
1. Kanisa ambalo uamuzi wake unajumlisha washirika wote wa kanisa hilo.
2. Mafundisho ya Biblia kuhusu viongozi wa kanisa.
3. Uongozi katika kanisa kulingana na karama.
4. Kuongoza kanisa kama Kristo Mwenyewe.
5. Uongozi kulingana na jinsi Mungu alivyo.

1. Kanisa ambalo uamuzi wake unajumlisha washirika wote wa kanisa hilo.

Jambo la kwanza tunafaa kuzingatia ni, uongozi katika kanisa ni jukumu la washirika wa kanisa lote. Biblia inafundisha kwamba uongozi katika kanisa ni wa washirika wote.

Katika makanisa mengi leo kuna kuchanganyikiwa kwingi kuhusu ni nani ambaye anaongoza kanisa na ni nani ambaye anafaa kutoa uamuzi wote kuhusu kanisa. Kuna wengine ambao wanasema kwamba hili jukumu la maaskofu au wachungaji. Wengine wao wanasema kwamba ni mchungaji pekee au yule ambaye anamwakilishi mchungaji wakati yeye hayuko. Katika haya yote kuna kuchanganyikiwa kwingi sana.

Katika Agano Jipya hakuna mpangilio kabisa jinsi ambapo ni nani anafaa kuongoza na ni nani anafaa kuwa mdogo wake. Lakini hii haimaanishi kwamba Biblia haisemi lolote kuhusu jinsi tunafaa kuliongoza kanisa la Mungu. Kuhusu maisha ndani ya Kanisa, Yesu Kristo alisema, "|Kama ndugu yako akikukosea, nenda ukamwonyeshe kosa lake, kati yenu ninyi wawili peke yenu. Kama akikusikiliza, utakuwa umempata tena ndugu yako. Lakini kama hatakusikiliza, nenda na mtu mwingine mmoja au wawili ili kila neno lithibitishwe na ushahidi wa mashahidi wawili au watatu. Kama akikataa kuwasikiliza hao, liambie kanisa, naye kama akikataa hata kulisikiliza kanisa, basi mtendeeni mtu huyo kama vile ambavyo mngemtendea asiyeamini" (Mathayo 18:15-17).

Katika mistari hii tunaona kwamba uamuzi wa mwisho si wa Askofu au mchungaji au msaidizi wa hawa, bali uamuzi huu ni wa kanisa lote kwa jumla. Katika Matendo ya Mitume 6:2-5 tunasoma, "Wale mitume kumi na wawili wakakusanya wanafunzi wote pamoja, wakasema, 'Haitakuwa vema sisi kuacha huduma ya neno la Mungu ili kutumika mezani. Kwa hiyo ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, watu wenye sifa njema, waliojawa na Roho Mtakatifu na hekima, ambao tunaweza kuwakabidhi kazi hii, wakati sisi tunatumia muda wetu mrefu kuomba na kulihudumia lile neno.'" Wakati mitume walisema hivi, kanisa lote lilifurahia jambo hili sana. Baadaye tunasoma kwamba kanisa liliwachagua watu hawa.

Hawa mitume ambao walisema maneno haya ni wale ambao kwa miaka michache walikuwa pamoja na Kristo Yesu katika huduma wake hapa ulimwenguni. Hawa ndiyo wale ambao majina yao yameandikwa katika jiwe katika Yerusalemu mpya (Ufunuo 21:14). Je, sisi ambao ni wachungaji leo tunafaa kufanya nini? Je, tunafaa kuongozwa aje katika majukumu yetu ndani ya kanisa?

Katika kifungu cha Matendo ya Mitume 6, tunawaona mitume wakilipatia kanisa nafasi ya kuamua ni kina nani ambao wanafaa kufanya mambo fulani fulani katika kanisa. Kwa kufanya hivi, walikuwa wanadhibitisha mafundisho ya Kristo katika Mathayo 18:15-17. Kanisa la Kristo Yesu ndilo liko na mamlaka ya kutekeleza majukumu kwa pamoja.

Katika Nyaraka za Paulo, tunaona kwamba nidhamu katika kanisa na mafundisho ya kweli yanatekelezwa kwa imani ndani ya Mungu na kanisa kwa ujumla. Hili ni jukumu la Mungu kwa kanisa lake. Kwa mfano kuhusu mambo ya nidhamu, Paulo anawahimiza watu Korintho kwamba, "Mnapokutana katika Jina la Bwana wetu Yesu nami nikiwepo pamoja nanyi katika roho na uweza wa Bwana Yesu ukiwepo, mkabidhini mtu huyu kwa Shetani, ili asili ya dhambi iangamizwe lakini roho yake iokolewe katika siku ya Bwana" (1 Wakorintho 5:4-5).

Hapa Paulo anahimiza kanisa lote kwamba wanafaa kumchukulia hatua yule ambaye alikuwa akifanya mambo ambayo hayakuambatana na imani ya kweli. Yeye alikuwa amekasirika na kanisa lote kwa sababu halikuwa limechukua hatua juu ya mtu huyu. Katika maneno yake, yeye hazungumzi tu na wachungaji au mashamasi, bali na kanisa lote kwa jumla.

Katika 2 Wakorintho 2:6, tunaona jinsi kanisa lilifanya kuhusu mtu huyu: "Adhabu hii aliyopewa na wengi inamtosha." Paulo alijua kwamba ni kazi ya kanisa kudumisha nidhamu katika kanisa lote. Paulo pia aliamini kwamba lilikuwa jukumu la kanisa lote kuhakikisha kwamba wanafundishwa neno la Mungu kwa uaminifu.

Wakati Paulo aliliandikia kanisa la Wagalatia, alisema, "Nashangaa kwamba mnamwacha upesi hivyo Yeye aliyewaita kwa neema ya Kristo na kuifuata injili nyingine, ambayo kwa kweli si injili kamwe, ila kwa dhahiri kuna watu wanaowachanganya na wanaotaka kuipotosha injili ya Kristo. Lakini hata ikiwa sisi au malaika atokaye mbinguni akihubiri injili nyingine tofauti na ile tuliowahubiria sisi, basi huyo mtu na alaaniwe! Kama vile tulivyokwisha kusema kabla, sasa nasema tena, ikiwa mtu yeyote atawahubiria injili kinyume na ile mliyoipokea na alaaniwe milele!" (Wagalatia 1:6-9).

Katika barua hii yote, Paulo anawahimiza hawa kwamba wanafaa kuhakikisha kwamba ile injili wanahubiriwa ni ya kweli. Paulo

anawaambia kwamba injili ambayo wamekuwa wakiisikiliza si injili ya kweli na kwa hivyo walifaa kuikataa kabisa. Katika maneno yake, Paulo hakumwandikia mchungaji wa kanisa hili, aliliandikia kanisa lote kwa sababu lilikuwa jukumu la kanisa lote kuhakikisha kwamba linahubiriwa injili ya kweli. Kanisa lilikuwa na mamlaka ya kuwachunguza wale wote ambao walidai kuwa wahubiri wa injili ili kuhakikisha kwamba wao walikuwa wahubiri wa kweli. Paulo alisisitiza jambo hili sana katika 2 Timotheo 4:3: "Maana wakati utakuja watu watakapokataa kuyakubali mafundisho yenye uzima, badala yake, ili kutimiza tamaa zao wenyewe watajikusanyia idadi kubwa ya walimu wapate kuwaambia yale ambayo masikio yao yanayowasha yanatamani kuyasikia."

Ikiwa uko katika kanisa ambapo injili ya kweli haihubiriwi, basi jua kwamba ni jukumu lako kuona kwamba injili inahubiriwa humo au uondoke na utafute mahali ambapo injili inahubiriwa kwa kweli. Ni jukumu la kanisa lote kuona kwamba injili ya Yesu Kristo inahubiriwa katika kanisa lao. Ikiwa uko katika kanisa ambamo injili haihubiriwi kwa kweli, jua kwamba mbele za Mungu wewe ni mwenye kosa. Kila kanisa yaani washirika wote wa kanisa hilo, wako na jukumu la kuhakikisha kwamba wanahubiriwa injili ya kweli na si ile ya uongo.

Wakati washirika wa kanisa wanazungumza kuhusu jambo fulani, iwe katika mikutano ya kanisa au wakati wako pamoja, ni lazima viongozi wa kanisa wawasikilize. Mchango wa kila mshirika wa kanisa katika mambo ya kanisa hilo ni wa muhimu sana na haufai kupuuzwa. Ni kweli kwamba huenda yale ambayo mshirika anasema hayatawezekana kufanywa wakati huo huo, lakini hata hivyo lazima asikilizwe kwa makini sana na kwa uangalifu bila kudharaliwa.

Washirika wa kanisa wanafaa kuhakikisha kwamba, yale ambayo wanahubiriwa ni ya kweli na kwamba miongoni mwao hudumu wa injili kwa wote utaendelea miongoni mwao na kwa wote. Washirika wote wako na jukumu la kuhakikisha kwamba Mungu anatukuzwa miongoni mwao kwa kuhakikisha kwamba Neno la Mungu linahubiriwa kwa uaminifu, Amri zake tunazitii na jinsi alivyo inadhihirika katika maisha yetu ya kila siku. Hili ni jukumu la kanisa kila mahali ulimwenguni kote.

Kanisa leo linafaa kufanya uamuzi wa pamoja katika mambo yote kama tu vile mitume walivyofanya. Uamuzi wowote katika kanisa, msingi wake ni Neno la Mungu na si mawazo yetu au hisia zetu. Washirika wa kanisa wanafaa kuhakikisha kwamba uamuzi na kutekelezwa kwa kila jambo miongoni mwao yanafanyika kulingana na neno la Mungu. Kazi ya mchungaji ni kwa Mungu na kwa kanisa ambalo analitumikia. Mchungaji asije akapuuza washirika wa kanisa lake kwa sababu ni Mungu ambaye anawatumia katika kanisa lake kutekeleza na kuamua juu ya mambo fulani fulani.

Viongozi na washirika wote wa kanisa wanajitahidi wote kudumisha umoja kupitia kwa kuwepo kwa amani na wanafanya kazi pamoja kuona kwamba kanisa linaendelea vyema na kwa utukufu wa Mungu. Wanafanya kazi pamoja kwa kufahamu kwamba neno na mapenzi ya Mungu yanatutosheleza kabisa katika maisha yetu yote.

Mpangilio wa uongozi katika kanisa unafaa kuongozwa na Kristo mwenyewe. Kristo Yesu ndiye kichwa cha kanisa; mamlaka yote yako mikononi mwake na anayatumia kwa njia ya kumtukuza Baba. Kristo amelipatia kanisa lake mamlaka ya kutekeleza majukumu fulani fulani ndani ya kanisa hilo. Vivyo hata wale ambao ni viongozi katika kanisa, Kristo amewapatia majukumu ambayo hawafai kupuuza hata kidogo.

Kila mkristo anafaa kuajibika katika kanisa, si tu kwa kuhudhuria kanisa siku ya Jumapili au kuomba au kutoa sadaka, bali zaidi ya haya, kila mkristo anafaa kujitolea kudumisha uhusiano wa kijamii na wakristo wenzake. Kila mkristo anafaa kuomba kwa ajili ya mkristo mwenzake na kufurahia wakati anasikia yale Mungu anafanya katika maisha ya wakristo wenzake. Kila mkristo anafaa kujali maslahi ya mkristo mwenzake. Mojawapo wa majukumu ya kila mkristo, ni kuhakikisha kwamba anawafahamu wakristo wenzake na pia yeye unahakikisha kwamba anafanya bidii ili wao wamfahamu vyema. Anafaa kufanya hivi kwa kusoma na kushiriki pamoja nao neno la Mungu. Hili ni jukumu la kila mshirika wa kanisa.

Kila mshirika anafaa kuhakikisha kwamba anakua katika neema ya Mungu na katika kufahamu neno la Mungu. Kila mkristo anafaa ajifahamu na kuwafahamu washirika wenzake. Anafaa kuwa mwangalifu kutumia vyema fursa za kuhubiri injili ambazo Mungu anaweka mbele za kanisa lake. Ni jukumu letu kama washirika wa kanisa kutumia fursa hizi vyema.

Kuna wale ambao Mungu amewapatia karama za kuhudumu kama viongozi katika kanisa. Kwa hivyo lazima tuwe na tamaa na tuwe waangalifu kuona kwamba katika makanisa yetu tunasaidia na kuheshimu viongozi. Ni jambo la hatari sana kwa maisha ya kiroho kuwa katika kanisa ambamo watu hawaamini uongozi wa kanisa au kuwa na watu ambao hawaaminiki. Washirika wa kanisa wanafaa kumshukuru Mungu kwa ajili ya viongozi ambao ametupatia katika kanisa. Ni lazima tumshukuru kwa wale ambao wako miongoni mwetu ambao amewapatia karama mbali mbali. Tuombe Mungu atusaidie tuwe watu wa kuwaamini wengine. Katika kitabu cha Waefeso 4, Paulo anazungumza kuhusu viongozi hawa katika kanisa na anasema kwamba viongozi hawa ni zawadi ya Mungu kwa kanisa. Tunafaa kuwa na makanisa ambayo yanamshukuru Mungu kwa kuwapa viongozi.

Katika kitabu cha Waebrania 13:17, tunasoma, "Watiini viongozi wenu na kujinyenyekeza chini ya mamlaka yao. Kwa maana hao wanakesha kwa ajili yenu kama watu watakaopaswa kutoa hesabu. Watiini ili kwamba wafanye kazi yao kwa furaha, wala si kama mzigo, maana hiyo haitakuwa na faida kwenu." Je, umeifanya kazi ya mchungaji wako kuwa yenye furaha na ya kuwahimiza wengi au umechangia katika kufanya kazi yake kuwa mzigo mkubwa sana kwake? Kifungu hiki kina maneno ambayo huwa hatutaki kusikia: "Watiini...Kujinyenyekeza." Haya maneno yapo katika neno la Mungu na tunafaa tuyatii.

Wengi huwa wanasema kwamba nitamtii kiongozi na kunyenyekea kwake kulingana na jinsi anavyoshughulikia mambo fulani na jinsi anavyovumilia katika mambo fulani fulani. Uongozi katika kanisa si kama uongozi katika mambo ya ulimwengu kwa sababu wengi katika mambo ya ulimwengu huwaza kwamba kiongozi ni mtu ambaye hakosei katika lolote. Kuna mafundisho katika Biblia kuhusu ni nani ambaye anafaa kuwa kiongozi. Katika 1 Timotheo 3:1-10 na Tito 1:5-9 tunasoma kuhusu mambo ambayo tunafaa kuzingatia katika wale ambao wanataka kuwa viongozi kanisani.

Tunafaa kuwa na imani na viongozi wetu tukifahamu kwamba wao ni kama tu sisi, yaani hawajakamilika. Ili tuweze kuwaamini lazima kwanza tumwamini Mungu ambaye ametupatia viongozi hawa (Waefeso 4:11-13). Hivi ndivyo kanisa linafaa kujiongoza kupitia kwa washirika wote wa kanisa.

2. Mafundisho ya Biblia kuhusu viongozi wa kanisa

Hapa tutatazama mafundisho ya Biblia kuhusu wale ambao wanafaa kuwa viongozi katika kanisa. Mimi kama mchungaji kila wakati ninaomba Mungu kwamba atupatie viongozi wazuri katika kanisa Lake. Haswa ninaomba sana kwamba Mungu ataleta miongoni mwetu kama kanisa watu ambao karama zao zinadhihirisha kuitwa kwao katika huduma wa uchungaji. Ikiwa imedhihirika kwa wazi kabisa kwamba mshirika fulani amepewa karama fulani na Mungu za uchungaji katika kanisa na baada ya maombi kanisa linakubaliana kwamba kweli karama hizi ziko, basi kanisa linafaa kumtenga mtu huyo kwa ajili ya kazi ya uchungaji. Katika makanisa mengi kuna watu ambao wanafanya kazi hii ya uchungaji bila wao kuitwa wachungaji.

Biblia inafundisha kuhusu kuwepo kwa wachungaji zaidi ya mmoja katika kanisa hata kama idadi kamili ya wachungaji ambao wanafaa kuwepo haijaelezwa. Agano Jipya linazungumza kuhusu wachungaji katika makanisa (Matendo ya Mitume 14:23; 16:4; 20:17; 21:18; Tito 1:5; Yakobo 5:14). Tunaposma katika kitabu cha Matendo ya Mitume na katika Nyaraka za Paulo, tunasoma kuhusu kuwepo kwa zaidi ya mchungaji mmoja katika kanisa.

Kuna jambo ambalo limenisaidia sana katika kazi yangu ya uchungaji na hili ni, kutambua wale ambao Mungu amewaita katika huduma wa uchungaji katika kanisa ambalo ninachunga. Hawa ni watu ambao washirika wa kanisa walitambua pia na kukubali kwamba wako na karama za kufanya huduma huu. Huwa tunakutana nao kila wakati na kuomba pamoja na pia kuzungumza kuhusu mambo fulani fulani na kwa kufanya hivi, huwa ninapata hekima katika mambo ambayo sikuwa ninayafahamu. Ni jambo la kuzingatia sana kwamba ni vyema zaidi kuwa na zaidi ya mchungaji mmoja katika kanisa na wachungaji hawa wawe wametoka miongoni mwa washirika wa kanisa na si watu ambao wametolewa nje ya kanisa.

Je, tutafanyaje ili tupate viongozi hawa katika makanisa yetu? Jibu ni kwamba, tuombe hekima kutoka kwa Mungu. Tuombe kwamba Mungu atatuongoza katika jambo hili. Pia tusome neno la Mungu haswa 1 Timotheo 3:1-10 na Tito 1:5-10. Katika vifungu hivi, tunaona ni nani ambaye anafaa kuwa mchungaji au shamasi katika kanisa. Hatufai tu kuwatafuta watu ambao wako na ushawishi katika kanisa, bali watu ambao wanakubaliwa na neno la Mungu.

Katika Agano Jipya kuna mistari ambayo inafundisha kwamba si lazima wachungaji hawa wote wawe ni wachungaji ambao wako na karama ya kuhubiri. Kwa mfano Paulo alipokuwa Korintho alijitolea kabisa kwa kuhubiri na kufundisha neno la Mungu kwa njia ambayo wachungaji wenzake katika kanisa hawangeweza kufanya hivyo (Matendo ya mitume 18:5; 1 Wakorintho 9:14; 1 Timotheo 4:13; 5:17). Katika kila kanisa Mungu amewapatia watu fulani fulani karama za kuwa wachungaji. Kwa kawaida wachungaji fulani watapewa karama ya kuhubiri mbele ya umati, wengine watakuwa na karama ya kufanya uinjilsti nyumba kwa nyumba, wengine watakuwa na karama ya kuwatembelea na kuwahimiza wagonjwa, wengine watakuwa na karama ya kutembelea jamii nyumbani mwao na kushiriki nao neno la Mungu. Lakini hata kama mambo yako hivi, kila mchungaji ako na jukumu la kufundisha neno la Mungu na kuwatembelea washirika wa kanisa.

Pia tunafaa kukumbuka kwamba uamuzi ambao huenda kanisa lisishirikishwe lote ni uamuzi ambao unafaa kutolewa na wachungaji wote na si mmoja. Kufanya uamuzi kama huu si jambo rahisi la kufanya lakini huwa linawasaidia wachungaji kutumia baadhi ya karama zao ambazo wako nazo. Wakati wanafanya uamuzi wa pamoja huwa inawalinda wote kutokana na malalamishi ambayo yanaweza kumlenga mmoja wao. Jambo hili linafanya kazi ya kuongoza katika kanisa kuwa rahisi na ambayo itaendelea hata ikiwa mmoja wa wachungaji hayupo. Jambo hili linafanya kanisa lichukue jukumu la kuona kwamba washirika wanakua katika imani yao na kufanya kanisa lisimtegemee yeyote bali Mungu pekee.

Washirika wengine katika makanisa wamechanganyikiwa sana kwa sababu wao huwaza kwamba kila kanisa linafaa kuwa na mchungaji mmoja tu, kamati ya wazee na mashamasi na wafanya kazi wengine wa kanisa. Afisi ya shamasi inapatikana katika Matendo ya Mitume 6. Kazi kuu ya shamasi ni kushughulikia mambo ya usaidizi kwa watu na kujua kwamba washirika wa kanisa wanashughulikiwa katika matatizo yao ya kila siku.

Je, unawaza kwamba kiongozi wa kanisa ni mtu wa aina gani? Je, wewe unawaza kuhusu mtu ambaye kazi yake ni kuwaambia wengine fanya hili au lile? Je, yeye ni mtu ambaye amehitimu na shahada ya uongozi katika chuo kikuu? Je, unawaza kuhusu mtu ambaye anajulikana na jamii fulani na mtu ambaye ni tajiri na anaheshimiwa sana?

Badala ya kutafuta watu ambao wamehitimu katika mambo ya kilimwengu, tunafaa kuwatafuta wale ambao wanajua neno, watu wavumilivu katika neno, watu ambao maisha yao yanaongozwa na neno la Mungu na watu ambao wanao uwezo wa kufundisha na kuhubiri neno la Mungu. Hawa ndio watu ambao tunafaa kutafuta na kuwakabidhi jukumu la kuongoza kanisa la Kristo. Ni vizuri kutafuta wale ambao tunaamini na wale ambao wanaamini katika washirika wa kanisa ambalo wanalichunga. Wanafaa kuwa wachungaji ambao wanakubali na kukubaliana na uamuzi wa kanisa lote na wako tayari kufanya kazi pamoja na kanisa hilo.

Hii ndiyo sababu Paulo katika 1 Timotheo 3, anasisitiza kwamba jinsi mchungaji anavyoshughulika na jamii yake, inadhihirisha jinsi atakuwa anashughulika na kanisa la Mungu. Pia katika kifungu hiki, tunaona jinsi mchungaji anafaa kuwa mtu wa kujitolea kuwatumikia wengine. Mchungaji hafai kuwa mtu ambaye anajijali tu au mtu ambaye anajali tu maslahi yake na ya jamii yake tu. Kazi yake ni kuwatumikia watu wa kanisa ambalo Mungu amempatia achunge. Yeye anafaa kuwa mtu ambaye tabia yake inakubalika na wengi. Mtindo wa maisha yako unafaa kuwa ule ambao ni wa kuwavutia wengi katika ufalme wa Mungu. Yeye anafaa kuwa mtu ambaye anaongoza jamii yake kwa njia mzuri kuambatana na neno la Mungu. Yeye anafaa kuwa mtu ambaye anaheshimiwa na wengine na mtu wa kiasi; mtu wa kuwakaribisha wengine na mtu ambaye ana uwezo wa kufundisha neno la Mungu; yeye hafai kuwa mtu wa ugomvi au vita au mwenye tamaa au mtu ambaye ameokoka juzijuzi na pia anafaa kuwa mtu ambaye sifa yake ni nzuri hata kwale ambao si wa imani.

Biblia inasema hivi kuhusu mashemasi, “Vivyo hivyo, shamasi nao wawe watu wanaostahili heshima, wasiwe wenye kauli mbili au wenye kujifurahisha kwa mvinyo, wala wanaotamani faida isiyo halali. Inawapasa kushikamana sana na ile siri ya imani kwa dhamira safi. Ni lazima wapimwe kwanza, kisha kama hakuna neno dhidi yao, basi na waruhusiwe kuhudumu kama mashemasi” (1 Timotheo 3:8-10).

Watu kama hawa ndiyo wanafaa kuwa viongozi katika kanisa. Viongozi ambao kazi yao si kunyanyasa watu wa Mungu bali nia yao ni kulinda na kuchunga watu wa Mungu kulingana na mafundisho ya Biblia. Hivi ndivyo viongozi wanafaa kuwa katika kanisa.

3. Uongozi katika kanisa kulingana na Karama.

Jambo lingine ambalo tunafaa kuzingatia ni uongozi katika kanisa kulingana na karama. Ninapozungumza kuhusu karama, simaanishi kuzungumza katika ndimi au kufanya miujiza au kutoa unabii. Kile ninamaanisha ni karama ambazo Mungu amepeana kwa neema ili watu fulani fulani katika kanisa waweze kutumikia kanisa lake. Biblia inafundisha kwamba Mungu hupeana karama katika kanisa ili watu wake waweze kukua katika imani. Hata wokovu wetu ni karama kutoka kwa Mungu. Karama za Roho Mtakatifu ni mfano mkuu wa neema ya Mungu kwa watu wake. Katika Warumi 5:17, Paulo alizungumza kuhusu karama kuu ya Mungu ambayo ni haki ya Kristo Yesu, na katika Warumi 6:23, anazungumza kuhusu karama nyingine kuu ambayo ni uzima wa milele kupitia kwa Kristo Yesu. Haki ya Kristo Yesu ni karama ya Mungu kwetu wenye dhambi.

Katika Warumi 11, Paulo anazungumza kuhusu karama ambazo Mungu alikuwa amewapatia watu wa Israeli (Warumi 11:29; 9:4-5). Katika Warumi 12:6-8, Paulo alitaja karama fulani fulani: "Tuna karama zilizotofautiana kila mmoja kutokana na neema tuliyopewa. Kama ni unabii na tutoe unabii kwa kadiri ya imani. Kama ni kuhudumu na tuhudumu, mwenye kufundisha na afundishe, kama ni kutia moyo na atie moyo, kama ni kuchangia kwa ajili ya mahitaji ya wengine na atoe kwa ukarimu, kama ni uongozi na aongoze kwa bidii, kama ni kuhurumia wengine na afanye hivyo kwa furaha." Karama hizi zote Mungu amezipeana kwa ajili ya kuwasaidia wakristo wote.

Katika 1 Wakorintho, Paulo anazungumza kuhusu karama za kufundisha, kuhimiza, kutoa kwa ukarimu, uongozi na kuonyesha huruma kuwa karama ambazo zimepeanwa kwa neema. Paulo aliwaambia wakristo wa kanisa la Korintho kwamba wao walikuwa watu ambao walikuwa wametajarishwa kwa kila hali (1 Wakorintho 1:5,7). Unapoendelea kusoma waraka huu wa 1 Wakorintho, utaona karama tofauti tofauti ambazo zimetajwa. Katika 1 Wakorintho 7:7, Biblia inasema kwamba kuna wale ambao wamepewa karama ya kutooa.

Mojawapo ya sababu za Paulo kuandika waraka huu wa 1 Wakorintho ilikuwa kwamba aweze kusahihisha mawazo yao kuhusu karama za Roho Mtakatifu na pia kuwafundisha jinsi karama hizi zinafaa kutumiwa na watu wa kanisa. Anasema, "Basi ndugu zangu, kuhusu karama za rohoni, sitaki mkose kufahamu" (1 Wakorintho 12:1). Kuanzia mstari wa 7, Paulo anapeana orodha ya karama tofauti tofauti na katika mstari wa 11, anasema kwamba, "Haya yote hufanywa na huyo huyo Roho mmoja, Roho naye humgawia kila mtu, kama apendaye mwenyewe." Katika mistari ya 27-31, Paulo tena anapeana orodha ya karama zingine na anawahimiza wakristo katika kanisa hilo kwamba, "Basi tamanini sana karama zilizo kuu." Katika 1 Timotheo 4:14 na 2 Timotheo 1:6, Paulo anasema kwamba kazi ya Timotheo ya kuhubiri injili ni karama ambayo ilipewa na Mungu. Kwa Waefeso, Paulo alisema, "Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyetubariki sisi kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo" (Waefeso 1:3).

Karama hizi zote ziko na lengo moja tu. Katika Warumi 1:11-12 tunaona kwamba Paulo alifahamu karama za roho zilipeanwa kwa ajili ya kuhimizana na kujengana kama wakristo. Katika 1 Wakorintho 12:4-7, tunaona wazi kwamba karama hizi zimepeanwa kuleta uzuri kwa kanisa la Kristo Yesu.

Mafundisho ya wazi kabisa kuhusu karama za rohoni yanapatikana katika 1 Wakorintho 14. Katika mstari wa 4, tunasoma kwamba, "Anenaye kwa lugha hujijenga mwenyewe, bali atoaye unabii hulijenga kanisa." Kuna wale ambao wanawaza kwamba kuna aina mbili ya kujijenga. Yaani wao wanawaza kwamba ikiwa mtu anataka kujijenga kiroho lazima azungumze kwa lugha na kuomba kwa lugha; na ikiwa kanisa linataka kukua, lazima litafute unabii. Paulo hamaanishi hayo hapa. Kwa mfano katika mstari wa kwanza, anawahimiza wakristo katika kanisa hili watamani haswa karama ya unabii. Baadaye katika mstari wa 12 anasema kwamba, "Kwa kuwa mnatamani kuwa na karama za rohoni, jitahidini kuzidi sana katika karama kwa ajili ya kulijenga kanisa." Katika mstari wa 19 anasema kwamba, "Lakini ndani ya kanisa ni afadhali niseme maneno matano ya kueleweka kwa akili ili niwafundishe wengine kuliko kusema maneno 10,000 kwa lugha." Kile Paulo anamaanisha hapa ni kwamba ni lazima uwe na uwezo wa kufahamu jambo ikiwa kweli utajengwa kiroho. Hili ndilo lengo la karama zote katika kanisa, yaani kulijenga kanisa.

Karama hizi zimepeanwa kwa ajili ya kujenga na kuimarisha mwili Kristo, yaani kanisa lake (1 Wakorintho 14:26). Hii ndiyo sababu kwa nini Roho Mtakatifu anapeana karama hizi kwa kanisa lake. Katika sura hii, Paulo anawakemea wote ambao wanatumia karama hizi kwa kujifaidisha wenyewe. Yeye anaonyesha wazi kabisa kwa nini karama hizi zinapeanwa na Roho Mtakatifu. Anasema kwamba karama hizi zilipeanwa kwa ajili ya kulijenga kanisa la Kristo. Yule ambaye anatamani na kujitahidi kulitumikia kanisa la Kristo Yesu ndiye yule ambaye atatumia karama zake kwa faida ya kanisa hilo: "Kila mmoja na atumie kipawa chochote alichopewa kuwahudumia wengine, kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za Mungu" (1 Petro 4:10).

Kwa sababu lengo kuu la karama ni kujenga na kuhimiza kanisa la Mungu, je tunafaa kufanya nini katika makanisa yetu? Hii inamaanisha kwamba tunafaa kutumia karama hizo ambazo zinalijenga kanisa la Kristo kwa uaminifu kabisa. Hii pia inamaanisha kwamba kazi kuu ya kulijenga kanisa la Kristo ni kupendana kama mandugu katika Kristo na kuombeana. Sisi sote tumeitwa kuwajali wengine na sisi kujijali kibnafsi. Kanisa linafaa kujitolea kabisa katika kufanya kazi pamoja ya kueneza injili, kuomba pamoja na kuishi kwa umoja, kupendana kama mandugu na madada katika Kristo Yesu, kusaidiana na kurekebishana; kuongozana kwa uaminifu, kukutana pamoja na kuomba pamoja na pia kushiriki neno la Mungu; kufurahiana na kuvumiliana na kuomba usaidizi wa Mungu katika haya yote.

Kwa mfano ikiwa kuna watu ambao wamekusanyika katika kanisa fulani na wako hapo kila mmoja anazungumza katika lugha yake, na mahali pengine kuna kikundi ambacho kinahudhuria mazishi ya mtu mmoja ambaye alikuwa mshirika wa kanisa lao, je, ni kikundi gani ambacho kinatekeleza majukumu yake kama kanisa? Ukweli ni kwamba ni kile ambacho kinamzika mmoja wao. Kanisa ni mahali ambapo kuna watu ambao wanajali wengine na wanafarijiana na kuhimizana katika mambo yote. Hiki ndicho kikundi ambacho Mungu anataka tuwe pamoja nacho.

Kuwa mkristo haimaanishi tu kuja kanisani na kusikiliza mhubiri anahubiri ni nini. Ukristo katika Agano Jipya unahusu jinsi unavyoishi na wale ambao wako karibu sana nawe. Ukristo wa kweli unahusu kujitolea kabisa kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu jinsi ameyafunua katika neno Lake. Roho Mtakatifu huwa anafanya kazi katika watu wa Mungu ili waweze kupendana na kushughulikiana. Ni karama ambayo Mungu amewapatia wengine ili waweze kuongoza ibada ya kumwabudu Mungu. Kuna wengine ambao wamepewa karama ya kuwatembelea wagonjwa na kuwahimiza kutoka kwa Biblia. Kuna wale ambao wamepewa karama ya kuongoza katika mambo fulani fulani ya kanisa. Kuna wale ambao wamepewa karama ya kufundisha neno la Mungu. Kuna wale ambao wamepewa karama ya kuwahimiza wengine kiroho. Mambo haya yote ni karama ambazo zimepewa watu wa Mungu na

Mungu mwenyewe. Roho Mtakatifu huwa anawaongoza watu wa Mungu kutumia karama zao. Ni lazima tufahamu kwamba kanisa huwa linaongozwa na karama tofauti ambazo zimepewa watu wa kanisa hilo.

Hivi ndivyo ilivyo na uongozi katika kanisa kulingana na karama.

4. Kuongoza kanisa kwa kufuata mfano wa Kristo Mwenyewe.

Je, umeshawahi kuona kanisa ambalo linaongozwa katika mfano wa Kristo mwenyewe. Katika maisha ya Kristo Yesu, kuna majukumu manne ambayo Kristo Yesu alitekeleza kama kiongozi. Haya ndio majukumu ambayo leo Kristo anataka yatekelezwe katika kanisa lake. Haya mambo ni ya muhimu sana katika uongozi wa kanisa.

1. Kiongozi ni mtu ambaye ana karama ya Kuongoza

Kristo Yesu aliamuru mambo mengi sana katika neno Lake. Kwa mfano alituamuru tuwaongoze wengine (Mathayo 28:20). Pia Paulo katika mafundisho yake aliwaeleza wakristo kwamba wanafaa kuwaongoza wengine na kuwaeleza kile wanafaa kukifanya. Paulo aliwaambia wachungaji kwamba wao ndiyo wanafaa kuamua kile ambacho kinafundishwa na kuhubiriwa katika kanisa kwa uvumilivu na kwa uangalifu sana (2 Timotheo 2:24-25; 4:2). Wale ambao ni wachungaji, tunafaa kufundisha kwa uangalifu sana neno la Mungu kwa sababu tutatoa hesabu mbele za Mungu jinsi tulivyofundisha neno lake (Yakobo 3:1). Kuna wakati ambapo wachungaji wa kanisa wanafaa kuwa mstari wa mbele katika kutoa uamuzi fulani na kuajibika kwa sababu ya uamuzi wao.

Kuna wengi ambao hawako tayari kufanya jambo hili. Bwana Yesu Kristo aliwaamuru wafuasi wake kufanya jambo hili. Wachungaji lazima wawe tayari kuajibika katika hali ambapo wanahitajika kufanya uamuzi fulani. Uongozi wa aina hii hatufai kuepuka hata kidogo. Ninajua kwamba kuna wale ambao wanatumia mamlaka yao vibaya sana. Ikiwa tutaongoza kulingana na neno la Mungu, basi wengi wataheshimu uongozi wetu.

2. Kiongozi ni mtu ambaye anawaongoza wengine vyema akiwa mfano wa kumfuatwa

Huu ni uongozi ambao mtumishi au watumishi wa Mungu wanaongoza kanisa wao wenyewe wakiwa mifano ya jinsi ya kuongoza kanisa. Uongozi bora ni kutoa mifano au kutoa mwelekeo katika mambo fulani fulani katika kanisa. Viongozi wazuri huwa wanaongoza kwa kuwa mfano au kwa kutoa mwelekeo.

Katika Yohana 13:34, Yesu alisema, “Amri mpya nawapa: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane.” Paulo aliandika, “Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu” (Wafilipi 2:5). Petro naye aliwaambia wakristo kwamba walifaa kukumbuka kwamba, “Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake” (1 Petro 2:21). Paulo naye aliandika kwamba, “Niigeni mimi kama nami ninavyomwiga Kristo” (1 Wakorintho 11:1). Pia Paulo aliwaambia Wathesalonike kwamba yeye alikuwa amefanya kazi ili awe mfano ambao wanaweza kujifunza kutoka kwake (2 Wathesalonike 3:7-9). Yeye alifanya kazi kusudi lake likiwa kuishi maisha matakatifu. Yeye alionyesha wasikilizaji wake jinsi walifaa kuishi maisha yao.

Hivi ndivyo tunafaa kufanya na kuishi maisha yetu. Ni jukumu letu kama viongozi katika kanisa kuwa mifano kwa wengine (Yohana 13:15; Wafilipi 3:17; 1 Timotheo 4:12; Tito 2:7; Yakobo 5:10).

3. Kiongozi ni mtu ambaye anawatayarisha wengine kufanya huduma tofauti tofauti kulingana na karama zao

Uongozi wa aina hii ni kama ule katika jeshi. Kuna yule ambaye anapeana mwelekeo halafu mwelekeo huo unahakikishwa na wale ambao wako mahali ambapo kazi yenyewe inafanyika. Uongozi huu una vikundi mbali mbali ambavyo vimetengenezwa kwa ajili ya kufanya kazi ya kanisa katika hali tofauti tofauti kwa kushughulikia kila sehemu katika kanisa. Kwa mfano, kuna wale katika huduma ya watoto, katika huduma ya kuandika vitabu, huduma ya kuweka kanisa safi na hudumu zinginezo.

Ikiwa Mungu ametupatia uwezo wa kuwaongoza wengine na kuwaonyesha jinsi ya kufanya kazi katika huduma zao, basi tunafaa tufanye hivyo kwa uaminifu na kwa uangalifu. Katika Luka 9 na 10, tunasoma kwamba Bwana Yesu Kristo aliwatayarisha wanafunzi wake na baadaye akawatuma kuhubiri injili kwa wote.

Hali yetu leo ni tofauti kwa sababu hatuwezi kuenda na wale ambao tunawatuma kuhubiri kwa sababu Yesu Kristo alikuwa pamoja na wanafunzi kiroho. Lakini sisi tunaweza kufanya vile Paulo alifanya. Katika barua yake ya mwisho, Paulo alimwagiza Timotheo kwamba, awafundishe wale ambao walikuwa na karama ya kuwafundisha wengine (2 Timotheo 2:2). Paulo alifahamu kwamba yeye anaweza kuendeleza huduma yake ikiwa angewasaidia wengi kutumia karama ambazo walikuwa wamepewa na Mungu kwa kuwahudumia wengine.

Kiongozi ni mtu ambaye anakubali Kutumika kwa ajili ya wengine

Huu ni uongozi ambao Kristo Yesu mwenyewe alionyesha kwetu. Kristo alionyesha uongozi huu kwa kufa msalabani kwa niaba yetu. Kristo ni kiongozi ambaye alijitolea kutumika na wala si kutumikiwa. Jambo hili linaonekana wazi katika Agano Jipya lote. Uongozi huu unaonekana wazi katika Wafilipi 2 na 1 Petro 2.

Huu ndio uongozi ambao Kristo anataka tuongoze nao kanisa lake. Petro aliandika, “Kwa wazee waliomo miongoni mwenu, nawasihi mimi nikiwa mzee mwenzenu, shahidi wa mateso ya Kristo na mshiriki katika utukufu utakaofunuliwa, lichungeni kundi la Mungu mlilokabidhiwa, mkitumika kama waangalizi, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari, kama Mungu anavyowataka mwe, si kwa tamaa ya fedha, bali mlio na bidii katika kutumika. Msijifanye mabwana juu ya wale walio chini ya uangalizi wenu, bali iweni vielelezo kwa hilo kundi. Naye Mchungaji Mkuu atakapodhihirishwa mtapokea taji ya utukufu isiyoharibika” (1 Petro 5:1-4). Hivi ndivyo tunafaa kuongoza kanisa.

5. Uongozi kulingana na Jinsi Mungu alivyo.

Tunapomalizia mafundisho kuhusu uongozi katika kanisa, tunafaa kuona jinsi ya kutekeleza uongozi huu katika kanisa inavyohusiana na jinsi Mungu alivyo.

Uongozi katika kanisa haupo kwa minajiri ya siasa. Ninasema hivi kwa sababu ninajua kuna wale ambao hawapendi kuongozwa na wanachukia sana mamlaka ya aina yoyote.

Wanadamu huwa hawataki kutii au kuishi chini ya mamlaka na pia wakati huo huo wakipewa mamlaka wanayatumia vibaya kwa sababu tumeanguka katika dhambi. Ukweli ni kwamba mamlaka bila kuongozwa na Mungu au mamlaka ambayo lengo lake si kumtukuza Mungu, ni mamlaka kutoka kwa shetani. Pia si jambo jema kukosa kuwa na imani katika uongozi wowote. Kukosa kuwa na imani katika uongozi wowote, ni kuonyesha kwamba kuna kasoro na mtu huyu au watu hao. Kuishi maisha yetu kulingana na neno la Mungu ni kuishi maisha yetu tukimwamini Kristo. Ikiwa tunamwamini Mungu, ni lazima pia tuwaamini wale ambao amewaweka katika mamlaka.

Kuwa na uwezo wa kuamini wale ambao Mungu ameweka katika mamlaka, ni kudhihirisha umbo la Mungu katika maisha yetu kwamba sisi ni watu ambao tunamtii Mungu wetu na Mwokozi wetu. Ni kufanya kazi kulingana na mapenzi ya Mungu na mipango Yake.

Katika Waefeso 3:14-21, Paulo anawaambia wakristo katika kanisa la Efeso kwamba aliwaombea kwa Baba ambaye kutoka Yeye ubaba wote wa kila jamaa za mbinguni na duniani unaitwa. Paulo hapa hasemi tu kwamba Mungu ni Baba wa jamii yake, bali pia anasema kwamba Mungu ndiye ametuumba katika mfano wake na pia kwamba mamlaka yote katika uongozi wowote hata katika familia, unatoka Kwake. Kwa hivyo mambo ya mamlaka kwetu wakristo ni mambo ya kuzingatiwa sana na kwa uangalifu kwa sababu uongozi na mamlaka ni mapenzi ya Mungu. Kwa kutii mamlaka na kuheshimu uongozi ni kuishi maisha yetu tukidhihirisha utukufu wa Mungu katika maisha yetu kama wakristo.

Jamii ni mahali ambapo Mungu ametuweka ili tuweze kujifunza kuongoza kwa upendo. Hapa ni mahali ambapo tunajifunza kuheshimu, kupenda, kutii na kuamini kama matayarisho ya kutuwezesha kuwa na uhusiano na wengine haswa na Mungu mwenyewe.

Tunafaa kutekeleza mamlaka kwa njia ambayo inafaa na ina mpangilio. Popote tuko ni lazima tuzingatie jambo hili. Tuwe kazini mwetu, au nyumbani mwetu au kanisani, lazima tuhakikishe kwamba utukufu wa Mungu unadhihirika kwa wote.

Jinsi tunavyoishi maisha yetu katika kanisa kulingana na kanuni za uongozi inafaa kulingana na mafundisho ya Biblia kuhusu injili. Tunafaa kuhakikisha kwamba maisha yetu yanafanya ujumbe wa injili upendeze na wala si kukashifiwa na wote. Tukifanya hivi, tutaweza kueneza ujumbe wa injili ya Kristo kwa wote. Tutaweza kuwaonyesha wote upendo wa Mungu kwa ulimwengu wote.

Hii ni kazi kuu ya kueneza ujumbe wake wa injili na wakati huo huo tuna jukumu kutoka kwa Mungu kutii mamlaka ya kanisa. Hii ni ishara ya kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho. Huu ni mwito wetu kama wakristo: kutii mamlaka. Hii ni baraka yetu. Ulimwengu unahitaji kuona na kujua kwamba kuna Mungu ambaye anaokoa na kuwafanya watu kuwa wapya kiroho. Tuombe Mungu tushikane na tuendeleze mapenzi ya Mungu katika makanisa yetu. Tujitahidi kudumisha afya ya kiroho katika makanisa yetu kwa utukufu wa Mungu.

Baadhi ya njia ambazo ni za kukusaidia katika kuongoza kanisa la Mungu vyema

Njia ambayo ni njema

Ikiwa kweli wale ambao tuko pamoja nao katika makanisa yetu wameokoka wote na wamejitolea katika kanisa, basi sura ya kanisa kulingana na mafundisho ya Agano Jipya kwamba ni mwili mmoja utakuwa imetimilika miongoni mwetu.

Mungu ametuita sisi tuishi maisha matakatifu tukiwa pamoja kama kanisa. Kwa sababu ya kuwa mmoja wa kanisa la Kristo, nimekua katika ukristo wangu kwa sababu ya kazi ya Mungu kupitia kwa ndugu na dada zangu wa kiroho. Mungu amekusudia kufanya kazi ndani mwetu kupitia kwa Roho Mtakatifu akiwatumia ndugu na dada zetu wa kiroho. Uhusiano mwema na wengine ni jambo la umuhimu sana katika kanisa lolote.

Amri ya tatu, Mungu anawaonya watu wake kwamba hawafai kulitaja jina la Bwana bure (Kutoka 20:7; Kumbukumbu la Torati 5:11). Katika hili Mungu alikuwa anamaanisha kwamba mtu yeyote hafai kujiita mfuasi wake ikiwa hataishi kama watu wake wanavoishi.

Amri hii pia ni kwetu kama kanisa leo. Makanisa mengi leo huwa yanajitakia yenyewe katika shughuli ambazo yanatekeleza. Wakati wanafanya haya yote, wao hudai kwamba wanakua kiroho. Huwa makanisa yanadanganyika kwamba yakitaka kumwabudu Mungu lazima wafanye mambo kama, Kuimba na kucheza muziki kwa sauti ya juu sana, kuomba kwa sauti ya juu sana na kuhubiri kwa kupiga makelele na mambo mengi kama haya. Huwa mara kwa mara tunaishi maisha ambayo ni ya kupenda ulimwengu badala ya kuishi maisha ambayo yako kinyume na ulimwengu (2 Timotheo 3:12). Leo makanisa mengi hayajali kamwe ishara ambazo ziko katika Biblia kuhusu jinsi makanisa yanafaa kutekeleza majukumu yake.

Maisha ya kiroho ya kanisa yanafaa kuwa jambo ambalo kila mshirika analizingatia kwa sababu linahusu maisha ya kiroho ya kila mkristo katika kanisa hilo haswa wale ambao wameitwa katika uongozi. Makanisa yetu yanafaa kudhihirisha utukufu wa injili ya Kristo kwa viumbe vyake kupitia kwa kila mtu ambaye ni mshirika wa kanisa. Pia utukufu huu unadhihirishwa kupitia kwa jinsi wakristo wanavyoshughulikiana. Hii ndiyo sababu ambayo imefanywa tuitwe na Mungu, yaani tumeitwa kudhihirisha Mungu na jinsi alivyo kwa njia ya utukufu sana kwa viumbe vyake vyote (Waefeso 3:10). Tunafaa kumtukuza kupitia kwa maisha yetu.

Jinsi ya Kuongoza

Waza kwamba kuna mchungaji mmoja ambaye atasimama katika mkutano wa kanisa na kuanza kusema wazi kwamba, ako na shaka kuhusu wokovu wa baadhi ya washirika, yeye hatawabatiza watoto, hataki tena kikundi kimoja cha waimbaji bali ni kanisa lote

ambalo litaimba pamoja, haamini katika kuwaita watu mbele ili waokoke, atafutilia mbali kamati ya wazee wa kanisa, hakuna kusherekea siku fulani fulani katika kanisa; hataki tena kuwaona wamama wakiongoza katika kanisa na kanisa litaanza kudumisha nidhamu. Pia atasema kwamba badala ya mambo haya yote, kanisa linafaa kuongeza ibada za Jumapili. Mchungaji kama huyu, atakataliwa kwa haraka sana na washirika.

Kile ninataka kuonyesha ni kwamba, ikiwa tutakuwa na uvumilivu, hekima, na kwa uangalifu kuongoza na kusaidia, tukifanya haya yote kwa maombi na kwa upendo, tutakuwa na makanisa ambayo yatamtukuza Mungu.

Hapa kuna mambo manne ambayo kila mchungaji anafaa kuzingatia katika uongozi wake wa kanisa.

1. Mchungaji anafaa kuwa mtu wa kusema ukweli.

Mwombe Mungu kwamba atakusaidia uwe mwaminifu kwa neno Lake. Mchungaji yeyote hafai kupuuza nguvu na baraka za kuhubiri neno la Mungu kwa uaminifu. Mwombe Mungu kwamba atakusaidia uwe mtu ambaye anaaminika. Mwombe kwamba Mungu atakusaidia uwe unasema ukweli kwa wote na si kuwaficha wengine mambo katika kanisa na kuyazungumza na wengine. Mwombe Mungu kwamba atakusaidia kusema ukweli kwa wote ambao wanakuuliza maswali na zaidi kwamba utawasaidia wale ambao hawakujui vyema waweze kukujua.

2. Mchungaji anafaa kuwa mtu ambaye anaaminika na washirika wake.

Mchungaji anafaa kuwa mtu ambaye anamtegemea Mungu na si kujitegemea mwenyewe na uwezo wake. Mchungaji anafaa kuwa mtu ambaye ana wakati wa kuomba akiwa peke yake, akiwa na wengine na pia akiwa na kanisa lake. Mchungaji anafaa kuwa mtu mvumilivu kila wakati akiyakumbuka maneno ya Paulo kwa Timotheo: “Huhubiri neno uwe tayari wakati ufao na wakati usiofaa, karipia, kemea na kuonya kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho mazuri” (2 Timotheo 4:2).

Mchungaji anafaa kila wakati kumwamini na kumtegemea Mungu pekee. Hafai kutegemea mawazo yake na mipango yake. Anafaa kila wakati kumwamini Mungu kwa ajili ya maisha yake. Anafaa kuwa tayari kila wakati akimwomba Mungu amwezeshe kila wakati kukubali mapenzi yake Mungu. Kuna wakati ambapo Mungu anawaacha mtu mahali fulani kwa muda mrefu sana hata wakati mwingine katika maisha yake yote mchungaji huyo anakuwa mahali pamoja tu. Pia kuna wakati ambapo Mungu anamwezesha mchungaji kuhudumu mahali tofauti tofauti. Lazima mchungaji awe tayari kuongozwa na Mungu na si mapenzi yake mwenyewe.

Mchungaji anafaa kumwomba Mungu kila wakati kwamba atamsaidia kuona kwamba kanisa la Kristo ni kuu sana kuliko mchungaji mwenyewe na mipango yake.

3. Mchungaji anafaa kuwa mtu wa tumaini wala si wa kulalamikia wengine na kuona tu ubaya wao.

Mchungaji anafaa kumwomba Mungu kwamba yeye hatakuwa mtu ambaye kila wakati anaona tu ubaya wa wengine na kulalamika tu. Mchungaji anafaa kuwa mtu wa kuwahimiza wengine na kuwaombea badala ya kuzungumza kuhusu ubaya wao. Mchungaji anafaa kwa wazi kabisa kuwaeleza watu kuhusu kusudi la kanisa na jinsi mipango yake inaambatana na kusudi hilo. Anafaa kuwaeleza mipango ambayo anayo kwa kanisa na mipango hiyo ni ya muda gani.

Mchungaji anafaa kumwomba Mungu kwamba yeye ataweza kuwa na uhusiano mwema na wa thabiti na washirika wote wa kanisa lake. Wala si washirika wachache tu. Anafaa kuomba Mungu kwamba atamwezesha kuwatayarisha wale ambao wako na karama katika kanisa hilo ili waweze kutumika vyema katika kanisa hilo (2 Timotheo 2:2). Anafaa kuomba kwamba Mungu atamfanya awe mfano mwema katika mambo ya kueneza injili hata kuwatuma wengi nje kuhubiri injili. Anafaa kuomba kwamba Mungu atazidisha tamaa yake ya kumtumikia. Pia kwamba Mungu atazidisha tamaa katika kanisa ya kumtumikia Mungu.

4. Mchungaji anafaa kujifunza kutokana na yale ambayo yalifanyika katika historia ya kanisa hilo.

Anafaa kujifunza kutoka kwa washirika wa zamani wa kanisa hilo. Kwa kufanya hivi, yeye huonyesha kwamba anaheshimu historia ya kanisa na kwamba pia ako tayari kujifunza mengi.

Mchungaji anafaa kuwa mstari wa mbele katika kutumia na kuzingatia yale ambayo yalikuwa ya muhimu katika historia ya kanisa hilo. Pia yeye anafaa kuwa mstari wa mbele katika kuongoza kanisa katika kumtii Mungu kwa yale ambayo ameyadhihirisha wazi katika neno lake.

Kumdhihirisha Mungu na jinsi alivyo katika maisha ya hapa ulimwenguni, ni jukumu ambalo Mungu ametupatia sisi wakristo. Hii ni baraka kubwa sana kwetu. Ninaomba Mungu kwamba atalifanya kanisa lako liwe kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho kwa kumtuma Roho Matakatifu katika kanisa hilo na makanisa yake yote ulimwenguni kwa ajili ya utukufu wake. Ninaomba kwamba Mungu atakubariki katika juhudi zako za kumtumikia kanisa lake.